



# **Open Bible Stories Translation Notes**

**Toleo. 4.1**

[sw]

# Haki miliki na leseni.

## Open Bible Stories Translation Notes

Tarehe: 2020-02-18

Toleo.: 4.1

Iliyochapishwa na: Door43

## Open Bible Stories

Tarehe: 2017-12-18

Toleo.: 4.1

Iliyochapishwa na: Door43

## unfoldingWord® Translation Academy

Tarehe: 2022-04-29

Toleo.: 27

Iliyochapishwa na: unfoldingWord®

## translationWords

Tarehe: 2018-09-25

Toleo.: 7.3

Iliyochapishwa na: Door43

## License

### Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International (CC BY-SA 4.0)

This is a human-readable summary of (and not a substitute for) the full license found at <http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/>.

#### You are free to:

- **Share** — copy and redistribute the material in any medium or format
- **Adapt** — remix, transform, and build upon the material for any purpose, even commercially.

The licensor cannot revoke these freedoms as long as you follow the license terms.

#### Under the following conditions:

- **Attribution** — You must give appropriate credit, provide a link to the license, and indicate if changes were made. You may do so in any reasonable manner, but not in any way that suggests the licensor endorses you or your use.
- **ShareAlike** — If you remix, transform, or build upon the material, you must distribute your contributions under the same license as the original.

**No additional restrictions** — You may not apply legal terms or technological measures that legally restrict others from doing anything the license permits.

**Notices:**

You do not have to comply with the license for elements of the material in the public domain or where your use is permitted by an applicable exception or limitation.

No warranties are given. The license may not give you all of the permissions necessary for your intended use. For example, other rights such as publicity, privacy, or moral rights may limit how you use the material.

# Jedwali la Yaliyomo

<b>Open Bible Stories Translation Notes</b> .....	<b>9</b>
1. Uumbaji .....	9
2. Dhambi Inaingia Ulimwenguni .....	36
3. Gharika .....	51
4. Agano la Mungu na Abrahamu .....	69
5. Mtoto wa Ahadi .....	79
6. Mungu anamjalilia Isaka .....	94
7. Mungu Anambariki Yakobo .....	102
8. Mungu anamuokoa Yusufu na Familia yake. ....	114
9. Mungu Anamwita Musa .....	133
10. Mapigo Kumi .....	151
11. Pasaka .....	166
12. Kutoka .....	174
13. Agano la Mungu na Israeli .....	191
14. Kuzunguka Jangwani .....	212
15. Nchi ya Ahadi .....	231
16. Wakombozi .....	247
17. Agano la Mungu na Daudi .....	271
18. Ufalme Uliogawanyika .....	286
19. Manabii .....	299
20. Kuchukuliwa Mateka na Kurudi .....	320
21. Mungu Anaahidi Ujio wa Masihi .....	337
22. Kuzaliwa kwa Yohana .....	359
23. Kuzaliwa kwa Yesu .....	369
24. Yohana Anambatiza Yesu .....	383
25. Shetani Anamjaribu Yesu .....	394
26. Yesu Anaanza Huduma yake. ....	404
27. Simulizi ya Msamaria Mwema .....	416
28. Kijana Tajiri Kiongozi .....	430
29. Simulizi ya Mtumishi Asiye na Huruma. ....	443
30. Yesu Anawalisha Watu Elfu Tano .....	454
31. Yesu Atembea Juu ya Maji .....	463
32. Yesu Amponya Mwanamume Aliyepagawa - pepo na Mwanamke Mgojwa .....	471
33. Simulizi ya Mkulima .....	489
34. Yesu Anafundisha Mambo Mengine .....	499
35. Habari za Baba mwenye Huruma .....	510
37. Kubadilika Sura .....	524
37. Yesu Amfufua Lazaro kutoka Wafu .....	531
38. Yesu Anasalitiwa .....	544
39. Yesu Anashitakiwa. ....	564
40. Yesu Anasulubiwa .....	580
41. Mungu Anamfufua Yesu kutoka katika Wafu .....	591
42. Yesu Anarudi Mbinguni .....	600
43. Kanisa Linaanza .....	613
44. Petro na Yohana Wamponya Ombaomba .....	628
45. Stephano na Filipo .....	640
46. Paulo Anakuwa Mkristo .....	655
47. Paulo na Sila wakiwa Filipi .....	668



48. Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa: .....	683
49. Agano Jipya la Mungu .....	701
50. Yesu Anarudi .....	723
<b>translationWords</b> .....	<b>745</b>
Abrahamu, Abramu .....	746
Abudu .....	747
Adamu .....	748
Adili, uadilifu .....	749
Agano .....	750
Ahabu .....	751
Ahadi .....	752
Amani .....	753
Amri kumi .....	754
Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru .....	755
Baali .....	756
Bahari ya shamu .....	757
Barnaba .....	758
Bathsheba .....	759
Batiza, ubatizo .....	760
baya, ovu, uovu .....	761
Bethlehemu .....	762
Bikira .....	763
Busara, hekima .....	764
bwana, mkuu .....	765
damu .....	766
Daudi .....	767
dhabihu, sadaka .....	768
dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi .....	769
dhihaki .....	770
Eliya .....	771
Esau .....	772
Farao, mfalme wa Misri. ....	773
Filipi .....	774
funga .....	775
furaha, mwenye furaha .....	776
Galilaya, Mgalilaya .....	777
Gari .....	778
Gibeoni. Wagibeoni .....	779
Gideoni .....	780
habari njema, injili .....	781
Hajiri .....	782
haki, adilifu .....	783
Haruni .....	784
hatia, mwenye hatia .....	785
Hawa .....	786
hekalu .....	787
hema la kukutania .....	788
hukumu .....	789
imani .....	790
imani, aminifu, .....	791
inua, inuka .....	792
Isaka .....	793

Isaya	794
Ishmaeli	795
Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli	796
Jehanamu, ziwa la moto	797
kaburi	798
Kalebu	799
Kanaani, Mkanaani	800
Kanisa	801
Kiburi	802
kifo, kufa, mfu	803
komboa, mkombozi, ukombozi	804
kondoo, kondoo dume, kondoo jike	805
Kristo, Masihi	806
Kuadhibu, adhabu	807
Kuamini, kuamini katika	808
Kubariki	809
kuhani mkuu	810
Kuhani, ukuhani	811
Kuhubiri	812
kujaribu, jaribu	813
Kundi la watu, watu	814
kuomba	815
Kuomba, maombi	816
Kupokea	817
kusaliti	818
Kusifu	819
Kutubu, toba	820
Kuwa na mapepo	821
Kuwatesa, mateso	822
kweli, ukweli, kuwa kweli	823
Laana, kulaaniwa	824
Lazaro	825
Madhabahu	826
maisha, uhai, kuishi, kuwa hai	827
Malaika, Malaika mkuu	828
Mariamamu, mama yake Yesu	829
mbingu, anga, mbinguni	830
mchungaji, kuchunga	831
mfalme	832
Mfalme wa Wayahudi	833
mfuasi	834
Midiani, Wamidiani	835
milele	836
Misri, Mmisri	837
Mji wa Babeli	838
Mkristo	839
Msalaba	840
Mto Nili, Mto wa Misri	841
Mto Yordani, Yordani	842
Mtume, utume	843
mtumishi, mtumwa, utumwa	844
Mungu	845


Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba .....	846
mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike .....	847
Musa .....	848
muujiza, ajabu, ishara .....	849
mwalimu, Mwalimu .....	850
mwaminifu, uaminifu .....	851
Mwamori .....	852
Mwana wa Mungu, Mwana .....	853
mwana, mwana wa .....	854
mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu .....	855
Myahudi, Yahudi, Wayahudi .....	856
Naamani .....	857
Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke. ....	858
Nathani .....	859
Nazarethi, Nazarini .....	860
Nchi ya ahadi .....	861
ndoto .....	862
Nebukadneza .....	863
Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko .....	864
Nguvu .....	865
Nuhu .....	866
nyenyekea, unyenyekevu .....	867
okoa, salama .....	868
Pasaka .....	869
Paulo, Sauli .....	870
pepo mbaya, roho ovu, roho chafu .....	871
Petro, Simoni Petro, Kefa .....	872
Pilato .....	873
Ponya, tibu .....	874
Rahabu .....	875
Rebeka .....	876
rehema .....	877
Rehoboamu .....	878
rithi, urithi, mrithi .....	879
Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana. ....	880
roho, kiroho .....	881
Rumi .....	882
Sabato .....	883
Samaria, Msamaria .....	884
samehe, kusamehe .....	885
Sara, Sarai .....	886
Sauli (A K) .....	887
sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe .....	888
Shetani, ibilisi, yule muovu .....	889
Sila, Silivanu .....	890
Sinai, Mlima Sinai .....	891
sio na hatia .....	892
Sulemani .....	893
Sulubisha .....	894
takatifu, utakatifu .....	895
teseka, kuteseka .....	896
tii, mtiifu, utiifu .....	897

timiza .....	898
Tohara .....	899
totii, mkaidi, kutotii .....	900
ufalme .....	901
ufalme wa Israeli .....	902
ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni .....	903
Ufufuo .....	904
upendo .....	905
Uria .....	906
ushuhuda, shuhudia .....	907
ushuru .....	908
utukufu, fahari .....	909
uzao, kutokana na .....	910
Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi .....	911
viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini .....	912
Waasi, uasi. ....	913
wema, uzuri .....	914
Yakobo, Israeli .....	915
Yaweh .....	916
Yeremia .....	917
Yeriko .....	918
Yeroboamu .....	919
Yerusalemu .....	920
Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu .....	921
Yohana (Mbatizaji) .....	922
Yohana (mtume) .....	923
Yoshua .....	924
Yuda Iskariote .....	925
Yuda, ufalme wa Yuda .....	926
Yusufu (Agano Jipya) .....	927
Yusufu (Agano la Kale) .....	928
Zakaria (Agano Jipya) .....	929
<b>Washiriki .....</b>	<b>930</b>
Open Bible Stories Translation Notes Washiriki .....	930
Open Bible Stories Washiriki .....	930
unfoldingWord® Translation Academy Washiriki .....	931
translationWords Washiriki .....	931

# Open Bible Stories Translation Notes

## 1. Uumbaji

01:01



Hivi ndivyo mwanzo wa kila kitu ulivyotokea. Mungu aliumba ulimwengu na vitu vyote katika siku sita. Maana nchi ilikuwa giza na tupu, na hakuna kilichokuwa kimeumbwa. Lakini Roho ya Mungu ilikuwa juu ya maji.

### Mwanzo

Huu ni, "mwanzo wa vitu vyote" kabla ya kuwepo kitu chochote isipokuwa Mungu.

### Aliumba

Hapa inatumika kumaanisha kutengeneza kitu pasipokutumia kitu.

### Ulimwengu

Hii inajumuisha kila kitu ambacho Mungu aliumba duniani na mbinguni, vyote vinavyo onekana na visivyo onekana.

### Dunia

Neno "Dunia" linamaanisha ulimwengu wote ambao watu wanaishi.

## **Giza**

Giza maana yake kutokuwepo na mwanga kabisa, kwasababu Mungu alikuwa bado hajaumba mwanga.

## **Utupu**

Mungu bado hajaumba kitu chochote isipokuwa Dunia iliyofunikwa na maji.

## **Hakuna kilichokuwa kimeumbwa**

Hapakuwepo na uumbaji wa vitu isipokuwa maji iliyofunika dunia.


## **Roho wa Mungu**

Roho wa Mungu, wakati mwingine huitwa Roho Mtakatifu, alikuwepo toka mwanzoni, alitembea juu ya dunia ili aumbe vyote alivyo kusudia.

## **translationWords**

- [Mungu](#)
- [Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.](#)

## 01:02



Ndipo **Mungu akasema**, "**Na iwe** mwanga." Na ikawa hivyo, Mungu aliona kuwa mwanga ni mzuri na akauita mchana, na akatenganisha kutoka giza, akauita usiku. Mungu aliumba mwanga siku ya kwanza ya uumbaji.

### **Mungu akasema**

Mungu aliumba mwanga kwa kutamka neno.

### **Na iwe**

Hii ni amri iliyotokea mara moja kwasababu ilinenwa na Mungu. Inaweza kutafsiriwa kwa njia ya kawaida kuwa ni neno lenye uhakika wa kutokea. Kwa mfano, unaweza kutafsiri kama, "Mungu akasema, 'Pawepo na Mwanga.'"

### **Mwanga**

Huu ni mwanga maalum ambao Mungu aliumba-jua halikuumbwa hadi baadaye.

### **Ikawa nzuri**

Maneno haya yalitumika mara kwa mara katika historia ya uumbaji, na kusesitiza kuwa kila hatua ya uumbaji ilikuwa ikimpendeza Mugu na kutimiza mipango na kusudi lake.

### **Uumbaji**


Neno hili limetumika hapa kumaanisha siku sita ambazo Mungu alivifanya vitu vyote vilivyoko.

## translationWords

- Mungu
- wema, uzuri



## 01:03



**Siku ya pili** ya uumbaji, Mungu alisema na kuumba anga juu ya dunia. Aliumba anga kwa kutenganisha na maji ya juu kutoka maji ya chini.

### **Siku ya pili**

Kazi za Mungu za uumbaji ulifuata utaratibu, makusudi na mpangilio. Vitu alivyoumba kwa kila siku zilijenga na kutegemea vitu vya siku iliyotangulia.

### **Mungu akasema**

Mungu aliumba anga kwa kusema neno.

### **Kuumba**

Mungu aliumba anga pasipokuwepo na kitu.


### **Anga**

Neno hili linamaanisha sehemu yote ya juu ya Dunia, hii ikiwa ni pamoja na hewa tunayovuta na mbingu.

### **translationWords**

- [Mungu](#)

**01:04**



**Siku ya tatu**, Mungu alisema na kutenganisha maji na nchi kavu. Nchi kavu akaiita "**dunia**," na maji akayaita "bahari." Mungu aliona kila kitu alichokiumba ya kuwa ni chema.

## **Siku ya tatu**

Ni siku iliyofuata kwenye mtiririko ambapo Mungu aliandaa Dunia kwa Maisha.

## **Mungu akasema**

Mungu aliumba nchi kavu kwa kuamuru.

## **dunia**

neni hili limetumika kumaanisha sehemu vumbi au udongo, ambayo ardhi iliyo kavu imetegenezwa.

## **Kuumba**

Neni hili linatumika kumaanisha, kutengeneza kitu pasipo kutumia kitu chochote.

## **translationWords**

- Mungu
- wema, uzuri

01:05



Ndipo **Mungu akasema**, "Nchi izee aina zote za miti na mimea." Na ndivyo ilivyotokea. Mungu aliona kila kitu alichokiumba ni chema.

## **Mungu akasema**

Mungu aliumba mimea yote kwa kuamuru.

## **Nchi na izee**

Hii ni amri iliyotokea mara moja kwa sababu Mungu alinena.

## **Aina zote**

Hii ni aina mbali mbali ya mimea na miti.

## **Kuumba**

Neno hili linatumika kumaanisha, kutengeneza kitu pasipo kutumia kitu chochote.

## **Kilikuwa chema**

Neno hili limetumika mara nyingi katika historia ya uumbaji, hii ikisitiza ya kuwa kila hatua ya uumbaji ilimpendeza Mungu na kutimiza lengo na kusudi yake.

## **translationWords**

- [Mungu](#)

- wema, uzuri



**01:06**

Katika **siku ya nne** ya uumbaji, Mungu alisema na kuumba jua, mwezi na nyota. Mungu aliviumba ili kuleta **mwanga** duniani na kuonesha mchana na usiku, nyakati na miaka. Mungu aliona alichokiumba ni chema.

**siku ya nne**

Ni siku ilyofuata kwa mpangilio wa uumbaji wa siku ambayo Mungu aliumba.

**Mungu akasema**

Mungu aliumba jua, mwezi, na nyota kwa kuamuru.

**mwanga**

Ni kitu ambacho kinang'aa angani na kutoa mwanga kwa dunia.

**usiku na mchana, nyakati na miaka**

Mungu aliumba mianga tofauti tofauti ili kutofautisha sehemu ya muda kuanzia ndogo hadi kubwa, na kuziweka zijirudia kwa wakati wote hadi mwisho wa wakati.

**Kuumba**

neni hili linatumika kumaanisha, kutegeneza kitu pasipo kutumia kitu chochote.

**translationWords**

- Mungu

- wema, uzuri

**01:07**

Siku ya tano, Mungu alisema na kuumba vitu vyote viishivyo majini na **ndege wote**. Mungu aliona kuwa **ni vyema**, na akavibariki.

### **siku ya tano**

Mungu aliendelea na mpangilio wake wa uumbaji ambayo alianza siku nne zilizopita.

### **Mungu akasema**

Mungu aliziumba ndege na vitu viishivyo majini kwa kuamuru.

### **Kila kiumbe kinacho ishi na kwenda majini**

Mungu hakuumba tu samaki, bali kila aina ya viumbe vyenye kuishi na kwenda ndani ya maji. Kila mmoja anaishi kwa sababu Mungu alichagua kuumba.

### **ndege wote**

Mungu hakuumba tu aina moja ya ndege, lakini aliumba aina mbalimbali za ndege wazuri ajabu wenye kutofautiana maumbo, ukubwa na rangi.

### **ni vyema**

Neno hili limetumika mara nyingi katika historia ya uumbaji, hii ikisisitiza kuwa kila hatua ya uumbaji ilikwenda kama ilivyokusudiwa kutokana na mpango wa hekima ya Mungu na kusudi lake.

## **aliwabariki**

Mungu aliongea nia yake kuwa wangebarikiwa na kwamba mambo yao yote yaengekwenda vema katika dunia aliowaweka.

## **translationWords**

- Mungu
- wema, uzuri
- Kubariki



**01:08**

Siku ya sita ya uumbaji, Mungu alisema, "Na iwe wanyama wa aina zote katika nchi." Na ilitokea kama Mungu alivyosema. Wengine walikuwa wa shambani, wengine wa kutambaa na wa **porini**. Na ilitokea kama yeye alivyotamka. Na Mungu aliona kwamba ilikuwa **ni vyema**.

**siku ya sita**

Jambo lililofuata, mpangilio katika mfuatano wa siku za matendo ya uumbaji.

**Mungu akasema**

Neno alilo liongea Mungu ndiyo njia ambayo wanyama waliumbwa.

**aina mbambali**

Hii inamaanisha vitu vingi tofauti tofauti, lakini vyenye mpangilio.

**wanyama wa nchi**

Ni aina mbalimbali ya wanyama walioishi juu ya aridhi, mbali na ndege, au wanyama walioishi majini.

**wanyama wa shambani**

Ni aina ya wanyama wanaishi kwa amani na watu juu ya ardhi, kwa jina lingine ni wale wanyama wa kufugwa.

**wanaotambaa juu ya nchi**

Hii inajumisha jamii ya wanyama wote watambaaao kama reptilia na wadudu.

## porini

Ni aina ya wanyama ambao mara nyingi hawaishi kwa amani na watu, hii ni kwa sababu wanaogopa watu, au ni hatari kwao.


## ni vyema

Neno hili limetumika mara nyingi katika historia ya uumbaji, hii ikisisitiza kuwa kila hatua ya uumbaji ilikwenda kama ilivyokusudiwa kutokana na mpango wa hekima ya Mungu na kusudi lake.

## translationWords

- Mungu
- wema, uzuri

01:09



Ndipo Mungu akasema, "**Na tumfanye** mtu **kwa mfano wetu** kuwa **kama sisi**. Watakuwa na **mamlaka** juu ya dunia na wanyama wote."

### **Na tumfanye**

Hii inaonyesha makusudi ya Mungu, kufanya maamuzi ya kumtengeneza mtu kwa namna ya aina yake na kwa makusudi fulani. Inawezekana kutafsiriwakama, "Tutafanya."

### **Sisi...yetu...sisi**

Biblia inafundisha kuwa kuna Mungu mmoja, lakini kwa maneno ya Agano la Kale "Mungu" iko katika neno la wingi. Na Mungu hutumia maneno ya wingi pale anapoongelea juu yake. Wengine wanafahamu hii kama njia maalumu ya kuelezea ukuu wa Mungu, na wengine hufahamu hii kama Mungu Baba akiongea kwa Mwanaye na Roho Mtakatifu, ambao wote ni Mungu.

### **kwa mfano wetu**

Mfano, ni taswira inayowakilisha sura ya kitu halisi au mtu. Watu walifanywa kwa namna ambayo wanaweza kuonyesha na kuwakilisha baadhi ya tabia na sifa za Mungu.

### **kama sisi**

Watu wanazishriki baadhi ya tabia za Mungu ila siyo tabia zote. Maneno haya yanaweza kutafsiriwa kuwa mwanadamu anafanana na Mungu, ila hayuko sawa na Mungu na au jinsi alivyo.

## **mamlaka**

Mungu aliwapa watu uhuru na nguvu ya kutawala, kuongoza na kuamua namna dunia na wanyama watakavyotumika.

## **translationWords**

- [Mungu](#)

**01:10**

Mungu **alichukua vumbi**, akamfanya **mtu**, na akapulizia **uhai** ndani yake. Akamwita Adamu kwa jina lake. Akatengeneza **bustani** ya Edeni akamweka aishi humo, na **aitunze**.

**alichukua vumbi**

Mungu alimfanya mwanadamu kwa kutumia mavumbi kutoka ardhini. Neno hili pengine linaweza kuwa tofauti na neno lililotumika mara kwa mara la neno dunia.

**alimfanya**

Neno hili linaonyesha kuwa Mungu mwenyewe alimtengeneza mwanadamu. Hii ni sawa na mwanadamu anavyo tengeneza kitu kwa mikono waye mwenyewe. Hakikisha neno lingine tofauti na "uumbaji" linatumika, hii ni tofauti na alivyo umba vitu vingine vyote ambavyo alifanya hivyo kwa kuamuru kwa kutamka tu.

**mtu**

Kwa wakati huu aliyetengenezwa ni mwanaume tu, mwanamke alitengenezwa baadaye kwa njia nyingine.

**akampulizia uhai**

Neno hili inaonyesha Nafsi ya Mungu, tendo la ukaribu la kuhamisha uhai wake kwenda kwenye mwili wa Adamu, linganisha na namna mtu anavyotoa hewa.

**uhai**

Katika tendo hili, Mungu alimpulizia mwanadamu uhai wa mwili na roho ndani ya mtu.

## **adamu**

Jina la adamu ni sawa na neno katika agano la kale lenye maana ya "mtu" na ni sawa na neno la udongo/mavumbi ambao alifanywa kwayo.

## **bustani**

Ni eneo la ardhi lililopandwa miti na mimea kwa kusudi-mara nyingi kuzalisha chakula au kufanya sehemu kuwa nzuri.

## **aitunze**

Kuendeleza bustani kwa kulimia, kupalilia, kunyeeshea, kuvuna, kupanda n.k.

## **translationWords**

- Mungu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- Adamu



**01:11**

Katikati ya **bustani**, Mungu alipanda miti miwili muhimu- mti wa uzima na wa **ujuzi wa mema na mabaya**. Mungu alimwambia Adamu anaweza kula aina zote za miti isipokuwa **mti wa ujuzi wa mema na mabaya**. Kama akila tunda la mti huu, atakufa.

**katikati**

Sehemu ya katikati hutia mkazo na umuhimu wa miti hizo miwili.

**bustani**

Ni eneo la ardhi lililopandwa miti n amimea kwa kusudi -mara nyingi kuzalisha chakula au kufanya sehemu kuwa nzuri.

**Mti wa uzima**

Mtu alaye matunda katika mti huu hatakufa kamwe.

**mti wa ujuzi wa mema na mabaya**

Matunda ya mti huu humuwezesha mtu kutambua mema na mabaya.

**ujuzi**

Kuelewa au kufahamu kwa kuwa na uzoefu nao.

## **mema na mabaya**

Mabaya ni kinyume cha mazuri. Kama ambavyo mazuri humaanisha yale mazuri yanayompendeza Mungu, mabaya humaanisha kitu chochote ambacho hakimpendezi Mungu.

## **kufa**

Katika hali hii, atakufa kimwili na kiroho.

## **translationWords**

- Mungu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- wema, uzuri
- baya, ovu, uovu
- Adamu
- kifo, kufa, mfu



**01:12**

Mungu alisema, "Si vyema mtu kuwa **peke yake**." Lakini hakuna hata mnyama mmoja aliyeweza kuwa msaidizi wa Adamu.

**siyo vema**

Hii ni mara ya kwanza katika uumbaji kwa kitu kutokuwa kizuri. Ina maanisha "bado haijawa nzuri" kwa sababu Mungu hajamaliza kazi ya kumuumba mwanadamu.

**peke yake**

Adamu alikuwa mwanadamu mwenyewe, pasipo kuwapo na nafasi ya kuwa na uhusiano na mwanadamu mwingine. Na hakuweza kuwazaa watoto na kuongezeka.

**Msaidizi wa Adamu**

Hapakuwepo yeyote aliyefanana kiasi cha Adamu kuweza kuungana naye kukamilisha shughuli alizopewa na Mungu. Hakuna mnyama awezaye kufanya havyo.

**translationWords**

- Mungu
- wema, uzuri
- Adamu

## 01:13



Ndipo Mungu alimletea Adamu **usingizi mzito**. Akatoa ubavu mmoja kwa Adamu na kutengeneza **mwanamke** na **akamleta kwake**.

### **usingizi mzito**

Huu ulikuwa usingizi usio wa kawaida.

### **akatoa ubavu mmoja na kutengeneza**

Maneno haya, yanaonyesha kitendo cha Mungu kutoa ubavu wa Adamu na kutengeneza mwanamke.

### **mwanamke**

Alikuwa mwanamke wa kwanza, mwanadamu mwenye jinsia ya kike ambaye alikuwa hajatengenezwa hadi wakati ule.

### **akamleta kwake**

Ni Mungu mwenyewe ndiye aliyewatambulisha. Alimleta Mwanamke kwa Adamu, kama kutoa zawadi nzuri kwake.

### **translationWords**

- Mungu
- Adamu

## 01:14



Adamu alipomwona, alisema, "Angalau! Huyu ni kama mimi! Ataitwa 'mwanamke' maana ametoka kwa mwanaume." Kwa maana mwanaume atamwacha baba na mama yake watakuwa pamoja na mkewe.

### **Hatimaye!**

Adamu alisema hivyo kuonyesha kuwa alikuwa akisubiri kitu kama mwanamke.

### **Kama mimi**

Mwanamke alikuwa ni mwanadamu kama Adamu, pamoja na kwamba kulikuwepo na tofauti za umuhimu kati yao.

### **Mwanamke**

Neno hili linamaanisha muundo wa kike ambayo siyo mwanaume.

### **kutengenezwa kutokana na mwanaume**

Mwanamke alitengenezwa kutokana na mwili wa Adamu.

### **mwanaume atamuacha**

Hii ilitamkwa kwa wakati uliopo ili kuonyesha mwenendo utakao kuwepo katika siku za baadaye. Adamu alikuwa hana mama wala baba, lakini wanaume wengine wote watakuwa nao.

## **watakuwa mmoja**

Mme na mke watashirikiana katika mahusiano ya karibu na kipekee, katika umoja na kujitoa kwa kila mmoja wao kwa mahusiano yanayozidi mahusiano na watu wengine wote.

## **translationWords**

- [Adamu](#)



**01:15**

Mungu aliumba mwanamke na mwanaume kwa mfano wake. Akawabariki akasema, "zaeni watoto na wajukuu mkajijaze dunia." Mungu aliona kila kitu alichokifanya ni **chema sana**, na alifurahishwa sana na kila kitu. Hii ilitokea katika siku ya sita ya uumbaji wake.

**Mungu alimtengeneza**

Mungu alimtengeneza mwanaume na mwanamke kwa namna ya kipekee.

**kwa sura yake**

Taswira au sura ni kiwakilishi halisi cha kitu au mtu. Mungu aliwatengeneza watu ili kuonyena na kuwakilisha baadhi ya tabia na sifa za Mungu, lakini siyo kuwa sawa na yeye.

**chema sana**

Hii inaonyesha zaidi ya maneno yaliyotumika hapo nyuma ya kama ni chema, vyema. Chema sana inamaanisha kwa uumbaji wote na siyo to kwa mwanaume na mwanamke. Kila kitu ilikuwa sawasawa na kama Mungu alivyokitaka kiwe.

**Uumbaji**

Siku sita ambazo Mungu alitumia kuumba kila kitu.

**translationWords**

- Mungu
- Kubariki
- wema, uzuri

**01:16**

Siku ya saba ilipofika, Mungu alikuwa **amemaliza kazi yake**. Hivyo Mungu alipumzika katika kila alichokifanya. **Aliibariki siku ya saba akaifanya takatifu** kwa sababu katika siku hii alipumzika. Hivyo ndivyo Mungu alivyounda **ulimwengu** na kila kitu ndani yake.

**siku ya saba**

Ni siku iliyofuata baada ya siku ya sita kuisha.

**amemaliza kazi yake**

Mungu alimaliza kazi ya uumbaji ila bado anafanya kazi zingine.

**Mungu akapumzika**

Mungu "alipumzika" kwa sababu kazi ya uumbaji ulikamilika. Mungu hakuchoka, au si kwamba ameshindwa kuendelea.

**Aliibariki siku ya saba**

Mungu alikuwa na mpango nzuri maalum kwa siku ya saba, na kwa kila siku ya saba baadaye.

**akaifanya takatifu**

Hii ina maana, "Mungu alitenga" siku hii kama siku maalum. Haitatumika kama siku nyingine za wiki.

## ulimwengu

Hii inajumuisha kila kitu alihoumba Mungu hapa duniani na mbinguni, yale yanayo onekana na yasiyo onekana.

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 1-2

## translationWords

- Mungu
- Kubariki
- takatifu, utakatifu

## 2. Dhambi Inaingia Ulimwenguni

02:01



Adamu na mke wake waliishi kwa furaha katika **bustani** nzuri ambayo Mungu aliwaandalia. Hawa wawili hawakuvaa nguo, lakini hawakuona **haya** kwa sababu hakukuwa na dhambi duniani. Mara nyingi walitembea katika bustani na **kuongea na Mungu**.

### **bustani**

Ni sehemu maalum yenye kila aina ya miti na mimea ambayo Mungu aliandaa kwa Adamu na Hawa kufurahia na kula mahali hapo.

### **kuongea na Mungu**

Neno "kuongea" ni kama lile la kuongea na mtu. Mungu huenda alivaa sura ya mwanadamu ili aweze kuongea na mwanaume na mwanamke kwani kifunguu hii kilionyesha kuwa waliongea uso kwa uso.

### **haya**

Ni hisia inayokuja kwa kujua kuwa tumefanya dhambi au tumepungukiwa kwa namna fulani.

### **translationWords**

- Adamu
- Mungu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi



**02:02**

Lakini kulikuwa na Nyoka **mwerevu** katika bustani. Alimuuliza mwanamke, "Je, ni kweli kwamba Mungu aliwaambia msile **matunda ya mti wowote** katika bustani?"

**mwerevu**

Mjanja na mwerevu, mwenye nia ya kudanganya.

**nyoka**

Ni mnyama wa ardhini mrefu, asiye na miguu anayetembea kwa kutambaa kwa tumbo lake. Hataivyo katika historia hii ilidhihirika kwamba nyoka ni Shetani, hataivyo kwenye kipengele hii haitajulikana hivyo.

**Je, ni kweli Mungu alikuambia**

Nyoka alimuuliza mwanamke kama ni kweli Mungu aliwaambia wasile katika mti wowote ndani ya bustani. Lakini alikuwa akijifanya hajui Mungu alisema nini kwa sababu alitaka kujenga shaka kwenye ufahamu wa mwanamke. Alitaka yeye aweke ulizo au shaka juu ya wema wa Mungu.

**matunda ya mti wowote**

Aina zote za matunda kutoka kwa kila aina ya mti ndani ya bustani.

**translationWords**

- [Mungu](#)

**02:03**

Mwanamke akajibu, "Mungu alisema twaweza kula **matunda** ya miti yote ya bustani isipokuwa matunda ya **mti wa ujuzi wa mema na mabaya**." Mungu alisema, "mukila au kugusa matunda ya mti huo, **mtakufa**."

**matunda**

Hatufahamu ilikuwa ni aina gani ya matunda. Tunafahamu tu kwamba ni tunda lililokuwa kwenye mti. Kwa hapa yafaa kutumia neno la jumla la tunda na siyo tunda fulani maalum.

**mti wa ujuzi wa mema na mabaya**

Mwanamke alijua kwa hakika kuwa hawaruhusiwi kula matunda kutoka katika mti huo ambao utawafanya wajue mema na mabaya.

**mtakufa**

Tumia neno lako la kawaida ya kufa, ni hali ya kufikia uko kwa maisha haya ya kimwili. usikwepe neno hili kwa sababu wazo la kifo linatisha.

**translationWords**

- Mungu
- wema, uzuri
- baya, ovu, uovu
- kifo, kufa, mfu

02:04



Yule Nyoka akamjibu mwanamke, "Hiyo sio kweli! Hamwezi kufa. Mungu anajua kwamba pindi mtakapokula mtakuwa **kama Mungu** kwa **kujua mema na mabaya** kama ajuavyo."

### **kama Mungu**

Mwanaume na mwanamke tayari wamefanywa kwa namna na sura ya Mungu. Nyoka anashauri kuwa mwanamke atakuwa kama Mungu zaidi kama akijua mabaya. Hata hivyo Mungu hakukusudia yeye kuwa na ufahamu huu.

### **kujua mema na mabaya**

Kujua kwa njia ya uzoefu mambo yaliyo mema na mambo yaliyo mabaya, au kuwa na uwezo wa kujua kuwa jambo ni jema au baya.

### **translationWords**

- kweli, ukweli, kuwa kweli
- kifo, kufa, mfu
- Mungu
- wema, uzuri
- baya, ovu, uovu



02:05



Mwanamke aliona kuwa matunda yalikuwa mazuri na yalionekana kuwa matamu. Pia alitaka kuwa na **hekima**, hivyo alichuma tunda akala. Kisha akampa mume wake **aliyekuwa pamoja naye**, naye pia akala.

## hekima

Mwanamke alitamani kuwa na uelewa na ufahamu kama nyoka anavyoonekana kuwa nayo, na kama aliyonayo Mungu.

## aliyekuwa pamoja naye

Hii ni habari muhimu kwani inaonyesha kuwa mwanaume alikuwepo wakati hawa anafanya maamuzi ya kula tunda.

## translationWords

- [Busara, hekima](#)

**02:06**

Mara macho yao yakafunguliwa, na **wakagundua kwamba walikuwa uchi**. Wakajaribu **kuficha miili yao** kwa kushona majani ili kujifanyia nguo.

### **mara macho yao yakafunguliwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa "waliona vitu kwa namna ya tofauti." Inaonyesha kuwa walijua kitu kwa mara ya kwanza. Katika lugha yenu unaweza kuwa na namna vyingine ya kuelezea hali hii.

### **wakagundua kwamba walikuwa uchi**

Baada ya Mwanaume na Mwanamke kutokumtii Mungu, waliona aibu kwa kuwa uchi. Ndiyo maana walijaribu kujifunika miili yao kwa kuvaa majani ya miti.

### **kuficha miili yao**

Mwanaume na mwanamke walijaribu kujifunika kwa kutumia majani ili kujificha mbele za Mungu.

02:07



Ndipo Adamu na mke wake wakasikia sauti ya **Mungu akitembea** katika bustani. Wote wakajificha. Mungu akamwita mwanaume, "**Uko wapi?**" Adamu akajibu, "Nimekusikia ukitembea katika bustani, nikaogopa kwa kuwa ni uchi, hivyo nikajificha."

### Mungu akitembea

Inaonekana kuwa Mungu alikuja mara kwa mara kuwatembelea Mwanaume na Mwanamke bustanini. Hatufahamu hili lilionekanaje. Kama inawezekana ni vizuri kutumia neno linalotumika kuelezea mtu anapotembea.

### Uko wapi?

Mungu tayari alijua majibu ya swali hilo. Kusudi la swali hili ni kumfanya mwanume na mwanamke waeleze kwanini wanajificha.

### translationWords

- Mungu
- Adamu



02:08



Kisha Mungu akamuuliza, "Ni nani aliyekuambia kuwa u uchi? Je, umekula tunda nililokuambia usile?" Mwanaume akajibu, "wewe ulinipa huyu mwanamke, naye **amenipa tunda.**" Ndipo Mungu akamuuliza mwanamke, "Umefanya nini?" Mwanamke akajibu, "**Nyoka alinidanganya.**"

### Nani aliyekuambia kuwa uko uchi?

Au "Ulijuaje kuwa uko uchi?" Mungu tayari alijua majibu ya maswali yote. Kwa kuuliza maswali na kufuatilia alikuwa anampa Adamu nafasi ya kukiri dhambi yake ya kutokutii. Kuwa uchi siyo dhambi kwani Mungu aliwaumba hivyo. Ufahamu wao juu ya kuwa uchi ndiyo tatizo. Aibu yao ilionyesha kuwa walikuwa wametenda dhambi.

### amenipa tunda

Mwanaume alimlaumu mwanake badala ya kutubu kwa kutokutii na kuwajibika kwa kutokumtii Mungu.

### ulifanya nini?

Au "Kwanini umefanya haya?" Mungu tayari alijua majibu ya swali hilo. Kwa kuuliza swali hili, alikuwa akimpa nafasi mwanamke akubali kosa lake. Pia Mungu alimaanisha kuwa asingefanya kile alichokifanya.

### Nyoka alinidanganya

Nyoka alinidanganya au alinipotisha. Nyoka alimuambia uongo. Usitumie neno linaloonyesha kama vile alimlogo au kuwa alimpa kitu kilichompofusha macho au kumfanya akili yake achanganyikiwe na kuamua bila yeye kujua. Mwanamke alimlaumu nyoka badala ya kutubu kosa lake la kutotii na kukubali kuwajibika kwa kutomtii Mungu.

### translationWords

- Mungu



02:09



Mungu akamwambia Nyoka, "**Umelaaniwa!** kwa tumbo lako utaenda na utakula mavumbi. Wewe na mwanamke **mtakuwa maadui**, watoto wake na watoto wako watakuwa maadui pia. Uzao wa mwanamke **utakuponda kichwa**, nawe **utamgonga kisigino** chake."

### **Umelaaniwa**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "Nimekulaani wewe" au "Tatizo baya litakujia." Usitumie neno lenye kuashiria uchawi.

### **mtakuwa maadui**

Mwanamke atamchukia nyoka na nyoka atamchukia mwanamke. Na uzao wa mwanamke utachukia uzao wa nyoka na uzao wa nyoka utachukia uzao wa mwanamke.

### **uzao wa mwanamke**

Inamaanisha moja wa uzao wake.

### **utakuponda kichwa**

Uzao wa mwanamke utaharibu (kuuwa) uzao wa nyoka.

### **utamgonga kisigino**

Uzao wa nyoka utamjeruhi uzao wa mwanamke kwenye kisigino.

## translationWords

- Mungu
- Laana, kulaaniwa
- uzao, kutokana na

## 02:10



Mungu akamwambia mwanamke, "Nitaongeza uchungu wakati wa kuzaa kwako. Hamu yako itakuwa juu ya mume wako, naye atakutawala."

### **nitaongeza uchungu wakati wa kuzaa kwako**

Huenda lugha nyingine zinahitaji kueleea hii kama kitenzi. Unaweza kusema, "Nitakufanya usikie uchungu mkubwa wakati wa kujifungua."

### **translationWords**

- Mungu

**02:11**

Mungu akamwambia mwanaume, "Umemsikiliza mke wako na hukunitii mimi. Sasa **ardhi imelaaniwa**, na utafanya kazi kwa bidii ili upate chakula. Na kisha **utakufa**, na mwili wako **utarudi katika uchafu**." Mwanaume akamwita mke wake jina Eva, akimaanisha "Mtoa uhai," kwakuwa atafanyika mama wa watu wote. Na Mungu akawavalisha Adamu na Eva mavazi ya ngozi ya Wanyama.

**ardhi imelaaniwa**

Kama adhabu kwa kutokutii kwa Adamu, ardhi haitatoa tena matunda. Itampasa Adamu kufanya kazi kwa nguvu nyingi ili apate chakula ya kula.

**utakufa**

Mwisho wa adhabu yao ni kifo. Kifo cha kiroho ni utengano wa sisi na Mungu. Kifo cha kimwili ni utengano na miili yetu.

**utarudi katika uchafu**

Mungu alimtengeneza Adamu katika mavumbi au uchafu na kumpa maisha. Kwa sababu ya dhambi, maisha yake yatachukuliwa kutoka kwake na mwili wake utaoza na kurudia kwenye uchafu tena.

**Hawa, yenye kumaanisha "mtoa maisha"**

Mungu alimpa uhai Adamu na Hawa, na uhai huo walipewa vizazi vyote kwa njia ya kuzaliwa (kuzaliwa kwa watoto).

**Mama wawatu wote**

Hii inamaana kuwa atakuwa mama wa kwanza kwa vizazi vyote vya watu. Lugha nyingine zinasema "atakuwa bibi" wa watu wote e

## translationWords

- Mungu
- totii, mkaidi, kutotii
- Laana, kulaaniwa
- kifo, kufa, mfu
- Hawa
- Adamu



**02:12**

Kisha Mungu akasema, "Kwakuwa sasa wanadamu wamekuwa **kama sisi kwa kujua mema na mabaya**, wasiruhusiwe kula **tunda** la **mti wa uzima** wakaishi milele." Hivyo Mungu aliwafukuza Adamu na Eva kutoka katika bustani nzuri ya Edeni. Mungu akaweka Malaika wenye nguvu kwenye malango ya bustani ili kuzuia mtu yeyote asile matunda ya mti wa uzima.

**kama sisi kwa kujua mema na mabaya**

Maneno haya, yanaonyesha namna mpya ambayo Adamu na Hawa watakuwa kama Mungu. Kwasababu wamefanya dhambi, wanajua mabaya na wanaweza kufanya. Unaweza kusema "kwasababu sasa wanajua mema na mabaya."

**tunda**

Ni aina ya tunda ambayo haukujulishwa au kuelezwa, kwa hiyo yafaa itafsiriwe kama tunda.

**mti wa uzima**

Huu ni mti halisi wenye matunda.

Simulizi ya Biblia Kutoka: Mwanzo 3

**translationWords**

- Mungu
- wema, uzuri
- baya, ovu, uovu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- Adamu
- Hawa

- [Malaika, Malaika mkuu](#)



### 3. Gharika

03:01



Baada ya muda mrefu, watu wengi waliishi katika ulimwengu. Nao walikuwa waovu na wenye vurugu. Hali ilikuwa mbaya sana hata Mungu akaaamua kuwaaangamiza kwa mafuriko.

#### **baada ya muda mrefu**

Simulizi hii ilitokea baada ya vizazi vingi (mamia ya miaka) baada ya uumbaji.

#### **walikuwa waovu na katili**

Ni rahisi kusema, "walikuwa waovu na walifanya mambo ya ukatili."

#### **ikawa mbaya**

Inaweza kueleweka kwa kusema "Watu walikuwa wakiishi kwa njia ya uovu na ubaya ambazo hazikumpendeza Mungu."

#### **Mungu aliamua kuwaangamiza**


Hii haimaanishi kuwa dunia itaharibiwa kabisa. Ila Mungu alikusudia kuwaangamiza watu wote waliomuasi Yeye na walio sababisha maovu na ukatili. Mafuriko pia itauwa wanyama na ndege wote katika nchi.

## **Mafuriko makubwa**

Maji mengi ambayo yengeifunika dunia, hata sehemu ambazo mara nyingi ardhi i kavu, na hata kufunika vilele vya milima mirefu.

## **translationWords**

- [Mungu](#)

**03:02**

Lakini Nuhu alipata neema machoni pa Mungu. Kwa sababu alikuwa ni mwenye haki miongoni mwa waovu. Mungu alimjulisha Nuhu kuhusu mpango wake wa kutuma mafuriko kwa wanadamu. Akamwambia Nuhu atengeneze Safina.

**akapata kibali**

Mungu alipendezwa na Nuhu, kwasababu alimcha na kumtii Mungu. Japokuwa siyo kwamba Nuhu hakuwa na dhambi, Mungu alimhurumia na akaweka mpango wa kumuokoa yeye na familia yake kutoka kwenye mafuriko makubwa. Hakikisha haitaonekana kana kwamba Nuhu alipata bahati, au kwamba ilitokea tu akaponyoka. Bali, ni mpango na chaguo la Mungu.

**Mafuriko**

Maji mengi yenye kuleta maafa.

**mpango wa kutuma**

Mungu alipanga kuleta mafuriko yatakayo funika dunia mzima kwa kuruhusu mvua nyingi. Hii ni kwamba alipanga kusababisha mafuriko ya mvua nyingi.

**translationWords**

- Nuhu
- Mungu
- Adili, uadilifu

**03:03**

Mungu alimwambia Nuhu atengeneze Safina yenye urefu wa meta 140, upana wa meta 23, na urefu kwenda juu meta 13.5. Nuhu alijenga Safina yenye ghorofa tatu, vyumba vingi, madirisha pamoja na paa kwa kutumia mbao. Nayo Safina ilikuwwa na uwezo wa kumtunza Nuhu, familia yake na kila aina ya wanyama kwa yale mafuriko.

**safina**

Safina ni aina ya mashua ambayo ni kubwa kiasi kwamba inaweza kubeba watu wanane, na wanyama wawili wawili kwa kila kundi la wanyama, pamoja na malisho yao kwa kadri ya muda wa mwaka mmoja.

**translationWords**

- Mungu
- Nuhu



**03:04**

Nuhu alimtii Mungu. Yeye pamoja na watoto wake watatu wa kiume walijenga Safina kama Mungu alivyo waagiza. Na kwa vile Safina ilivyokuwa kubwa, ilichukua miaka mingi kukamilika. Vile vile Nuhu aliwapa watu angalizo juu ya mafuriko yajayo, akawasihi **wamrudie Mungu**, lakini hawakumwamini.

**Nuhu aliwaonya**

Nuhu aliwaambia watu wote kuwa Mungu ataiangamiza dunia kwa sababu ya dhambi.

**wamrudie Mungu**

Hii ilimaanisha kuacha kufanya dhambi na kuanza kumtii Mungu.

**translationWords**


- Nuhu
- tii, mtiifu, utiifu
- Mungu

**03:05**



Pia Mungu alimwamuru Nuhu na familia yake, akusanye chakula cha kutosha kwa ajili yao na wanyama. Na kila kitu kilipo kamilika, Mungu akamwambia Nuhu na mke wake, watoto wake watatu wa kiume, na wake zao waingie ndani ya Safina. Jumla yao ilikuwa watu wanane.

03:06



**Mungu akatuma** kwa Nuhu wanyama na ndege wawili wawili dume na jike, waingie katika Safina ili waokolewe na gharika. Mungu alituma wanyama wengine saba saba madume na saba majike wa kila aina ya wanyama, watakao tumika kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa. Baada ya wote kuingia ndani ya Safina, Mungu mwenyewe akafunga mlango.

### **Mungu akatuma**

Muhu alikuwa hana haja ya kuwatafuat wanyama bali Mungu aliwatuma kwake.

### **waliotumika kwa sadaka ya kuteketezwa**

Kwa lugha nyingie, inaweza kuwa rahisi kusema kuwa "wanyama wale waliokubalika na Mungu kwa sadaka ya kuteketezwa." Mungu aliamua watu wamtotee wanyama kama sadaka ya kuteketezwa, hata hivyo aliwaruhusu tu Kumtolea aina fulani ya wanyama.

### **Mungu mwenyewe alifunga mlango**

Hii inatia mkazo kuwa ni Mungu mwenyewe ndiye aliyefunga mlango.

### **translationWords**

- [Mungu](#)
- [Nuhu](#)
- [dhabihu, sadaka](#)



**03:07**



Mvua ikaanza kunyesha, na kunyesha, na kunyesha. Ilinyesha kwa siku arobaini usiku na mchana bila kukata! Maji yalizidi kuongezeka na kuijaza dunia yote. Kila kitu katika dunia kilifunikwa na maji, hadi milima mirefu zaidi ilifunikwa.

### **mvua ikaanza kunyesha, na kunyesha , na kunyesha**

Hii inasisitiza kuwa kulikuwa na mvua isyokuwa ya kawaida, mvua kubwa sana. Lugha nyingine huenda zina namna ya kutia mkazo.

### **maji pia yalitokea ardhini**

Hii iliashiria kulikuwa na maji mengi yaliyotokea ardhini.


### **Dunia yote ikafunikwa**

Hii ilimaanisha dunia yote ilifunikwa na maji.

**03:08**



Kila kitu kilichoishi katika aridhi kilikufa, isipokuwa watu na wanyama waliokuwa katika Safina ndiyo walio salia. Safina ilielea juu ya maji na vyote vilivyokuwa ndani ya safina havikuzama.

**03:09**

Baada ya mvua kukata, Safina ilielea kwenye maji kwa muda wa miezi mitano, na baadaye maji yalianza kupungua. Hatimae siku moja Safina ikatulia juu ya mlima, wakati huo maji yalikuwa bado yameenea duniani kote. Na miezi mitatu baadaye, vilele vya milima vilianza kuonekana.

### **Mvua kukatika**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "mvua iliacha kunyesha."

### **Safina ikatua**

Kulikuwepo na maji mengi kutokana na mvua iliyofunika hata milima. Safina ilielea mlimani na maji yalipoanza kwenda chini, safina ilienda chini na maji na safina ikatulia kwenye mlima.

### **miezi mitatu baadaye**

Maji yaliendelea kupungua kwa muda wa miezi mitatu baadaye.

### **milima ilionekana**

Njia nyingine za kutafsiri hii ni "vilionekana" "vikatokeza", vilikuwa vimeonekana. "Inaweza ikawa rahisi kusema, "Baada ya miezi mitatu, maji yalishuka kiasi kwamba Nuhu na familia yake walianza kuona vilele vya milima.



## 03:10



Baada ya siku arobaini zaidi, Nuhu alimtuma Kunguru kwenda kutazama kama maji yamekauka. Lakini Kunguru alipopaa hakupata mahali pa kutua, kwani maji yalikuwa bado yameijaza nchi.

### **kunguru**

Aina ya ndege mweusi anayeruka na kula aina ya majani na wanyama, ikiwa ni pamoja na nyama zilizoza za wanyama.

### **translationWords**

- [Nuhu](#)

**03:11**

Baadaye Nuhu alimtuma **njiwa**. Lakini Njiwa pia hakupata mahali pa nchi kavu, hivyo alirudi kwa Nuhu. Wiki moja baadaye Nuhu alituma tena Njiwa, Safari hii njiwa alirudi na **tawi la mzabibu** mdomoni mwake! Hii ilionyesha kuwa maji yameanza kukauka, na miti imeanza kukua tena.

**njiwa**

Ndege mdogo mweupe na kijivu mwenye kuruka na kula mbegu na matunda.

**tawi la mzabibu**

Mti wa mzabibu una mafuta ambayo watu hutumia kupikia na kujipaka. Kama lugha yako haina neno la "tawi la mzabibu" unaweza kutafsiri kama ni tawi linalotokana na mti uitwao "mzabibu" au tawi kutoka kwa "mti wenye mafuta."


**maji yalianza kukauka/kwenda chini**

Inaweza ikawa rahisi kwa lugha yako kusema, maji yaliendelea kuisha, au "kiwango cha maji kilipungua au kilishuka."

**translationWords**

- [Nuhu](#)

## 03:12



Nuhu **alisubiri wiki moja zaidi** akamtuma Njiwa kwa mara ya tatu. Wakati huu, Njiwa alipata mahali pa kutua na hakurudi kwa Nuhu. Maji yalikuwa yamekauka!

### **alisubiri wiki moja zaidi**

Unaweza kusema, alisubiri suku zaidi, Neno "kusubiri" inaonyesha kuwa Nuhu alisubiri ili maji yakauke kabla ya kumtuma njiwa tena.

### **translationWords**

- [Nuhu](#)



**03:13**

**Miezi miwili baadaye**, Mungu alisema na Nuhu, "wewe na familia yako na wanyama wote sasa mwaweza kutoka nje ya Safina. Mzae watoto na wajukuu muijaze nchi." Ndipo Nuhu na familia yake wakatoka nje.

**Miezi miwili baadaye**

Hii ina maana miezi miwili baada ya Nuhu kumuachia njiwa kutoka katika safina. Huenda ni muhimu kusema hii kwa lugha rahisi kama haijaleweka.

**Muwe na watoto wengi**

Hakikisha inaeleweka kuwa ni amri na shauku ya Mungu, unaweza kusema "Ni lazima kuwa na watoto wengi" au "Nataka ninyi muwe na watoto wengi."

**Muijaze nchi**

Kama haijaleweka, unaweza ukasema "muijaze dunia na watu" au "ili pawepo na watu wengi waishio duniani."

**translationWords**

- Mungu
- Nuhu



**03:14**

Baada ya Nuhu kutoka nje ya Safina, Nuhu alimjengea Mungu madhabahu na akamtolea sadaka ya aina ya wanyama waliopaswa kutolewa sadaka. **Mungu alifurahishwa** na sadaka hiyo akambariki Nuhu pamoja na familia yake.

**aina ya wanyama waliopaswa kutolewa dhabihu**


Njia nyingine ya kusema hii ni, "wanyama ambao watu hutumia kumtolea Mungu dhabihu ya kuteketezwa."

**Mungu alifurahishwa**

Mungu alipendezwa na Nuhu kwa kumtolea dhabihu ya kuteketezwa kwa wanyama hao.

**translationWords**

- Nuhu
- Madhabahu
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- Kubariki

**03:15**

Mungu aliahidi, "hata laani tena ardhi kwa sababu ya maovu wayafanyayo wanadamu, au kuharibu dunia kwa mafuriko. Japokuwa **watu ni wenye dhambi tangu utotoni mwao.**"

**kamwe tena**

Hii inamaana "hatarudia tena" au "hatarudia tena wakati wowote" mifano: "Sitalaani tena ardhi" au sitalaani tena ardhi kwa wakati wowote au kwa hakika sitalaani tena ardhi.

**kulaani ardhi**

Ardhi na viumbe vingine vyote hutaabika kwa sababu ya dhambi za wanadamu.

**Dunia**


Hii inamaanisha ardhi na viumbe vingine vyote vinavyoishi duniani.

**watu ni wenye dhambi tangu utotoni mwao**

Njia nyingine ya kusema hii ni, "watu hufanya matendo maovu kwa maisha yao yote."

**translationWords**

- Mungu
- Ahadi
- Laana, kulaaniwa
- baya, ovu, uovu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**03:16**

Mungu akatengeneza **upinde wa mvua** kama **ishara ya ahadi yake**. Kila upinde wa mvua unapotokea angani, Mungu akumbuke ahadi yake vilevile watu wake wakumbuke ahadi ya Mungu.

**upinde wa mvua**

Huu ni upinde wa mwanga wenye rangi ambazo mara nyingi hutokea angani pale panapo kuwepo na mvua ya ngurumo.

**ishara**

Ishara ni kama kitu au tukio ambayo ina maana fulani au inayoashiria kitu ambacho ni cha kweli au kitatokea.

**ishara ya ahadi yake**

Kwa lugha nyingine inaweza ikawa vizuri kusema "kuonyesha kuwa ameahidi."

**kila wakati**

Hakikisha inafahamika ya kuwa, ni kila wakati upinde wa mvua inaponekana na kuendelea. Huenda ni Muhimu kuongeza, "Kuanzia sasa na kila wakati."

**alicho ahidi**

Hii inarejea, ile hali ambayo Mungu aliahidi kutoangamiza dunia tena kwa kutumia mafuriko.

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 6-8

## translationWords

- Mungu
- Ahadi



## 4. Agano la Mungu na Abrahamu

04:01



**Miaka mingi baada ya gharika**, watu wakaongezeka sana juu ya nchi. Wakati huo wakiwa wanaongea lugha moja. Badala ya kujaza nchi kama Mungu alivyoamuru, walikusanyika sehemu moja wakajenga **mji**.

### **Miaka mingi baada ya gharika**

Vizazi vingi vimepita baada ya gharika

### **tena, watu wengi**

Familia ya Noah iliongezeka na kuwa na watu wengi wa kuujaza mji

### **lugha inayofanana**

Hii inamaanisha kulikuwa na lugha moja hivyo watu walielewana

### **mji**

Ni vyema kutumia neno la jumla linaloamaanisha mji kwakuwa kifungu hakitaji jina maalumu.

### **translationWords**

- [Mungu](#)



**04:02**

Walikuwa na majivuno na hawakujali kama Mungu alivyosema. Wakajenga mji wakaweka mnara mrefu uliokaribia kufika mbinguni. Mungu akaona watu hawa wakiendelea kufanya uovu pamoja, watafanya matendo ya dhambi zaidi.

**mnara mrefu kuifikia mbingu**

mnara huo ulikuwa mrefu kiasi kwamba ncha yake ilifika angani.

**Mbingu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama "anga."

**translationWords**

- Kiburi
- Mungu
- mbingu, anga, mbinguni
- baya, ovu, uovu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

## 04:03



Mungu akagawanya lugha zao zikatokea lugha nyingi. Wakatawanyika juu ya dunia yote. Na jina la ule mji ukaitwa **Babeli** kwa kuwa" hawakuelewana."

### **alibadili lugha yao**

Kwa ghafla Mungu aliwapa lugha tofauti tofauti na hivyo hawakuweza kuelewana tena.

### **lugha nyingi mbalimbali**

Badala ya kundi moja kubwa kuzungumza lugha moja, sasa waligawaanyika katika makundi mengi madogo madogo na kila kundi likawa na lugha yake.

### **aliwatawanya watu**

Wakati Mungu alipobadilisha lugha zao, alisababisha watu hao kutawanyika na kila kundi lilienda sehemu yake.

### **Babeli**

Hatujui kwa hakika mahali ambapo mji huu ulikuwa, zaidi ya kwamba ulikuwa mahali fulani huko Mashariki ya kati.

### **alichanganya**

Hii inaelezea jinsi ambavyo watu walichanganywa wakati ambapo hawakuweza kuelewana baada ya Mungu kubadili lugha yao.

## translationWords

- Mungu

**04:04**

Miaka mamia baadaye Mungu aliongea na mtu aitwaye Abrahamu. "Toka katika nchi yako na jamaa zako uende mpaka nchi nitakayokuonesha. Nitakubariki na kukufanya taifa kubwa nitalikuza jina lako. Nitawabariki wakubarikio, Nitawalaani wakulaanio. Na katika wewe jamaa zote za dunia zitabarikiwa ."

**Mamia ya miaka baadaye**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "vizazi vingi baada ya watu kugawanyika katika lugha mbalimbali."

**Ondoka katika nchi yako**

Hii inaelezea eneo ambalo Abram ualiziwa na kuishi.

**na familia yako**

Mungu alikuwa anamwita Abram na familia yake tu, na kuwaacha ndugu zake wengine.


**kukufanya kuwa taifa kubwa**

Mungu angemfanya Abram kuwa na watoto wengi, na wangukuwa taifa kubwa na la muhimu.

**translationWords**

- Mungu
- Abrahamu, Abram
- Kubariki
- Laana, kulaaniwa



**04:05**

Hivyo, Abrahamu akamtii Mungu. Akamchukua Sarai mkewe, na watumishi wake na mali zote alizokuwa nazo, akaenda mpaka nchi ile Mungu aliyomuonesha **nchi ya Kanaani**.

**alichukua**

lugha zingine zinaweza kusema "alileta"

**Mungu alimuonesha**

kwa namna fulani Mungu alimudokezea Abram u kuhusu mahali alipopaswa kwenda. Kifungu hiki hakielezi jinsi ambavyo Mungu alimuonesha.

**nchi ya Kanaani**

jina la nchi hiyo iliitwa "Kanaani."

**translationWords**

- Abrahamu, Abram
- tii, mtiifu, utiifu
- Mungu
- Sara, Sarai
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Kanaani, Mkanaani



## 04:06



Abrahamu alipofika Kanaani, Mungu akamwambia, "Tazama nitakupa nchi hii yote unayoiona wewe na uzao wako kuwa urithi wako." Kisha Abrahamu akaishi katika nchi ile.

### **ardhi yote utakayoiona**

Kama Abramumu alikuwa amesimama juu mlimani, angeweza kuona eneo kubwa.

### **kama urithi**


Mungu aliahidi kumpa Abramumu na uzao wake ardhi kama vile baba huwa watoto wake ardhi mali.

### **Kisha Abramumu akakaa katika nchi**

Abramumu aliishi mahali pale pamoja na wote alioenda nao.

### **translationWords**

- Abrahamu, Abramumu
- Kanaani, Mkanaani
- Mungu
- uzao, kutokana na
- rithi, urithi, mrithi

**04:07**

Siku moja Abrahamu akakutana na **Melkizedeki**, kuhani mkuu wa **Mungu aliye juu**. Melkizedeki akambariki Abrahamu akasema, "Mungu Mkuu mmiliki wa mbingu na dunia ambariki Abrahamu." Abrahamu akamtolea Melkizedeki fungu la kumi toka katika mali alizonazo.

**Melkizedeki**

Melkizedeki alikuwa ni mtu mwenye mamlaka ya dini katika Kanaani ambaye alipokea sadaka na kuziwasilisha kwa Mungu.

**Mungu aliye juu**

Watu wa Kanaani waliabudu miungu mingi ya uongo. Jina "Mungu aliye juu" lilimtambulisha Mungu wa kweli ambaye Melkizedeki alimwabudu.

**translationWords**

- Abrahamu, Abram
- Kuhani, ukuhani
- Mungu
- Kubariki
- mbingu, anga, mbinguni

**04:08**

Abrahamu na Sarai waliishi miaka mingi bila kupata mtoto. Mungu Akasema na Abrahamu na kumuahidi tena kuwa atampa mtoto wa kiume na uzao mwingi kama nyota za angani. Abrahamu akaamini ahadi ya Mungu. Mungu akamwita Abrahamu mwenye haki kwa kuwa aliamini ahadi yake.

**Miaka mingi**

Miaka mingi ilipita tangu Mungu alipomuahidi Abramu mtoto.

**kama nyota angani**

msemu huu unamaanisha kuwa uzao wa Abramu utakuwa na watu wengi kiasi kwamba hakuna atakayeweza kuwahesabu.

**translationWords**

- Abrahamu, Abram
- Sara, Sarai
- mwana, mwana wa
- Mungu
- Ahadi
- uzao, kutokana na
- Kuamini, kuamini katika
- Adili, uadilifu

**04:09**

Mungu akaweka tena agano na Abrahamu. Agano ni patano kati ya wawili. Mungu akamwambia "Nitakupa mtoto wa kiume kutoka katika mwili wako. Nitawapa uzao wako nchi ya Kanaani." Lakini Abrahamu bado alikuwa hajapata mtoto.

**pande mbili**

sehemu hizi mbili zinaweza kuwa, watu wawili, makundi mawili ya watu, au mtu mmoja na kundi la watu. Katika hili patano lilikuwa kati ya Mungu na Abram.

**kutokana na mwili wako**

Kwa mwili wake binafsi Abram angempa mimba mkewe, ili kwa pamoja wapate mtoto wao kwa njia ya asili. Hii ilikuwa ni ahadi ya ajabu sana maana Abram na sara walikuwa wazee sana.

**Hawakuwa na mtoto wa kiume**

Abram hakuwa na uzao ambao wangeirithi ardhi yake.

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 11-15

**translationWords**

- Mungu
- Agano
- Abrahamu, Abram
- mwana, mwana wa
- Kanaani, Mkanaani
- uzao, kutokana na



## 5. Mtoto wa Ahadi

05:01



Baada ya kuishi miaka kumi katika nchi ya Kaanani, Abraham na Sarai hawakuwa na mtoto. Sarai mke wa Abraham akamwambia, "kwa kuwa Mungu hajanipa mtoto nami ni mzee sana siwezi kupata mtoto. Mchukue Hajiri mjakazi wangu umwoe ili anizalie mtoto."

### bado hakuwa na mtoto

bila mtoto, Abram hakuwa na uzao wa kumfanya yeye kuwa taifa kubwa.

### Amuoe naye pia

Abramu angemchukua Hagai kuwa mke wake wa pili, lakini Hagai asingekuwa mke halali wa Abram kama alivyokuwa Sarai. Bado alikuwa mtumishi wa Sarai.

### upate mtoto kwa ajili yangu

Kwa kuwa Hagai alikuwa mtumishi wa Sarai, basi Sarai angehesabiwa kuwa ndiye mama wa mtoto ambaye angezaliwa.

### translationWords

- Abrahamu, Abram
- Sara, Sarai
- Kanaani, Mkanaani
- Mungu
- mtumishi, mtumwa, utumwa



- Hajiri

**05:02**

Hivyo Abraham akamwoa Hajiri. Hajiri akapata mtoto wa kiume, Abrahamu akampa jina Ishmaeli. Lakini Sarai akamwonea wivu Hajiri. Alipotimiza umri wa miaka kumi na tatu, Mungu akaongea na Abrahamu.

**ameolewa**

Hagai akawa suria wa Abram - mke wa pili kisheria. Lakini Hagai bado alikuwa mtumishi wa Sarai.

**alimuonea Hagai wivu**

Sarai alimuonea Hagai wivu kwa sababu alipata mtoto na yeye asingeweza kupata mtoto.

**translationWords**

- Abrahamu, Abram
- Hajiri
- Ishmaeli
- Sara, Sarai
- Mungu

**05:03**

Mungu akasema, "Mimi ni Mungu mkuu. nitafanya agano pamoja nawe. "Kisha Abrahamu akasujudu. Pia Mungu akamwambia Abrahamu, "Utakuwa **baba wa mataifa mengi**. Nitakupatia wewe na uzao wako nchi ya kanaani kuwa miliki yao na nitakuwa Mungu wao milele. Nawe utawatairi wanaume wote wa familia yako."

### **baba wa mataifa mengi**

Abramu angekuwa na uzao mkubwa na wangukuwa na ardhi yao na kujiongoza wenyewe.

### **Nitakuwa Mungu wao**

Njia nyingine ya kusema hili ni, "Nitakuwa kwao Mungu watakayemwabudu."

### **kila mtu mme katika familia**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kila kijana na mwanaume katika familia yako."

### **translationWords**

- Mungu
- Agano
- Abrahamu, Abramu
- uzao, kutokana na
- Kanaani, Mkanaani
- Tohara

**05:04**

Mkeo Sarai, atapata mtoto wa kiume, atakuwa **mtoto wa ahadi**. Utamwita Isaka. Nitafanya Agano langu pamoja naye. Naye atakuwa taifa kubwa. Nitamfanya Ishmaeli kuwa Taifa kubwa pia. Lakini Agano langu litakuwa pamoja na Isaka. "Kisha Mungu akabadili jina la Abrahamu kuwa Ibrahimu, maana ya jina hilo ni "**baba wa wengi**." Mungu pia akabadili jina la Sarai kuwa Sara, maana yake "mtoto wa mfalme ."

**mtoto wa ahadi**

Isaka alikuwa mtoto ambaye Mungu aliwaahidia Sarai na Abram. Na pia atakuwa mtoto ambaye Abram atapata uzao mwingi kwake

**Nitafanya agano langu na yeye**

Hili litakuwa agano sawa na lile ambalo Mungu alifanya na Abram.

**baba wa wengi**

Kama Mungu alivyoahidi, Abrahamu atakuwa baba wa watu wengi ambao pia watakuwa mataifa mengi.

**Binti wa mfalme**


Majina ya Sarai na Hagai yote yalikuwa na maana sawa yaani "Binti wa mfalme."

**translationWords**

- Sara, Sarai
- mwana, mwana wa
- Ahadi
- Isaka

- Agano
- Ishmaeli
- Mungu
- Abrahamu, Abram
- Sara, Sarai



**05:05**

Siku hiyo Abrahamu akawatairi wanaume wote wa nyumba yake. Baada ya mwaka mmoja, Ibrahimu alitimiza miaka 100 na Sara miaka 90, Sara akazaa na Ibrahimu mtoto wa kiume. Wakamwita jina lake Isaka kama Mungu alivyowaagiza.

### **wanaume wote wa nyumbani kwake**

Hii ina maana ya wanaume na wavulana wote ambao Abrahamu aliwatunza pamoja na watumishi wake wote wa kiume, wadogo kwa wakubwa.

### **translationWords**

- Abrahamu, Abram
- Tohara
- Sara, Sarai
- mwana, mwana wa
- Isaka
- Mungu

**05:06**

Isaka alipokuwa kijana, Mungu akaijaribu imani ya Ibrahimu na kumwambia, "Mchukue, Isaka kijana wako wa pekee, na umuue kama sadaka ya kuteketezwa kwa ajili yangu. "Ibrahimu alimtii Mungu na kumwanda kijana kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa.

**Mungu aliijaribu imani ya Abrahamu**

Mungu alitaka Abrahamu aoneshe ya kuwa amejitoa kikamilifu kwa kwake, na kwamba angetii chochote ambacho Mungu angemwambia.

**Muue**

Mungu hakutaka sadaka ya kutekezwa ya mtu. Mungu alitaka kuona ya kuwa Abrahamu alimpenda Mungu zaidi kuliko mtoto wake.

**alijiandaa kutoa sadaka ya kuteketezwa**

Abrahamu alijiandaa kumtoa mwanae kuwa sadaka ya kuteketezwa. Mungu alimzuia kabla hajamuua kijana wake.

**translationWords**

- Isaka
- Mungu
- Abrahamu, Abramu
- imani
- mwana, mwana wa
- dhabihu, sadaka
- tii, mtiifu, utiifu

05:07



Ibrahimu na Isaka walipokuwa wakitembea kuelekea eneo la kutoa sadaka, Isaka akauliza. "Baba, **kuni kwa ajili ya sadaka** tunazo, lakini kondoo yuko wapi?" Ibrahimu akajibu. "Mungu **atajipatia** kondoo kwa ajili ya sadaka, mtoto wangu."

### alitembea kwenda eneo la kutolea sadaka

Mungu alimwagiza Abrahamu akamtoe Isaka sadaka juu ya mlima maalumu ambao ulikuwa umbali wa mwendo wa siku tatu kutoka alikokuwa anaishi.

### kuni kwa ajili ya sadaka

Kawaida, kondoo aliuawa kwa ajili ya sadaka na kuwekwa juu ya kuni ili kwamba kuni na sadaka viungue pamoja.

### mwanakondoo

mwanakondoo au mbuzi ndiyo walikuwa wanyama wanaostahili kwa sadaka.

### atajipatia

Yawezekana Abrahamu aliamini kuwa Isaka ndiye alikuwa badala ya "mwanakondoo" ambaye Mungu alimpatia. Hata hivyo Mungu alitimiza maneno ya Abrahamu kwa kumpatia mwanakondoo kwa ajili ya sadaka.


### translationWords

- Abrahamu, Abram
- Isaka
- dhabihu, sadaka
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu

- Mungu



05:08



Walipofika eneo la kutoa sadaka, Ibrahimu akamfunga kijana wake Isaka na kumlaza juu ya mazabahu. Alikuwa anajiandaa kumwua kijana wake Mungu akasema, "Acha! Usimdhuru kijana! Sasa natambua **unaniogopa** mimi kwa sababu hukumwacha kijana kwa ajili yangu."

### kumuua kijana wake

Mungu hakutaka sadaka ya binadamu bali alimpima Abrahamu kujua imani yake.

### Acha? usimdhuru kijana!

Mungu alimlinda Isaka na akamkinga Abrahamu asimdhuru.

### unaniogopa

Abrahamu alimwogopa Mungu. Hii ilijumuisha heshima na uchaji wa Mungu. Kwa sababu ya mambo hayo, alimtii Mungu.

### kijana wako wa pekee

Ishimaeli pia alikuwa mtoto wa Abrahamu, lakini Isaka ndiye alikuwa mtoto wa Abrahamu na Sarai. Agano la Mungu na Abrahamu lilikuwa juu ya Isaka.

### translationWords

- dhabihu, sadaka
- Abrahamu, Abramu
- mwana, mwana wa
- Isaka



- [Madhabahu](#)
- [Mungu](#)

05:09



Karibu naye, Ibrahimu akaona kondoo amejinasa kwenye kichaka. Mungu akampatia kondoo kuwa sadaka ya kuteketezwa badala ya Isaka. Ibrahimu kwa furaha akamtoa kondoo kuwa sadaka ya kutekezwa.

## Mwanambuzi

Mwanambuzi ni mbuzi dume.

## Mungu alimpatia mwanambuzi

Kwa muda muafaka, Mungu alimleta mwanambuzi aliyenaswa kwenye kichaka.

## translationWords

- Abrahamu, Abramu
- Mungu
- dhabihu, sadaka
- Isaka

**05:10**

Kisha Mungu akamwambia Ibrahimu. "Kwa sababu ulikuwa tayari kutoa kila kitu kwa ajili yangu hata kijana wako wa pekee, naahidi kukubariki wewe. Uzao wako utaongezeka zaidi kama **nyota za angani**. Kwa sababu umenitii mimi, familia zote ulimwenguni watabarikiwa kwa sababu ya familia yako ."

**Mwano wa pekee**

Isaka ndiye alikuwa mtoto pekee wa Abrahamu na Sarai.

**nyota za angani**

uzao wa Abrahamu ungekuwa kama nyota angani, hauhesabiki

**familia zote duniani**

neni "familia" hapa linamaanisha kundi fulani la watu duniani, licha ya wazazi na watoto.

**umebarikiwa kupitia familia yako**

hapa familia ina maana ya uzao mkubwa ambao Abrahamu angepewa.

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 16 - 22

**translationWords**

- Mungu
- Abrahamu, Abram
- mwana, mwana wa
- Ahadi

- Kubariki
- uzao, kutokana na
- tii, mtiifu, utiifu

## 6. Mungu anamjalia Isaka

06:01



Wakati Ibrahimu alipokuwa mzee sana, mtoto wake wa kiume, Isaka alikuwa amekuwa mtu mzima. Ibrahimu alimtuma mmoja wa watumishi wake kwenda katika nchi walioishi ndugu zake na Ibrahimu ili kumtafutia mke kwa ajili ya mtoto wake, Isaka.

### Alimtuma mmoja wa watumishi wake.

Hii inaweza kutafasiriwa kuwa "alimwambia mmoja wa watumishi wake kurudi nyuma." Neno "nyuma" linamaana kuwa mtumishi anatakiwa arudi sehemu ambayo Ibrahimu aliishi miaka mingi iliyopita kabla hajaenda Kaanani. Hakikisha tafsiri ya sehemu hii ina maana kamili.

### Kwenye ardhi.

Ardhi hii ilikua mashariki ambapo Ibrahimu alikuwa akiishi sasa hivi.

### Kumleta mke kwa ajili ya mtoto wake Isaka.

Hii inaweza kutafasiriwa kama "kumleta mwanamke ambae hajaolewa ili mwanae Isaka amuo."

### translationWords

- Abrahamu, Abramu
- mwana, mwana wa
- Isaka
- mtumishi, mtumwa, utumwa



## 06:02



Baada ya safari ndefu ya kwenda walikoishi ndugu zake na Ibrahimu, Mungu alimwongoza mtumishi wa Ibrahimu kwa Rebeka. Rebeka alikuwa ni mjukuu wa kaka yake na Ibrahimu.

### **Mjukuu wa kaka yake na Abrahamu.**

Alikua binti wa mtoto wa kaka yake na Abrahamu. Babu yake alikuwa kaka yake na Abrahamu.

### **translationWords**

- Abrahamu, Abramu
- Mungu
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Rebeka

## 06:03



**Rebeka alikubali** kuiacha familia yake na kwenda pamoja na yule mtumishi wa Ibrahimu hadi nyumbani kwa Isaka. Na mara baada ya kufika huko, Isaka alimuoa Rebeka.

### **Rebeka alikubali**

Japokuwa wazazi wa Rebeka walipanga ndoa yake, hawakumlazimisha kwenda kuolewa na Isaka.

### **translationWords**

- [Rebeka](#)
- [mtumishi, mtumwa, utumwa](#)
- [Isaka](#)

**06:04**

Baada ya muda mrefu, Ibrahimu alifariki na ahadi zote alizokuwa ameahidiwa na Mungu katika agano zilihamishwa kwa Isaka, mwanae. Mungu alikuwa ameahidi kuwa Ibrahimu atakuwa na uzao mwingi usiohesabika, lakini Rebeka, mkewe Isaka, hakujaliwa kuwa na watoto.

**Ahadi... zilizorithishwa**

Ahadi za agano ambalo Mungu aliweka na Abrahamu hazikuwa kwa ajili yake tu, bali kwa ajili ya kizazi chake.

**Isiyohesabika**

Hii inaweza kutafasiriwa kama "nyingi sana." Neno "isiyohesabika" ina maana vitakuwepo vizazi vingi ambavyo watu watahindwa kuvihesabu.

**translationWords**

- Abrahamu, Abram
- Ahadi
- Mungu
- Agano
- Isaka
- uzao, kutokana na
- Rebeka

**06:05**



Isaka alimwomba Rebeka. Mungu alimjibu na Rebeka akabeba mimba ya mapacha. Wale watoto wawili walikuwa wakishindana tumboni mwa Rebeka. Rebeka akamwuliza Mungu juu ya hicho kilichokuwa kikitokea tumboni mwake.

### **Tumboni mwa Rebeka**

Hii ni, "ndani ya tumbo lake."

### **translationWords**

- [Isaka](#)
- [Rebeka](#)
- [Mungu](#)



## 06:06



Mungu akamwambia Rebeka, "Mataifa mawili yatatokea kutokana na watoto wawili wa kiume walio tumboni mwako. Na kutakuwa na ushindani kati yao, na mtoto mkubwa atamtumikia mdogo."

### **Toka wa wanawe wawili**

Hii ni, "kutoka kwenye uzao wa watoto wawili."

### **Watashindana wenyewe kwa wenyewe**

Watoto wote wawili na taifa ambalo litatokana na wao wataendelea kushindana.

### **Mtoto mkubwa**

Japokua watoto walikua mapacha, mtoto anayezaliwa wa kwanza ndiye anayepewa nafasi kama mtoto wa kwanza.


### **Kumtumikia mdogo**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "mwana mdogo anatakiwa kufanya yale atakayoambiwa na mkubwa ayafanye."

### **translationWords**

- Mungu
- Rebeka
- mwana, mwana wa



**06:07**

Na siku ile walipozaliwa watoto wa Rebeka, mtoto mkubwa alitoka akiwa mwekundu na mwenye nywele nyingi katika mwili wake; walimwita jina lake, Esau. Mtoto mdogo alizaliwa huku akiwa amekishikilia kisigino cha Esau, naye walimwita jina lake, Yakobo.

**Watoto wa Rebeka walizaliwa.**

Lugha nyingine zina njia tofauti ya kusema haya kama, "pale Rebeka alipowaona na kuwachukua" au, "pale Rebeka alipowaleta kwenye mwanga."

**Mtoto mkubwa ..... mtoto mdogo**

Hii inaweza kutafasiriwa kuwa, "mtoto atakayekuja kwanza ... mtoto wa pili atakayekuja." Hakikisha kuwa namna ambavyo "mkubwa" na "mdogo" inatafsiriwa iendelee kuleta maana kuwa watoto hawa ni mapacha.

**Nyekundu**

Hii inaweza kumaanaisha kuwa ngozi yake ilikua nyekundu sana au nywele katika mwili wake zilikua nyekundu.

**Nywele**

Esau alikua na nywele nyingi mwilini mwake. Waweza kusema kuwa "mtoto mkubwa alikua mwekundu na mwenye nywele nyingi."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 24 :1-25:26

**translationWords**

- [Rebeka](#)

- mwana, mwana wa
- Esau
- Yakobo, Israeli

## 7. Mungu Anambariki Yakobo

07:01



Wavulana walipokomaa, Yakobo alipenda kukaa nyumbani, ila Esau alipenda kuwinda. **Rebeka alipenda Yakobo, ila Isaka alipenda Esau.**

### Alipenda kukaa nyumbani ... alipenda kuwinda

Lugha nyingine hutumia neno "kupenda" ambavyo ni tofauti na ilivyotumika hapa, "Rebeka alipenda Yakobo." Kwa mfano hii inaweza kutafasiriwa kama "alipenda kukaa nyumbani" ... "alipenda kuwinda" au "alipendelea kukaa nyumbani" ... "alipendelea kuwinda."

### Nyumbani

Maelezo haya yanaelezea ni eneo ambalo familia wanaishi. Yakobo alipenda kukaa karibu na hema sehemu walipoishi. Lugha nyingine zina maelezo ya kipekee juu ya "nyumba."

### Rebeka alipenda Yakobo, ila Isaka alipenda Esau.

Hii inaweza kutafasiriwa kama "Rebeka alipenda sana Yakobo na Isaka alipenda sana Esau." Hii haimaanishi kuwa Rebeka na Isaka hawakumpenda mtoto mwingine lakini kila mzazi alikua naupendeleo wake.

### translationWords

- [Yakobo, Israeli](#)
- [Esau](#)
- [Rebeka](#)
- [Isaka](#)

**07:02**

Siku moja Esau alipotoka kuwinda, alikuwa na njaa sana, Esau alisema kwa Yakobo, "tafadhali naomba chakula ulichopika." Yakobo akajibu akamwambia, "kwanza nipe mimi haki yako ya mtoto mkubwa". Ndipo Esau akampa haki yake ya mtoto mkubwa."Hivyo Esau alimpa Yakobo chakula.

### **Nipe mimi sehemu ya chakula ... nipe mimi haki zako**

luga nyingine zingependelea kutumia maneno mawili tofauti kwenye neno "nipe." Hii pia hutumika kama "Esau alimpa ... Yakobo alimpa" kwenye sentensi mbili za mwisho.

### **Haki kama mtoto mkubwa**

Kutokana na desturi, kwa kuwa Esau alikua mtoto mkubwa, alipaswa kupokea mara mbili ya utajiri wa baba yake endapo baba yao atafariki. Yakobo alitafta njia ya kuchukua haki za mtoto wa kwanza toka kwa Esau.

### **translationWords**

- Esau
- Yakobo, Israeli



**07:03**

Isaka alitaka kumpa Esau baraka zake. Kabla ya kufanya hivyo, Rebeka na Yakobo wamdanganya kwa Yakobo kujifanya kuwa Esau. Isaka alikuwa mzee na hakuweza kuona. Yakobo alivaa nguo za Esau na ngozi za mbuzi mikononi na shingoni.

### **Akampa baraka zake**

Ilikua desturi kwa baba kuelezea shauku zao juu ya mambo mema yatakayotokea kwa watoto wao. Kwa kawaida mtoto mkubwa anapokea ahadi nzuri. Isaka alitaka baraka zaidi zitokee kwa Esau.

### **Alimdanganya kwa hila**

Neno "hila" inamaanisha kufanya jambo kwa ajili ya kumdanganya mtu. Rebeka alikuja na mpango wa kumlaghai Isaka ampe Yakobo baraka ya pekee badala ya Esau.

### **Kuigiza**

Neno "kuigiza" linaonesha namna ambavyo Yakobo alimdanganya baba yake (aliyekua na uwezo mdogo wa kuona kutokana na umri wake kuwa mkubwa).

### **Ngozi ya mbuzi**

Manyoya yaliyopo katika ngozi ya mbuzi yalingemfanya Yakobo aonekane kama Esau.

### **translationWords**

- [Isaka](#)
- [Kubariki](#)
- [Esau](#)



- [Rebeka](#)
- [Yakobo, Israeli](#)

**07:04**



Yakobo alikuja kwa Isaka akasema, "mimi ni Esau. Nimekuja ili kwamba unibariki." Isaka aliposikia harufu na kuhisi nywele za mbuzi na kunusa nguo, alidhani ni Esau na akambariki.

### **Yakobo akaja kwa Isaka**

Kwenye lugha zingine inaweza kuwa na uhalisia zaidi kwa kusema "Jakobo alikwenda kwa Isaka."

### **Alidhani kuwa ni Esau.**

Alidhani kuwa mtu aliyemshika na kusikia harufu yake alikua Esau.

### **translationWords**

- [Yakobo, Israeli](#)
- [Isaka](#)
- [Esau](#)
- [Kubariki](#)

**07:05**



Esau alimchukia Yakobo kwa kuwa Yakobo alikuwa ameiba haki yake ya kuwa mkubwa na baraka zake. Hivyo alipanga moyoni mwake kumuua baada ya baba yao kufariki.

### **Haki kama mtoto wa kwanza**

Yakobo alitafta namna ya kupata sehemu kubwa ya mali ya baba yake iliyotakiwa kwenda kwa Esau kama mtoto wa kwanza.

### **Baraka yake.**

Yakobo pia alimlaghai baba yao katika kumpa yeye ahadi ya utajiri wa baraka ya kipekee ambayo Isaka alikusudia kumpa Esau.

### **translationWords**

- Esau
- Yakobo, Israeli
- Kubariki

**07:06**

Rebeka alisikia mpango wa Esau. Yeye na Isaka walimtorosha Yakobo aende mbali akaishi na ndugu zake.

## **Mpango ya Esau**

Mpango wa Esau ulikua ni kumuua Yakobo baada ya kifo cha baba yake.

## **Rebeka na Isaka wakamtuma Yakobo.**

Rebeka alitaka kumlinda Yakobo toka kwa Esau hivyo akaongea na Isaka juu ya kumtuma yakobo aende zake.

## **kwenda mbali kuishi na ndugu zake**

Hii ilikua sehemu ile ile ambayo Rebeka aliishi kipindi ambacho mtumwa wa Ibrahimu alimchukua kuwa mke wa Isaka. Kuliweka hili wazi unaweza kuongeza kuwa "ndugu wa ardhi ile ile alipokua akiishi." Arhi ile ilikua mashariki, umbali wa maili mamia.

## **Ndugu zake**

hii inaweza kutafsairikwa kama "ndugu zao" Kwa kuwa kaka yake na Abraham alikua babu yake na Rebeka, ndugu zake na Rebeka pia walikua ndugu wa Isaka.

## **translationWords**

- [Rebeka](#)
- [Esau](#)
- [Isaka](#)
- [Yakobo, Israeli](#)



**07:07**



Yakobo akaishi na ndugu zake Rebeka kwa miaka mingi. Katika kipindi hicho alioa na akazaa watoto wa kiume kumi na wawili na wa kike mmoja. Mungu akamtajirisha sana.

## Utajiri

Hii inajumuisha pesa, kundi kubwa ya wanyama na vyote alivyomiliki.

## translationWords

- Yakobo, Israeli
- Rebeka
- Mungu



**07:08**



Baada ya kuishi nje ya Kanaani kwa miaka ishirini, Yakobo alirudi nyumbani na familia yake, watumwa wake, na mifugo yake yote.


### **Baada ya miaka ishirini.**

Yakobo aliishi miaka ishirini kwenye nchi aliyotoka mama yake. Kama hiyo haijaleweka unaweza kusema "Baada ya miaka ishirini akiishi katika nchi ambayo ndugu zake waliishi pia."

### **translationWords**

- Kanaani, Mkanaani
- Yakobo, Israeli
- mtumishi, mtumwa, utumwa

07:09



Yakobo aliogopa sana kwa sababu alidhani Esau bado alitaka kumuua. Akatuma makundi ya mifugo kwa Esau kama zawadi. Watumwa waliopeleka mifugo wakasema kwa Esau, "Mtumwa wako Yakobo anakupa wewe mifugo hii. Anakuja hivi karibuni."

### Mtumishi wako Yakobo

Yakobo hakika hakua mtumishi wa Esau. lakini alimwambia watumishi wake kusema hivi kwa sababu alitaka kumuonyesha Esau kuwa alimwendea kwa unyenyekevu na heshima ili Esau asiendelee kua na hasira juu yake.

### translationWords

- Yakobo, Israeli
- Esau
- mtumishi, mtumwa, utumwa

**07:10**

Ila Esau alikuwa amemsamehe Yakobo, na walifurahi kuonana tena kila mmoja. Yakobo akaishi Kanaani kwa amani. Isaka akafa huko, Esau na Yakobo wakamzika. Ahadi za agano, Mungu alizomhaidia Ibrahimu kumpata zikatoka kwa Isaka kwenda kwa Yakobo.

**Waliishi kwa amani**

Hii inaelezea kuwa Esau na Yakobo hawakukasirikiana na kugombana wao kwa wao.

**Wakamzika**

Hii inaweza kumaanisha kuwa walichimba shimo kwenye ardhi wakauweka mwili wa Isaka na kufunika shimo hilo kwa kutumia udongo au jiwe. au inaweza kumaanisha kuwa waliuweka mwili wa Isaka kwenye pango na kufunika sehemu ya wazi.

**Agano la ahadi**

Hizi ni ahadi alizozifanya Mungu kwenye agano lake na Ibrahimu.

**Ikapita toka kwa Isaka kwenda kwa Yakobo**

Ahadi zilizotoka kwa Ibrahimu kwenda kwa mwanawe Isaka na sasa twenda kwa Yakobo mtoto wa Isaka. Esau hakuzipokea ahadi.

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 25:27 - 33:20

**translationWords**

- [Esau](#)

- samehe, kusamehe
- Yakobo, Israeli
- Amani
- Kanaani, Mkanaani
- Isaka
- Agano
- Ahadi
- Mungu
- Abrahamu, Abram

## 8. Mungu anamuokoa Yusufu na Familia yake.

08:01



Baada ya miaka mingi kupita, Yakobo alipokuwa mzee sana, alimuagiza kijana wake aitwaye Yusufu, kuwatembelea kaka zake waliokuwa wakichunga mifugo ya baba yao.

### Alimtuma

Neno hili linamaanisha Yakobo alimwambia Yusufu aende na Yusufu akaenda.

### Mtoto aliyependwa

Hii inaweza kutafasiriwa kama "mtoto aliyependwa zaidi kuliko watoto wengine."

### Kukagua

Hii inamaanisha Yusufu alienda na kuangalia kama kila kitu kipo sawa kwa ndugu zake. Lugha nyingine zinaweza kusema "kuangalia hali ya kaka zake."

### Kaka

Hawa walikua kaka zake wakubwa na Yusufu.

### Kuangalia kundi la mifugo

Kwa kuwa ilikuwa safari ya siku kadhaa, unaweza kusema "waliokuwa mbali wakichunga mifugo."



## translationWords

- Yakobo, Israeli
- Yusufu (Agano la Kale)

## 08:02



Kwakuwa Yusufu alikuwa anapendwa sana na baba yake, na kwamba siku moja aliwahi kuota ndoto na akawasimulia kaka zake kwamba yeye atakuwa mtawala wao hapo baadae, kaka zake walimchukia. Hivyo, Yusufu alipofika kwa kaka zake, walimteka na wakamuuzwa kwa watu wenye kufanya biashara ya watumwa.

### **Alikwenda kwa kaka zake**

Njia nyingine ya kutafasiri hili ni "akafika eneo ambalo kaka zake walikuwepo."

### **Kutekwa**

Walimchukua kinyume na matakwa yake. Haikua sahihi kwa wao kufanya hivi.


### **Wafanya biashara ya utumwa**

Walikua watu waliofanya biashara ya kununua watu toka kwa mmiliki mmoja na kuwauza kama watumwa kwa mmiliki mwingine.

### **translationWords**

- Yusufu (Agano la Kale)
- ndoto
- mtumishi, mtumwa, utumwa

## 08:03



Basi kaka zake na Yusufu walipotaka kurudi nyumbani, walikubaliana kwa hila kuzichanachana nguo za mdogo wao, Yusufu, kisha wakaziloweka kwenye damu ya mbuzi. Walipofika wakamuonyesha baba yao nguo hizo zenye damu, ili kumuaminisha kuwa kuna mnyama mkali wa porini amemrarua na kumuua Yusufu. Basi Yakobo aliposikia habari hiyo alimhuzunikia sana Yusufu.

### Damu ya mbuzi

Kaka zake na Yusufu walitaka Yakobo afikiri kuwa damu iliyokuwa katika nguo ni damu ya Yusufu.

### translationWords

- Yusufu (Agano la Kale)
- Yakobo, Israeli

**08:04**

Na ndipo wale wafanyabiashara ya watumwa, wakamsafirisha Yusufu hadi nchi ya mbali sana iitwayo Misri. Nchi ya Misri ilikuwa maarufu na hodari kwa mambo mengi katika nchi za mwambao wa mto Naili. Yusufu akauzwa kama mtumwa katika nyumba ya afisa mmoja wa serikali ya misri aliyekuwa tajiri sana. Naye Yusufu akatumika kwa uaminifu sana katika nyumba ya bwana wake, na Mungu akambariki sana Yusufu.

**Kiongozi wa serikali**

Mtu huyu alikua sehemu ya serikali ya Misri. Njia nyingine ya kusema hivi ni "kiongozi katika serikali ya Misri."

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Yusufu (Agano la Kale)
- Misri, Mmisri
- Mto Nili, Mto wa Misri
- Mungu
- Kubariki

**08:05**

Mke wa tajiri yake alimtaka Yusufu ili azini naye, lakini Yusufu alikataa ili asimkosee Mungu. Kisha baada ya hayo, yule mwanamke, mke wa tajiri, alikasirika sana, hata akamtuhumu Yusufu kwa kumsingizia ili Yusufu akamatwe na kufungwa gerezani. Hata hivyo, Yusufu aliendelea kuwa mwaminifu mbele za Mungu hata alipokuwa amefungwa gerezani, na Mwenyezi Mungu akambariki. Hata ilipotimia miaka miwili baadae, Yusufu alikuwa bado yumo gerezani, japo hakuwa na kosa lolote.

### **Akajaribu kulala na Yusufu**

Njia nyingine ya kusema hivi ni "alijaribu kumshawishi Yusufu awe naye kimwili." "Kulala na" ni njia ya kuelezea ili kuepuka kuwa neno la kuchukwaza.

### **Kumtenda Mungu dhambi**

Ni kinyume na amri za Mungu kwa watu kulala pamoja kabla hawajaoana. Yusufu hakutaka kufanya dhambi kwa kutokutii amri za Mungu.

### **Kuendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu**

Njia nyingine ya kusema haya yaweza kuwa "kuendelea kumtii Mungu."

### **translationWords**

- Yusufu (Agano la Kale)
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- mwaminifu, uaminifu
- Kubariki



**08:06**

Yusufu alikuwa bado yumo gerezani hadi miaka miwili baadae, japo hakuwa na kosa lolote. Siku moja nyakati za usiku, Farao, mfalme wa Wamisri, aliota ndoto mbili zikamsumbua sana mawazoni mwake usiku ule. Miongoni mwa washauri wake wote na wenye hekima, hapakuwa na mtu yeyote mwenye uwezo wa kutoa maana ya ndoto hizo.

**Ilimsumbua sana**

Hii inamaanisha kuwa Mfalme aliogopa na kuchanganyikiwa (kwa sababu ya alichokuwa amekiona kwenye ndoto).

**Washauri wake**

Walikua wanaume wenye uwezo na maarifa ya pekee wenye uwezo wa kueleza maana ya ndoto. Tafisiri nyingine zinawaelezea kama "wazee wenye hekima."

**Maana ya ndoto**

Watu wa Misri waliamini kuwa ndoto zilikuwa na ujumbe toka kwa miungu ikiwaambia kitakachotokea baadaye. Mungu alitumia ndoto za Farao kumwambia kitakachotokea.

**translationWords**

- Yusufu (Agano la Kale)
- sio na hatia
- Farao, mfalme wa Misri.
- Misri, Mmisri
- mfalme
- ndoto

**08:07**

Kwakuwa Mwenyezi Mungu alikuwa amemjalia Yusufu uwezo wa kipekee wa kutafsiri ndoto, Farao, mfalme wa Misri, aliamuru **Yusufu aletwe kwake** kutoka gerezani ili atoe maana halisi ya ndoto hiyo. Kwa kuongozwa na Mwenyezi Mungu, Yusufu akasimama mbele ya Farao kutafsiri ndoto zile akisema; "Wakati unakuja ambapo Mwenyezi Mungu ataruhusu pawepo na kipindi cha miaka saba ya mavuno mengi, itakayofuatiwa na miaka mingine saba ya ukame na njaa."

**Kutafsiri ndoto**

"Kutafsiri" ni kusema maana ya kitu fulani. Hivyo Yusufu alikua na uwezo wa kuwaambia watu maana ya ndoto zao.

**Yusufu aletwe kwake**

Njia nyingine ya kusema hivi inaweza kuwa "aliwaamuru watumishi wake wampeleke Yusufu kwake."

**Mungu atatuma**

Mungu atasababisha mazao yakue vizuri kwa miaka saba na baada ya hapo atasababisha wazalishe chakula kidogo sana ili watu na wanyama wasiwe na chakula cha kutosha.

**Njaa**

Bustani na mashamba yatazalisha chakula kidogo sana hivyo watu na wanyama hawatakua na chakula cha kutosha.

**translationWords**

- [Mungu](#)
- [Yusufu \(Agano la Kale\)](#)

- ndoto
- Farao, mfalme wa Misri.

**08:08**



Yusufu akateuliwa kuwa mtu wa pili kwa mamlaka katika nchi yote ya Misri, kwa kuwa Farao, mfalme wa Misri, alifurahishwa na kuvutiwa sana na Yusufu.

### **Alishawishiwa na**

Farao alishangazwa na hekima za Yusufu na akampa heshima. Alimuamini Yusufu afanye maamuzi yenye hekima ambayo yatawafaidisha watu. Ingekua sahihi kusema "alishawishiwa na hekima za Yusufu."

### **Mtu wa pili mwenye mamlaka makubwa**

Farao alimfanya Yusufu kuwa mwenye nguvu na kiongozi wa muhimu sana katika Misri. Farao tuu ndiye aliyekua mwenye nguvu na muhimu kuliko Yusufu.

### **translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Yusufu (Agano la Kale)
- Misri, Mmisri



**08:09**



Basi Yusufu akawatangazia watu wote wa Misri kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha watakapovuna katika kipindi cha miaka saba ya mavuno mengi. Ilipowadia ile miaka saba mingine ya njaa, ndipo Yusufu akatumia sehemu ya akiba ya chakula kuwauzia watu ili kiwafae katika kile kipindi cha miaka saba ya njaa.

**Kuhifadhi vyakula vingi.**

Walichukua vyakula toka kwenye mavuno mengi na kupeleka mijini na kuvihifadhi huko. Hivyo vyakula vikawa vya Farao.

**translationWords**

- Yusufu ([Agano la Kale](#))



## 08:10



Hali ya ukame na njaa, ikazidi kuwaathiri watu wengi wa Misri yenyewe na hata nchi ya Kanaan alikoishi Yakobo baba yake na Yusufu pamoja na familia yake.

### Misri lakini pia Kanaanani

Kwenye lugha nyingine inaweza kueleweka vizuri au kua na uhalisia zaidi ukisema "nchi ya Misri, lakini pia nchi ya Kanaanani."

### Njaa ilikua kali

Njaa ilikua mbaya sana. Kulikua na chakula kidogo sana na watu wengi nje ya Misri walikua na njaa kali.

### translationWords

- Misri, Mmisri
- Kanaanani, Mkanaanani
- Yakobo, Israeli

## 08:11



Hivyo, Yakobo akawaagiza vijana wake wakubwa kwenda Misri kununua chakula. Walipokuwa wakingojea zamu yao ya kununua chakula, Yusufu aliwaona kaka zake na akawatambua, ila wao walikuwa wamemsahau Yusufu.

### **Watoto wake wakubwa**


Hawa walikua kaka zake wakubwa na Yusufu waliomuza utumwani.

### **Hawakumtambua Yusufu**

Hawakujua kama yule mtu ni Yusufu, kwa kuwa sasa Yusufu alikua na umri mkubwa tofauti na mara ya mwisho walipomuona na alikua amevaa kama kiongozi wa Wamisri.

### **translationWords**

- [Yakobo, Israeli](#)
- [Misri, Mmisri](#)
- [Yusufu \(Agano la Kale\)](#)

**08:12**

Yusufu aliamua kufanya mahojiano nao akitaka kujua iwapo walikuwa wamebadilika kitabia, kisha akawaambia hivi: "msihofu ndugu zangu, mimi mnaeniona ndiye mdogo wenu Yusufu. Najua fika hamkuwa na nia njema na mimi mliponiiza kama mtumwa, lakini Mwenyezi Mungu alitumia nia yenu mbaya kwa ajili ya kusudi jema." Nawakaribisha muwe huru kuja kuishi hapa Misri ili niwatunze ninyi na familia zenu.

**Aliwajaribu kaka zake**

Yusufu aliwaweka kaka zake wakubwa kwenye wakati mgumu kuona kama watamlinda mdogo wao au watamtendea mabaya kama walivyomtendea Yusufu. Walipomlinda mdogo wao Yusufu akajua kuwa wamebadilika.

**Kama wamebadilika**

Njia nyingine ya kusema hivi ni, "kama wamekua tofauti na walivyokua." Miaka iliyopita kaka zake na Yusufu walimuza utumwani. Yusufu alitaka kujua kama sasa wapo tayari kufanya yaliyo mema.

**Msiogope**

Njia nyingine ya kusema hivi ni, "Hampaswi kuogopa adhabu yoyote toka kwangu." Kaka zake Yusufu waliogopa kwa sababu walimkosea sana Yusufu na sasa kama kiongozi mkubwa ana mamlaka ya kuwaadhibu. Yusufu angekataa kuwauzia chakula, au hata kuwaweka gerezani au kuwaua.

**Ubaya kwa wema**

Kaka zake Yusufu wakafanya yaliyo mabaya kwa kumuza Yusufu kama mtumwa na akapeleka Misri. Lakini Mungu aliliruhusu hilo ili Yusufu awahudumie maelfu ya watu toka katika njaa ikiwemo familia yake yenyewe. Hili lilikuwa jambo zuri sana.

## translationWords

- Yusufu (Agano la Kale)
- baya, ovu, uovu
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Mungu
- wema, uzuri
- Misri, Mmisri


**08:13**



Ndipo kaka zake Yusufu waliporudi nyumbani kwao, Kanaani, walimpasha habari baba yao kuwa Yusufu , mwanae mpendwa bado yuko hai; Yakobo baba yake na Yusufu alijawa na furaha isiyo kifani.



## 08:14



Katika kipindi hicho, Yakobo alikuwa amekwisha kuwa mzee sana. Lakini akalazimika kuhamia katika nchi ya Misri yeye na familia yake yote. Hivyo, Yakobo akaishi pamoja na familia yake katika nchi ya Misri na kabla hajafariki akawapa mibaraka wanae wote, kila mmoja na mbaraka wake.

### Japokuwa Yakobo alikuwa mzee alienda Misri


Kulikua na umbali toka Kaanani kwenda Misri na ilikua vigumu kwa mzee kutembea au kuendesha mkokoteni kwa umbali huo.

### Kabla Yakobo hajafa

Yakobo alifia Misri. Hakuweza kurudi Kaanani nchi ambayo Mungu alimuahidi kumpa yeye pamoja na uzao wake.

### translationWords

- Yakobo, Israeli
- Misri, Mmisri
- Kubariki

**08:15**

Kama ambavyo Mwenyezi Mungu alikuwa amemuahidi Ibrahimu, maagano yote yakarithishwa kwa vizazi vyake yaani, Isaka, kisha Yakobo, na hatimaye watoto kumi na wawili wa Yakobo pamoja na uzao wao, ambao ndio wanaounda kabila kumi na mbili za Israeli.

**Agano la ahadi**

Muda mrefu uliopita Mungu aliweka makubaliano na Ibrahimu kuwa atampa uzao mwingi, wataimiliki ardhi ya Kaanani na kuwa taifa kubwa. Mungu pia aliahidi kua watu wote watabarikiwa kupitia uzao cha Ibrahimu.

**Kurithisha kwa**

Njia nyingine ya kusema hivi yaweza kuwa "kurithisha kwa" au "kumpa" au "kutumika kwa." Ahadi za Mungu kwa Ibrahimu pia zilikuwa kwa watoto wake na wajukuu na kwa uzao wake wote. Tazama pia maelezo katika OBS 6-4.

**Makabila kumi na mbili ya Israeli**

Mungu alimuahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo kuwa uzao wao utakua taifa kubwa. Baadae Mungu alibadili jina la Yakobo kuwa Israeli. Kuzao wa watoto 12 wa Yakobo ukawa makabila makubwa 12. Makabila haya 12 yalitengeneza taifa lililoitwa Israeli ambalo liliitwa kwa jina jipya la Yakobo.

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 37-50


**translationWords**

- [Agano](#)
- [Ahadi](#)
- [Mungu](#)
- [Abrahamu, Abram](#)
- [Isaka](#)

- Yakobo, Israeli
- uzao, kutokana na
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

## 9. Mungu Anamwita Musa

09:01



Yusufu alipofariki, ndugu zake walidumu kuishi huko Misri. Wao pamoja na wazazi wao, kwa miaka mingi waliongezeka na walikuwa na watoto wengi. Kabila hilo waliitwa Waisraeli

### Waliitwa waisraeli


Kundi la uzao wa Yakobo uliitwa "Israeli" ambalo ni jina alilopewa Yakobo na Mungu. Watu wa kundi lile waliitwa "Waisraeli."

### translationWords

- Yusufu (Agano la Kale)
- Misri, Mmisri
- uzao, kutokana na
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli



09:02



Mamia ya miaka mingi ilipita, wakazidi kuongezeka. Wamisri walimsahau Yusufu na kazi nzuri alizozifanya kwa Wamisri. Wamisri waliwaogopa Waisraeli kwa kuwa walikuwa wengi na **Farao** wa kipindi hicho aliwafanya kuwa watumwa kwa Wamisri.

## Farao

"Farao" ni neno la kimisri linalomaanisha kuwa mfalme wao. Yawezekana Farao huyu alikua ni mtoto wa Farao aliyekufa, ambaye ni uzao wa Farao aliyefahamika na Yusufu.

## Kuwafanya wana wa Israeli watumwa

Hiyo ni "kuwalazimisha waisraeli kufanya kazi ngumu kinyume na matakwa yao na kuwatumikisha kwa ukatili mbaya."

## translationWords

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Misri, Mmisri
- Yusufu (Agano la Kale)
- Farao, mfalme wa Misri.
- mtumishi, mtumwa, utumwa



**09:03**



Waisraeli walitumikishwa na Wamisri kwa kazi ngumu kwa kujenga majumba na miji mikubwa. Ugumu wa kazi ulisababisha huzuni kimaisha. Bali baraka za Mungu ziliwazidishia watoto kwa wingi.

## **Mateso**

Hii inamaanisha waliteseka sana kwa sababu ya namna walivyotumikishwa na kulazimishwa kufanya kazi. Walikatishwa tamaa.


## **Mungu aliwabariki**

Mungu aliwajali na kuwawezesha kuvumilia mateso na pia kuwawezesha kuwa wengi kwa kuwapa watoto.

## **translationWords**

- Misri, Mmisri
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Kubariki

**09:04**



Farao aliona kuwa Waisraeli walikuwa wanazaa watoto wengi, aliamuru watoto wa kiume wauawe kwa kutupwa katika mto Naili.

## **Kuona**

Njia nyingine ya kusema neno hili ni "aligundua" au "alijua."

## **translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mto Nili, Mto wa Misri

09:05



Mtoto wa kiume alizaliwa na mama mmoja wa Kiisraeli. Wazazi wa mtoto huyo walimficha kwa muda walioweza.

**Kwa kwadri walivyoweza.**

Walimficha mtoto toka kwa waisraeli mpaka ilipokua ngumu kumuweka mtoto katika hali ya usalama nyumbani kwao.

### translationWords

- [Israeli](#), [Waisraeli](#), [taifa la Israeli](#)

**09:06**

Mtoto huyo alipokuwa hawezi kufichika tena, ili kumuokoa wazazi walimweka katika kikapu kieleacho na kukiweka katika majani kando ya mto Naili. Ili kujua kuwa ni jambo gani lingempata mtoto huko mtoni dada yake alikuwa akifanya uchunguzi.

## Mto Nile

Ukweli Nile ni mto uliopo kaskazini mashariki mwa Afrika

Mto Nile unapita Misri na kumwaga maji yake bahari ya Mediteranian. Mazao yalikuwa vizuri kwenye bonde lenye rutuba wamisri wengi waliishi karibu na Mto Nile kwa kuwa ilikua ni chanzo muhimu cha maji na mazao ya chakula.

## translationWords

- [Mto Nili](#), [Mto wa Misri](#)



09:07



Mtoto wa kike wa Farao aliona kikapu na alichungulia ndani yake. Alipona mtoto, alimchukua awe wake na kumwajiri mwanamke wa Kiyahudi amtunze. Bila kutambua, mama huyo mlezi ndiye alikuwa mzazi wa mtoto huyo. Mtoto alipoacha kunyonya alikabidhiwa kwa binti Farao naye akamwita jina lake Musa.

### Alimchukua kama mtoto wake

Alikuwa mtoto wa kike wa mfalme. Alipomfanya musakuwa mwanawe, Musa akawa mtoto wa kiume wa mfalme Misri.

### Kumlea

Njia nyingine ya kusema hivi ni "kumyonyesha yule mtoto Musa."

### translationWords

- Farao, mfalme wa Misri.
- mwana, mwana wa
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Musa



09:08



Akiwa mtu mzima, siku moja Musa alimkuta Mmisri akimpiga mtumwa wa Kiisraeli. Na alijitahidi kumuokoa Mwisraeli mwenzake.

## Kukua

Njia nyingine ya kusema hivi ni "akawa mtu mzima"

## Muisraeli mwenzake

Aya hii ina maanisha mtumwa wa kiisraeli. Neno "mwenzake" linaonyesha kuwa Musa pia alikua muisraeli. Japokuwa mtoto wa Farao wa Misri alimlea Musa lakini Musa alikumbuka kuwa yeye ni Muisraeli halisi.

## translationWords

- Musa
- Misri, Mmisri
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- okoa, salama

**09:09**



Musa alimuua Mmisri na kuuzika mwili wake akidhani kwamba hakuna mtu ambaye angemwona. Kumbe mtu mmoja alimwona akifanya kitendo hicho.

**09:10**



Habari za mauaji zilipomfikia Farao, aliazimia kumuua Musa. Musa alitoroka kutoka Misri na kukimbilia nyikani ili kujiokoa na walinzi wa Farao.

## Jangwani

Jangwani ni sehemu kubwa yenye mwamba na kame. Ardhi hiyo sio nzuri kwa kukuzia mazao ya chakula na watu wachache wanaishi hapo.

## translationWords

- Farao, mfalme wa Misri.
- Musa
- Misri, Mmisri

## 09:11



Musa alikuwa mchungaji wa kondoo huko nyikani mbali na nchi ya Misri. Alioa huko na kuzaa watoto wawili wa kiume.

## Jangwani

Angalia jinsi ya kutafasili hili katika 9-10.

## translationWords

- Musa
- mchungaji, kuchunga
- Misri, Mmisri



**09:12**

Siku moja Musa alikuwa akichunga kondoo wake, aliona kichaka kilichowaka moto bila kuteketea. Musa alisogea kuona vizuri, alipokaribia, Mungu alisikika akisema, "Musa vua viatu vyako. Ardhi uliyosimama juu yake ni takatifu".

**Alikuwa akichunga kondoo zake**

Hii inamaanisha alikuwa akifanya kazi ya kuchunga kwa kuwaongoza kondoo kwenye maji na majani na kuwalinda. Pia inaweza kutafasiriwa kama "kuwahudumia kondoo"

**Kichaka hakikuteketea**

Mungu alitengeneza kichaka chenye moto lakini moto huo haukuteketeza kichaka kile.

**Sauti ya Mungu ikasema**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "Mungu akasema kwa sauti kubwa." Musa akasikia Mungu akisema lakini hakumuona Mungu.

**Vua viatu vyako**

Mungu alimtaka Musa avue viatu vyake ili kuonyesha heshima kwa Mungu. Kuweka sawa sababu ya jambo hili waweza kusema "vua viatu vyako maana upo kwenye ardhi takatifu."

**Ardhi takatifu**

Ilikuwa takatifu kwa namna ambavyo Mungu alitenga na ardhi nyingine ya kawaida na kuifanya kuwa ya pekee ambayo anaweza kujidhihirisha.



## translationWords

- Musa
- kondoo, kondoo dume, kondoo jike
- Mungu
- takatifu, utakatifu

**09:13**

Mungu alimwambia Musa, "Nimeyaona mateso ya watu wangu. Ili kuwakomboa kutoka utumwani huko Misri, nitakutuma wewe kwa Farao ukawaondoe Waisraeli kutoka utumwani Misri. Nami nitawapa nchi ya Kanaani, niliyowaahidia Ibrahimu, Isaka na Yakobo."

**Mateso ya watu wangu**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "mateso makali ambayo watu wangu wanayapitia. lugha nyingine zinaweza kutafasiri kama "namna wamisri walivyowapa maumivu makali watu wangu".

**Watu wangu**

Hii inawaelezea wana wa Israeli. Mungu aliweka agano pamoja na Ibrahimu na kizazi chake kuwa atawabariki na kuwafanya kuwa taifa kubwa. Kupitia agano hili wana wa Israeli wakawa watu wake Mungu.

**kuwatoa..... nje ya utumwa wao Misri**

Hii inaweza kuatafasiriwa kuwa "kuwaweka huru toka kwenye utumwa huko Misri" au "Kuwatoa nje ya Misri walipokuwa watumwa."

**translationWords**

- Mungu
- tseseka, kuteseka
- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Misri, Mmisri
- Kanaani, Mkanaani
- Ahadi

- Abrahamu, Abram
- Isaka
- Yakobo, Israeli

**09:14**

Musa akauliza, watakapotaka kujua Ni nani aliyenituma kwao nisemeje? Mungu akasema, "**MIMI NIKO AMBAYE NIKO**. Waambie AMBAE NIKO amenituma. Mimi ni YEHOVA Mungu wa baba zenu Ibrahimu, Isaka na Yakobo. **Jina langu** ndilo hilo milele."

**NIKO AMBAYE NIKO**

Maelezo haya yanaonyesha kuwa Mungu anaweza kujielezea mwenyewe na sio kwa kitu kingine tunachokifahamu na hawezi kufananishwa na kitu kingine.

**MIMI NIKO**

Jina hili linasisitiza kuwa ni Mungu pekee aliyekuwepo kabla na ataendelea kuishi.

**Jina langu**

Jina ambalo Mungu alimwambia Musa na wana wa Israeli wote wamuite ni "Yahweh" linalofanana na "MIMI NIKO" lenye maana "YEYE YUKO".

**Jina langu**

Jina ambalo Mungu alimwambia Musa na wa Israeli wote kwa kutumia kwa ajili yake ni "Bwana," ambayo ni kuhusiana na "MIMI NIKO" na inaonekana kumaanisha, "NDIYE."

**Watu**

Tazama tafasiri katika [09:13](#)

## translationWords

- Musa
- Mungu
- Yaweh
- Abrahamu, Abram
- Isaka
- Yakobo, Israeli



09:15



Musa hakutaka kwenda kwa Farao kwani aliogopa, kwa sababu alihofia kutoweza kuongea vizuri. Mungu alimruhusu Haruni nduguye amsaidie. Aliwaonya kuwa Farao atakuwa na moyo mgumu.

### aliogopa na hakutaka kwenda

Musa alijua kuwa Farao alitaka kumuua na hakuamini kama ataweza kufanya mambo ambayo Mungu alitaka ayafanye.

### Kaka yake na Musa

Haruni alikua kaka yake na Musa toka kwa mama na baba wa kiisraeli. Haruni alikua na miaka mingi zaidi kuliko Musa.

### Msumbufu

Hii inamaanisha Farao alikataa kumtii Mungu. unaweza pia kuongeza "alikua msumbufu na hakukubali kusikiliza (au hakutii)"


Simulizi ya Biblia katika: Kutoka 1-4

### translationWords

- [Musa](#)
- [Farao, mfalme wa Misri.](#)
- [Mungu](#)
- [Haruni](#)

## 10. Mapigo Kumi

10:01



Watu wawili ambao ni Musa na Haruni walimwendea Farao na kumweleza kwamba, "**Mungu wa Israeli** anasema hivi, waruhusu watu wangu kuondoka katika nchi ya Misri." Farao hakukubali, alichofanya ni kuongeza uzito wa kazi kuliko hapo awali.

### Kwa Farao

Inaweza kuwa wazi kusema "kwenye nyumba ya kifalme ya Farao ili kuongea naye."

### Mungu wa Israeli

Inaweza kutafasiriwa kuwa "Mungu aliyewachagua waisraeli kuwa watu wake" au "Mungu aliyewaongoza wana wa israeli" au "Mungu anayeabudiwa na wana wa Israeli"

### Waache watu wangu waende

Njia nyingine ya kusema hivi yaweza kuwa "Waruhusu watu wangu wawe huru kuondoka" au "waachie watu wangu wawe huru kuondoka Misri"

### Kusikiliza

Hii inaweza kutafasiriwa kama "tilia maanani" au "kutii."

### translationWords

- [Musa](#)

- Haruni
- Farao, mfalme wa Misri.
- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

**10:02**

Farao aliendelea kuwakatalia Waisraeli wasiondoke, kwa sababu hiyo Mungu alileta mapigo kumi kwa Wamisri ya madhara makubwa sana. Kwa kufanya hivyo Mungu alionesha kuwa yeye anao uwezo mkubwa kuliko Farao na miungu yote ya Wamisri.

**Watu**

Hii inamaanisha watu wa Israeli pia unaweza kuwaita "waisraeli"

**Mapigo hatari kumi**

Pigo ni kitu kibaya sana au cha kutisha ambacho kinaweza kutokea kwa mtu au kwa kitu fulani. Pigo mara nyingi ni kitu ambacho kinaathiri watu wengi au eneo kubwa. Neno lingine la "pigo" laweza kuwa "majanga."

**miungu yote ya Misri**

Inaweza kuelezwa zaidi kwa kusema "miungu yote ambayo watu wa misri waliabudu" watu wa Misri waliabudu miungu mingi ya uongo. Hii miungu ya uongo ni roho ambayo Mungu wa Israeli aliziumba au hazikuwepo kabisa.

**translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Mungu
- Misri, Mmisri
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike



**10:03**

Mungu aliyabadilisha maji ya mto Naili kuwa damu. Pamoja na pigo kama hilo Farao hakutoa ruhusa kwa Waisraeli kuondoka katika nchi ya Misri.

**Akabadili mto Nile kuwa damu.**

Kwenye lugha nyingine tunaweza kusema "akabadili maji ya mto Nile kuwa damu" Badala ya maji kwenye mto kulikuwa na damu, hivyo samaki walikufa na watu walikosa maji ya kunywa.

**translationWords**

- Mungu
- Mto Nili, Mto wa Misri
- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli



**10:04**

Mungu alileta vyura kuwasumbua Wamisri wote. Farao alimwomba Musa aombe ili vyura wasiendelee kuwepo. Lakini baada ya Musa kuomba na vyura kutoweka moyo wa Farao uliendelea kuwa mgumu asiwaruhusu Waisraeli kuondoka katika nchi ya Misri.

**Mungu akatuma Vyura wengi Misri yote**

Hii inaweza kutafasiriwa kuwa "Mungu alisababisha vyura wengi sana kutokea katika maeneo yote ya Misri"

**Akaufanya Moyo wake kuwa mgumu**

Alikuwa msumbufu tena na akakataa kumtii Mungu.

**translationWords**

- Mungu
- Misri, Mmisri
- Farao, mfalme wa Misri.
- kuomba
- Musa
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

**10:05**

Kwa sababu hiyo Mungu alileta pigo la chawa. Zaidi ya hapo Mungu alileta nzi, pigo ambalo lilimfanya Farao kuwaita Musa na Haruni kuwaambia kuwa kama janga hilo wataliondoa watapewa ruhusa ya kuondoka katika nchi ya Misri. Musa alimwomba Mungu kuondoa janga la nzi na Mungu akawaondoa nzi wote. Hata hivyo moyo wa Farao ulikuwa mgumu asiwaruhusu Waisraeli kuondoka.

**Mungu alituma pigo**

Hii inaweza kutafasiriwa kuwa "Mungu alisababisha kuwepo kwa mapigo" au "Mungu alisababisha mapigo (mbu) yaje juu ya nchi ya Misri.

**Mbu**

Hawa walikuwa wadogo , wanaon'gata na kuruka katika makundi makubwa, walikuwa wakiwadhi na walitua juu ya watu na wanyama wa Misri.

**Nzi**

Hawa walikuwa wadudu wakubwa zaidi ambao walikua wanaudhi na wenye kuharibu. Walikuwa wengi sana wakafunika kilakitu ikiwemo nyumba za Wamisri.

**kuufanya moyo wake mgumu**

Angalia maelezo katika 10-4.

**translationWords**

- Mungu
- Farao, mfalme wa Misri.

- Musa
- Haruni
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Misri, Mmisri

## 10:06



Mungu alileta pigo la ugonjwa kwa mifugo wa Wamisri kwamba mifugo iliugua na kufa. Hata hivyo Farao alikuwa kaidi kuweza kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

### Wanyama wa shambani

Hii inaelezea wanyama wakubwa ambao Wana wa Israeli walitumia katika kuwasaidia kazi zao, mfano wa wanyama hao ni Farasi, punda, ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi.

### Moyo ulikua mgumu

Angalia maelezo katika 10-4.

### translationWords

- Mungu
- Misri, Mmisri
- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

**10:07**

Ndipo Mungu akamwambia Musa kupeperusha majivu angani machoni pa Farao. Majivu hayo yalisababisha majipu yenye vidonda kwa Wamisri peke yake, Waisraeli hawakudhurika na majipu hayo. Mungu alimfanya Farao kuwa na moyo wa ukaidi na hivyo hakuweza kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

**Mungu akaufanya moyo wa Farao kuwa mgumu**

Mungu akasababisha Farao akaendelea kuwa msumbufu.

**translationWords**

- Mungu
- Musa
- Farao, mfalme wa Misri.
- Misri, Mmisri
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli



**10:08**

Baada ya janga la majipu, Mungu alileta mvua ya mawe iliyo haribu mazao na kuleta maafa kwa mtu yeyote aliyenyeshewa na mvua hiyo katika nchi ya Misri. Farao alionekana kujuta aliwaita Musa na Haruni na kusema, "nimefanya dhambi," sasa nitawaruhusu kuondoka. Musa alimwomba Mungu, mvua haikuendelea kunyesha.

**Baada ya hapo**

Hii inamaanisha kuwa baada ya Mungu kusababisha maumivu ya majipu juu ya ngozi za wana wa Israeli.

**Mungu alituma mvua ya Mawe**

Mungu alisababisha mvua ya mawe kuanguka toka angani.

**Mvua ya mawe**

Mvua ya mawe ni vipande vya barafu vinavyoanguka toka kwenye anga mvua ikiwa inanyesha. Vipande hivi vinaweza kuwa vikubwa au vidogo. Vipande vikubwa vinaweza kusababisa maumivu au kuuha vikianguka.

**Ninyi mwaweza kwenda**

Neno "wewe" linamuelezea Musa, Haruni na wana wa Israeli.

**translationWords**

- Mungu
- Misri, Mmisri
- Farao, mfalme wa Misri.
- Musa
- Haruni

- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kuomba, maombi

## 10:09



Farao hata hivyo, hakuacha kutenda dhambi na moyo wake ukaendelea kuwa wenye ukaidi kwa kutowaachia uhuru Waisraeli kuondoka.

### Miyoyo migumu

Angalia maelezo katika 10-4.

### translationWords

- Farao, mfalme wa Misri.
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

## 10:10



Kwa sababu hiyo Mungu alituma nzige wengi sana walioharibu mazao yote yaliyosalia na mvua ya mawe katika nchi ya Misri

### **Kundi la nzige**

Nzige ni panzi ambao huruka kwa pamoja katika kundi au makundi makubwa na huweza kuharibu eneo kubwa la mimea na mazao ya chakula kwa kuyala.

### **Mvua ya mawe**

Mvua ya mawe ni vipande vya barafu vinavyoshuka kutoka kwenye mawingi mvua ikiwa inanyesha.

### **translationWords**

- Mungu
- Misri, Mmisri



**10:11**

Ndipo Mungu alileta giza totoro katika nchi ya Misri lililosababisha Wamisri wabakie majumbani mwao, wasitoke kwa muda wa siku tatu. Lakini mahali Waisraeli walipokuwa hapakuwa na giza.

**Mungu akatuma giza**

Mungu alisababisha giza kutanda juu ya Misri. Kwa maneno mengine Mungu aliondoa mwanga sehemu hii ya Misri.

**Giza lililodumu kwa siku tatu**

Giza hili lilikua giza nene zaidi ya giza la usiku na liliendelea kuwa giza nene kwa siku tatu.

**translationWords**

- Mungu
- Misri, Mmisri
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli



**10:12**

Ingawa kulitokea mapigo tisa Farao hakukubali kuwaruhusu Waisraeli kuondoka. Kwa kuwa Farao hangeweza kusikiliza Mungu alikusudia kuleta pigo la mwisho. Pigo hili lingemfanya Farao kubadilisha mawazo yake.

**Haya mapigo tisa**

Hii inamaanisha "majanga haya tisa ambayo yalisababishwa na Mungu"

**Kwa kuwa Farao hakisikiliza**

Hii inaweza kutafasiriwa kama "Kwa kuwa Farao hakufanya yale aliyoambiwa na Mungu ayafanye" au "kwa kuwa Farao hakumtii Mungu"

**Hii ingeweza kubadili nia ya Farao**

Njia nyingine ya kusema haya ni "Hili pigo la mwisho litamfanya Farao abadili mtazamo wake juu ya Mungu hatimaye aliwacha wana wa Israeli waende.


Simulizi ya Biblia katika: Kutoka 5-10

**translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu

## 11. Pasaka

### 11:01



Mungu alimuonya Farao ikiwa hatawaruhusu Waisraeli kuondoka, ya kuwa atawaua wazaliwa wa kwanza wote wa kiume wa watu wa Misri na wa wanyama. Baada ya kusikia hayo Farao aliendelea kutomwamini wala kumtii Mungu.

### Mzaliwa wa kwanza wa kiume wa watu na wa wanyama

Hii inaweza kutafsiriwa kama, mtoto wa kwanza kwa kila familia na mzaliwa wa kwanza wa kiume wa yeyote wa wanyama

### translationWords

- Mungu
- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kuamini, kuamini katika
- tii, mtiifu, utiifu

**11:02**

Mungu alifanya njia ya kuwaokoa wazaliwa wa kwanza wa kiume kwa yeyote atakayemwamini Yeye. Kila nyumba ya Israeli ilipaswa kuchagua mwanakondoo aliye mkamilifu na kumchinja.

**Mungu katoa**

Mungu ndie mmoja tu ambaye angeweza kutoa njia ya kuwaokoa Wana Israeli na mauti.

**Mwanakondoo mkamilifu**

Kwamba ni, Mwanakondoo au Mbuzi ambae hatalaumiwa wala kukosolewa.

**translationWords**

- Mungu
- okoa, salama
- mwana, mwana wa
- Kuamini, kuamini katika
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu

**11:03**

Mungu aliwaelekeza Waisraeli kupaka damu ya Mwanakondoo kwenye milango yao, kuichoma nyama ya Mwanakondoo na kuila kwa haraka pamoja na mikate isiyowekewa amira. Vile vile Mungu aliwaambia mara baada ya kula wawe tayari kuondoka Misri.

**Isiyotiwa chachu**

Chachu ni kitu kinachochanganywa na unga wa mkate, kinachofanya unga uumuke na pia kufanya unga kupanuka na pia kufanya unga kuinuka kuwa kama bakeri. Hii inaweza kutafsiliwa kama alifanya bila kitua ambacho kinge iinua, kufanya Mkate na chachu ingekuwa kupoteza muda mrefu, hivyo kupitia Mkate usiotiwa chachu ilikuwa njia ya yajiandaa kuondoka Misri kwa haraka.

**Wakati wakila**

Hii inamaanisha walihitaji kuwa tayari kuondoka kabla ya kuanza kula.

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu
- damu
- Misri, Mmisri



**11:04**

Waisraeli walitimiza yote waliyoagizwa na Mungu. Usiku wa manane Mungu alipita juu ya Wamisri wote na kuwaua wazaliwa wao wote wa kwanza wa kiume.

**Kila mzariwa wa kwanza**

Hii inamaanusha kila mzariwa wa kwanza kwenye familia ambae hajatoa sadaka ya damu yule ambae ni Mmisri, kufanya hii wazi unaweza ukahitaji kuongeza, "Kila mzaliwa wa kwanza wa Misri." Tangu familia zote za Israeli walipakaa damu juu ya Milango yao.

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Misri, Mmisri



**11:05**

Nyumba zote za Waisraeli zilipakwa damu katika milango yake, hivyo Mungu alipita juu ya nyumba zao. Katika nyumba hizo wote waliokolewa. Walipona kwa sababu ya damu ya Mwanakondoo.

**Alipita juu**

Hii inamaanisha kuwa Mungu alipita kila Nyumba wala hakuacha kuuu mtu yeyote huko. Msemo huu ulikuwa ni jina la Tamasha la Wayahudi yaani "Pasaka."

**Waliokolewa**


Mungu hakuwaua wazariwa wake wa kwanza.

**Kwa sababu ya damu ya Kondoo**

Hii inaweza kutafsiwa kama, "kwasababu Damu ya Kondoo ipo kwenye Milango yao," akaona ya kwamba waliwaua kondoo zao kwa amri, kwahi nae hakuwauwa watoto wao.

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- damu
- Mungu
- okoa, salama
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu

**11:06**

Wamisri hawakuamini wala kutii maelekezo ya Mungu. Hivyo basi Mungu hakupita juu ya nyumba zao. Akawauwa wazaliwa wao wa kwanza wa kiume.

**Hawakumwamini Mungu wala kutii Amri zake**

Kwa baadhi ya lugha inaweza kuwa zaidi ya asili au wazi kusema, "hawakuamini Mungu na hivyo hakuwa na kutii amri zake."

**Hakupita juu**

Naye hakupita kwenye nyumba zao, badala yake walisimama katika kila nyumba na kuwaua watoto wao wakubwa.

**translationWords**

- Misri, Mmisri
- Kuamini, kuamini katika
- Mungu

**11:07**

Kila mzaliwa wa kwanza wa kiume wa Wamisri alikufa, tangu mzaliwa wa kwanza wa aliyekuwa gerezani mpaka mzaliwa wa kiume wa kwanza wa Farao. Wengi walilia na kuomboleza kwa ajili ya huzuni kubwa iliyowapata.


**tangu mzaliwa wa kwanza wa mfungwa katika jela, hadi mzaliwa wa kwanza wa Farao**

Hii ni njia ya kusema kwamba kila mtu mzaliwa wa kwanza alikufa-kutoka mwana wa mtu angalau muhimu mwana wa mtu muhimu zaidi, na kila mtu kati yao.

**translationWords**

- Misri, Mmisri
- Farao, mfalme wa Misri.



**11:08**

Usiku ule ule, Farao aliwaita Musa na Haruni na kuwaambia, "wachukueni Waisraeli muondoke haraka." Hata Wamisri pia waliwasihi Waisraeli watoke haraka.

**walioitwa kwa ajili ya**

Hii inamaanisha kwamba Farao aliwaambia watumishi wake wamwambie Musa na Haruni waende kwake

**Akasema**

Farao akasema maneno ya fuatayo kwa Musa na Haruni baada ya wao kuja kwake. Katika baadhi ya lugha hii inaweza kutafsiriwa kama, "na akawaambia au baada ya kuja, Farao akawaambia."


Simulizi ya Biblia: Kutoka 11:1-12:32

**translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Musa
- Haruni
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Misri, Mmisri

## 12. Kutoka

### 12:01



Waisraeli walifurahia sana kutoka katika nchi ya Misri. **Hawakuwa watumwa tena.** Walikuwa wakienda katika nchi ya ahadi! Wamisri waliwapa Waisraeli chochote walichohitaji, hata dhahabu na shaba na mali zingine za thamani. Waliondoka na watu wa mataifa mengine waliomwamini Mungu wa Israeli.

### Hawakuwa watumwa tena

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "hawakuwa watumwa tena."

### Kwenda

Baadhi ya lugha hutumia baadhi ya maneno maalumu kama "kusafiri" tangu walipokuwa wakienda umbali mrefu kuelekea Nchi ya ahadi.

### Nchi ya Ahadi

Hii ni Nchi ambayo Mungu aliahidi ya kwamba atawapatia kizazi cha Ibrahimu.

### translationWords

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Misri, Mmisri
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Nchi ya ahadi
- Kuamini, kuamini katika
- Mungu



**12:02**

Mungu aliwaongoza Waisraeli kwa nguzo ya wingu iliyokuwa juu yao wakati wa mchana, ambayo wakati wa usiku ilibadilika na kuwa nguzo ya moto. Mungu alikuwa pamoja na Waisraeli na kuwaongoza. Walichopaswa kufanya ni kumfuata yeye pekee.

**Nguzo ndefu ya Wingu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "mawingu marefu" au "mawingu muundo wa nguzo."

**Nguzo ndefu ya Moto**

Hii ilikuwa safu ya moto kwamba ning'inia au pachikwa angani mbele ya Israeli.

**Aliwaongoza**

Mungu aliwaonyesha njia kwa kuweka nguzo kuelekea mbele yao ili waweze kuifuata.

**translationWords**

- Mungu

**12:03**

Baada ya kipindi kifupi Farao na washauri wake walibadili mawazo na kutaka Waisraeli wawe watumwa wao tena. Mungu aliushupaza moyo wa Farao ili kwamba watu wajue kuwa yeye ni Mungu mmoja wa kweli, na wajue kwamba yeye, Yawe, ni mwenye uwezo mkuu kuliko Farao na miungu yake.

**Baada ya muda mfupi**

Pengine angalau baada ya siku mbili walikuwa wamekwenda. Ili iweze kueleweka inaweza kutafsiriwa kama, "baada ya siku chache" au, "siku chache baada ya Waisraeli kuoindoka Misiri."

**Badilisha mawazo yake**

Msemu huu unamaanisha, "walianza kufikiri tofauti kuliko walivyokuwa kabla." Baadhi ya lugha haziwezi kuwa na maelezo ambayo hueleza hiyo maana moja kwa moja.

**translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Mungu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike

**12:04**

Kwa hiyo Farao alilituma jeshi lake ili wawafuate Waisraeli ili kusudi waendeleo kuwa watumwa wao. Na Waisraeli walipotambua kuna majeshi ya Farao yanawafuata na ya kwamba mbele yao kuna Bahari ya Shamu, mioyo yao ilijaa hofu na wakaanza kulia, "kwa nini tumetoka Misri? Tutakufa!"

**wao walikuwa wamenaswa kati ya Bahari Nyekundu**

Njia nyingine ya kusema hii itakuwa, "hapakuwa na mahali wangeweza kwenda ili kutoroka huku nyuma yao Wamisri wanawafuata na mbele yao kuna Bahari Nyekundu."

**Kwa nini tuliondoka Misri**

Hii ina maana, "Hatukupaswa kuondoka Misri!" Hawakuwa sahihi kuuliza sababu. Kwa sababu walikuwa na hofu, katika wakati huu waliamini kuwa hawataondoka Misri, (ingawa kulikuwa kugumu sana kwa wao huko).

**translationWords**

- Farao, mfalme wa Misri.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Misri, Mmisri
- Bahari ya shamu



**12:05**

Musa akawambia Waisraeli, "msiogope, kwa sababu Mungu atawapigania na kuwaokoa dhidi ya majeshi ya Farao. Kisha Mungu akamwambia Musa, waambie Waisraeli wasonge mbele kuelekea Bahari ya Shamu.

**Mungu atakupigania wewe leo na kukuokoa**

Njia nyingine ya kusema hii itakuwa, "Leo Mungu atawashindia Wamisri kwa ajili yenu, na kuwaweka ili wasiwadhuru ninyi."

**Endelea**

Baadhi ya lugha itakuwa maalum zaidi na kusema "endelea."

**translationWords**

- Musa
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- okoa, salama
- Bahari ya shamu

## 12:06



Kisha Mungu akaiweka ile nguzo ya wingu kati ya Waisraeli na Wamisri ili Wamisri wasiwaone Waisraeli.

### **Hawakuweza kuona**

Nguzo ya Wingu ilikuwa kubwa na nene kiasi kwamba Wamisri hawakuweza tena kuwaona Waisraeli. Kuona katika 12-2.

### **hakuweza kuona**

Wingu nguzo ilikuwa hivyo kubwa na nene kwamba Wamisri hakuweza tena kumuona yoyote wa Israeli.

### **translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Misri, Mmisri



**12:07**

Mungu akamwambia Musa ainue mkono wake kuelekea kwenye Bahari na kuyagawanya maji. Ndipo Mungu akaleta upepo ulio sababisha kuyatenga maji ya Bahari upande wa kushoto na upande wa kulia na kukawa na njia kubwa katikati ya Bahari.

**Aliinua mkono wake juu ya Bahari**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "alinyoosha mkono wake juu ya Bahari. Hii ilikuwa ishara ya kuonyesha kuwa Mungu alikuwa akifanya muujiza kupitia Musa.

**translationWords**

- Mungu
- Musa

**12:08**



Waisraeli walipita katika ile nchi kavu baharini wakiwa wamezungukwa na maji pande zote.

### **Walitembea**

Hii inaweza kutafsiriwa kama " walitembea" au, "walienda."

### **Na ukuta wa Maji kila upande wao**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "na maji katika pande zote yaliwazunguka yaliyosimama marefu na yaliyonyooka kama ukuta."

### **translationWords**

- [Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli](#)

**12:09**



Kisha Mungu akaiondoa ile nguzo ya wingu aliyoiweka ili kwamba Wamisri, waliokuwa wakiwafuata washuhudie vile ambavyo Waisraeli walivyokuwa wakikimbia. Wamisri wakaamua kuwafuatilia.



**12:10**

Kwa hiyo Wamisri wakawafuata Waisraeli kwa kupitia njia ile ya Bahari. Mungu akawatia hofu Wamisri na magari yao yakakwama. Ndipo Wamisri wakaambizana, "tukimbie maana Mungu anawapigania Waisraeli!"

**Katisha kwenye Bahari**

Hili lilikuwa eneo kavu la ardhi lililokata chini ya Bahari na ukuta wa maji kila upande.

**Kuwa na wasiwasi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "kupata hofu na kuchanganyikiwa."

**wakakwama**

Magari yao ya farasi hayakuweza kuendelea na safari

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Misri, Mmisri
- Gari



**12:11**

Baada ya Waisraeli wote kuvuka na kufika upande wa pili wa bahari, Mungu akamwambia Musa nyosha mkono wako tena. Alipotii, maji yalirudi kwenye sehemu yake na kuwafunika Wamisri wote waliokuwa wakiwafuatilia. Jeshi lote la Wamisri wakafa maji.

**Wakavuka salama kwenda upande mwingine**

Hii inawezakutafsiriwa kama, "walitembea salama upande wa pili" au "walifika salama upande mwingine" au "walitembea upande mwingine na walikuwa salama kutoka kwa Wamisri na Bahari."

**nyoosha mkono wake tena**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "nyoosha mkono wake kuelekea baharini tena" au "kama amri ya moja kwa moja, kama ilivyo katika "Mungu alimwambia Musa, 'Nyoosha mkono wako tena.'"

**Kurudi kwenye nafasi yake ya kawaida**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kujaza nafasi tena pale ambapo njia ilipokuwa," au "alijaza bahari yote tena" au "yalirudi kama yalivyokuwa kabla Mungu hajaigawanya."

**jeshi lote la Wamisri**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "kila mmoja katika jeshi la Misri."

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Musa

- [Misri, Mmisri](#)

## 12:12



Waisraeli walipowaona Wamisri wamekufa, walimsifu Mungu na kuamini kuwa Musa alikuwa nabii wa Mungu.

### **Kuamini katika Mungu**

Kwa maneno mengine, watu sasa waliamini kwamba Mungu ana nguvu na angeweza kuwalinda wao.

### **translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Misri, Mmisri
- Mungu
- Kuamini, kuamini katika
- Musa
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

**12:13**

Waisraeli walifurahi sana vile ambavyo Mungu alivyo waokoa **kutoka katika kifo na utumwa!** Sasa walikuwa huru kumtumikia Mungu. Waisrali waliimba nyimbo nyingi kusherehekea uhuru wao na kumsifu Mungu kwa kuwa amewaokoa kutoka majeshi ya Wamisri.

**walifurahi pamoja kwa msisimko sana**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "walikuwa na furaha na waliionesha kwa shauku," au "waliionesha kwa moyo wote" au "kwa nguvu zao zote."

**kutoka katika kifo na utumwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kutoka katika kuuliwa au kufanywa watumwa na Wamisri."

**huru kutumika**

Mungu aliwaweka huru, au aliwaokoa, Waisraeli kutoka katika hali ya kuwa watumwa katika Misri ili kwamba waweze kumtumikia.

**Mungu asifiwe**

Katika baadhi ya lugha hii inaweza kutafsiriwa kama, 'kuinua jina la Mungu' au, 'kusema kwamba Mungu ni kubwa.'

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- okoa, salama
- mtumishi, mtumwa, utumwa



- [Kusifu](#)
- [Misri, Mmisri](#)

**12:14**

Mungu aliwaamuru Waisraeli kuazimisha **Pasaka** kila mwaka **kukumbuka jinsi Mungu alivyowapa ushindi** dhidi ya Wamisri na kuwaokoa na utumwa. Walisherehekea kwa kuchinja mwanakondoo mkamilifu, na kumla pamoja na mikate isiyo na amira.

**Pasaka**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "shughuli ya Pasaka" au, "sikukuu ya Pasaka" au, "mlo wa Pasaka."

**kukumbuka jinsi Mungu alivyowapa ushindi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "mara kwa mara kujikumbusha ushindi wa Mungu." Neno 'kumbuka' hapa haina maana tu kwa kusahau; pia ina maana rasmi kuadhimisha kitu.

**Kondoo Mkamilifu**

Neno "kamili" hapa linahusu kondoo asiye na ugonjwa au kitu kingine chochote kibaya. Njia nyingine ya kusema hii inaweza kuwa, "Afya kamilifu na Kondoo aliyetakaswa."

**Mkate uliotengenezwa bila chachu**

Njia nyingine ya kusema hii ni, "Mkate usiotiwa chachu."

Simulizi ya Biblia: Kutoka:12:33-15:21

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

- Pasaka
- Misri, Mmisri
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu

## 13. Agano la Mungu na Israeli

### 13:01



Baada ya Mungu kuwaongoza wana wa Israeli kupita bahari nyekundu, aliwaongoza kupitia nyikani hadi mlima ulioitwa Sinai. Mlima huu ndio mlima Musa alikiona kichaka kilichokuwa kikiwaka moto. Watu **waliweka mahema yao** pembezoni mwa mlima.

### Kichaka kinachowaka moto

Kabla ya Musa kurudi Misri, Mungu alikuwa amesema naye kutoka kwenye kichaka kilichokuwa kikiwaka moto bila kuteketea. Kuona katika 9-12.

### waliweka mahema yao

Waisraeli walikuwa na safari ndefu kutoka Misri hadi Nchi ya Ahadi. Basi walichukua mahema pamoja nao ili waweze kuyatumia kama nyumba walalapo njiani. Baadhi ya lugha inaweza kutafsiri hii kama, "kuweka hema zao."

### chini ya mlima

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "chini ya mlima." Hii ina maana ya eneo la ardhi ambayo iko karibu na mahali ambapo ardhi huanza mshazari zaidi na kuunda mlima.

### translationWords

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Bahari ya shamu
- Sinai, Mlima Sinai



- [Musa](#)

**13:02**

Mungu akasema na Musa na wana wa Israeli, "kama mtanitii na kulishika agano langu mtakuwa miliki yangu ya thamani, Makuhani wa Kifalme na taifa takatifu."

**tunza Agano langu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kufanya kile ambacho agano linahitaji ufanye." Kutii na kushika agano si mambo mawili tofauti. Moja ya njia ya kufanya liwe wazi itakuwa kusema, "munitii kwa kushika agano langu."

**Miliki yangu ya thamani**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Wewe utakuwa miliki yangu yenye thamani zaidi" au, "utakuwa mtu ninaemtegemea zaidi kuliko kundi la watu wengine" au, "mtakuwa watu wangu wenyewe thamani."

**Utakuwa ufalme wa Makuhani**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Mimi nitakuwa mfalme wako na utakuwa kama kuhani.' Waisraeli walipaswa kuwafundisha mataifa mengine kuhusu Mungu na kuwa mpatanishi kati ya Mungu na mataifa. Kama ilivyokuwa kwa makuhani katika taifa la Israeli kwenda kati ya Mungu na Israeli.

**translationWords**

- Mungu
- Musa
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- tii, mtiifu, utiifu
- Agano
- ufalme
- Kuhani, ukuhani
- takatifu, utakatifu

**13:03**

Baada ya siku tatu, watu walipokuwa wamejiandaa kiroho, Mungu alishuka juu ya mlima Sinai kwa ngurumo na radi, moshi na sauti ya mvumo wa tarumbeta. Musa peke yake aliruhusiwa kupanda mlimani.

**Siku tatu baadae**

Kwa maneno mengine, siku tatu baada ya kufika katika Mlima Sinai na Mungu kwanza alizungumza nao.

**wakajiweka tayari kiroho**

Hii inahusu utakaso wa kisherehe katika maandalizi ya kukutana Mungu. Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'kuwa tayari kukutana Mungu' au, 'wajiandae wenyewe kukutana Mungu.'

**Sauti kubwa ya Tarumbeta**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'na sauti kubwa ilikuja kutoka pembe' au, 'na pembe ilipopigwa na ilifanya sauti kubwa' au, 'na waliposikia sauti kubwa ya mbiu.' Baragumu iliyotengenezwa na pembe za kondoo dume. Wataitumia siku hiyo kuwaita watu kukusanyika katika mlima na kukutana na Mungu.

**Musa tu aliruhusiwa kwenda juu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Mungu alimruhusu Musa kwenda juu Mlimani, lakini hakutoa kibali kwa mtu mwingine yeyote kwenda huko.

**translationWords**

- [Mungu](#)
- [Sinai, Mlima Sinai](#)
- [Musa](#)

**13:04**

Kisha Mungu aliwapa Agano akisema, "Mimi ni Yawe, Mungu wako **aliyekuokoa kutoka utumwani** Misri. Msiabudu miungu mingine."

**Kisha Mungu akawapa Agano na kusema**

Anachosema Mungu hapa ni muktadha wa agano, yaani, anawaambia watu mambo ambayo ni lazima kutii. Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Kisha Mungu aliwaambia ahadi yake. Alisema 'au,' Mungu akafanya agano hili pamoja nao '

**Yahweh, Mungu wako**

Katika lughanyingine inaweza kuwa zaidi ya asili kubadili utaratibu na kusema 'Mungu wenu Bwana.' Kuhakikisha haifanani kama Waisraeli walikuwa na zaidi ya Mungu moja. Ni lazima kuwa wazi kuwa Bwana ni Mungu pekee. Njia nyingine ya kutafsiri hii itakuwa, Bwana, ni nani aliye Mungu wako 'au,' Mungu wako, ambaye jina lake ni Bwana. '

**aliyekuokoa kutoka utumwani**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Mimi nimekombolewa kutoka utumwani

**translationWords**

- Mungu
- Agano
- Yaweh
- okoa, salama
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Misri, Mmisri
- Abudu



- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike

**13:05**

"Usijifanyie sanamu ya kuchonga wala usiabu, kwa sababu mimi Yawe ni Mungu mwenye wivu. Msilitaje bure jina la Bwana Mungu. Ikumbukeni siku ya sabato na kuitakasa. Kwa maneno mengine, fanya kazi kwa siku sita na siku ya saba ni sabato ya kupumzika kunikumbuka mimi."

**Mimi, Bwana, ni Mungu mwenye wivu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Mimi, Bwana, huwa na hasira kama wewe unaabudu au unaheshimu jambo lolote zaidi yangu mimi. Mungu anataka sana watu wake kumpenda, kumtumikia, na kumtii zaidi kuliko kitu chochote au mtu mwingine. Ni lazima awe bwana pekee juu ya maisha yao.

**Usilitumie jina langu kwa namna isiyofaa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Je, si majadiliano juu yangu katika njia ambayo haina kuonyesha heshima na heshima' au, 'Msiongee juu yangu kwa njia isiyo ya heshima na adabu'

**Siku ya Saba**

kutafsiri hii, ni bora kutumia idadi ( 'saba') badala ya kutoa jina la siku maalum ya wiki.

**Ili unikumbuke**

Hili linaweza kutafsiriwa kama, ' niweke akili' au, 'kwa heshima yangu.

**translationWords**

- [mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike](#)
- [Abudu](#)
- [Yaweh](#)

- Mungu
- Sabato
- takatifu, utakatifu

**13:06**

Waheshimu Baba yako na Mama yako, usiue, usizini, usiibe., usiseme uongo, usimtamani mke wa jirani yako, nyumba yake au chochote kilicho chini ya milki yake.

**Usizini**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Usifanye mahusiano ya uzinzi na mke wa mtu mwingine" au, "Usiwe na mahusiano ya ndoa na mke wa mtu mwingine au mume wa mwanamke mwingine" Kuwa na uhakika wa kutafsiri ili katika njia ambayo haiwezi kuwakosea au kuwaaibisha watu. Lugha mara nyingi inatafsida, tumia njia ya heshima katika kusema ili, kama vile, "Usilale na"

**Usidanganye**

Hii inamaanisha, "Usisema mambo ya uongo kuhusu watu wengine".

**translationWords**

- Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi



**13:07**

Ndipo Mungu akaandika amri kumi katika mbao mbili za mawe akampa Musa. Vilevile Mungu alitoa sheria na amri nyingi na miongozo ya kufuata. Ikiwa watu wataziti sheria hizo, Mungu aliwaahidi kuwalinda na kuwabariki. Kama hawatamtii, Mungu angewaadhibu.

**Amri hizi kumi**

Hii ina maana ya amri za Mungu alizompa Musa kwa ajili ya Waisraeli kutii. Zimeorodheshwa kwenye Ubao.

**Mbao za mawe**

Hivi vilikuwa vipande bapa vya mawe

**Mungu aliwapa pia**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "Hata hivyo Mungu aliwaambia."

**Kufuata**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "Kwamba ni lazima kutii" au, 'kwamba ni lazima kuweka."

**translationWords**

- Mungu
- Amri kumi
- Musa
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe
- tii, mtiifu, utiifu
- Ahadi

- Kubariki
- totii, mkaidi, kutotii
- Kuadhibu, adhabu

**13:08**

Mungu aliwapa Waisraeli maelekezo ya kina ya namna hema alivyota liwe. liliitwa hema la kukutania, na lilikuwa na vyumba viwili vilivyogawanywa kwa pazia kubwa. Kuhani Mkuu peke yake aliruhusiwa kuingia kwenye chumba nyuma ya pazia. Kwa sababu Mungu aliishi humo.

**Maelezo ya kina**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "Mungu alieleza kwa undani" au, "Mungu aliwaambia hasa jinsi gani aliwataka kufanya hivyo."

**Liliitwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "Waliitwa hivyo" au, "Musa alitwa hivyo."

**Chumba nyuma ya Pazia**

Hiki chumba kilizibwa kwa pazia. Baadhi ya lugha hukiita chumba hiki, "chumba mbele ya pazia."

**Mungu aliishi pale**

Kama msemo huu ungeweza kusababisha watu kufikiri kwamba Mungu alikuwa mdogo anaeweza kuishi kwenye hema, hapa kuna baadhi ya njia za kutafsiri "Mungu alikuwa pale" au, "Mungu alijifunua kwa wanadamu pale."

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- hema la kukutania
- kuhani mkuu

**13:09**

Kila ambaye hakuzitii sheria za Mungu, alipaswa kuleta mnyama kwenye madhabahu mbele ya hema ya kukutania kama dhabihu kwa Mungu. Kuhani alimchinja huyo mnyama na kumteketeza juu ya madhabahu. Damu ya mnyama huyo ilikuwa dhabihu ya kufunika dhambi za mtu na kuwa safi machoni pa Mungu. Mungu alimchagua Haruni ndugu yake na Musa na uzao wa Haruni kuwa Makuhani.

**Sheria za Mungu**

Hii hurejea kwenye amri zote na maelekezo ambayo Mungu aliwaambia Waisraeli kutii

**kwenye Hema la Kukutania**

Hawakuleta mnyama ndani ya Hema la Kukutania, bali kwenye madhabahu mbele ya Hema la Kukutania. Kwa hakika usitumie kielelezo kinachomaanisha kwamba walileta

**ilifunika dhambi ya mtu**

Wakati watu walipoleta wanyama kutoa dhabihu Mungu alichagua kuona damu ya wanyama kama kifuniko juu ya dhambi zao. Hii ni kama kuficha kitu ambacho ni kibaya au kichafu kwa kukifunika.

**safi mbele za Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa kwamba, "kama kwamba hakuwa na dhambi kulingana na mtazamo wa Mungu" au "kutokuhukumiwa kwa kuvunja sheria za Mungu"

**translationWords**

- totii, mkaidi, kutotii
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe

- hema la kukutania
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- Kuhani, ukuhani
- Madhabahu
- damu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Musa
- Haruni
- uzao, kutokana na



**13:10**

Watu walikubali kutii sheria ambazo Mungu aliwapa, kumwabudu Mungu pekee na kuwa **watu wake maalumu**. Lakini **muda mfupi** baada ya kuahidi kumtii Mungu, walimwasi vibaya sana.

**wapatie**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'amewaambia kutii.'

**watu wake maalumu**

Kutoka katika mataifa yote, Mungu ameamua kuichagua Israeli kwa kusudi lake maalum. Hii inaweza kutafsiriwa kwamba 'taifa lake maalum' au, 'watu wake mwenyewe' au, 'taifa alichagua kuwa watu wake.'

**muda mfupi**

Watu walitenda dhambi wakati wa siku arobaini ambazo Musa alikuwa mlimani na Mungu.

**walitenda dhambi sana**

Walifanya dhambi kwa njia ambayo ilikuwa chukizo kwa Mungu. Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'wao walitenda dhambi vibaya sana,' au 'walivyofanya kitu ambacho kilikuwa kibaya sana' au, 'walivyofanya kitu kibaya kilimfanya Mungu kuwa na hasira.'

**translationWords**

- tii, mtiifu, utiifu
- Mungu
- Abudu
- Ahadi

- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**13:11**

Kwa siku nyingi, Musa alikuwa juu ya mlima Sinai akizungumza na Mungu. Watu walichoka kumsubiri alipokawia kurudi. Kwa hiyo walimletea Haruni dhahabu na kumtaka awatengenezee sanamu kwa ajili yao!

**Watu walichoka kusubiri**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'watu walihuzunika kwa sababu hakurudi haraka' au, 'watu hawakutaka kusubiri tena kumsubiria arudi.'

**alileta dhahabu**

Hivi vilikuwa vitu na vitu vilivyotengenezwa kwa dhahabu, ambavyo vinaweza kuyeyushwa na kutengeneza vitu vingine

**translationWords**

- Musa
- Sinai, Mlima Sinai
- Mungu
- Haruni
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike

**13:12**

Haruni alitengeneza sanamu ya dhahabu kwa sura ya ndama. Watu walianza kuiabudu sanamu ya dhahabu nyikani na kutoa dhabihu juu yake. Mungu aliwakasirikia kwa sababu ya dhambi yao na kupanga kuwaangamiza. Bali Musa aliwaombea, na Mungu akasiliza maombi yake na kutokuwaangamiza.

**alifanya sanamu ya dhahabu**

Haruni alichukua vitu vilivyotengenezwa kwa dhahabu ambavyo watu walikuwa wakivileta kwake, aliviyusha pamoja navyo na kuvitengeneza katika sura ya ndama.

**ibada ya kishenzi**

watu walikuwa wakifanya dhambi kwa kuabudu sanamu na pia kwa kufanya mambo ya dhambi walipokuwa wakiabudu.

**alisikia maombi yake**

Mungu daima anasikia maombi. Katika hali hii, 'alisikia' maana yake ni kwamba Mungu alikubali kufanya kile ambacho Musa aliuliza.

**translationWords**

- Haruni
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Abudu
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Musa
- Kuomba, maombi

## 13:13



Musa aliposhuka mlimani na kuiona hiyo sanamu alikasirika sana akazivunja hizo mbao za mawe zilizoandikwa amri kumi za Mungu.

### **kuvunja Mawe**

Yeye alirusha mawe chini ya ardhi na wao kuyavunja katika vipande kidogo.

### **translationWords**

- Musa
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Mungu
- Amri kumi



## 13:14



Musa aliisagasaga sanamu na kuwa unga na kuutupa huo unga katika maji na watu kunywa hayo maji . Mungu alituma **pigo** kwa watu na wengi wao walikufa.

### **alizivunja sanamu kuwa kama unga**

Musa akaziangamiza hizo sanamu kwa kuziponda katika vipande vidogo vidogo.

### **ndani ya kiasi cha maji**

Musa akatawanya unga wa dhahabu juu ya maji mengi.

### **pigo**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'ugonjwa wa kutisha.'

### **translationWords**

- Musa
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Mungu

**13:15**

Musa alitengeneza mbao mpya za mawe za amri kumi za Mungu sawa na zile za kwanza zilizovunjika. Kisha alipanda tena mlimani na kuomba kwamba awasamehe hao watu. Musa alishuka mlimani na hizo mbao mpya za mawe zilizoandikwa amri kumi za Mungu. Kisha Mungu aliwaongoza Waisraeli kutoka mlima Sinai kuelekea nchi ya ahadi.

**Musa akatengeneza**

Musa alichonga mbao za mawe kwa zana kama vile nyundo na patasi.

**alimsikiliza**

Ona ni jinsi msemu huu ulivyotafsiriwa katika 13-12.

Simulizi ya Biblia: Kutoka 19-34

**translationWords**

- [Musa](#)
- [Kuomba, maombi](#)
- [Mungu](#)
- [samehe, kusamehe](#)
- [Amri kumi](#)
- [Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli](#)
- [Sinai, Mlima Sinai](#)
- [Nchi ya ahadi](#)

## 14. Kuzunguka Jangwani

14:01



Mungu alipokwisha kuwaambia Waisraeli sheria ambazo alitaka wazitii kama sehemu ya Agano lake na wao, walitoka Mlima Sinai. Mungu alianza kuwaongoza kuelekea Nchi ya Ahadi iliyoitwa Kanaani. Nguzo ya wingu ilikwenda mbele yao ikiwangoza kwenda Kanaani na wao waliifuata.

### nguzo ya Wingu

Ona ni jinsi gani unaweza kutafsiriwa huu msemo katika (12-1)

### translationWords

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Agano
- Sinai, Mlima Sinai
- Nchi ya ahadi
- Kanaani, Mkanaani

**14:02**

Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo kwamba atawapa wazao wao nchi ya ahadi, lakini wakati huo kulikuwa na makundi ya watu wengi waliokuwa wakiishi humo. Walikuwa wakiitwa Wakanaani. Wakanaani hawakumwamini wala kumtii Mungu. Waliabudu miungu yao ya uongo na walifanya maovu mengi.



**14:03**

Mungu aliwaambia Waisraeli, "Lazima muwaangamize Wakanaani wote kabisa katika Nchi ya Ahadi. Msifanye amani nao wala **msioane nao**. Lazima muangamize kabisa miungu yao. Iwapo hamnitii mimi, **mtaabudu miungu yao!**"

**Ondoa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'wapate kutoka nje ya nchi' au, 'kuwaondoa wao kwenye nchi.

**msifanye amani pamoja nao**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Msiishi kwa amani miongoni mwao au pamoja nao" au, " hakuahidi kuishi kwa amani pamoja nao".

**msioane nao**

Mungu hakutaka mtu yeyote wa Israeli kuoana na Mkanaani.

**mtaabudu miungu yao**


Kama Waisraeli wakiwa marafiki na Wakanaani na hawakuharibu sanamu zao, wataweza kujaribiwa na kuabudu sanamu badala ya Mungu. Unaweza kusema, "itakuwa mwisho wao kuabudu" ili kuweka wazi kwamba hii itapelekea au itasababishwa na kuishi karibu na Wakanaani na kujifunza njia zao.

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kanaani, Mkanaani



- Nchi ya ahadi
- Amani
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- tii, mtiifu, utiifu
- Abudu

**14:04**

Waisraeli walipofika mpakani mwa Kanaani, Musa alichagua wanaume kumi na wawili, mmoja kutoka kila kabila la Israeli. Aliwapa maelekezo ya kwenda kuipeleleza nchi kuona ilivyo. Walipaswa pia kuwachunguza wakanaani kuona kama ni wenye nguvu au dhaifu.

**kupeleleza Nchi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kwa siri kupata taarifa kuhusu nchi" au, "siri kujifunza kuhusu nchi". Sehemu ya kazi ya wapelelezi ilikuwa kujua ni aina gani ya chakula nchi inaweza kuzalisha.

**peleleza Kanaani**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kwa siri kupata taarifa kuhusu watu wa Kanaani" au, kwa siri kujifunza kuhusu Wakanaani".

**ili kuona kama walikuwa na nguvu au dhaifu**

Walitaka kujua kama Wakanaani wamejiandaa kupigana nao. Hii inaweza kutafsiriwa kama, "ili kujua ni nguvu ya kiasi gani majeshi ya Mkanaani walikuwa nayo"

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kanaani, Mkanaani
- Musa

**14:05**

Wale wanaume kumi na wawili walisafiri ndani ya nchi ya Kanaani kwa muda wa siku arobaini na baadaye walirejea. Waliwaambia watu, "Nchi ina rutuba sana na ina mazao kwa wingi." Lakini wapelelezi kumi walisema, "Miji ni imara sana na watu wake ni wenye miraba minne." Kama tutapigana nao, watatushinda na kutuua."

**walirudi**

Walirudi ambapo wengine wa Waisraeli walikuwa wakisubiri nje kidogo ya mpaka wa Kanani.

**Miji ina nguvu sana**

mji ulikuwa na ukuta imara unaoizunguka, hivyo itakuwa vigumu sana kwa Waisraeli kuwashambulia

**watu wana maumbo makubwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "watu ni kama majitu ukilinganisha na sisi!" au, "watu ni warefu sana na wenye nguvu kuliko tulivyo!"

**translationWords**

- [Kanaani, Mkanaani](#)

**14:06**

Hapo hapo, Kalebu na Yoshua, wapelelezi wengine wawili walisema, "Ni kweli kwamba **watu wa Kanaani** ni warefu na wenye nguvu lakini kwa hakika tunaweza kuwashinda! **Mungu atatupigania!**"

**watu wa Kanaani**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "watu ambao wanaishi Kanaani" au, "Wakanaani."

**kwa hakika tutashinda.! Mungu atatupigania**

Kuonyesha uhusiano kati ya kauli hizi mbili, inaweza kuwa muhimu kusema, 'kwa hakika tunaweza kuwashinda kwa sababu Mungu atatupigania!'


**Mungu atatupigania**

Hii inaweza kutafsiriwa kama: "Mungu atapambana pamoja nasi na kutusaidia kuwashinda wao! ' Hii inaonesha wazi kwamba Waisraeli pia watapigana dhidi ya Wakanaani.

**translationWords**

- Kalebu
- Yoshua
- Kanaani, Mkanaani
- Mungu



**14:07**

Lakini watu hawakuwasikiliza Kalebu na Yoshua. Walimkasirikia Musa na Haruni na kusema, "Kwa nini umetuleta sehemu hii hatari? Tulipaswa kubaki Misri badala ya kuuawa vitani na wake zetu na watoto kufanywa watumwa." Watu walitaka kuchagua kiongozi mpya awarudishe Misri.

**kwa nini ulituleta sisi**

Hili sio swali halisi. Ni njia kwamba baadhi ya lugha hutumia kusema, 'hukupaswa kutuleta sisi.'

**mahali hapa pa ovyo**

Wao waliichukulia Kanaani kuwa 'ovyo' kwa sababu wao walidhani ilikuwa hatari kwamba wangeweza wote kuuawa.


**badala ya kuuawa katika vita na wake zetu na watoto kufanywa watumwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Kama sisi tukipigana na hao Wakanaani, na kutuua wanaume na kuwalazimisha wake zetu na watoto kuwa watumwa wao.'

**translationWords**

- Kalebu
- Yoshua
- Musa
- Haruni
- Misri, Mmisri
- mtumishi, mtumwa, utumwa



**14:08**

Mungu alikasirika sana na akaja kwenye hema la kukutania. Mungu akasema, "Kwa sababu mmeniasi mimi, watu wote mtazunguka jangwani. Isipokuwa Yoshua na Kaleb, kila mmoja aliye na miaka ishirini au zaidi atafia humo na kamwe hataingia katika nchi ya ahadi.

**alikuja**

Mungu hakuonekana kama mtu, lakini alikuja kwa njia nyingine ambayo ilioesha utukufu wake na nguvu.

**Kutangatanga Jangwani**

Mungu angeweza kuwaongoza watu katika jangwa bila mwelekeo maalumu mpaka watu wazima ambao walimwasi wafe.

**translationWords**

- Mungu
- hema la kukutania
- Yoshua
- Kaleb
- Nchi ya ahadi

**14:09**

Mara watu waliposikia hivyo, walisikitika kwamba wametenda dhambi. Walichukua silaha zao na kwenda kuwavamia Wakanaani. Musa aliwaonya wasiende kwa sababu **Mungu hakuwa pamoja nao**, lakini wao hawakumsikiliza.

**walitenda Dhambi**

Inaweza kuwa muhimu kuongeza, 'walikuwa wamefanya dhambi kwa kutotii amri za Mungu za kuwashinda watu wa Kanaani.'

**Musa aliwaonya wao wasiende**

Hii ina maana kwamba Musa aliwaambia wasiende kupigana na Wakanaani kwasababu wangukuwa katika hatari kama wamefanya hivyo.

**Mungu hakuwa pamoja nao**

Kwa maneno mengine, Mungu hakuwa pamoja nao ili kuwasaidia. Kwa sababu ya kutotii kwao, Mungu aliwaacha Waisraeli bila uwepo wake, ulinzi na nguvu.

**lakini hawakutaka kumsikiliza**


Hawakumtii Musa. Wakaenda kuwashambulia Wakanaani.

**translationWords**

- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kanaani, Mkanaani
- Musa

- [Mungu](#)

## 14:10



Mungu hakwenda nao katika vita hivi, kwa hiyo walishindwa vitani na wengi wao waliuawa. Kisha Waisraeli walirudi kutoka Kanaani nao wakazunguka jangwani kwa miaka arobaini.

### **Mungu hakuenenda pamoja nao katika vita hii**

Kwa maneno mengine, Mungu hakuwasaidia katika vita hii.

### **wakarudi kutoka Kanaani**

Waliondoka Kanaani na kurudi nyikani ambapo walikuwako kabla.


### **walitangatanga Jangwani**

Waliishi katika jangwa, na kwa pamoja walisogea kutoka sehemu moja hadi nyingine , ardhi kavu, kutafuta chakula na maji kwa ajili yao wenyewe na wanyama wao.

### **translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kanaani, Mkanaani



**14:11**

Kwa kipindi cha miaka arobaini Waisraeli walizunguka jangwani, Mungu aliwapa mahitaji. Aliwapa mkate kutoka mbinguni, ulioitwa, "mana." Pia aliwatumia kware (ambao ni ndege wa umbo la kati) katika kambi zao ili wapate nyama ya kula. Kwa muda wote huo, Mungu alitunza nguo zao na viatu vyao visiharibike.

**Mungu aliwahudumia**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Mungu aliwapa kila kitu walichohitaji kwa chakula, maji, na maladhi.'

**mkate kutoka mbinguni, ulioitwa 'mana'**

Hiki ni chakula aina ya mkate mwembamba ulishuka kutoka mbinguni mara moja kwenye majani kama umande. Uliitwa 'mana'. Karibu kila siku watu waliipata hii 'mana' na kuipika kama chakula chao.

**Pia alituma makundi ya kware**

Njia nyingine ya kusema hii itakuwa, 'Yeye pia alisababishwa idadi kubwa ya kware kuruka katika kambi yao.' Kama kware ni hawajulikani, tumia neno tofauti sawa na aina ya ndege inayoweza kutumika. Au inaweza kutafsiriwa kama, 'idadi kubwa ya ndege.'

**Kambi yao**

mahali ambapo Waisraeli waliweka hema zao kulala paliitwa 'kambi'. Ilikuwa ni kama mji na mahema badala ya majengo.

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu



**14:12**

Mungu kwa miujiza aliwapa maji kutoka katika mwamba. Lakini pamoja na hayo yote, Waisraeli walimlalamikia na kumnung'unikia Mungu. **Hata hivyo**, Mungu alikuwa mwaminifu kutunza ahadi zake kwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo.

**kimiujiza akawapa maji kutoka kwenye mwamba**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'kwa kufanya kitu ambacho Mungu tu anaweza kufanya, alifanya maji kumwagika kutoka kwenye mwamba hivyo watu na wanyama wakaweza kunywa.'

**Lakini pamoja na yote hayo**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Lakini, hata kama Mungu aliwapatia chakula, maji, mavazi, na kila kitu ambacho walihitaji.'

**Hata hivyo**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Japokuwa Waisraeli walilalamika na kunung'unika dhidi yake.'

**Mungu bado alikuwa mwaminifu kwa ahadi zake**

Hii inaweza kutafsiriwa hivi, 'Mungu aliendelea kufanya kama alivyomwambia Abrahamu, Isaka na Yakobo kuwa angefanya.' Alitoa kiza chao kama walivyohitaji hivyo kwamba wanaweza kuishi na kuwa taifa kubwa na hatimaye kumiliki nchi ya Kanaani.

**translationWords**

- [Mungu](#)
- [Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli](#)

- Musa
- mwaminifu, uaminifu
- Ahadi
- Abrahamu, Abram
- Isaka
- Yakobo, Israeli

**14:13**

Wakati mwingine watu walipokuwa hawana maji yoyote, Mungu alimwambia Musa, "Uambie mwamba, na maji yatatoka humo." Lakini **Musa hakumheshimu Mungu** mbele ya watu wote kwa kuupiga mwamba mara mbili kwa fimbo badala ya kuuambia. Maji yalitoka katika mwamba kwa ajili ya kila mmoja kunywa, lakini Mungu alimkasirikia Musa na kusema, "Hutaingia katika nchi ya ahadi."

**Musa hakumheshimu Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa, 'Musa kutomtii Mungu' au, 'Musa kutomheshimu Mungu.' Mungu alikuwa na njia maalumu ambayo alitaka Musa kuonesha watu uwezo wa Mungu kwa ajili yao. Wakati Musa akiacha kumtii Mungu kwa kufanya hivyo kwa njia tofauti alionyesha ukosefu wa hesima kwa Mungu.

**kwa kupiga mwamba mara mbili kwa fimbo baaada ya kuzungumza nao.**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, 'Musa hakuongea na mwamba; yeye aliupiga mara mbili kwa fimbo.'

**translationWords**

- [Mungu](#)
- [Musa](#)
- [Nchi ya ahadi](#)

**14:14**

Baada ya Waisraeli kuzunguka jangwani kwa miaka arobaini, wale waliokuwa wamemwasi Mungu walikwishakufa. Kisha Mungu aliwaongoza **watu** hadi mpakani mwa nchi ya ahadi tena. Musa alikuwa mzee sana, hivyo Mungu alimchagua Yoshua kumsaidia kuongoza watu. Mungu pia alimwahidi Musa siku ile, kwamba atamtuma nabii mwingine kama Musa.

**waliokuwa wameasi dhidi ya Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "ambaye alikataa kumtii Mungu alipowaambia waende katika nchi ya ahadi".

**watu**

Yaani, watoto wa kizazi kilichokufa.

**siku moja**

Hii ina maana, 'wakati fulani katika siku zijazo.'

**Nabii mwingine kama Musa**

Kama Musa, mtu huyu atakuwa Muisraeli, atakayeweza kusema maneno ya Mungu kwa watu, nae ataweza kuwaongoza watu.

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Waasi, uasi.
- Mungu
- Nchi ya ahadi

- Musa
- Yoshua
- Ahadi
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.



**14:15**

Kisha Mungu alimwambia Musa kwenda juu ya kilele cha mlima ili aione nchi ya ahadi. Musa aliiona nchi ya ahadi lakini Mungu hakumruhusu kuiingia. Kisha Musa alikufa, na Waisraeli walimwombolezea kwa siku thelathini. Yoshua akawa kiongozi wao. Yoshua alikuwa kiongozi mzuri kwa sababu alimtegemea na kumtii Mungu.

**waliomboleza kwa siku thelathini**

Kwa muda wa siku thelathini watu wote wa Israeli wilia na kuonesha kuwa walikuwa wakisikitika sana kwamba Musa alikuwa amekufa.

Simulizi ya Biblia Kutoka: Waamuzi 16-17; Hesabu 10-14; 20; 27; Kumbukumbu la Torati 34

**translationWords**

- Mungu
- Musa
- Nchi ya ahadi
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Yoshua
- imani, aminifu,
- tii, mtiifu, utiifu

## 15. Nchi ya Ahadi

### 15:01



Hatimaye wana Israeli wanaingia Kaanani, nchi ya ahadi. Yoshua akatuma wapelelezi wawili Yeriko, mji wa wakaanani ambao ulikua ukilindwa kwa kuta zenye nguvu. Ndani ya mji kulikua na Rahabu, kahaba akiishi na ambaye aliwaficha wapelelezi, baadae akawasaidia kutoroka. Aliwaficha sababu alimwamini Mungu. Wapelelezi walihaidi kumlinda Rahabu na **familia yake** wakati Waisraeli watakapokuja kuangamiza Yeriko.

### Hatimaye ulifika wakati wa

"Hatimaye" inamaanisha "Mwishowe" au "baada ya kungoja kwa muda mrefu."

### Wapelelezi wawili kwenda Yeriko mji wa Kanaani

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "watu wawili kwenda Yeriko, mji wa kanaani, kutafuta habari za mji huo."

### umelindwa kwa kuta imara

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "umelindwa kwa kuta nene, imara zilizojengwa kwa mawe kuwakinga dhidi ya adui zao."

### toroka

Ni sawa pia kuongeza, "toroka kutoka kwa watu ambao walitaka kuwadhuru huko Yeriko."

## **familia yake**

Rahabu aliomba ulinzi kwa kwa ajili ya baba, mama, kaka, na dada zake. Tumia neno katika lugha yako ambalo linajumuisha watu hawa.

## **translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kanaani, Mkanaani
- Nchi ya ahadi
- Yoshua
- Yeriko
- Rahabu
- Kuamini, kuamini katika
- Mungu
- Ahadi

**15:02**

Waisraeli walipaswa kuvuka mto Yordani walipotaka kwenda kwenye nchi ya ahadi. Mungu akamwambia Yoshua, "**Makuhani waanze kwenda kwanza**". Wakati makuhani walipoanza kupiga hatua kwenye mto Yordani, mkondo ukasimama kutiririsha maji na Waisraeli wakaweza kuvuka mto kwenye ardhi kavu na kwenda upande wa pili.

**Makuhani waanze kwenda kwanza**

kwa baadhi ya lugha inaweza kusaidia ukiongeza, "Waache Makuhani watangulie kuvuka mto kwanza kabla ya watu wengine."

**mkondo wa maji ukasimama kutiririsha maji**

Kwa baadhi ya lugha inaweza kusaidia ukiongeza, "na maji yaliyokuwa mbele yao yalitiririka kwenye chini."

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mto Yordani, Yordani
- Nchi ya ahadi
- Mungu
- Yoshua
- Kuhani, ukuhani



**15:03**

Baada ya kuvuka mto Yordani, Mungu akamwambia Yoshua jinsi ya kuuvamia mji wenye nguvu wa Yeriko. Watu wakamtii Mungu. Kama ambavyo Mungu alivyowaambia, kwa wanajeshi na makuhani kuuzunguka mji wa Yeriko mara moja kwa siku sita.

**Baada ya watu kuvuka mto Yorodani**

Kwa baadhi ya lugha ni vyema kusema, "Watu walivuka mto Yorodani na kisha..."

**jinsi ya kuvamia**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "uhalisia wa namna ambavyo angefanya ili kuvamia."

**mara moja kila siku kwa muda wa siku saba**


Hii ni kwamba, waliuzunguka mji mara moja kila siku kwa muda wa siku saba.

**translationWords**

- Mto Yordani, Yordani
- Mungu
- Yoshua
- Yeriko
- tii, mtiifu, utiifu
- Kuhani, ukuhani



## 15:04



Na katika siku ya saba, Waisraeli wakauzunguka mji kwa mara saba zaidi. Wakati walipokua wakiuzunguka mji kwa mara ya mwisho, wanajeshi wakapiga kelele ilihali makuhani **walipuliza tarumbeta zao**.

### **wakati walipotembea kuuzunguka mji kwa mara ya mwisho**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "Wakati wa mzunguko wao wa mwisho kwenye mji ule."

### **walipuliza tarumbeta zao**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "Walipiga tarumbeta zao" au, "walicheza tarumbeta zao."

### **translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kuhani, ukuhani

**15:05**

Tena kuta za Yeriko zikaanguka chini! Waisraeli waliharibu kila kitu kilichokuepo ndani ya mji kama Mungu alivyoamuru. Walimwacha Rahabupeke yake na familia yake, ambaye alifanyika kua sehemu ya Waisraeli. Na watu wengine waliokua wakiishi katika nchi ya Kanaan waliposikia Waisraeli wameuharibu mji wa Yeriko, waliogopeshwa maana Waisraeli wangewavamia wao pia.

**alifanyika kuwa sehemu ya**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "ambao baadaye waliungana na jamii ya Israeli" au, "ambaye baadaye walifanyika kuwa sehemu ya taifa la Israeli."

**translationWords**

- Yeriko
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Rahabu
- Kanaani, Mkanaani

**15:06**

Mungu akawamuru waisraeli kutokufanya **makubaliano ya amani** na makundi yoyote ya watu katika nchi ya Kanaanani. Lakini kundi moja la wakaanani, lililoitwa Wagibeoni, walimdanganya Yoshua na wakasema wametoka mbali na nchi ya Kanaanani. Wakamuuliza Yoshua kufanya makubaliano ya amani na wao. Yoshua na Waisraeli hawakumuuliza Mungu kuwa **ni wapi Wagibeoni wametokea**. Yoshua akafanya makubaliano ya amani nao.

**makubaliano ya amani**

Haya ni makubaliano baina ya makundi mawili ya watu kwamba wataishi kwa amani.

**Lakini kundi moja la Wakanaani lililoitwa Wagibeoni**

Baadhi ya lugha zinaweza kuanza na, "Lakini siku moja kundi moja la Wakanaani waitwao Wagibeoni..."

**walimdanganya Yoshua wakisema**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "Walimdanganya Yoshua kwa kusema..."

**ni wapi Wagibeoni wametokea**


Kwamba, "Wagibeoni walikoishi" au, "yalipokuwa makao ya Wagibeoni."

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Amani
- Kanaani, Mkanaani
- Gibeoni. Wagibeoni

- [Yoshua](#)



**15:07**

Waisraeli waliingiwa na hasira pale walipogundua wamedanganywa na Wagibeoni, lakini waliamua kutunza makubaliano ya amani nao kwa sababu ilikua ahadi mbele za Mungu. Lakina baadae mfalme mwingine wa kundi lingine la watu katika Kanaan, wa Waamori, aliposikia Wagibeoni wamefanya makubaliano ya amani na Waisraeli, wakaamua kuunganisha majeshi yao kuwa jeshi moja kubwa na kuwavamia Wagibeoni. Wagibeoni **wakatuma ujumbe kwa Yoshua wakiomba msaada.**

**wakatuma ujumbe kwa Yoshua wakiomba msaada**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "waliwatuma baadhi ya watu wao kumwambia Yoshua kuwa walihitaji Waisraeli wawasaidie kujikinga na maadui."

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Gibeoni. Wagibeoni
- Amani
- Ahadi
- Mungu
- mfalme
- Kanaan, Mkanaan
- Mwamori
- Yoshua



**15:08**

Kwa hiyo Yoshua akalikusanya jeshi la Waisraeli na wakatembea usiku kucha kufika kwa Wagibeoni. Na asubuhi na mapema wakalishangaza jeshi la Waamori na kuwavamia.

**kuwafikia Wagibeoni**

Kwamba, "kufika kwa Wagibeoni" au, "kufika mahali ambapo Wagibeoni waliishi." Wagibeoni waliishi Kanaani, lakini Kanaani ilikuwa kubwa kiasi kwamba jeshi la Israeli lilisafiri usiku kucha kufika mahali walipokuwa Wagibeoni.


**wakawashitukiza majeshi ya Waamori**

Waamori hawakujua kwamba Waisraeli walikuwa wanakuja kuwavamia.

**translationWords**

- [Yoshua](#)
- [Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli](#)
- [Gibeoni. Wagibeoni](#)
- [Mwamori](#)

**15:09**



**Mungu akaipigania Israeli** katika siku hiyo. Akasababisha Waamori kuchanganyikiwa na akatuma mvua ya mawe makubwa toka mbinguni ambayo yaliwaua Waamori wengi.

### **Mungu akaipigania Israeli**

Mungu alikuwa upande wa Israeli dhidi ya adui zao

### **akasababisha Waamori kuchanganyikiwa**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "aliwafanya Waamori wahamaki"

### **mawe makubwa ya mvua**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "mapande makubwa ya barafu yalianguka chini kutoka angani."

### **translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mwamori

**15:10**

**Mungu** pia akasababisha jua kukaa sehemu moja katika anga ili **Israeli** iwe na muda wa kutosha wa kumaliza na kuwashinda kabisa **Waamori**. Katika siku hii, Mungu akashinda ushindi mkuu kwa Israeli.

**Mungu**

Katika Biblia, neno "Mungu" humaanisha nafsi ya milele aitwaye "Yahweh," ambaye aliumba ulimwengu pasipo kitu. Yahweh ana nafsi tatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu

**Israeli**

Israeli ni jina ambalo Mungu alimpa Yakobo. Israeli maana yake ni, "Alipambana na Mungu." Kizazi cha Yakobo walijulikana kama watu wa Israeli, taifa la Israeli, au Waisraeli.


**Waamori**

Waamori walikuwa kikundi cha watu walioishi Kanaani kipindi cha Yoshua. Waamori waliishi katika miji ya karibu na mto Yorodani. Kila mji uliongozwa na mfalme. Mungu aliahidi kuwapa Israeli ardhi ya Kanaani pamoja na ardhi ya Waamori.

**translationWords**

- [Mungu](#)
- [Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli](#)
- [Mwamori](#)



**15:11**

Baada ya Mungu kuyashinda majeshi hayo, makundi mengine ya watu wa Wakaanani waliunganika pamoja kuishambulia Israeli. YOSHUA na Waisraeli **wakawavamia na kuwaangamiza**.

**wakawavamia na kuwaangamiza**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "walipigana nao na kuwashinda."

**translationWords**

- Kanaani, Mkanaani
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- YOSHUA

**15:12**

Baada ya vita hii, Mungu akatoa kwa kila kabila sehemu yake katika nchi ya ahadi. Tena Mungu **akaipa Israeli amani kwenye mipaka yake yote.**

**Mungu alitoa...ardhi**

hii inaweza kutafasiriwa kama, "Mungu aliwapa kila kabila kipande cha ardhi"


**akaipa Israeli amani kwenye mipaka yake yote**

hii inaweza kutafasiriwa kama, "Mungu aliwafanya Waisraeli kupata amani na makundi ya watu waliowazunguka" au, "nchi nyingine katika Israeli."

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Nchi ya ahadi
- Amani



**15:13**

Wakati Yoshua alipokua mzee, akawaita watu wote wa Israeli pamoja. Tena Yoshua akawakumbusha watu wajibu wao wa kutii agano ambalo Mungu aliliweka na Waisraeli Sinai. Watu wakamuhaidi **kubaki kuwa waaminifu kwa Mungu** na **kuzifuata sheria zake**.

**Wakati Yoshua alipokuwa mzee**

Inaweza kueleweka zaidi ukisema, "Miaka mingi baadaye, wakati yoshua alikuwa mzee." Yoshua alikuwa na zaidi ya miaka 100 kwa kipindi hiki.

**kubaki kuwa waaminifu kwa Mungu**

kwa maneno mengine, wangukuwa watii kwa Mungu. Wangemwabudu na kumtumikia Mungu pekee; wasingeabudu au kutumikia miungu mingine.

**kuzifuata sheria zake**

Hii inamaanisha kwamba watu wangetii sheria ambazo Mungu aliwapa hapo kwanza kama sehemu ya agano.

Simulizi ya Biblia kutoka: Yoshua 1-24

**translationWords**

- Yoshua
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- tii, mtiifu, utiifu
- Agano
- Mungu
- Sinai, Mlima Sinai
- Ahadi

- mwaminifu, uaminifu
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe

## 16. Wakombozi

### 16:01



Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli hawakumtii Mungu na hawakuwaondoa Wakanaani wala kuzitii amri za Mungu. Waisraeli walianza kuhabudu miungu ya Wakanaani badala ya Yehova, **Mungu wa kweli**. Waisraeli hawakuwa na mfalme, kwa hiyo kila mmoja alifanya alichofikiri ni sahihi.

#### **Na hawakuwaondoa.**

Hii inaelezea jinsi ambavyo hawakumtii Mungu, hivyo katika baadhi ya lugha ingekuwa vyema kuianza hii kama sentensi mpya, "Hawakufanya"

#### **Kuwaondoa Wakanaani waliobakia**

Hii inaweza kutafasiriwa, "kupigana na wakanaani waliobakia na kuwalazimisha waondoke kwenye nchi.

#### **Au kutii sheria za Mungu.**

hii ina manisha ya kuwa pia watu hawakuzitii sheria ambazo Mungu aliwapa waisrael katika Mlima Sinai.

#### **Mungu wa kweli**

Ni kwamba, "Mungu halisi" Yehova ndiye pekee ambaye watu wanapaswa kumwabudu.


#### **Jinsi walivyofikiri ya kuwa ingekuwa sahihi kwa ajili yao**

Hii inamanisha ya kuwa wote walifanya yale waliyotaka kufanya, ikiwa ni pamoja na uovu mwingi.

## translationWords

- Yoshua
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- totii, mkaidi, kutotii
- Mungu
- Kanaani, Mkanaani
- tii, mtiifu, utiifu
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Yaweh
- kweli, ukweli, kuwa kweli
- mfalme



**16:02**

Kwa sababu Waisraeli waliendelea kutomtii Mungu, aliwaadhibu kwa kuruhusu maadaui zao kuwashinda. Hawa maadui walichukua vitu kutoka kwa Waisraeli, wakaharibu mali zao na kuwaua wengi wao. Baada ya miaka mingi ya kutomtii Mungu na kuteswa na maadui, Waisraeli walitubu na kumuomba Mungu awaokoe.

**Walimuomba Mungu awaepushe.**

Hii ni kwamba, walimwomba Mungu awasaidie na kuwaweka huru kutoka kwa maadui zao.

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- totii, mkaidi, kutotii
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- Kutubu, toba

**16:03**

Baadaye **Mungu alituma** mkombozi aliyewaokoa kutoka kwa maadui zao na kuleta amani katika nchi. Lakini baadaye watu walimsahau Mungu na kuunza kuhabudu miungu yao tena. Kwa hiyo Mungu akaruhusu Wamidiani, kundi la watu maadui wakaribu, kuwashinda.

**Mungu alituma**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "Mungu alichagua" au "Mungu alimteuwa" au " Mungu alimwinua."

**Alileta Amani**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "aliruhusu watu waishi bila kuwa na hofu" au "alimaliza mapigano" au "aliwazuia maadui zao kuwateka".

**Nchi.**

Hiyo inaelezea Kanaani, nchi ya ahadi ambayo Mungu alimpa Ibrahim.


**Watu walimsahau Mungu.**

Inamanisha ya kuwa, " Watu waliacha kufikiri kuhusu Mungu na kupuuzia alichokuwa amewaamuru."

**translationWords**

- Mungu
- komboa, mkombozi, ukombozi
- Amani
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike

- [Midiani, Wamidiani](#)

**16:04**

Wamidiani walichukua mazao yote ya Waisrael kwa miaka saba. Waisraeli wakaogopa sana; wakajificha mapangoni ili Wamidiani wasiwapate. Hatimaye, wakamuomba Mungu awaokoe.

**Mazao**

Hii inaelezea Mimea ambayo waisrael waliyokuwa wakilima katika bustani zao au mashamba yao, kwa ajili ya chakula.

**Waliogopa sana, wakajificha.**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "Wali waogopa sana Wamidiani, hivyo wakajificha."

**Wakamlilia**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "waliita kwa sauti" or "Waliomba kwa uchungu sana."

**Awaokoe**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "kuwaweka huru" au "kuwanusuru na maadui hawa."

**translationWords**

- Midiani, Wamidiani
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- okoa, salama



**16:05**

Siku moja, mtu wa Israeli jina lake Gidioni alikuwa akipura ngano katika sehemu ya siri ili Wamidiani wasije wakaiba. Malaika wa Yehova alimtokea Gidioni na kusema "Usiogope, Mungu yuko pamoja na wewe. Nenda ukawaokoe Waisraeli kutoka kwa Wamidiani."

**Siku Moja.**

Aya hii inatambulisha tukio lililo tokea kipindi cha nyuma, lakini haikutaja muda maalumu. Lugha mbalimbali zina namna sawa za kuelezea simulizi ya kweli.

**Kupura nafaka**

Nafaka ilikuwa ni ngano, yenye vipande vidogo vya nafaka, au mbegu juu ya maganda yake. "Kupura" ni kuachanisha mbegu za mimea kutoka kwenye maganda kwa kupepeta vipande vya nafaka. Mbegu ni chakula lakini maganda sio chakula.

**Sirini.**

hapa ni pale Gideoni alikuwa akipura nafaka katika sehemu iliyofichika, kwa hiyo Wamidiani hawakuweza kumuona.

**Mungu yupo pamoja nanyi**

hii humanisha " Mungu yupo pamoja na wewe kwa namna yaki pekee" or "Mungu anayo malengo ya kukutumia kwa namna ya kipekee."

**translationWords**

- [Gideoni](#)

- Midiani, Wamidiani
- Malaika, Malaika mkuu
- Yaweh
- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

**16:06**

Baba yake Gidioni alikuwa na madhabahu aliyoweka wakifu kwa mungu. Mungu akamwambia Gidioni kuvunja madhabahu hiyo. Lakini Gidioni aliogopa watu, hivyo akasubiri hadi ilipofika wakati wa usiku. Kisha akaivunjavunja madhabahu vipande vipande. Akamjengea Mungu madhabahu mpya karibu na ilipokuwa madhabahu ya mungu na kumtolea Mungu sadaka juu yake.

**Kuvunja**

Hii inamanisha kuwa, "kuleta chini hasa," au "kuiharibu au kuiteketeza kabisa."

**Aliogopa watu.**

Gidioni aliogopa ya kuwa wenzake wa israel waliokuwa wakiabudu sanamu ile ile wangemkasirikia.

**Walisubiri mpka wakati wa usiku.**

Namna nyingine ya kusema maneno haya ni, "walisubiri mpka giza lilipoingia". Gidioni aliivunja madhabahu usiku wake ambapo kila mtu alikuwa amelala ili asiwepo wa kumuona.

**translationWords**

- Gideoni
- Madhabahu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Mungu
- dhabihu, sadaka

**16:07**

Asubuhi yake watu waliona mtu fulani amevunja na kuharibu madhabahu, na wakakasirika sana. Wakaenda nyumbani kwa Gidioni kumua, lakini baba yake Gidioni akasema, "**Kwa nini mnajaribu kumsaidia mungu wenu?** Kama ni mungu, muacheni ajilinde mwenyewe!" Kwa sababu alisema hayo, watu hawakumuua Gidioni.

**Kwa nini mnajaribu kumsaidia mungu wenu?**

Hili sio swali sahihi la kuulizia taarifa. Namna nyingine ya kusema inaweza kuwa ni, "hamtakiwi kumsaidia mungu wenu" au " hampaswi kumsaidia mungu wenu."


**Na kama ni mungu, ajilinde mwenyewe**

Hii inamaana ya kuwa, "kama angelikuwa ni mungu wa kweli, angekuwa na uwezo wa kujitetea mwenyewe."

**translationWords**

- Madhabahu
- Gideoni
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike



**16:08**

Baadaye Wamidiani walikwenda tena kuiba kwa Waisraeli. Walikuwa wengi sana kiasi cha kutohesabika. Gidioni alikusanya Waisraeli pamoja ili kupigana nao. Gidioni akamuuliza Mungu ishara mbili zitakazompa uhakika kwamba Mungu atamtumia kuokoa Israeli.

**Walikuja tena kuwaibia waisrael.**

Hii ingetafasiriwa kama "walikuja tena kwenye nchi ya waisrael kuwaibia vitu."

**hawakuweza kuhesabika.**

Hii ingetafasiriwa kama, " idadi ya Wamediani ilikuwa ni kubwa kiasi cha kutohesabika" au " ilikuwa ni ngumu kuwahesabu Wamediani wote."

**kwa ishara mbili**

Hii ingetafasiriwa kama, "kutenda miujuiza mara mbili" au " kufanya mambo mawili yasiyowezekana yawezekane."

**Kwamba Mungu angemtumia.**

Hii ingetafasiriwa kama, "Mungu angemwezesha" au "Mungu angelimsaidia" au " Mungu alikuwa akimuita."

**Kuiokoa israel.**

Hii ingetafasiriwa kama, " Kuinusuru Israel kutoka kwa Wamidiani."

## translationWords

- Midiani, Wamidiani
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Gideoni
- Mungu
- okoa, salama

**16:09**

Kwa ishara ya kwanza, Gidioni alitandika ngozi ya kondoo juu ya ardhi na akamwambia Mungu kuwa umande wote ufikie juu ya hiyo ngozi tu na sio juu ya ardhi. Mungu akafanya kama alivyoomba. Usiku uliofuata, akaomba ardhi ilowane maji lakini ngozi ibaki kuwa kavu. Na Mungu akafanya kama alivyoomba pia. **Ishara** hizi mbili zilimhamasisha Gidioni kuwa Mungu atamtumia kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Wamidiani.

**Ishara**

Hii ingetafasiriwa kama, "Miujiiza" au " Mambo yasiyowezekana"

**Ngozi ya Kondoo**

Hii ni ngozi ya kondoo yenye manyoya juu yake, Manyoya ni kama sufu ambayo hukamata maji mengi(hushikilia maji mengi),kwa tafasiri hii inatoa udhibitisho kuwa ngozi hii imefunikwa na nywele laini na nyembamba

**Na kuwe na umande asubuhi.**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, " umande utokee asubuhi" au " umande ushuke asubuhi." "Umande" haya ni matone ya maji ambayo huonekana kwenye aridhi wakati wa asubuhi". kiuhalisia umande hufunika kila kitu kwa pamoja."

**Mungu alifanya hivyo.**


Hii ingetafasiriwa kama, "Mungu alitenda kile ambacho Gidioni alichomuomba atende."

**translationWords**

- Gideoni
- kondoo, kondoo dume, kondoo jike

- Mungu
- okoa, salama
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Midiani, Wamidiani



**16:10**

Maaskari 32,000 wa Kiisraeli walikwenda kwa Gidioni, lakini Mungu akamwambia kuwa hao ni wengi mno. Ndipo Gidioni akawarudisha 22,000 waliokuwa na hofu ya kupigana. Mungu akamwambia Gidioni kuwa bado ana wanaume wengi sana. Hivyo Gidioni kuwarudisha wote nyumbani isipokuwa maaskari 300.

**Askari 32,000 walikuja kwa Gidioni.**

Baadhi ya lugha zingeweza kuiweka sentensi ifuatayo mwanzoni mwa simulizi; Gididoni aliwaita waisrael ili waje wapigane na Wamidiani.

**Wengi sana.**


Ni kwamba, walikuwa askari wengi sana tofauti na jinsi Mungu alivyokuwa akihitaji kwa ajili ya mapigano. Kama askari wengi wangepigana na kushinda, wangepikiri ya kuwa wameshinda vita kwa nguvu zao wenyewe na wasingetambua ya kuwa Mungu ndiye ametenda.

**Isipokuwa Askari 300.**

Sentensi hii ingemanisha ya kuwa, "Hivyo Gidioni akaruhusu Askari 300 tu kubaki, na wengine walielekea nyumbani."

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Gideoni
- Mungu

**16:11**

Usiku huo ndipo Mungu akamwambia Gidioni, " Shuka chini kwenye kambi ya Wamidiani na utakaposikia wanachoongea, usiogope." Kwa hiyo usiku huo, Gidioni akashuka chini kambini kwa Wamidiani na akasikia askari midiani akimwambia rafiki yake kuhusu ndoto aliyoota. Rafiki yake akamwambia, "Ndoto hii inamaanisha kwamba jeshi la Gidioni litashinda jeshi la Wamidiani!" Gidioni aliposikia hivyo akamwabudu Mungu.

**Kushuka chini.**

Askari wa Midiani waliweka kambi kule bondeni na walikuwa chini zaidi ya askari wa israel.

**Hamtakuwa na hofu kamwe.**


Hii inamaanisha kuwa," hamtaogopa tena"

**Alichokuwa amekiota**

Hii ni kwamba,"kitu ambacho alikuwa amekiona kwenye ndoto" au " ndoto aliyokuwa nayo."

**translationWords**

- Mungu
- Gideoni
- Midiani, Wamidiani
- ndoto
- Abudu

**16:12**

Baadaye Gidioni akarudi kwa wanajeshi wake na kuwapa pembe, vyungu na kurunzi. Wakazunguka kambi ambayo Wamidiani walikuwa wamelala. Maaskari 300 wa Gidioni walikuwa na kurunzi zilizokuwa zimefichwa ndani ya vyungu ili kwamba Wamidiani wasije wakaona mwanga wa hizo kurunzi.

**Pembe**

Hii ingetafasiriwa kama, " tarumbeta" au "Pembe ya tarumbeta." Pembe hizi zilitoka kwenye kondoo dume na zilitumika kuwaita wanaume kwa ajili ya vita(mapigano).

**Kurunzi**

kuna uwezekano kuwa ilikuwa ni kipande cha kuni kilichofunikwa na nguo na iliyosokotwa kwenye mafuta ilikusudi iweze kuwaka vizuri. (hii haikuwa kurunzi ya kisasa iwakayo kwa betri)

**translationWords**

- [Gideoni](#)
- [Midiani, Wamidiani](#)



**16:13**

Ndipo, wanajeshi wote wa Gidioni walipovunja vile vyungu kwa pamoja, ghafla pakatokea mwanga wa kurunzi. Wakatoa pembe zao na kupaza sauti, "**Upanga** kwa Yehova na kwa Gidioni!"

**Wakapaza sauti.**

Hii ingetafasiriwa kama, "alitoa sauti kubwa" au " kusema kwa sauti kubwa"

**Upanga**


Upanga ni siraha yenye kisu kirefu, chnye makali na mkono wa kushikia. Watu hushika sehemu ya mkono na kumpiga au kumchoma adui na kupitia sehem yenye makali. Kama watu wako wasipokuwa na siraha kama namna hii, ungetafasiri kama, "kisu kirefu" au "panga" "kisu cha porini"

**Upanga kwaYehova kwa Gidioni.**

Inamanisha ya kuwa, " tutapigana wa Yehova na kwa Gidioni."

**translationWords**

- Gideoni
- Yaweh

**16:14**

Mungu aliwachanaganya Wamidiani, kiasi kwamba walianza kupigana na kuuwana wao kwa wao. Mara ghafla, Waisraeli wengine waliitwa kutoka kwenye miji yao ili kuja kusaidia kufukuza Wamidiani. Wakawaua wengi wao na kuwafukuza waliobaki kutoka katika nchi ya Waisraeli. Wamidiani 120,000 waliuwawa siku hiyo. Mungu akaiokoa Israeli.

**Mungu aliwachanganya Wamidiani.**

Mungu alisababisha Wamidiani wachanganyikiwe. Walitaka kuwashambulia Waisrael, lakini badala yake walijishambuliana wao kwa wao.

**Waisrael waliobaki**

Hii ingetafasiriwa kama, " Waisrael wengi wa kiume". inaelezea baada ya Askari kurudi nyumbani.


**Waliitwa.**

Ni kwamba, " waliitwa nje" au " waliombwa kuja" sentensi hii ingetafasiriwa kama, " Gidioni alituma watu kuwaita wanaume wa israel kutoka kwenye nyumba zao"

**translationWords**

- Mungu
- Midiani, Wamidiani
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- okoa, salama



**16:15**

Watu walitaka kumuweka Gidioni kuwa mfalme wao. Lakini Gidioni hakuwaruhusu kufanya hivyo, lakini akawaomba baadhi ya pete za dhahabu walizochukua kutoka kwa Wamidiani. Watu wakampatia Gidioni kiasi kikubwa cha dhahabu.

**Hakuwarusu wafanye haya**

Gidioni alijua ya kuwa ilikuwa ni vyema Waisrael wamfanye Mungu kama Mfalme wao.

**Lakini aliwauliza**

Aya hii inaanza na "lakini" kwa sababu alichokifanya badaye hakikuwa na hekima.

**translationWords**

- Gideoni
- mfalme
- Midiani, Wamidiani

**16:16**

Baadaye Gidioni akatumia hizo dhahabu kutengeneza vazi maalumu kama lililokuwa likivaliwa na kuhani mkuu. Lakini watu wakaanza kulihabudi kana kwamba lilikuwa mungu. Kwa hiyo Mungu akaiadhibu Israeli tena kwa sababubu ya kuhabudu miungu. Mungu akaruhusu maadui wawashinde. Hatimaye walimuomba Mungu awasaidie tena, na Mungu aliwatumia mkombozi mwingine.

**Gidioni alitumia dhahabu kutengeneza vazi maalumu.**

Hii ingetafasiriwa kama, "Gidioni aliiyeyusha dhahabu ambayo watu walimpatia na akatengeneza vazi la maalumu kutoka kwenye dhahabu.

**Walimuacha Mungu.**

Hii ingetafasiriwa kama, "hawakumtii Mungu" au " waliacha kumwabudu Mungu."

**translationWords**

- Gideoni
- kuhani mkuu
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- komboa, mkombozi, ukombozi

**16:17**

Tukio hili lilijirudia mara kwa mara: Waisraeli walipotenda dhambi, Mungu aliwaadhibu, walipotubu, na Mungu alituma mkombozi kwao. Yapata miaka mingi, Mungu alikuwa akituma wakombozi wa kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa maadui zao.

**Hali hii ilijirudia mara kwa mara**

Hii ingetafasiriwa kama, " Mambo haya yaliendelea kujirudia mara kwa mara" au " Mambo haya yalitokea mara nyingi"

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- Kutubu, toba
- komboa, mkombozi, ukombozi
- okoa, salama



**16:18**

Mwishowe, watu walimuomba Mungu awape mfalme kama mataifa mengine. Walitaka mfalme aliyekuwa mrefu na mwenye nguvu, na atakayeweza kuwaongoza vitani. Mungu hakupendezwa na ombi hilo, lakini akawapatia mfalme sawa na ombi lao.

**Hatimaye**

Hii ingetafasiriwa kama, " Baada ya aduu zao kuwashambulia mara nyingi" au " Baada ya miaka mingi ya kushambuliwa na mataifa mengi tofauti."

**Wakamuomba Mungu awape Mfalme**

Hii ingetafasiriwa kama, "walimtaka Mungu awape Mfalme" au "waliendelea kumuomba Mungu kwa ajili ya Mfalme."

**Kama mataifa mengine**

Mataifa mengine yalikuwa na Mfalme. Waisrael walitaka wawe kama wao na wapate Mfalme.

**Mungu hakulitaka Ombi hili**

Hii ingetafasiriwa kama, " Mungu hakukubaliana na walichomuomba," Mungu alijua yakuwa walikuwa wakimkataa kama Mtawala wao na badala yake walichagua kuwafuata viongozi wao.

Simulizi ya Biblia kutoka: Waumuzi 1-3; 6-8

**translationWords**

- Mungu



- [mfalme](#)

## 17. Agano la Mungu na Daudi

17:01



Sauli alikuwa mfalme wa kwanza wa Israel. Alikuwa mrefu na mzuri, kama watu walivyopenda. Sauli alikuwa mfalme mwema kwa miaka michache ya mwanzoni aliyotawala Israel. Lakini, baadaye alikuwa mfalme muovu ambaye hakumtii Mungu, Kwa hiyo Mungu alimchagua mtu mwingine ambaye angekuwa mfalme badala yake.

### Mfalme wa kwanza wa Israel

Hii ingetafasiriwa kama, " Mfalme wa kwanza kutawala Israel."

### Siku moja

Hii ingetafasiriwa kama, "Wakati mwingine badaye" au " Miaka badaye."

### Angekuwa Mfalme katika nafasi yake.

Namna nyingine ya kusema ni, " kuchukua nafasi yake kama Mfalme wa Israel" au " Kutawala kama Mfalme badala yake."

### translationWords

- Sauli (A K)
- mfalme
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- tii, mtiifu, utiifu
- Mungu

**17:02**

Mungu alimchagua kijana mwisraeli aliyetwa Daudi kuwa mfalme baada ya Sauli. Daudi alikuwa mchungaji kutoka mji wa Bethlehemu. Mara kadhaa wakati Daudi akiwa anachunga kondoo wa baba yake, Daudi alikuwa ameua simba na dubu waliokuwa wameshambulia kondoo. Daudi alikuwa mtu mnyenyekevu na mwenyehaki aliye mtumaini na kumtii Mungu.

**Kuchunga**

Inamanisha, "kutunza kwa ajili ya" au "kulinda" au "kujali kwa ajili ya."

**translationWords**

- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Daudi
- mfalme
- Sauli (A K)
- mchungaji, kuchunga
- Bethlehemu
- kondoo, kondoo dume, kondoo jike
- nyenyekea, unyenyekevu
- Adili, uadilifu
- imani, aminifu,
- tii, mtiifu, utiifu

**17:03**

Daudi alikuwa askari na kiongozi mwenye nguvu. Wakati Daudi alipo kuwa kijana, alipigana na jitu aliyetwa Goliati. Goliati alikuwa askari aliyefuzu, na mwenye nguvu, na alikuwa takribani na urefu wa mita tatu! Lakini Mungu alimsaidia Daudi kumuua Goliati na kuwaokoa Israeli. Baada ya hapo, Daudi aliwashinda maadui wengi wa Israeli na hii ndiyo sababu watu walimsifu Daudi.

**Jitu kubwa liitwalo Goliathi.**

"Jitu kubwa" hii inaelezea Mtu mkubwa asiye wa kawaida na mwenye nguvu. Goliathi alikuwa ni Askari mkubwa kwenye jeshi lililokuwa likipigana na israel

**translationWords**

- Daudi
- Mungu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kusifu



**17:04**

Sauli aliona wivu kutokana na upendo wa watu kwa Daudi. Sauli alijaribu kumuua Daudi mara nyingi, kwa hiyo Daudi akajificha mbele ya Sauli. Siku moja, Sauli alikuwa akimtafuta Daudi ili apate kumuua. Sauli akaenda kwenye pango ambalo Daudi alikuwa amejificha lakini hakumuona. Kwa sasa Daudi alikuwa karibu sana na Sauli kiasi kwamba angeweza kumuua lakini hakufanya hivyo. Badala yake, alikata kipande cha nguo ya Sauli kumthibitisha kuwa hakuweza kumuua ili awe mfalme.

**Siku moja.**

Aya hii inatambulisha tukio lililotokea kipindi cha nyuma lakini hakuna muda maalumu uliotajwa wa tukio kutokea. Lungha nyingi zinamfanano katika kusimulia simuliz hizi za kweli.

**Kuthibitisha kwa Sauli.**

hii ni kwamba, " kumshawishi Sauli" au " Kumhakikishia Sauli."

**Kuwa Mfalme.**

Daudi hakutaka kumkosea Mungu kwa kumuua Mtu ambaye Mungu alimuweka kama Mfalme wa Israel.

**translationWords**

- Sauli (A K)
- upendo
- Daudi
- mfalme

**17:05**

Mwishowe, Sauli aliuawa vitani na Daudi akawa mfalme wa Israeli. Alikuwa mfalme mwema na watu walimpenda. Mungu alimbariki Daudi na kumfanya kuwa mwenye mafanikio. Daudi alipigana vita nyingi na Mungu akamsaidia kuwashinda maadui wa Israel. Daudi akauhusuru mji wa Yerusalemu na kuufanya makao makuu yake. Katika kipindi cha utawala wake, Israeli likawa taifa lenye nguvu na lenye utajiri.

**Alimfanikisha**

Hii ni kwamba, "alimsaidia kukamilisha mambo mazuri aliyotaka kuyafanya."

**Mji mkuu wake**

Huu ni, "Mji mkuu katiaka ufalme wake." Daudi aliishii Yerusalemu na akatawala huko.


**Kipindi cha utawala wa Daudi**

Hii ni, "katika kipindi ambacho Daudi alikuwa Mfalme wa israel." au "Daudi alitawala kama Mfalme wa israel."

**translationWords**

- Sauli (A K)
- Daudi
- mfalme
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- upendo
- Mungu
- Kubariki
- Yerusalemu

## 17:06



Daudi alitaka kujenga hekalu ambalo watu wange mwabudu Mungu na kumtolea sadaka. Kwa takribani miaka 400, watu walikuwa wakimwabudu Mungu na kumtolea sadaka katika hema ya kukutania ambayo Musa alijenga.

## Jenga Hekalu

Daudi alitaka kujenga jengo la kudumu kwa ajili ya kumwabudu Mungu ambalo lingekaa badala ya hema la kukutania.

## translationWords

- Daudi
- hekalu
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Abudu
- Mungu
- dhabihu, sadaka
- hema la kukutania
- Musa



**17:07**

Lakini Mungu alimtuma nabii Nathani aende kwa Daudi na ujumbe huu, "Kwa kuwa wewe ni mtu wa vita, hautajenga hekalu hili kwa ajili yangu. Mtoto wako wa kiume ndiye atakaye lijenga. Lakini, wewe nitakubariki sana. Mmoja kati ya watu wa uzao wako atatawala kama mfalme juu ya watu wangu milele". Mtu pekee wa uzao wa Daudi ambaye angetawala milele alikuwa ni Masihi. Masihi alikuwa ni mteule wa Mungu ambaye angewaokoa watu wa dunia katika dhambi zao.

**Nabii Nadhani**

inaweza ikawa halisi zaidi katika lugha zingine kusema, "Nabii alietwa Nadhani."

**Mtu wa vita**

Inamanisha kuwa " Mtu ambaye anapigana vita" Daudi aliwa watu wengi sana katika vita dhidi ya maadui wa israel. Mungu hakuwa anamuadhibu Daudi lakini Mungu alihitaji mtu wa amani wa kujenga Hekalu ambapo watu wangemwabudu yeye.

**Hekalu hili**

Inamaana ya kuwa, "Jengo hili la kuabudia" au " Sehemu hii ya kuabu."

**Kutoka dhambini**


Inamaana ya kuwa, "Mabaya yaliyowapata kutokana na matokeo ya dhambi zao."

**translationWords**

- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.



- Nathani
- Daudi
- hekalu
- mwana, mwana wa
- Kubariki
- mfalme
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kristo, Masihi
- uzao, kutokana na
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**17:08**

Daudi aliposikia maneno haya, mara alimshukuru na kumtukuza Mungu kwa sababu amemwahidia Daudi heshima na baraka tele. Daudi hakujua ni wakati gani Mungu angefanya mambo haya. Lakini kama ilivyotokea, Waisrael wangukuwa wamesubiri kwa muda mrefu kabla ya Masihi kuja, takribani miaka 1000.

**Maneno haya**

Inamanisha ya kuwa, "Maneno ambayo Nabii aliyasema." hiii inarejea kwenye ahadi.

**Ni heshima kubwa**

Watu walioishi kabla, walimuheshimu Daudi kwa sababu baadhi ya uzao wake walikuwa wafalme wa israel na mmoja wao angelikuwa Masihi.

**translationWords**

- Daudi
- Kusifu
- Mungu
- Ahadi
- Kubariki
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kristo, Masihi

**17:09**

Daudi alitawala kwa haki na uaminifu kwa miaka mingi, na Mungu alimbariki. Hata hivyo, mwishoni mwa maisha yake alitenda dhambi mbaya kinyume na Mungu.

### **Daudi alitawala kwa haki na uaminifu kwa miaka mingi.**

inaweza kutafasirirwa kama, " Daudi alipowatawala watu kwa miaka mingi alitenda yale yaliyokuwa sahihi na sawa, na alikuwa mwaminifu kwa Mungu."

### **Kuelekea mwisho wa maisha yake**

Inaweza tafasiriwa kama, "Daudi alipokuwa Mzee" au " badaye katika maisha ya Daudi."

### **Kutenda dhambi hasa**

Ni sawa na kusema, "'kutenda dhambi kwa kuasi." Dhambi ya Daudi ilikuwa ya Uasi.

### **translationWords**

- Daudi
- haki, adilifu
- mwaminifu, uaminifu
- Mungu
- Kubariki
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**17:10**

Siku moja, wakati maaskari wote wa Daudi walipokuwa vitani mbali na nyumbani, Daudi alitazama nje ya nyumba ya kifalme na akaona mwanamke mzuri akioga. jina lake alitwa Betisheba.

**Siku moja.**

Aya hii inatambulisha tukio lililo tokea kipindi cha nyuma, lakini haijaonesha mda sahihi wa tukio kutokea. Lugha nyingi zinamfanano kwa kaunza kuelezea simulizi za kweli.

**Akaona**

Betisheba aliekuwa akioga nje ya nyumba yake, lakini sehemu ya Daudi ilikuwa juu na alikuwa na uwezo wa kuona juu ya ukuta uliokuwa chini

**Kuoga**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, " alikuwa akioga" au " alikuwa akijiosha."

**translationWords**

- [Daudi](#)
- [Bathsheba](#)



## 17:11



Badala ya kutazama upande, Daudi akatuma mtu kwenda kumleta mwanamke huyu kwake. Akalala naye na baadaye akamrudisha nyumbani kwake. Muda mfupi baadae Betisheba akatuma ujumbe kwa Daudi akisema kwamba alikuwa na mimba.

### **Badala ya kutazama pembeni**

Inamanisha ya kuwa, Daudi hakutazama upande kipindi mwanamke alikuwa anaoga, kama alivyotakiwa kufanya.

### **Alilala naye**

Hii ni sawa na kussema ya kuwa Daudi alifanya tendo la ndoa na Betisheba.

### **translationWords**

- [Daudi](#)
- [Bathsheba](#)

**17:12**

Mume wa Betisheba, aliyetitwa Uria, alikuwa askari hodari miongoni mwa askari wa Daudi. Daudi akamuita Uria arudi nyumbani kwake kutoka vitani na kumwambia aende kuwa na mke wake. Lakini Uria alikataa kurudi nyumbani wakati askari wenzake wakiwa bado vitani. Kwa hiyo Daudi akamtuma tena Uria arudi vitani na akamwambia mkuu wa jeshi kumuweka Uria mahali palipo na mapigano makali ili apate kuuwawa.

**Kuwa na mke wake**

inamaanisha kuwa, " aende nyumbani akakae mkewe." Daudi aliwataka watu hasa Uria, ili waamini ya kuwa Betisheba alikuwa na mimba yenye mtoto wa Uria.

**Pale ambapo adui alikuwa na nguvu**

Inamaanisha kuwa, sehemu fulani kwenye vita ambapo mapigano yalikuwa yakiendelea.

**translationWords**

- [Bathsheba](#)
- [Uria](#)
- [Daudi](#)

**17:13**

Baada ya Uria kuuwawa, Daudi akamwoa Betisheba. Baadaye akamzalizia Daudi mtoto wa kiume. Mungu alikasirika sana kutokana na kitendo kile alichokifanya Daudi, kwa hiyo Mungu akamtuma nabii Nathani kumwambia Daudi jinsi gani dhambi yake ilikuwa mbaya. Daudi akatubu dhambi yake na Mungu akamsamehe. Katika maisha yake yaliyosalia, Daudi alimfuata na kumtii Mungu, hata katika nyakati ngumu.

**Alichokuwa amekifanya Daudi**

Hii inarejea kuzini kwa Daudi na Betisheba pamoja na mauwaji ya mmewe, Uria.

**translationWords**

- Uria
- Daudi
- Bathsheba
- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Nathani
- baya, ovu, uovu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kutubu, toba
- samehe, kusamehe
- tii, mtiifu, utiifu



**17:14**

Lakini kama adhabu kwa dhambi ya Daudi, mtoto wake wa kiume alifariki. Kukawa pia na mapigano katika familia ya Daudi kwa maisha yake yaliyosalia, na nguvu ya Daudi ilizidi kufifia mno. Ingawa Daudi hakuwa mwaminifu kwa Mungu, Mungu alizidi kuwa mwaminifu katika ahadi zake. Baadaye Daudi na Betisheba walipata mtoto mwingine, na wakamuita Sulemani.

**Mapigano katika Nyumba ya Daudi**

"Mapigano" haya yalikuwa makali. katika mambo haya, mmoja wa watoto wake alimuwa mtoto wake na kuchukua nafasi ya Daudi kama Mfalme wakati ambao Daudi alikuwa akitawala. Ikiwezekana tumia neno ambalo litapunguza ukali wa ugomvi ndani ya familia.

**Nguvu ya Daudi ilidhoofika sana.**

inaweza kutafasiriwa kama, " Daudi akawa hana nguvu tena" au " Daudi akapoteza Mamlaka yake .

Simulizi ya Biblia kutoka: 1Samwel 10; 15-19; 24; 31; 2Samuel 5; 7; 11-12

**translationWords**

- Kuadhibu, adhabu
- Daudi
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- mwaminifu, uaminifu
- Ahadi
- Bathsheba
- Sulemani



## 18. Ufalme Uliogawanyika

### 18:01




Baada ya miaka mingi Daudi alifariki, na mwanae aitwaye Solomoni akatawala Israeli badala yake. Mungu alimuuliza Solomoni kitu muhimu amabcho angetaka apewe. Mungu alimpa Solomoni hekima nyingi kuliko watu wote kama alivyoomba. Naye alijifunza mambo mengi na kutawala kwa haki. Pia Mungu alimpa Solomoni utajiri mwingi.

### Aliomba hekima

Hii inaweza kutafasiriwa kama, " alimuomba Mungu ampe hekima."

### translationWords

- Daudi
- Sulemani
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Busara, hekima
- hukumu

**18:02**

Katika mji wa Jerusalemu, Solomoni alijenga Hekalu ambayo Baba yake Daudi alikusudia kuujenga na hivyo kuandaa vifaa vya ujenzi. Watu walianza kumuabudu na kumtolea Mungu sadaka ndani ya Hekalu badala ya kwenye hema ya kukutania. Mungu alishuka na kukaa ndani ya hekalu na kuishi pamoja na watu wake.

**Alikuwemo ndani ya Hekalu**

inamaanisha kuwa, " alikuwemo ndani ya hekalu kwa namna ya pekee." Hata hivyo Mungu alikuwepo kila mahali mda wote, alijidhihirisha mwenyewe kwa hali ya upekee kwa watu ndani ya hekalu.

**Na watu wake**

inaweza kutafasiriwa kama, " katikati ya watu wake" au " kati ya watu wake."

**translationWords**

- Yerusalemu
- Sulemani
- hekalu
- Daudi
- Abudu
- Mungu
- dhabihu, sadaka
- hema la kukutania

**18:03**

Lakini Solomoni aliwapenda wanawake wa mataifa mengine .Hakumtii Mungu kwa kuwaoa wanawake wengi. Aliwaoa karibu wake 1000. Hao wanawake waliolewa na Solomoni kutoka mataifa mengine walileta na kuaendelea kuabudu miungu yao . Hata Solomoni alipokuwa mzee, naye akaabudu hizo miungu.

**Waliileta miungu yao pamoja na nao.**

Walileta sanamu zao na namna zao za kuziabudu sanam huko israel.

**translationWords**

- Sulemani
- totii, mkaidi, kutotii
- Mungu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Abudu



## 18:04



Mungu alimkasirikia Solomoni, na kukusudia kumuadhibu kwasababu ya kukosa uaminifu. Hivyo Mungu akaahidi kugawa Taifa la Israeli kuwa falme mbili baada ya kifo chake.

### **Kama adhabu ya Selemani kwa sababu ya kukosa uaminifu, aliahidi kuligawa**

inamaanisha ya kuwa, "kumuadhibu Selemani kwa kukosa uaminifu, Hivyo Mungu akasema ataligawa taifa"

### **translationWords**

- Mungu
- Sulemani
- Kuadhibu, adhabu
- Ahadi
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- ufalme



**18:05**

Baada ya Solomoni kufa, Rehoboamu mwanaye , akawa Mfalme. Rehoboamu alikuwa mfalme mpumbavu , watu wote wa Israeli walimridhia yeye kuwa mfalme wao. Watu walimjia na kumlalamikia kuwa Baba yake Solomoni aliwatesa kwa kazi ngumu na kuwatoza gharama kubwa ya kodi.

**Kumthibitisha yeye kama Mfalme**

Inamaana ya kuwa, " kumwambia ya kuwa walifurahia yeye kuwa Mfalme na wangepanya kila alichokisema."

**translationWords**

- Sulemani
- Rehoboamu
- mfalme
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

## 18:06




Mfalme Rehoboamu aliwajibu kwa upumbavu kuwa , msidhani ya kuwa baba yangu aliwapa ninyi kazi nguu , kwani mimi nitawafanya ninyi mfanye kazi ngumu zaidi kuliko alizowapa Baba yangu na kuwapatia ninyi adhabu zaidi kuliko yale ya Baba yangu.

### Kujibu kwa upumbavu

jibu la Rehoboam lilikuwa la ukali, na ilisababisha watu kumgeuka yeye.

### translationWords

- Rehoboamu
- Sulemani
- Kuadhibu, adhabu

**18:07**

Makabila kumi ya Taifa la Israeli yalimuasi mfalme Rehoboamu , na makabila mawili yaliendelea kuwa waaminifu kwake. Hayo makabila mawili yaliunda ufalme wa Yuda.

**Makabila ya taifa la israel**

Kila uzao wa watoto wa Yakobo ulifanyika kuwa "kabila" au kikundi kikubwa cha familia katika taifa la israel. Kila mmoja katika israel alikuwa sehemu ya makabila kumi na mbili.

**Yalimuasi Rehoboamu**

inamaana ya kuwa, "walikataa kumfata Rehoboam kama Mfalme wao." inaweza ikasaidia kuanza sentensi hii kama, "kwa hiyo" au, "kwa sababu hiyo" au " kwa sababu alichokisema Rehoboamu."

**Walibaki kuwa waaminifu kwake**

inamaanisha ya kuwa, " waliendelea kwa waaminifu kwake" au waliendelea kumuunga mkono kama Mfalme."

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Waasi, uasi.
- Rehoboamu
- mwaminifu, uaminifu
- Yuda, ufalme wa Yuda

**18:08**

Makabila yale kumi ya Israeli yaliyo muasi Rehoboamu, waliungana na kumchagua mtu aitwaye Jeroboamu kuwa mfalme wao. Wao walikaa kazikazini mwa nchi ya Israeli. Makabila hayo kumi yaliunda ufalme wa Israeli.

**Walikaa na kuutengeneza ufalme wao.**

inaweza kutafasiriwa kama, " walianzisha" au "kujenga" sentensi hii pia inaweza ikatafasiriwa kama, " walijitenga mbali na yale makabila mawili na wakakaa(wakaishi) kazikazini mwa nchi. na wakaiita nchi yao Israel."

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Rehoboamu
- Yeroboamu
- mfalme
- ufalme
- ufalme wa Israeli



**18:09**

Jeroboamu alimuasi Mungu a kuwafanya watu kutenda dhambi. Alitengeneza sanamu mbili na kuwafanya watu kuiabudu badala ya kumuabudu Mungu wa kweli anayeabuduiwa katika Hekalu lililoko Yuda.

**Alisababisha watu watende dhambi**

Hii ingeweza kutafasiriwa kama, " kuwafanya watu watende dhambi" au " aliwapelekea watu dhambini," Rehoboamu aliwapelekea watu dhambini kwa kutengeneza sanamu kwa ajili ya wao kuabudu."

**Badala ya wao kumwabudu Mungu...Yuda.**

Inaweza kutafasiriwa kama, "ilikusudi wasimwabudu Mungu" au " badala ya kwenda kwenye ufalme wa Yuda kwa ajili ya kumwabudu Mungu kwenye hekalu."

**translationWords**

- Yeroboamu
- Waasi, uasi.
- Mungu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Abudu
- hekalu
- Yuda, ufalme wa Yuda

## 18:10



Ufalme wa **Yuda na Israeli** wakawa maadui, na mara nyingi hupigana wao kwa wao

## Yuda na Israel

Watu wa Yuda na Israel, wote walikuwa ni uzao wa Yakobo na sehemu ya watu wa Mungu. Hata hivyo, hawakumtii Mungu

## translationWords

- [ufalme](#)
- [Yuda, ufalme wa Yuda](#)
- [ufalme wa Israeli](#)

## 18:11



Katika Ufalme mpya wa Israeli wafalme wote walikuwa waovu, na wafalme wengi waliuwawa na waisraeli waliotaka kuwa wafalme badala yao

## Waisrael

Hapa " waisrael" inarejea watu walioishi kazikazini mwa ufalme wa israel, sio kwa watu waliokuwa wakiishi kusini mwa ufalme wa Yuda.

## translationWords

- ufalme
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mfalme
- baya, ovu, uovu



## 18:12



Wafalme wote , na watu wengi waliopo katika ufalme wa Israeli waliabudu sanamu. Baadhi ya vitu walivyoabudu ni pamoja na uzinzi na kutoa kafara ya watoto wao.

### Kafara ya watoto

Waliwauwa watoto na kuwafanya kafara kwa miungu yao.

### translationWords

- mfalme
- ufalme wa Israeli
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- dhabihu, sadaka



**18:13**

Wafalme wa Yuda ni wazaliwa wa Daudi, baadhi ya wafalme hao waliongoza kwa haki na kumuabudu Mungu, hata hivyo wengi wa wafalme wa Yuda walikuwa waovu na walarushwa, baadhi yao hutoa watoto wao kama kafara kwa miungu. Pia watu wengi wa ufalme wa Yuda walimuasi Mungu na kuabudu miungu mingine.

**Alitawala kwa haki**

inamaanisha ya kuwa alitawala kutokana na Sheria za Mungu. inaweza kutafasiriwa kama, " walipotawala, walifanya yaliyokuwa sahihi."

**Rushwa**

Inaweza kutafasiriwa kama, "walifanya yasiyosahihi ilikusudi kujipatia waliyokuwa wakiyahitaji."


Simulizi ya Biblia kutoka: 1Wafalme 1-6; 11-12

**translationWords**

- mfalme
- Yuda, ufalme wa Yuda
- uzao, kutokana na
- Daudi
- wema, uzuri
- haki, adilifu
- Abudu
- Mungu
- baya, ovu, uovu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- dhabihu, sadaka
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Waasi, uasi.

## 19. Manabii

### 19:01



Katika historia ya wana wa Israel ,Mungu aliwatumia manabii wake. manabii walisikia ujumbe kutoka kwa Mungu na kuwambia watu wa Mungu neno lake.

### Kupitia Historia ya


Msemu huu una maana kuwa Mungu alituma manabii wengi katika nyakati nyingi tofauti kupitia miaka yote ambayo Israeli na Yuda walikuwepo.

### Waisraeli

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hapa kama, "Falme za Israeli na Yuda."Vizazi vyote vya Yakobo kujumlisha wote katika ufalme wa Yuda, waliendelea kuitwa "Waisraeli."

### translationWords

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

**19:02**

Na Elia alikuwa nabii katika taifa la Israel chini ya ufalme wa Mfalme Ahabu. Mfalme Ahabu ali asi na kuwalazimisha watu waabudu mungu wake asiye wa ukweli aitwaye Baal. Ndipo nabii Elia akamwambia Ahabu "hapatakuwa na mvua wala ukungu katika Israel mpka nitakaposema" na Mfalme Ahabu aligadhabika saana.

**Mpaka nisema hivyo**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Mpaka niamuru mvua na umande kuja tena."

**Hii ilimkasirisha sana Ahabu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Wakati Ahabu alisikia kile Eliya alichosema, alikuwa na hasira sana."

**translationWords**

- Eliya
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Ahabu
- mfalme
- ufalme wa Israeli
- baya, ovu, uovu
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Baali



**19:03**

Ndipo Mungu akamwambia Elia, " nenda katika jangwa na huko ukajifiche mbali na uso wa Mfalme Ahabu maana anataka kukuuwa, na alipokuwa huko ndege walimpelekea Mkate na nyama kwa ajili ya chakula asubuhi na jioni. Hata alipokuwa huko majeshi ya Ahabu yalimtafuta na yasimpate. Hivyo ukame ukazidi na mifereji kukauka

**Porini**

Hili ni eneo porini mahali ambapo pana watu wachache. Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "jangwa" au "vichakani."

**Ukame**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "upungufu wa mvua." Ukame huu ulikuwa matokeo ya tamko la Eliya kwamba kungekuwa na mvua.

**translationWords**

- Mungu
- Eliya
- Ahabu



**19:04**

Ndipo nabii Elia akaenda katika nchi ya karibu huko akamkuta mwanamke mjane aliyekuwa na mtoto wake wa kiume hawakuwa na chakula kwa sababu ya ukosefu wa mvua na njaa kali, yule mama mjane akampokea Elia na kumkarimu, na yule mama mjane Mungu alimbariki yeye pamoja na mwanae hata kipindi chote cha njaa kali, hivyo mifuko ya unga na chupa zake za mafuta havikumuishia. Na Elia kaishii huko mda mrefu.

**Nchi jirani**

Hii inaonyesha nchi ile ilikuwa karibu, au inayoshirikiana mpaka na Israeli.

**Njaa**

Kwa kweli inaweza kutafsiriwa kama, "njaa iliyosababishwa na ukame."

**Alimtunza**

Hii ina maana walimpa mahali kwa kukaa katika nyumba yao na walimpa chakula. Haina maana kuwa alikuwa mgonjwa.

**Mungu aliwapatia...haikupungukiwa kamwe**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Mungu alitunza chombo chao cha unga na chupa yao ya mafuta visipungukiwe," au "Mungu alisababisha... kutopungukiwa kamwe."

**chombo cha unga**

Hii inaonyesha kuwa chombo cha udongo ambacho mjane alitunza unga wake.

## Chupa ya mafuta

Katika Israeli, mafuta ya mzeituni yalitumika kwa kupikia. Hii inawezakutafasiriwa kama, "chupa ya mafuta ya kupikia." Mjane alitumia unga na mafuta kwa kutengeneza mkate.

### translationWords

- Eliya
- Mungu

19:05



Baada ya miaka mitatu na nusu, Mungu akasema na Elia" Nenda ukaonane na Mfalme Ahabu maana nitaleta mvua " na ndipo Mfalme Ahabu alipomuona Elia akasema " ewe mkorofi" Elia akajibu " wewe ndiye mkorofi, umemwacha Yawee, Mungu wa kweli na kumwabudu Baal,walete watu wote wa taifa la Israel katika mlima wa kamel"

### **Ongea na Ahabu kwasababu alikuwa anakwenda kutuma**

Hii inaweza kutafasiriwa kama. "Mwambie Ahabu kwamba Mungu alikuwa anakwenda kutuma"

### **Msababishaji wa matatizo**

Hii inamaanisha, "Wewe ni msababishaji wa matatizo!" Ahabu alikuwa ana mlaumu Eliya kwa kusababisha matatizo kwa kumwambia mfalme kuwa alikuwa anafanya mabaya na pia kwa kuzuia mvua.

### **Umemutelekeza Yahwe**

Kwamba Ahabu aliwaongoza Israeli kuacha kumwabudu na kumtii Yawhe

### **Mlima wa Karmeli**

Mlima wa Karmeli ni jina la mlima uliokuwa kaskazini mwa Israeli. Una urefu wa mita 500.

### **translationWords**

- Mungu
- Eliya
- ufalme wa Israeli
- Ahabu
- Yaweh

- [Abudu](#)
- [Baali](#)



**19:06**

Ndipo taifa la Israel na manabii wa Baal 450 wote wakaja katika mlima wa kamel. Elia akasema" ni mpka lini akili zenu zitabadilika? kama Yawee ni Mungu na mumtumikie na kama Baal ni Mungu mumtumikie".

**Mlima wa Karmeli**

Ni jina la mlima uliokuwa kaskazini mwa Israeli.

**Kama Yahwe ni Mungu...Kama Baali ni Mungu**

Hii haina maana kwamba Eliya alikuwa hana maamuzi. Alifahamu kuwa Yahwe ni Mungu hakika. Alitaka watu kuelewa kwamba wakati wana wanaabudu miungu ya uongo, wanamkataa Yahwe kama Mungu wa kweli pekee. Tafasiri hii inaonyesha kuwa watu wanapaswa kufanya uchaguzi.

**Kwa muda gani mta...**

Hili si swali halisi liulizwalo kwa maelezo. Eliya alikuwa anawaonya Waisraeli kwa kugeuka geuka na kubadilika mawazo yao kuhusu labda watamtumikia Mungu au Baal. Lugha zingine zinapaswa kueleza hii kama maelezo kama vile "Msibadilishe mawazo yenu juu ya nani mtamwabudu"

**translationWords**

- [ufalme wa Israeli](#)
- [Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.](#)
- [Baali](#)
- [Eliya](#)
- [Yaweh](#)
- [Mungu](#)

## 19:07



Ndipo Elia akawambia manabii wa Baal wauwe ng'ombe kwa ajili ya sadaka, na musiwashe moto, na nitafanya viyohivyo. Na Mungu atakaeachilia moto ndiye atakuwa Mungu wa kweli. na makuhani wa Baal wakaandaa sadaka lakini moto haukwaka.

### **Anayejibu kwa moto**

Hii ni "Ambaye kwa miujiza hutuma moto ili kuteketeza dhabihu."

### **Mungu kweli**

Ina maanisha Mungu mmoja na wa kweli tu

### **translationWords**

- Eliya
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Baali
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- Kuhani, ukuhani

**19:08**

Na hata manabii wa Baal wakaomba kwa mungu wao " tusikie Baal" wakapiga kelele kutwaa wakiomba na kujikata kwa visu lakini mungu wao asiwajibu.

**Waliomba kwa Baal**

Manabii wa Baali walimwomba Baali kutuma moto juu ya ng'ombe waliyemwandaa kama dhabihu.

**Walipaza sauti**

Walipaza au kumwita kwa nguvu Baali

**Walijikata wao wenyewe kwa visu**

Walijijeruhi wao wenyewe kwa visu kama kuonyesha maombi yao kwa Baali, tarajio kwamba hii ingelimsukuma kuwasikia.

**Hakukuwa na jibu**

Hakukuwa na majibu ya aina yote kwa kupaza sauti kwao, na hakuna moto ulikuja kuteketeza dhabihu.

**translationWords**

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Baali
- Kuomba, maombi

**19:09**



Ndipo Elia akaandaa sadaka kwa Mungu na akawaambia watu wote "mwageni maji, mapipa kumi na mbili, na juu ya sadaka wekeni nyama, kuni na madhabahu yote ikajaa maji na kulowana.



**19:10**

hivyo Elia akaomba akisema " Yawee Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, na ujioneshe leo kuwa wewe ni Mungu wa Israel.**Nijibu** na watu wako wajue wewe ni Mungu wa kweli.

**tuoneshe**

Ni kwamba "tuthibitishie"au "jioneshe kwetu.

**mimi ni mtumishi wako**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, " Wewe umenipa mamlaka ya kukutumikia na kufanya vitu hivi."

**Nijibu**

Hili ni "Jibu kwa maombi yangu" au "tuma moto ule nimeomba kwako."

**Hawa watu watajua**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "Watu hawa wataona na kuelewa."

**translationWords**

- Eliya
- Kuomba, maombi
- Yaweh
- Mungu
- Abrahamu, Abram
- Isaka
- Yakobo, Israeli

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- kweli, ukweli, kuwa kweli

**19:11**

Na ndipo moto ukashuka toka juu na kuteketeza nyama, kuni miamba, uchafu na maji yote kwenye madhabahu. na watu wote walipokwisha kuona hivyo wakaanguka chini na kusema Yawee ni Mungu Yawee ni Mungu".

**anguka kutoka angani**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "gafla ulikuja chini kutoka angani."

**shuka ardhini**

Walianguka chini au walipiga magoti juu ya ardhi. Wamliogopa Yahwe kwa sababu waliona nguvu zake. Walijua kwamba Mungu wa kweli tu anaweza kufanya vile na walisujudu chini kumheshimu na kumwabudu.

**Yahweh ni Mungu**

Hii inamaanisha kwamba walielewa kuwa Yahweh ni Mungu pekee, si mmoja wa miungu wengine.

**translationWords**

- [Madhabahu](#)
- [Yaweh](#)
- [Mungu](#)

## 19:12



Elia akaamuru manabii wote wa Baal wakamatwe na asitoweke hata mmoja. Watu wote wakawakamata manabii wa Baal na kuwapeleka mbali na kuwauwa.

### **toroka**

Manabii wa Baali walijaribu kukimbia mbali baada ya mungu wao kuthibitishwa kuwa mungu wa uongo.

### **kamatwa**

Hii ni kuchukuliwa na kushikiliwa

### **translationWords**

- Eliya
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Baali



**19:13**

Elia akamwambia Ahabu "rudi mjini maana kuna mvua kubwa inakuja" Ndipo anga likawa jeusi na mvua kubwaikaanza kunyesha. Hivyo ikajulikana kuwa Yawee ndie Mungu wa kweli na ukame ukaisha.

**Wingu likawa jeusi**

Hii ni, "Anga likawa jeusi sana" Mawingu mazito ya mvua yalifunika anga, ilifanya kuonekana giza la kijivu au jeusi.

**Ukame**

Hii ni, "kipindi kirefu kisicho na mvua."

**translationWords**

- Eliya
- mfalme
- Ahabu
- Yaweh
- Mungu

**19:14**

Baada ya Elia, Mungu akainua nabii mwingine aitwae Elisha, na Mungu akatenda miujiza kupitia Elisha pamoja na kuonya ukoma wa Naamani aliekuwa kamanda wa vita. Baada ya Naaman kumsikia nabii Elisha, akamwendea na kumuomba amponye ukoma wake. ndipo Elisha akamwambia Naaman nenda katika mto Jordani ni huko uoge mara saba.

**Kamanda adui**

Naamani alikuwa kamanda wa jeshi moja la nchi adui za Israeli.

**Alikuwa amekwisha sikia Elisha**

Hii ina maanisha kwamba wale watu walikwisha mwambia Naamani kuwa Elisha alikuwa anaweza kufanya miujiza.


**Alikwenda na kumuuliza Elisha**

Maana yake, "Alikwenda kumwona Elisha na kumuuliza." Naamani alipaswa kwenda Israeli kumtafuta Elisha na kumuuliza kufanya hivi.

**translationWords**

- Eliya
- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- muujiza, ajabu, ishara
- Naamani
- Ponya, tibu
- Mto Yordani, Yordani

## 19:15



na mara ya kwanza Naaman alionekana kukasirika na kuona kama ni ujinga, badae alibadili mawazo yake na kuoga mara saba, na alipokwisha mailiza mara ya saba ngozi yake ilitakasika na ukoma ukaisha na Mungu akamponya.

### **Ungeliacha kufanya hivyo, itaonekana kama ni upumbavu**

Naamani asingefanya kile Elisha alisema kwasababu alifahamu kwamba kuoga peke yake kusingeliponya ugonjwa wake.

### **Alibadirisha mawazo yake**

Hii ni, "aliamua kufanya kile Elisha alimwambia kufanya."

### **translationWords**

- Naamani
- Mto Yordani, Yordani
- Ponya, tibu
- Mungu



**19:16**

Mungu akatuma manabii wengi kuwafundisha watu wawe na huruma na ukarimu wao kwa wao, manabii wakawaonya watu wasiabudu sanamu manabii wakawaonya watu waache mabaya na kummuheshimu Mungu wa kweli. Manabii wakawambia watu wasipotii Mungu atawahukumu atawaadhibu.

**Anza kuonyesha haki na huruma**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "anza kuwa na haki na huruma" au "anza kuonyesha haki na huruma."

**translationWords**

- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- haki, adilifu
- rehema
- baya, ovu, uovu
- tii, mtiifu, utiifu
- hukumu
- hatia, mwenye hatia
- Kuadhibu, adhabu



**19:17**

watu wakaacha kumtii Mungu, wakawatesa na wakati mwingine wakawauwa manabii. mfano Jeremia aliekuwa nabii wa Mungu alichukuliwa na kuwekwa kwenye kisima kikavu na akadumbukizwa kwenye matope na kuachwa huko akafe. Ndipo Mfalme akamuhurumia Jeremia na kutuma watumishi wake wakamwokoe kabla hajafa.

**Kisima kikavu**

Kisima hakikuwa na maji yoyote ndani yake, lakini bado kina matope chini . Hii inaweza kutafsiriwa kama " kisima tupu."

**Alikuwa na huruma kwake**

Hii ina maana alikuwa aina yaJeremia na alimsaidia

**translationWords**

- tii, mtiifu, utiifu
- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Yeremia
- mfalme
- rehema

## 19:18



Hivyo manabii wakaendelea kuwambiana watu habari njema japo watu waliwachukia, wakiwaonya kuwa Mungu atawaadhibu wasipotubu maana mwokozi atakuja.

### **Aliendelea kuongea kwa niaba ya Mungu**

Hii ni "aliendelea kuwaambia watu kile Mungu alitaka kuwaambia,"

### **ahidiwa kwamba masihi wa Mungu angekuja**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kwamba Mungu aliwaahidi kuwa Masihi angekuja kuokoa watu wake."

Simulizi ya Biblia kutoka: Wafalme ya kwanza 16-18; Wafalme ya pili 5; Yeria 38

### **translationWords**

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Mungu
- Kutubu, toba
- Ahadi
- Kristo, Masihi

## 20. Kuchukuliwa Mateka na Kurudi

20:01



Ufalme wa Israel na ufalme wa Yuda walitenda dhambi mbele za Mungu. walivunja agano waliloweka na Mungu Sinai. Mungu aliwatuma Manabii wake kuwaonya ili watubu na kumuabudu yeye lakini walikataa.

### Walivunja agano

Hii ni kwamba, " hawakuzitii amri za Mungu alizowapa ndani ya agano lake katika Mlima Sinai."

### Aliwaonya watubu na wamwabudu yeye tena.

Namna nyingine ya kutafasiri ni, " aliwambia waache kutenda dhambi na wamwabudu Yawee badala ya miungu mingine, au mabaya yatawapata."

### translationWords

- ufalme wa Israeli
- Yuda, ufalme wa Yuda
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- Agano
- Sinai, Mlima Sinai
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kutubu, toba
- Abudu
- tii, mtiifu, utiifu



**20:02**

Ndipo Mungu aliadhibu falme zote kwa kuruhusu maadui zao kuwapiga. Ufame wa Ashuru ulikua ni ufalme wenye nguvu, taifa korofi likaharibu ufalme wa Israel. katika ufalme wa Israel Waashuru waliwaua watu wengi sana na kuwanyag'anya kila kitu cha thamani kisha kuchoma moto sehemu kubwa ya ardhi yao.

**Falme zote**

Hii ilimanisha falme zote za Israel na Yuda.

**Ufalme**

Nchi iliitwa "Ufalme" pale ambapo ilikuwa na nguvu kuongeza mamlaka yake kuzitawala nchi zingine."

**Kunyang'anya**

Hii ni inamaanisha kuwa, "kuiba". waliiba baadhi ya vitu na wakavibeba kuvipeleka Ashuru.

**translationWords**

- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru
- ufalme wa Israeli



## 20:03



Waashuru waliwakusanya viongozi wote, matajiri na watu wenye ujuzi kisha kuwapeleka Ashuru. Masikini ambao hawakuuawa ndio waliobaki Israeli.

### Wenye ujuzi

Hii inarejea ujuzi wa vitendo kama vile, fundi wa mbao, mtengeneza vyuma na mjenzi.


### Walibakia

Inamaanisha, " walibaki" au " waliachwa" au " waliruhusiwa kubaki"

### translationWords

- [Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru](#)
- [Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli](#)
- [ufalme wa Israeli](#)

## 20:04



Waashuru waliwaleta wageni ili waishi katika nchi ya Israel. Wageni hao walijenga miji iliyoharibiwa na kuoa waisrael waliobaki. Kizazi cha wana wa Israel waliooana wa wageni kiliitwa Wasamaria.

### **Wageni katika nchi isiyokuwa yao.**

Hii inarejea watu wasiyokuwa wa israel.( wageni katika nchi ya israel).

### **translationWords**

- Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru
- ufalme wa Israeli
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- uzao, kutokana na
- Samaria, Msamaria

**20:05**

Watu wa ufame wa Yuda waliona jinsi ambavyo Mungu alivyowaadhibu watu wa Israel kwa kutokumtii na kumwamini Mungu. lakini waliendelea kuiabudu miungu na akiwemo Mungu wa wakaanani. Mungu alituma manabii kuwaonya lakini hawakusikia.

**Kwa kutokumuamini na kumtii yeye**

Namna nyingine ya kusema ni, "Kwa sababu hawakumuamini na kumtii yeye."

**Aliwaonya.**

Hii ni kwamba, "Aliwaambia waache kutenda dhambi au mabaya yatawapata.

**Walikataa kusikia.**

Inamaana ya kuwa, "walikataa kutii" au "walikataa kuziacha tabia zao za uovu."

**translationWords**

- Yuda, ufalme wa Yuda
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- ufalme wa Israeli
- Kuamini, kuamini katika
- tii, mtiifu, utiifu
- Abudu
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike
- Kanaani, Mkanaani
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.



**20:06**

Takribani miaka 100 baada ya Waashuru kuharibu ufalme wa Israeli Mungu alimtuma Nebukadneza mfalme wa Babiloni kuvamia taifa la Yuda. Babiloni lilikua taifa yenye nguvu. Mfalme wa Yuda akakubali kuwa mtumishi wa Nebukadneza na kulipwa pesa nyingi kila mwaka.

**Ufalme**

Angalia namna ilivyotafasiriwa hapo juu

**Walikubali kuwa**

Mfalme wa Yuda alilazimishwa kati ya kuhudumia ufalme wa babiloni au uharibiwe

**Kuwa mtumishi wa Nebukadneza**

Inamaanisha ya kuwa, "Kuongoza Yuda chini ya Amri ya Nebukadneza."

**translationWords**

- Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru
- ufalme wa Israeli
- Mungu
- Nebukadneza
- mfalme
- Mji wa Babeli
- Yuda, ufalme wa Yuda
- mtumishi, mtumwa, utumwa



## 20:07



Miaka michace baadae Mfalme wa Yuda akasi juu ya Babiloni. Ndipo wababiloni wakarudi na kuuteka ufalme wa Yuda. Waliuvamia mji wa Yerusalem wakaharibu hekalu na kuchukua vitu vyote vya thamani vilivyokuwemo katika mji.

### Walirudi

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "kurudi" au "wakarudi Yuda tena."

### Wakauteka Mji

Hii ni kwamba, "wakautawala Mji na watu wake,"

### Kunyang'anya

Walichukua vitu vya thamani na kuvipeleka Babiloni.

### translationWords

- Yuda, ufalme wa Yuda
- Waasi, uasi.
- Mji wa Babeli
- Yerusalemu
- hekalu

**20:08**

Kwa sababu ya uasi Askari wa Mfalme Nebukadneza waliwaua watoto wote wa mfalme wa Yuda mbele ya macho yake kisha wakamharibu macho yake. Baada ya hayo wakamchukua mfalme na kumpeleka gerezani Babiloni ili afie huko.

**Kuadhibu**

Nebukadneza alimuadhibu mfalme wa Yuda kwa kuwaambia askari wake wafanye mambo haya.

**Mbele yake**


inamaanisha ya kuwa, " ambapo angeona" au " ili kwamba angeweza kuona" au " mbele ya macho yake."

**akamfanya kipofu**

inaweza kutafasiriwa kama, " akamharibu macho yake."

**translationWords**

- Kuadhibu, adhabu
- mfalme
- Yuda, ufalme wa Yuda
- Nebukadneza
- mwana, mwana wa
- Mji wa Babeli

**20:09**

Mfalme Nebukadneza pamoja na jeshi lake waliwapeleka watu wengi wa Yuda Babiloni, wakawaacha masikini ili wafanye kazi katika mashamba. Kipindi ambacho watu wa Mungu walilazimishwa kuondoka nchi ya ahadi kilitwa kipindi cha Mateka.

**Kuacha.... nyuma**

Hii ni, " kuwaacha watu masikini waishi Yuda" au "kuwaruhusu watu masikini wabaki Yuda."

**kwa kipindi hiki**

inaweza kutafasiriwa kama, "ichagua aya inayoonyesha mda mrefu, kwa sababu utumwa ulikaa miaka sabini.


**mateka**

Neno "mateka" liinamanisha mtu anaondolewa kutoka katika nchi yao kwa nguvu. "Utumwa" ulikuwa ni kipindi cha miaka sabini wakati ambapo waisrael walilazimishwa kuishi Babiloni.

**translationWords**

- [Nebukadneza](#)
- [Yuda, ufalme wa Yuda](#)
- [Mji wa Babeli](#)
- [Mungu](#)
- [Nchi ya ahadi](#)



**20:10**

Japokua Mungu aliwaadhibu watu wake kwa dhambi zao kwa kuwafanya **mateka** lakini hakuwasahau watu wake na ahadi aliyowaahidi. Mungu aliendelea kuwaangalia na kuzungumza nao kupitia manabii. Aliwaahidi kua baada ya miaka sabini atawarudisha kwenye nchi ya ahadi.

**mateka**

Angalia tafasiri kwenye simulizi hapo juu

**Hakusahau**

Hii ingetafasiriwa kama, "hakupuza" au "hakumtelekeza" kifungu hiki cha maneno kingeweza kutafasiriwa kama, "aliendelea kudhamini kujitoka kwake kwa watu wake na ahadi zake,"

**kulinda**

Hii ni "kufanya uangalizi wa karibu"

**Ongea nao kwa njia ya manabii**

Hii ingetafasiriwa kama, waambie manabii wake ujumbe ambao alitaka kuwaambia wa

**translationWords**

- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Ahadi
- Nabii, unabii, mwanaji, nabii mwanamke.



- [Nchi ya ahadi](#)

**20:11**

Miaka sabini baadae mfalme wa Uajemi alimshinda Babiloni hivyo ufalme wa Uajemi ukachukua nafasi ya ufalme wa Babiloni. Waisrael wakaanza kuitwa wayahudi na wengi wao waliishi Babiloni. Wachache waliokua wazee waliikumbuka nchi ya Yuda.

**miaka sabini baadaye**

Hii inamaanisha baada ya kuwa imepita miaka sabini ya jeshi la Babiloni kuwachukua watu wa Yerusalemu utumwani.

**Koreshi**

Koreshi pia iliitwa, "Koresha yenye nguvu." Jina "Koreshi" ilimanisha " kama jua" kwa lugha ya Uajemi. kwa sababu Koresha ilikuwa ya kihistoria ingekuwa vyema kutafasiri jina lake, kuliko kutafasiri maana.

**Waajemi**

Ufalme wa kiajemi ulikua na kumiliki eneo lote kuanzia Urusi ya kati mpka Misri. mahali pake pa kuishi ilikuwa ni sehemu kubwa ya sehemu ya leo iitwayo Irani

**Waisrael wakitwa Wayahudi**

Hii ingetafasiriwa kama, kwa sasa watu wa Israel huitwa Wayahudi."

**Nchi ya Yuda**

Hii ni " Sehemu ambapo Ufalme wa Yuda ulikuwepo kabla ya utumwa.Yerusalemi ulikuwa ni mji mkuu wa Yuda.

## translationWords

- mfalme
- Mji wa Babeli
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi

**20:12**

Ufalme wa Uajemi ulikua na nguvu lakini ulikua na huruma kwa watu waliowateka. Baada ya **Koreshi** kua Mfalme wa Uajemi alitoa amri kuwa Myahudi yeyote anaetaka **kurudi Yuda** anaweza kuondoka uajemi na kurudi Yuda. Aliwapa pesa kwa ajili ya kujenga upya hekalu. Baada ya miaka sabini ya kuwa **mateka** wayahudi wachache walirudi Yuda katika mji wa Yerusalemu.

**Ufalme wa uajemi**

Angalia namna ilivyotafasiriwa hapo juu

**Koreshi**

Angalia namna ilivyotafasiriwa hapo juu

**Yuda**

Angalia maelezo kuhusu Yuda kwenye simulizi

**kurudi kwa Yuda**

kwa sababu Wayahudi wengi walikuwa wana na wajukuu wa wale waliobakia Yuda, hawakuwa wameishi Yuda kabla. Baadhi ya Lugha ingekuwa vizuri kusema, " kwenda Yuda."

**mateka**

Angalia ambavyo imetafasiriwa kwenye simulizi hapo juu




## **kurudi**

Inamaanisha, " walirudi." Lugha zingine zingependa kusema, "rudi" kwa sababu watu wengi hawakuwa wamewahi kufika Yerusalemu.

## **translationWords**

- [rehema](#)
- [Myahudi, Yahudi, Wayahudi](#)
- [hekalu](#)
- [Yerusalemu](#)

**20:13**

Waliporudi Yerusalemu walijenga upya hekalu pamoja na ukuta wa mji. Japokua walikua wakitawaliwa na watu wengine lakini walipata nafasi ya kuishi kwenye nchi ya ahadi na kumwabudu Mungu hekaluni.

**Watu**

Hawa ni waisrael, uzao wa Yakobo, ambao kwa sasa wanaitwa Wayahudi.

**Ukuta**

ukuta huu ulikuwa mpana(2.5 mita) na ulijengwa ili kulinda mji dhidi ya maadui.

**walitawaliwa na watu wengine**

Hii ni kwamba, " taifa jingine liliwatawala. Wayahudi walitawaliwa na Waajemi wakati ule, na badaye mataifa mengine yaliwatawala.

**Kwa nafasi nyingine.**

kwenye baadhi ya Lugha hii ingetafasiriwa kama, "sasa" au " kama ambavyo mababu zao walifanya" au " kabla tu ya utumwa."

**Waliabudu kwenye Hekalu**

Walimwabudu Yawee, yeye aliye Mungu wa kweli, katika hekalu walilojenga.

Simulizi ya Biblia kutoka: 2Wafalme 17; 24-25; 2Mambo ya nyakati 36; Ezra 1-10; Nehemia 1-13

## translationWords

- Yerusalemu
- hekalu
- Nchi ya ahadi
- Abudu

## 21. Mungu Anaahidi Ujio wa Masihi

21:01



**Tangu mwanzo** Mungu alipanga kumtuma masihi na ahadi ya kwanza ilikuwa kwa Adamu na Eva, Mungu akaahidi uzao kutoka kwa Eva kuwa atamponda Nyoka kichwa, Kwa maana aliyemdanganya Eva alikuwa Nyoka nae ni Shetani, ahadi hii inamaanisha mwokozi atakuja kumshinda Shetani.

### Tangu mwanzo

Hiki ni kipindi dunia ilipoumbwa kwa mara ya kwanza.

### Kumponda nyoka kichwa .

Pasipo kichwa cha nyoka kupondwa, nyoka anaweza kumjeruhi mtu. Tumia neno "kuponda" likiwasilisha kwamba kichwa chake kimeharibiwa .

### Nyoka alikuwa shetani

Shetani aliongea na Eva katika umbo la nyoka. Hii haimaanishi kwamba shetani ni nyoka kwa sasa. "Nyoka alikuwa... ni muonekano wa shetani".

### aliyemdanganya Eva

Hii ni kwamba, "aliyemdanganya Eva." Nyoka alimdanganya Eva kwa kumfanya kutia shaka kile Mungu alichokisema ,na kumrubuni asimtii Mungu.



## translationWords

- Mungu
- Kristo, Masihi
- Ahadi
- Adamu
- Hawa
- uzao, kutokana na
- Shetani, ibilisi, yule muovu

## 21:02



Mungu alimuahidi Ibrahim kuwa kupitia yeye watu wote Duniani watabarikiwa, ahadi hii itatimia pale mwokozi atakapokuja, na watu katika makundi wa ulimwengu wataokoka kupitia ujio wa masihi.

### **Kwa yeye**

Hii ni kwamba," sababu ya mmoja wa wazao wake."

### **translationWords**

- Mungu
- Abrahamu, Abram
- Kundi la watu, watu
- Kubariki
- timiza
- Kristo, Masihi
- okoa, salama

## 21:03



Mungu alimuahidi Musa yakwamba baada ya yeye kumaliza atamuinua Nabii mwingine kama yeye, na hii ni ahadi nyingine juu ya ujio wa Masihi kwa siku zijazo.

### **Kuinua nabii mwingine kama Musa.**

Hii ni," kuteua nabii mwingine kama Musa "au," kusababisha nabii mwingine aje atakaye kuwa kama Musa."


### **Nabii kama Musa**

kuwa kama Musa, nabii ajaye atakuwa na mamlaka kuu kutoka kwa Mungu ya kuongoza na kuokoa watu wake.

### **translationWords**

- Mungu
- Ahadi
- Musa
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi

## 21:04



Mungu alimuahidi Mfalme Daudi yakwamba mmoja kati ya mzaliwa wa vizazi vyake atainuliwa nakuwa Mfalme wa watu wa Mungu milele, hii inamaanisha kwamba masihi atakuwa miongoni kizazi kutoka kwa Daudi.

### Uzao wake Daudi

Namna nyingine ya kusema hili, ni "atakuwa mzawa moja kwa moja wa Daudi mwenyewe"

### translationWords

- Mungu
- Ahadi
- Daudi
- Kristo, Masihi
- uzao, kutokana na



**21:05**

KUpitia Nabii Nehemia Mungu aliahidi kuweka maagano mapya, lakini hayatafanana na maagano aliyoweka kwa Wayahudi kwa iziraeli, kwenye maagano mapya Mungu ataandika sheria zake ndani ya miyoyo ya watu ili waweze kumjua kumjua Mungu nao watakuwa watu wake, na Mungu kuwasamehe dhambi zao, masihi kuanza maagano mapya.

**Kupitia nabii Yereimia Mungu aliahidi**

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "Kupitia jumbe ambazo Mungu alimpa Yereimia, Mungu aliahidi, "au, "Nabii Yereimia aliwaambia watu ahadi za Mungu".

**Lakini si kama**

Agano jipya litakuwa kweli na enye matunda. watu watamjua Mungu kweli, wataishi kweli kama watu wake, na atawasamehe dhambi zao kabisa, kutokana na dhabihu ya Masihi mwenyewe kujitoa mara moja kwa wote wamwaminio.

**Andika sheria yake kwenye mioyo ya watu**

Huu ni mfano wa maana, "saidia watu wake kufahamu sheria zake na kutamani kuzitii kwa uaminifu. Ikiwa inawezekana, tunza picha ya maandiko kwenye mioyo yao, tangu hii tofauti ya njia ya Mungu aliaandika sheria zake kwenye vibao vya mawe kwa ajili ya Waesraeli. Ikiwa haiwezekani unaweza kutafsiri maana.

**Kuwa watu wake**

Hii itaweza kuwa imetafsiriwa hivi, "kuwa watu wake wa dhamani," kuwa watu wake wa kipekee."

## Kuanza agano jipya

Hii kwamba, "Kuwa mmoja wa kusababisha agano kuleta matokeo," au, "kuleta agano jipya kwa watu wake."

### translationWords

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Yeria
- Mungu
- Ahadi
- Agano
- Agano
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Sinai, Mlima Sinai
- samehe, kusamehe
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kristo, Masihi

## 21:06




Manabii wa Mungu wanasema masihi nae atakuwa nabii, Kuhani na Mfalme. Maana nabii ni mtu anaesikia neno la Mungu na kulitangaza kwa watu nae aliyeahidiwa kutumwa na Mungu atakuwa ni nabii wa kweli.

### Nabii mkamilifu

Masihi atakuwa ni nabii ambaye ni mkamilifu katika kumtii Mungu, na kuwapa watu kila neno lililonenwa na Mungu, na atamwakilisha Mungu vizuri na kuwasaidia kumjua na kumfahamu Mungu.

### translationWords

- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- Kuhani, ukuhani
- mfalme

**21:07**

Makuhani wa iziraeli walimtolea Mungu dhabihu kwa niaba ya watu kwa hukumu ya dhambi zao pia humuomba Mungu kwaajili ya watu, Mwokozi ni kuhani aliyejitoa kuwa dhabihu kamilifu kwa Mungu.

**Kwa niaba ya**

Hii inaweza kutafsiriwa hivi,"kwa manufaa ya ,"au," kwa sehemu ya ,"

**Kama mbadala wa kuadhibiwa dhambi zao.**

Mungu aliwaruhusu watu kuleta wanyama ili kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zao kama kukumbushwa adhabu ya makosa ya wategemezi wao waliyofanya kwa Mungu na kuondoa dhambi zao. Mungu alizikubali hizo dhambi kama njia ya kufunika dhambi kwa muda mfupi na hakuwadhibu watu kwa ajili ya hilo.

**Kuhani mkuu mkamilifu**

Tofauti na makuhani wakuu wengine, Masihi hatafanya dhambi, na ataondoa kabisa dhambi za watu.

**Kujitoea peke yake.**

Hii ni, " aliruhusu kuuwawa."

**Dhabihu kamilifu**

Hii ni ,"dhabihu ambayo haina kosa, au mawaa".



## translationWords

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Kuhani, ukuhani
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kuomba, maombi
- Kristo, Masihi
- kuhani mkuu

## 21:08



Mfalme ni mtu anaetawala falme na kutoa hukumu kwa watu, mwokozi atakuwa Mfalme mkamilifu na kuweza kumiliki nafasi ya Daudi ili atawale na kutoa hukumu ya haki.

### **kukaa enzini mwa baba zake Daudi**

Kwa desturi, Enzi ni kiti cha mfalme au malkia ambacho kina wakilisha mamlaka yao. Maelezo haya yanaweza kutafsiriwa hivi, "Kuwa na mamlaka ya kutawala kama baba yake Mfalme Daudi alivyofanya", au, "kuwa uzao wa mfalme Daudi na kuendeleza utawala wake juu ya watu wa Mungu."

### **Dunia yote**

Hii ingeweza kutafsiriwa hivi, "Kila mtu kila mahali,"

### **translationWords**

- mfalme
- ufalme
- hukumu
- Kristo, Masihi
- Daudi

**21:09**

Manabii wa Mungu walitabili mengi kuhusu masihi, nabii **Malaki** alitabili ujio wa nabii mkubwa kabla wa Masihi kuja, nae nabii Isaya alitabili mwokozi kuzaliwa na bikila, nabii Maiko alisema masihi atazaliwa katika mji wa Betelehemu.

**Malaki**

Malaki alikuwa nabii wa mwisho katika agano la kale

**Kunenwa kabla**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi,"aliyetabiriwa "au,"aliyetolewa unabii."Ina maana kusema kwamba kitu kitatokea baadaye.Malaki aliongea ujumbe wa Mungu kwa watu miaka 400 kabla ya Masihi kuja.

**Aliyetabiriwa**

Kwa muktadha huu ,"aliyetolewa unabii"ina maana sawa na" aliyetabiriwa"na "anayetazamiwa," inamaanisha nabii alisema kitu ambacho itatokea kwa muda mrefu wa baadaye.

**Masihi atazaliwa na bikira**

Njia nyingine ya kusema hii itaweza kuwa," bikira anatajifungua Masihi."

**Mika**

Mika alikuwa nabii wa Mungu katika Agano la kale ambaye, kama Isaya, aliongea ujumbe kutoka kwa Mungu takriban miaka 800 kabla ya Masihi kuja

## translationWords

- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- Isaya
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Bikira
- Bethlehemu



**21:10**

Nabii Isaya alisemamasihi ataishi Galilaya, atawafariji waliopondeka moyo na kutangaza uhuru kwa waliofungwa, pia walitabili masihi ataponya wagonjwa, viziwi, vipofu na mabubu.

**Watu waliovunjika moyo**

Hii inaeleza na kurejea watu waopitia katika huzuni iliyokithiri

**Kuwatangazia uhuru mateka**

Hii ni kwamba, "kuwambia wafungwa wanaweza kuwa huru." Hii pia iaweza kumaanisha kuweka huru watu kutoka kwenye utumwa wa dhambi.

**kuwatoa magerezani**

Ni kwamba, "atawaweka huru wote waliokuwa na dhuluma waliokuwa ndani ya kifungo". Hii inaweza pia kurejea kuwaweka watu huru kutoka kwenye mzigo wa dhambi

**Wasiweze kusikia, kuona, kuongea, au kutembea.**

Inaweza kuwa vizuri kusema, "wasiosikia, wasioona, wasioongea, au wasiotembea, Baadhi ya lugha zingine zina maneno ya kipekee katika hali hizi, "kiziwi" "kipofu".

**translationWords**

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Isaya
- Galilaya, Mgalilaya
- Kristo, Masihi

- [Ponya, tibu](#)

**21:11**

Nabii Isaya alitabili juu ya kujchukiwa masihi atachukiwa bila sababu na kukataliwa, manabii wengine walinena yakwamba watakao kumuua masihi watagawa nguo zake na msaliti atakuwa mtu wa kalibu yake, nae nabii **Zakaria** akanena yakwamba sarafu thesini za fedha zitatumika kumlipa awezekumsaliti masihi.

**Kuchukiwa bila sababu na kukataliwa.**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi, "kuchukiwa na kukataliwa, hata hivyo hakufanya chochote cha tofauti, "au" hata hivyo hakuwa na hatia."

**Kunenwa kabla**

Hii inamaanisha kwamba aliyenena kuhusu vitu vinaweza kutoka kwa baadaye. Maneno mengine yenye maana sawa ni "aliyetabiriwa" aliyetolewa unabii"

**Kugawa nguo zake**

Hii ni, "kucheza mchezo wa kamari na kutambua ambaye anaweza kushinda nguo zake."

**Zakaria**

Zakaria alikuwa nabii katika agano la kale ambaye aliongea na watu wa Mungu baada ya kurudi katika nchi waliyoahidiwa kutoka utumwani Babeli. Hii ilikuwakati miaka 500 kabla ya masihi kuja .

**Sarafu thelathini za fedha .**

Kwa wakati huo kila sarafu ilikuwa na thamani ya kiasi cha fedha ya mtu kuweza kuingiza kwa siku nne.

## translationWords

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Isaya
- Kristo, Masihi
- kusaliti



## 21:12



Manabii walisema ni jinsi gani mwokozi atakufa, Isaya alitabili yakwamba watu wata mtemea mate, kumdhihaki na kumpiga masihi, kumsulubisha wataamchoma mkuki nae atakufa na maumivu makali ijapokuwa hakutenda lolote baya.

### Kuchomwa

Hii ni, "kumchoma," kitu chenye ncha kali kitakachoweza kupenyeza mwilini mwake kama sehemu ya kuadhibiwa kwa dhambi za watu.

### translationWords

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- kifo, kufa, mfu
- Isaya

**21:13**

Manabii walisema yakwamba masihi alikuwa mkamilifu na hakuwa na dhambi, alikufa ili azichukue dhambi za watu, mateso yake yataleta amani kati ya Mungu na wanadamu kwa maana hiyo ndipo Mungu akamsuribisha masihi.

**Hakuwa na dhambi**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa "Hakuwahi kutenda dhambi,"

**Anapokea adhabu kwa ajili ya dhambi za watu wengine**

Hii ni kusema, "Kuchukua pekee yake adhabu ambazo wengine walitenda," au "kuadhibiwa katika sehemu ya watu wengine."

**Ilikuwa Utayari wa Mungu**

Hii ni , "kujazwa kusudi la Mungu." kipengele hiki kinaamania kwamba kifo cha Masihi kilikuwa tayari kimepangwa na Mungu kutokea ili kwamba dhambi itaweza kulipia dhambi za watu.

**kuharibu**


Ni kwamba , "kutupa kabisa," kuuu, "au, kumaliza kuharibu,"

**translationWords**

- Nabii, unabii, mwanaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- kifo, kufa, mfu

- Kupokea
- Kuadhibu, adhabu
- Amani
- Mungu

## 21:14



Manabii walinena yakwamba masihi atakufa na Mungu atamuinua kutoka kwa wafu, kutokana na kifo na kufufuka kwa masihi, Mungu amekamilisha mpango wake wa kuokoa na dhambi na kuanza agano jipya.

### **Kumfufua yeye katika wafu**

Ni kwamba" kumsababisha yeye kuwa hai tena ,"

### **Kupitia kifo cha Masihi na ufufuo ,Mungu ataweza.**

Hii inaweza ikawa imetafsiriwa hivi,"Mungu ataweza kutumia kifo cha masihi na ufufuo "au" kifo cha Masihi na ufufuo kinaweza kuwa njia ambayo Mungu ataweza.


### **Kuanza agano jipya**

Ni kwamba 'kuweka agano jipya ndani ya matokeo."

### **translationWords**

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- kifo, kufa, mfu
- Mungu
- inua, inuka
- Ufufuo
- okoa, salama
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Agano



**21:15**

Mungu aliwaonyesha mambo mengi kwa manabii kuhusu mwokozi, bali masihi hakuja kwa wakati wa manabii wengine na ni zaidi ya miaka, 400 baada ya nabii wa mwisho kupitta na wakati timilifu Mungu alimtuma masihi Duniani.

**Ndani ya ulimwengu**

Hii ingeweza kutafsiri kama, "Kwa watu wa ulimwengu." Masihi atatumwa si tu kwa wayahudi, bali kwa watu wote.

Simuliza ya Biblia Kutoka: Mwanzo 3:15; 12:1-3; Kumbukumbu la Torati 18:15; 2Samweli 7; Yeremia 31; Isaya 59:16; Danieli 7; Malaki 4:5; Isaya 7:14; Mika 5:2; Isaya 9:1-7; 35:3-5; 61; 53; Zaburi 22:18; 35:19; 69:4; 41:9; Zakaria 11:12-13; Isaya 50:6; Zaburi 16:10-11

**translationWords**

- Mungu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi

## 22. Kuzaliwa kwa Yohana

22:01



Hapo zamani Mungu alikua akiongea na watu wake kwa kupitia Malaika na Manabii. Ilipita miaka 400 Mungu alikua hajazungumza na watu wake. Ghafila Malaika alikuja na ujumbe kutoka kwa Mungu kwenda kwa kuhani mzee aitwae Zakaria. Zakaria na mke wake Elizabeti walikua ni watu wa Mungu lakini Elizabeti alikuwa hajapata mtoto yeyote.

### Watu wake

Hii ingeweza kuwa imetafsiriwa kama, "watu wake wa Israeli "au" watu wake, Wayahudi." Lakini inajumuisha maelezo ya nyongeza kama haijaleweka watu hawa walikuwa wakina nani.

### Miaka 400 iliopita

Namna nyingine ya kusema hili ingekuwa, "miaka 400 ilipita," au hii ilikuwa miaka 400." Miaka 400 ilikuwa imepita tangu Malaki, nabii wa mwisho katika agano la kale.

### Wakati hakuongea nao.

Hiki ni, "kipindi ambacho Mungu hakukuwapa jumbe manabii wake kwa ajili ya watu wake."

### Watu wanaomcha Mungu

Ni kwamb,a "watu waliomtii Mungu."

## translationWords

- Mungu
- Malaika, Malaika mkuu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kuhani, ukuhani
- Zakaria (Agano Jipya)

**22:02**

**Malaika** akamwambia Zakaria "tazama mke wako atapata mtoto wa kiume, nawe utamuita jina lake Yohana. Nae atajazwa Roho Mtakatifu na atawaandaa watu kwaajili ya Kristo!". Zakaria akamjibu "Mimi na mke wangu tu wazee sana kuweza kupata watoto. Nitajuaje kama haya yatatokea?"

**Malaika**

Hii inamaanisha malaika aliyekuja kwa Zakaria ".

**Aliyejazwa na Roho Mtakatifu**

Ni kwamba," aliyelongozwa na Roho Mtakatifu "au" aliyepewa hekima na nguvu na Roho Mtakatifu."

**Ninawezaje kujua hili litatokea?**

Njia nyingine ya kutafsiriwa ni, "Ninawezaje kuwa na uhakika kwamba hili litatokea kweli?"

**translationWords**

- Malaika, Malaika mkuu
- Zakaria (Agano Jipya)
- Yohana (Mbatizaji)
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Kristo, Masihi



**22:03**

Malaika akamjibu Zakaria akasema " tazama nilitumwa na Mungu kukuletea habari hizi njema. Kwakua umeshindwa kuniamini hutaweza kuongea mpaka pale mtoto atakapozaliwa" Hapohapo Zakaria hakuweza kuongea. Ndipo malaika alimuacha Zakaria. Baada ya hapo Zakaria alirudi nyumbani na mke wake akapata mimba.

**Kuwa mjamzito**

Baadhi ya lugha zingine zina njia zenye adabu na kusema , "kuwa mjamzito" Tumia maelezo ambayo hayatawadhalilisha wasomaji.

**translationWords**

- Malaika, Malaika mkuu
- Mungu
- Kuamini, kuamini katika
- Zakaria (Agano Jipya)

**22:04**

Elizabeth alipokuwa na mimba ya miezi sita, malaika yule yule alimtokea ndugu yake Elizabeth aliyelitwa Maria. Alikuwa ni bikira na alikuwa amechumbiwa aolewe na kijana aitwae Yusufu. Malaika akamwambia "Tazama utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume. Utamuita jina lake Yesu. Atakuwa ni mtoto wa Mungu aliye juu na atatawala milele."

**Mimba ya miezi sita**

Alishakuwa tayari na ujuzito wa miezi sita au alikuwa ndani ya miezi sita ya mimba yake.

**Mjamzito.**

Lugha tofauti zina tamaduni tofauti za kuongea kuhusu ujuzito, kama alikuwana mtoto, "au" alikuwa na mmoja kwenye mwili wake au "alikuwa na tumbo." Baadhi ya lugha zina njia za kipekee zenye adabu, kama anatarajia. "Tumia maelezo ya kwamba ambayo hayatawadhalilisha wasomaji.

**Elizabeth.**

Alikuwa mke wa Zakaria. Malaika alimwambia Zakaria kwamba Elizabeth angejifungua mtoto mwanaume.

**Jamaa ya Elizabeth**

Tafsiri nyingi zinasema "binamu" lakini hapa hatuwezi kujua kwa uhakika namna gani hawa wanawake wawili walirandana. Neno la jumla kama "jamaa" au "binamu" litaweza kuwa limetumika.

**Alikuwa amechumbiwa .**

Ni kwamba ilikuwa ahadi.

## translationWords

- Malaika, Malaika mkuu
- Mariamu, mama yake Yesu
- Bikira
- Yusufu (Agano Jipya)
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba

**22:05**

Maria akajibu "Inawezekanaje jambo hili kutokea ingali mimi ni bikira?" Malaika akamwambia "Roho wa Bwana atakuja kwako na nguvu za Mungu zitakuwa juu yako na kukufunika kama kivuli. Kwa sababu hiyo mtoto atakuwa mtakatifu, mwana wa Mungu". Maria akaamini na kukubali alichambiwa na malaika.

**Namna gani hii inaweza kuwa.**

Ni kwa kwamba "Namna gani naweza kuwa mjamzito?" Mariamu hakuwa na mashaka na ukweli wa maneno ya malaika, lakini anauliza inawezaje kutokea.

**Roho Mtakatifu atakuja na nguvu ya Mungu itakufunika**

Hizi ni njia mbili zinasema kitu kimoja." Kwa nguvu ya Mungu, Roho Mtakatifu atakusababisha kwa muujiza uwe mjamzito." Akikisha tafsiri ya maneno haya hayatamkwi kama kulikuwa mawasiliano yoyote ya kimwili yaliyojumuishwa. Hii ilikuwa muujiza.

**translationWords**

- Mariamu, mama yake Yesu
- Bikira
- Malaika, Malaika mkuu
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Nguvu
- Mungu
- takatifu, utakatifu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Kuamini, kuamini katika



**22:06**

Baada ya malaika kuongea na Maria, Maria akaenda kumtembelea Elizabeti. Baada ya Elizabeti kusikia salaamu ya Maria mtoto aliekuwepo tumboni kwake aliruka. Na wote wawili walishangilia kwa furaha mambo mazuri waliotendewa. Baada ya Maria kumtembelea Elizabeti kwa miezi mitatu. Maria alirudi nyumbani kwake.

**Elizbethi**

Angalia maelezo kuhusu Elizabeti

**Upesi Elizabeti aliposikia salamu ya Mariamu**

Kwa baadhi ya lugha zingine ingekuwa vizuri kusema, "Mariamu alipomsalimia Elizabeti na ghafla Elizabeti alimsikia.

**Kichanga kiliruka ndani yake**

Kichanga kilisogea haraka ndani ya tumbo la Elizabeti na kujibu salamu ya Mariamu .

**Nini Mungu alifanya kwao**

Hii inarejea kwamba wanawake wote wawili walikuwa wajawazito kupitia uwezo wa kimungu .Mariamu alibeba mimba bila mwanaume, na Elizabeti alibeba mimba na Zakaria baada ya kupitisha muda wa kuzaa mtoto.

**translationWords**

- Malaika, Malaika mkuu
- Mariamu, mama yake Yesu
- Mungu

**22:07**

Baada ya **Elizabeti** kujifungua mtoto wake wa kiume, Zakaria na Elizabeti walimuita huyo mtoto Yohana, kama malaika alivyoamuru. Kisha Mungu alifungua kinywa cha Zakaria na akaweza kusema tena. Zakaria alisema "Asifiwe Mungu kwa kuwa amewakumbuka watu wake! Nawe mwanangu utaitwa nabii wa Mungu aliye juu utakae waambia watu jinsi ya kupokea msamaha wa dhambi zao.

**Elizabeti**

Angalia maelezo kuhusu Elizabeti

**Mungu asifiwe**

Ni kwamba , "Wote tunaweza kumsifu Mungu."

**Ataitwa**

Hii ni njia nyingine ya kusema", ingekuwa , "au'itajulikana kama, Kwa hakika Yohana aliweza kuwa nabii wa Mungu aliye juu.

**Nabii**

Ni kwamba , "nabii muhimu sana" Yohana angekuwa nabii ambapo agano la kale manabii waliotabiriwa wangekuja kabla ya masihi.

## Mungu mkuu

Njia nyingine kusema hii ingekuwa Mungu ambaye ni mkuu sana kuliko vitu vyote" au "Mungu ambaye anatawala juu ya kila kitu."

Simulizi ya Biblia kutoka: Luka 1

## translationWords

- Zakaria (Agano Jipya)
- Yohana (Mbatizaji)
- Malaika, Malaika mkuu
- Mungu
- Zakaria (Agano Jipya)
- Kusifu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- samehe, kusamehe
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

## 23. Kuzaliwa kwa Yesu

23:01



Mariamu alikuwa amechumbiwa na mtu mwadilifu aitwaye Yusufu. Yusufu kwasababu ya uhaki hakutaka Mariamu apate aibu kwaajili ya ujauzito ambao haukumhusu hivyo akaanza kutafuta njia akwepe kwa siri. Malaika akamtokea Yusufu katika ndoto.

### Alijua hakuwa mtoto wake

Ni kwamba,"alijua kwamba si ye mmoja ambaye alisababisha yeye kuwa mjamzito."

### Kumuabisha Mariamu

Ni kwamba ,"kusababisha Mariamu kufedheheka au," kumdhalilisha Mariamu katika jamii ,"Yusufu alikuwa mtiifu kwa Mariamu hata hivyo ingeonekana kama alikuwa kwenye uzinzi.

### Alipanga kwa siri kumuacha

Hii inaweza ikatafsiriwa kuwa alipanga kumuacha bila kuwambia wengine kwa nini" ,au alipanga kumuacha yeye bila kuwambia wengine kuhusu ujauzito wake ."Kwa sababu Yosefu alikuwa mwenye haki, alitaka kutatua hali hiyo kwa njia nzuri inayowezekana, ambayo ndani ya tamaduni inaweza kumpa talaka kwa siri.

### Kumuacha

Kwa baadhi ya lugha zingine ingekuwa vizuri kusema,"kuvunja uchumba"au Yusufu na Mariamu walichumbiana au,"waliahidiana kuoana," Lakini utamaduni wa Kiyahudi kuchana ilikuwa inatakiwa ili kuvunja uchumba.




## **Kwenye ndoto**

Ni kwamba,wakati alikuwa amelala na ndotoni"

### **translationWords**

- Mariamu, mama yake Yesu
- Adili, uadilifu
- Yusufu (Agano Jipya)
- Malaika, Malaika mkuu
- ndoto

**23:02**

Ndipo Malaika akamtahadharisha Yusufu kwamba asimwache Mariamu kwasababu mimba hiyo ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu hivyo asiwe na wasiwasi. Mtoto atakayezaliwa ni wa kiume ataitwa jina lake Yesu (yaani Yehova huokoa), kwa kuwa atawaokoa watu waondoke dhambini.

**Usogope kumchukua Mariamu kama mkeo**

Hii pia iliweza kuwa imetafsiriwa hivi, Acha kufikiri hutaweza kumuoa Mariamu"au,"Usisite kuwa na Mariamu kama mke wako."

**Ni kutokana na Roho Mtakatifu**

Ni kwamba,"alibeba mimba kwa muujiza wa Roho Mtakatifu."

**translationWords**

- Malaika, Malaika mkuu
- Yusufu (Agano Jipya)
- Mariamu, mama yake Yesu
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- mwana, mwana wa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Yaweh
- okoa, salama
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

## 23:03



Yusufu aliamua kumchukua Mariamu kuwa mkewe; lakini, hawakukaribiana mpaka pale Mariamu atakapomzaa mwana.

### Hakulala naye

Ni kwamba , "hakushiriki tendo la ndoa naye." Alitunza ubikira wake mpaka kuzaliwa kwa mtoto.

### translationWords

- Yusufu (Agano Jipya)
- Mariamu, mama yake Yesu

**23:04**

wakati Mariamu alipokaribia kuzaa, ni kipindi kile utawala wa Rumi ulielekeza kila mtu ahesabiwe katika jamii anayotokea. Hapa inabidi sasa Yusufu na Mariamu wasafiri safari ndefu waelekee Bethlehemu tokea Nazareti kwa sababu ndiyo mji wao kwa asali yaani mji wa Daudi.

**Wakati muda ulipofika wa Mariamu kuzaa**

Ni kwamba, "Wakati ulipokaribia mwisho wa ujauzito wa Mariamu."

**Serikali ya Kirumi**

Rumi ilikuwa imeteka na kutawala juu ya Israeli kwa wakati huu.

**Kwa ajili ya Sensa**

Ni kwamba Kuwa wamehesabiwa kwa ajili ya kunakili. "au," Kwamba serikali iweze kuandika majina yao kwenye orodha "au wawe wamehesabiwa na serikali." Sensa hii ilikuwa haswa inafanywa kwakusudi la kuwatoza watu kodi.

**translationWords**

- [Mariamu, mama yake Yesu](#)
- [Rumi](#)
- [Yusufu \(Agano Jipya\)](#)
- [Nazarethi, Nazarini](#)
- [Bethlehemu](#)
- [Daudi](#)



**23:05**

Baada ya kufika Bethlehemu hapakuwa na mahali ya kujihifadhi. Nafasi waliyopata ni pale mifugo ilihifadhiwa, ndipo mtoto alipozaliwa na mama yake alimlaza kwenye lishio la ng'ombe kwa kuwa hakuna kitanda; jina lake alitwa Yesu.

**Hakuna nafasi ya kukaa**

Ni kwamba ",hakuna nafasi ya kawaida ya kukaa".Kwa sababu Bethlehemu ilijaa watu wengi kwa wakati ule.vyumba vya kawaida kwa wageni tayari vilishajaa.

**Eneo ambalo wanyama waliishi.**

Hili lilikuwa ni eneo la kulaza wanyama,siyo eneo waliloishi watu.Tafsiri hili kwa neno kwamba lilikuwa kwa kawaida eneo la kulishia wanyama.

**Hori la kulishia**

Ni kwamba ,"boksi la kulisha wanyama"au,la mbao,au boksi la jiwe kwa ajili ya kulishia wanyama."Boksi lilokuwa limejazwa na nyasi kavu kupatia nyasi laini usoni kwa mtoto kulazwa chini.

**translationWords**

- [Bethlehemu](#)
- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)

**23:06**

Usiku ule ule walikuwepo wachungaji wa maeneo jirani wakilinda mifugo yao. Ghafla waliona malaika akin'gaa mbele yao wakatekewa; Malaika akasema, "msiwe na wasiwasi ninazo habari nzuri. Kristo Bwana amezaliwa Bethlehem!"

**Wakichunga mifugo yao**

"Mifugo" ni kundi la kondoo wachungaji walikuwa wakilinda kondoo ,na kuwalindaa kutoka wezi.

**Mng'ao wa malaika**

Hii ingeweza pia kuwa imetafsiriwa hivi,"malaika alizungukwa na mwanga mkali."Mng'ao wa mwanga ulionekana kama mwanga unaoshabihiana na giza la usiku.

**Waliogopa**

Kutokea kwa malaika mwenye nguvu ya ki

**Msiogope.**

Hii mara zote humanisha , "acha kuwa na mashaka."Wachungaji walikuwa na mashakawakati walipomuona malaika alikuwa akiwaambia hamhitaji kuwa na wasiwasi.

**translationWords**

- mchungaji, kuchunga
- Malaika, Malaika mkuu
- Kristo, Masihi
- bwana, mkuu

- [Bethlehemu](#)

**23:07**

Akaongeza; "nendeni kwa mtoto, mtamuona amefungwa nguo akiwa amelazwa kwenye lishio la mifugo."  
Mawinguni walionekana Malaika, wakitukuza na kuimba Utukufu uko mbinguni kwa Mungu na amani duniani kwa wapendwa."

**Hori la kulisha**

Ni kwamba,"Boksi la kulishia wanyama."Pia angalia namna hii ilivyotafsiriwa

**Alifungwa kwenye vipande vya nguo.**

tamaduni za wakati huo zilikuwa kuwabana watoto wanaozaliwa ndani nguo ndefu .Ingeweza kuwa muhimu kusema,alifungwa kwenye nguo ndefu zinazotawala ndani ya njia za kitamaduni."

**Walijazwa na malaika**

Hii inaamaanisha kwamba pale palikuwa na malaika walioona kujaa kwa mawingu

**Utukufu kwa Mungu**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa ,"Acha tumpe Mungu utukufu!"au"Mungu anastahiliheshima yote na utukufu!"au,Wote tumpe utukufu Mungu!"

**Amani duniani**

Njia nyingine kusema hii ingeweza kuwa," amani iwepo duniani ,"



## Watu aliwaridhia

Hii iwe imetafsiriwa hivi,'watu ambao Mungu huwaangalia juu kwa kuwaridhia furaha ,au kuwapa matumaini mema."

## translationWords

- Malaika, Malaika mkuu
- Mungu
- utukufu, fahari
- mbingu, anga, mbinguni
- Amani

## 23:08



Wachungaji walifika mahali pale alipokuwa Yesu kama maelekezo ya malaika yalivyokuwa wakiwa wamejawa furaha. Baada ya hapo wakarudi ilipokuwa mifugo yao; wakimtukuza Mungu kwa yale waliyosikia na kuyaona.

### Yote waliyosikia na kuona

Ni kwamba , " kwa kila kitu walichosikia na kuona."Hii inajumuisha Malaika wa utukufu na ujumbe wa ajabu pamoja kuona

### translationWords

- mchungaji, kuchunga
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Malaika, Malaika mkuu
- Mariamu, mama yake Yesu
- Kusifu
- Mungu

**23:09**

Badaye wenye ujuzi tokea mashariki ya mbali wakiongozwa na nyota walifika Bethlehemu na hapo wakatambua ile nyota ilimaanisha Mfalme wa Wayahudi. Hivyo wakasafiri safari ndefu na wakaipata nyumba alimokuwa Yesu akiwa pamoja na wazazi wake.

**Baadaye**

Haikuwa sahihi ni muda gani ulikuwa baada ya kuzaliwa mtoto kabla wenye busara alipoiona nyota, lakini inaweza kuchukua muda wa miaka miwili kwa wao kujianda kwa safari na kusafiri kwenda Bethlehemu.

**Wenye busara**

"Wenye busara" walikuwa waganga ambao wamesoma nyota , Pia walikuwa na uwezo wa kuwa manabii katika agano la kale waliandika na kutabiri kuzaliwa kwa masihi

**Nyota isiyo ya kawada**

Nyota walivyotaarifiwa haikuwa nyota ya kawada. Ilikuwa ni kitu ambacho kilitokea muda aliozaliwa Yesu .

**Waligundua**

Baadhi ya lugha zinaongeza kutoka katika masomo yao, hawa wanafunzi waligundua."

**Nyumba**

Hawakukaa tena kwenye eneo la wanyama ambapo alizaliwa.

## translationWords

- Busara, hekima
- Mfalme wa Wayahudi
- Bethlehemu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



## 23:10



Na wataalamu hawa walipomuona Yesu na mama yake, wakainama na kumwabudu. Ndipo walimpa Yesu zawadi za gharama kubwa. Wakarudi kwao mashariki.

### Wenye busara

Wenye busara

### Wakainama

Ni kwamba,"wakainama chini kwenye ardhi,"wakati huo hii ilikuwa desturi ya kuonyesha heshima kubwa au kuheshimu

### Ya ghali

Ni kwamba,"yenye dhamani sana."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 1; Luka 2

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Abudu

## 24. Yohana Anambatiza Yesu

### 24:01



Yohana mwana wa Zakaria na Elizabeth alikuwa na akawa nabii .Aliishi nyikani akila asali ya porini, nzige ,na kuvaa nguo zilizotengenezwa na manyoya ya ngamia.

### Nyikani

Ni kwamba , "jangwa" eneo la kijijini, "Palikuwa na watu wachache waliokuwa wakiishi kwenye eneo hilo

### Asali ya porini

,Hii asali ilikuwa ni alisi kutoka kwenye nyuki. huko nyikani.Haikuwa inalimwa na watu.Ikiwa kwamba watu wanaelewa kwa neno "asali" haitajiki kuitwa "pori."

### Nzige

Hawa walikuwa wakubwa wadudu warukao kwa mabawa ,kama wakubwa panzi .Baadhi ya watu wanaoishi jangwani huwala.

### Manyoya ya ngamia

Ngamia ni mnyama ambaye ana nywele zisizo na mpangilio.Watu huweza kutengeneza nguo nje ya hiyo.Hii inaweza kuwa imetafsiriwa kama mnyama mwenye nywele zisizo na mpangilio.

## **mavazi yaliyotengenezwa na nywele za ngamia.**

Ni kwamba,mavazi ya singa yaliyotengenezwa na nywele za ngamia.Nguo hizo huwezi kiraisi kuvaa nje ya jangwani kama nguo zingine zinavyovaliwa.

### **translationWords**

- Yohana (Mbatizaji)
- Zakaria (Agano Jipya)
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

## 24:02



Watu wengi walimfuata Yohana nyikani kumsikiliza. Aliwahubiri akisema, "tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia"

### Jangwani

Angalia jinsi wewe unaweza kutafasili hili neno katika 24-1

### Tubu

Ingekuwa vizuri kusema , "tubu kutoka katika dhambi zako."

### Ufalme wa Mungu uko karibu

Ni kwamba , "Ufalme wa Mungu upo tayari kutokea" au, "ufalme wa Mungu utakuja upesi." Hii inarejea Mungu kutawala juu ya watu, .Hii pia inaweza kuwa imetafsiriwa . "Mungu anatawala ni kuhusu mwanzo." au. "Upesi Mungu atatawala juu yetu kama mfalme."

### translationWords

- Yohana (Mbatizaji)
- Kuhubiri
- Kutubu, toba
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni



**24:03**

Wakati watu waliposikia ujumbe wa Yohana wengi walitubu dhambi zao na kubatizwa .Viongozi wengi wa dini walikuja kubatizwa na Yohana lakini hawakutubu wala kuungama dhambi zao .

**Wakatubu kutoka katika dhambi zao**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa kama , "walitubu kulingana na dhambi zao" au, "walitoka katika dhambi zao."

**Hawakutubu**


Ni kwamba, "hawakutoka katika dhambi zao."

**Kuungama dhambi zao.**

Kuungama ni kukubali kwamba kitu chochote ni kweli. Hawa viongozi hawakutaka kukubali kuwa walifanya dhambi. Hii inaweza kuwa imetafsiriwa kama kuungama kwamba wamefanya dhambi, ".

**translationWords**

- Yohana (Mbatizaji)
- Kutubu, toba
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Batiza, ubatizo
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini

**24:04**

Yohana akawaambia viongozi wa dini" enyi nyoka wenye sumu! tubuni na kubadilisha tabia zenu. **Kila mti usiozaa matunda mema** hukatwa na kutupwa motoni. **Yohana alitimiza** kile kilichosemwa na manabii "angalia namtuma mjumbe wangu mbele yenu ambaye atawandalia njia zenu."

**Enyi nyoka wenye sumu**

Hii inawezakuwa imetafsiriwa , "Mmelala kama nyoka wenye sumu!" Yohana aliwaita wenye sumu ya nyoka kwa sababu walikuwahatari na wadanganyifu.

**Kila mti usiozaa matunda mema**

Yohana hakuwa kweli akiongea kuhusu miti .Haya ni maelezo kwamba matunda mema kwa matendo mema na mtazamo kwamba hutoka kwa Mungu.

**Yatakatwa chini na kutupwa motoni**

Hii inamaanisha, "yatahukumiwa na kuadhibiwa na Mungu."

**Yohana alitimiza**

Ni kwamba, "Yohana alifanya "ambacho nabii alisema kama mjumbe wa Mungu anaweza fanya.

**Angalia**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa kama , "Tazama" na angalia "au," weka utulivu!.

## **Mjumbe wangu**

Ni kwamba,"Mimi Yahwe nitamtuma mjumbe wangu."Kwa baadhi ya lugha zingine inaweza kuwa zaidi halisi kutumia moja kwa moja nukuu kwa maneno haya,kama :*"Ni kipi nabii Isaya alitabiri wakati aliposema kwamba Mungu anaweza kumtuma mjumbe wake."*

## **Mbele yenu**

Kwenye kipengele hiki neno, "yenu" kinarejea kwa Masihi.

## **Andaa njia yenu**

Ujumbe wa Mungu uliwaandaa watu kumsikiliza masihi.

## **translationWords**

- [Yohana \(Mbatizaji\)](#)
- [viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini](#)
- [Kutubu, toba](#)
- [timiza](#)
- [Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.](#)

## 24:05



Baadhi ya Wayahudi wakamwuliza Yohana kama yeye ni Kristo ,Yohana akajibu mimi siyo Kristo lakini kuna mmoja ajaye baada yangu ambaye ni mkuu sanakwani sistahili kufungua kamba ya viatu vyake .

### **Mkuu sana**

Ni muhimu sana


### **Hata sistahili kufungua viatu vyake**

Kwa maneno mengine , "yalilinganisha naye,Mimi siye muhimu kutosha hata kaziduni kwake.kuvifungua kamba viatu ilikuwa kazi duni ,jambo hilo linaweza kufanywa na mtumwa.

### **translationWords**

- [Myahudi, Yahudi, Wayahudi](#)
- [Yohana \(Mbatizaji\)](#)
- [Kristo, Masihi](#)



**24:06**

Siku iliyofuata Yesu alikuja ili abatizwe na Yohana .Wakati alipomwona Yohana alisema,'angalia huyu ni mwanakondoo wa Mungu atakayechukua dhambi ya ulimwengu.

**Kuna**

Kwa lugha nyingine Hii inaweza kuwa, "Hapa ni ",au "Yule mtu ni."

**Mwana kondoo wa Mungu**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi," Mwanakondoo kutoka kwa Mungu" au dhabihu ya Mwanakondoo ambayo Mungu alitupatia".Anatimiza taswira ambayo iliwakilishwa na dhabihu ya kondoo katika agano la kale.

**Atakayechukua dhambi ya ulimwengu**

Dhabihu ya Yesu ilimfanya Mungu kuangalia dhambi zetu kama hazitatendeka tena

**Dhambi ya ulimwengu**

Ni kwamba ,"dhambi za watu ndani ya dunia ."

**translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)
- [Batiza, ubatizo](#)
- [Yohana \(Mbatizaji\)](#)
- [mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu](#)
- [Mungu](#)
- [dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi](#)

**24:07**

Yohana akamwambia Yesu mimi sistahili kukubatiza wewe ila wewe unastahili kunibatiza mimi. Lakini Yesu akasema "ni lazima kunibatiza mimi kwa sababu ni kitu sahihi kwa hiyo Yohana akambatiza Yesu pamoja na kwamba Yesu hakuwahi kutenda dhambi.

**Sistahili kukubatiza wewe**

Hii inaweza kuwa, " imetafsiriwa hivi , "mimi sistahili kutosha kukubatiza wewe", au , "Mimi ni mwenye dhambi hivyo siwezi kukubatiza wewe,

**Ni kitu sahihi kufanya**

Hii inaweza pia kuwa imetafsiriwa hivi, ni kitu sahihi kufanya , "Hii ni namna Mungu anataka mimi kufanya."

**translationWords**

- Yohana (Mbatizaji)
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Batiza, ubatizo
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**24:08**

Wakati Yesu alipotoka majini baada ya kubatizwa Roho wa Mungu alitokea katika umbo la njiwa alishuka akatulia juu yake. Wakati huo sauti ya Mungu ikaongea kutoka mbinguni na kusema "Wewe ni mwanangu ambaye ninakupenda na ninayependezwa naye".

**Mwana wangu ambaye nakupenda**

Akikisha tafsiri ya hii haitamkwi kama palikuwa na mwana mwingine. Inaweza kuwa lazima kusema, "wewe ni mwanangu. Ninakupenda sana na ninapendezwa nawe."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Batiza, ubatizo
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- mbingu, anga, mbinguni
- Mwana wa Mungu, Mwana
- upendo



**24:09**

Mungu akamwambia Yohana, "Roho wa Mungu atakuja juu ya mtu ambaye umembatiza .Na mtu huyo ni mwana wa Mungu ,"Kuna Mungu mmoja tu.Lakini wakati Yohana alipokuwa akimbatiza Yesu alisikia Baba Mungu akisema na akamuona Mungu mwana ,ambaye ni Yesu ,na akamwona Roho Mtakatifu.

**Mungu alimwambiaYohana**

Ni kwamba,"Kabla ya hii ,Mungu alimwambia Yohana au,"Kabla ya Yesu kuja kubatizwa na Yohana,Mungu alimwambia Yohana."

Simulizi ya Biblia kutoka: Matayo 3; Marko1:9-11; Luka 3:1-23

**translationWords**

- Mungu
- Yohana (Mbatizaji)
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Batiza, ubatizo
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana



## 25. Shetani Anamjaribu Yesu

25:01



Mara tu Yesu alipokwisha kubatizwa, **Roho Mtakatifu alimwongoza** Yesu nyikani, huko alifunga siku arobaini mchana na usiku. kisha Shetani alifika kumjaribu Yesu ili atende dhambi.

### Roho Mtakatifu alimwongoza

Ni kwamba,"Roho Mtakatifu alimlinda" au," Roho Mtakatifu alisababisha yeye kwenda."

### Nyikani

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi,"jangwa"au,"kijijini, eneo la kuzikia watu wachache."Hili eneo kwa hakika lilikuwa na miti michache au mimea mingine,hivyo watu wengi hawakuweza kuwa tayari kuishi.

### Siku arobaini mchana na usiku

Hii inaanisha "siku arobaini, zote wakati wa mchana na wakati wa usiku ,"Akikisha kwamba tafsiri ya hiki kifungu hakitamkwi kama kipindi cha siku nane.

### Alimjaribu yeye kufanya dhambi

Kabla Yesu hakufanya dhambi,akikisha kwamba unatumia maneno ambayo hayamfanyi shetani kufaulu katika kumshawishi Yesu kutenda dhambi.Kipengele hiki kinaweza kuwa kimetafsiriwa hivi, Alijaribu kushawishi atende dhambi."

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Batiza, ubatizo
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- funga
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- kujaribu, jaribu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

## 25:02



Shetani alimjaribu Yesu akisema; "Kama wewe ni mwana wa Mungu yaamuru mawe haya yawe mikate upate kula".

### **Amuru mawe haya yawe mikate**

Hii inaweza pia kuwa imetafsiriwa hivi, "tengeneza mawe haya yawe mikate" au muujiza kubadilisha mawe kuwa mikate."

### **Mkate**

Hii inaweza kutafsiriwa hivi, "chakula" Kwa lugha ambapo mikate siyo chakula cha kawaida .Kwa tamaduni za Wayahudi mikate ulikuwa chakula kikuu.

### **translationWords**

- Shetani, ibilisi, yule muovu
- kujaribu, jaribu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana

## 25:03



Yesu akajibu; "Imeandikwa katika neno la Mungu, watu hawahitaji mkate pekee ili wapate kuishi, bali wanahitaji kila neno linalosemwa na Mungu".

### Mkate

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi , "kwa lugha ambapo mkate siyo chakula cha kawaida .Kwa tamaduni za Wayahudi mkate ulikuwa chakula kikuu.


### Lakini wanahitaji kila neno lilosemwa na Mungu

Njia nyingine kutafsiri hii inaweza kuwa badala yake watu wanahitaji kusikiliza na kutii kila kitu kisemwacho na Mungu au badala yake watu

### translationWords

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)
- [Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko](#)
- [Mungu](#)



**25:04**

Kisha Shetani alimchukua Yesu mpaka juu ya mnara wa hekalu na kumwambia; "Kama wewe ni Mwana wa Mungu jirushe mwenyewe chini, kwa vile imeandikwa, Mungu atakuagizia malaika wake wakuchukue ili usijigonge mguu wako katika jiwe".

**Jirushe mwenyewe chini**

"Ni kwamba , "Kuruka kutoka juu ya hili jengo hadi ardhini."

**Imeandikwa**

Ni kwamba, "nabii wa Mungu aliandikiwa miaka mingi."

**Mguu wako hautagonga jiwe**

Hii inamaanisha, "Kwamba hutaumizwa kwa yote ,hata hivyo mguu wako hatakuwa umejeruhiwa kwenye jiwe." Inaweza pia kuwa imetafsiriwa, "hata hivyo mguu wako hautagoma kinyume na jiwe hautakuwa umejeruhiwakwa yote."

**translationWords**

- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- hekalu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Mungu
- Malaika, Malaika mkuu

**25:05**

Lakini Yesu alimjibu Shetani kwa kunukuu Maandiko akisema; " Katika neno la Mungu, anaagiza watu wake, usimjaribu **Bwana Mungu wako**".

**Katika neno la Mungu ,anaagiza watu wake ,usimjaribu Bwana Mungu wako.**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa moja kwa moja kwa nukuu:"Mungu anatuamuru kwenye neno lake kwamba tusiweze kumpima Bwana Mungu wetu."

**Usimpime Bwana Mungu wako**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi," Usimfanya Bwana Mungu wako kuthibitishwa kwako"au,Usimfanya Bwana Mungu wako kuthibitisha kwamba yeye ni mwema"

**Bwana Mungu wako**

Ni kwamba,Yahwe,Mungu wako"au,Yahwe,ambaye ni Mungu na ana mamlaka juu yako."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- bwana, mkuu
- Mungu

## 25:06



Kisha Shetani alimwonyesha Yesu falme zote za ulimwengu na fahari zake zote na akasema; "**Nitakupa hivi vyote** iwapo utanisujudia na kuniabudu mimi".

### Falme za ulimwengu

Hii inarejea kwa miji yote mikubwa ,nchi,na tawala za dunia

### Utukufu wao

Ni kwamba,"nguvu na utajiri wao,"

### Nitakupa hivi vyote

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa kama,"nitakupa utajiri wote na nguvu wa hizi falme"au nitakufanya mtawala juu ya nchi,miji,na watu."

### translationWords

- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ufalme
- utukufu, fahari
- Abudu



**25:07**

Yesu akajibu; ondoka kwangu Shetani! Katika neno la Mungu ameagiza, "Mwabudu **Bwana Mungu wako** na kumtumikia Yeye peke yake".

**Ondoka kwangu**

Hii inaweza pia kuwa imetafsiriwa kama,"Niache mimi "au,Niache peke yangu."

**Katika maneno ya Mungu anaagiza watu wake ,"mwamudu peke yake Bwana Mungu wako na kumtumikia peke yake"**

Hii inaweza kuwa imeandikwa kama siyo moja kwa moja kama nukuu, katika Maneno ya Mungu anatuagiza kwamba ni lazima tumwabudu na kumtumikia Bwana Mungu peke yake ambaye anatawala juu yetu."

**Bwana Mungu wako**

Hii inaweza kuwa kama Mungu anatuagiza kwamba ni lazima tumwabudu na kumtumikia Bwana Mungu peke yake ambaye anatawala juu yetu.

**Na kumtumikia peke yake**

Njia nyingine kusema hii itaweza kuwa ," Ni Yeye peke tunaweza kumtumikia".


**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Abudu



- bwana, mkuu
- Mungu

## 25:08



Yesu hakujitia chini ya majaribu ya Shetani, hivyo Shetani aliondoka akamwacha. kisha malaika walikuja na kumhudumia Yesu.

*Simulizi ya Biblia Kutoka: Mathayo 4:1-11;*

### **Yesu hakujitia chini ya**

Hii inaweza kuwa imetafsiriwa hivi, "hakufanya kitu ambacho shetani alikuwa anamjaribu afanye."


Marko 1:12-13; Luka 4:1-13

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- kujaribu, jaribu
- Malaika, Malaika mkuu

## 26. Yesu Anaanza Huduma yake.

26:01



Baada ya kushinda majaribu ya Ibilisi Yesu alirudi kwa nguvu za Roho mtakatifu katika mkoa wa Galilaya. Yesu alienda sehemu moja baada ya nyigine akifundisha. **Kila mmoja** alisema vyema juu yake.

### Baada ya kushinda majaribu ya shetani, Yesu alirudi

Unaweza kuliweka jambo hili katika sentensi mbili na kusema, " Yesu hakufanya mambo mabaya ambayo shetani alijaribu kumshawishi kufanya na kwa hiyo alimshinda. Na baada ya hayo, Yesu alirudi." Neno "kushinda" linaweza pia kutafasiriwa kwa " Kupinga" au "Kukataa" au "Kutokubali"

### Katika Nguvu ya Roho Mtakatifu

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Wakati nguvu ya Roho Mtakatifu ikifanya kazi ndani yake" au " Na Roho Mtakatifu alikuwa akimwongoza kwa nguvu."

### Alikwenda kila mahali akifundisha

Hii ni kwamba, "Alisafiri kwenda miji tofauti na sehemu zingine na akafundisha watu pale."

### Kila mmoja

Hii ni kwamba, "Kila mmoja aliye mjua au kusikia habari zake."

## **Alimsema vizuri**

Hii ni kwamba, "Alisma mambo mema juu yake."

## **translationWords**

- Shetani, ibilisi, yule muovu
- kujaribu, jaribu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Nguvu
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Galilaya, Mgalilaya



**26:02**

Yesu akaenda mji wa Nazareti alikokuwa akiishi wakati wa utoto wake. Siku ya sabato, alienda sehemu ya kuabudia. wakamkabidhi chuo cha nabii isaya ili aweze kusoma. Yesu akakifungua chuo na kusoma sehemu yake mbele za watu.

**Mahali pa ibada**

Hii ni, "Jengo ambalo wayahudi walikusanyika kumwabudu Mungu." Hii pia inaweza kutafsiriwa kama jengo la ibada."

**Gombo**

Gombo lilikuwa ni karatasi ndefu au ngozi ambayo ilikunjwa ambayo ilikuwa na maandishi juu yake.

**Gombo la nabii Isaya**

Hii ni, " Gombo ambalo lilikuwa na maneno ambayo nabii Isaya alikuwa ameandika." Isaya alikuwa ameandika juu ya gombo mamia ya miaka kabla. Hii ilikuwa ni nakala ya gombo hilo.

**Alifungua gombo**


Hii inaweza kutafsiliwa kama, "Alifungua gombo" au, "Alilikunjua gombo.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Nazarethi, Nazarini
- Sabato
- Abudu

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Isaya

## 26:03



Yesu kasema "Bwana amenipa Roho wake ili kwamba nitangaze habari njema kwa maskini, uhuru kwa wafungwa, vipofu kuona, kutolewa waliodhurumiwa. huu ni mwaka wa Bwana uliokubalika.

### **Tangaza habari njema kwa masikini**

Hii ni, "Waambie masikini na wahitaji habari njema kwamba Mungu atawasaidia."

### **Uhuru wa ufungwa**

Hii ni, Kuwaambia watu ambao ni wacosaji kifungoni kwamba wataachiliwa."

### **translationWords**

- Mungu
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- habari njema, injili
- bwana, mkuu

## 26:04



Tena Yesu akaa chini "Kila mmoja akamsogelea na kumtazama. walijua aya aliyoisoma inamhusu masia. Yesu akasema "**Maneno niliyosoma mbele yenu yanatokea sasa**. watu wote wakashangaa. huyu si mwana wa Yusufu"? Walisema.

### **Maneno niliyosoma mbele yenu yanatokea sasa**

Njia zingine za kutafsiri hii zingekuwa, "Maneno ambayo umeyasikia nikiyasoma yametimilika sasa" au "Leo maneno niliyoyasoma kwenu yametimi kama mliyoyasikia."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Kristo, Masihi
- Yusufu (Agano Jipya)



**26:05**

Tena Yesu akasema "Ni kweli kwamba **hakuna nabii anayekubalika katika mji wa kwao**. Wakati wa nabii Eliya, kulikuwa na wajane katika Israeli. lakini mvua iliposimama bila kunyesha kwa miaka mitatu na nusu, Mungu hakumtuma Eliya kumsaidia mwanamke mjane kutoka Israel, badala yake alikuwa ni mjane kutoka taifa tofauti"

**hakuna nabii anayekubalika katika mji wa kwao**

Sentensi hii inamaanisha, "watu hawatambuwi mamlaka ya nabii aliyekulia katikati yao."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kweli, ukweli, kuwa kweli
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Eliya
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Mungu

**26:06**

Yesu akaendelea kusema "Kipindi cha nabii **Elisha** kulikuwa na watu wengi katika Israeli wenye magonjwa ya Ngozi. lakini Elisha hakumponya hata mmoja wao. lakini aliponya ugonjwa wa ngozi wa Naamani pekee aliyekuwa **kamanda** wa maadui wa Israel. watu waliokuwa wanamsikiliza Yesu walikuwa ni wayahudi. Kwa hiyo walipomsikia anasema hayo **wakawa na hasira juu yake**.

**Elisha**

Elisha alikuwa nabii wa Mungu ambaye alikuja baada ya Eliya. Kama vile Eliya, Elisha aliwakabili wafalme wa waisrael ambao walifanya dhambi dhidi ya Munguna alifanya miujiza ambayo Mungu alimpa uwezo wa kuifanya.

**kamanda**

Huyu ni "kiongozi wa jeshi."

**wakawa na hasira juu yake.**

Wayahudi hawakupenda kusikia kuwa Mungu amebariki kundi la watu wowote isipokuwa waowenyewe, kwahiyo wakawa na hasira kwa kile ambacho Yesu alifanya.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Ponya, tibu
- Naamani
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi

## 26:07



Watu wa Nazareti wakamvuta Yesu mbali na **mahali pa kuabudia** na kumtupa nje ili wamwue. **Lakini Yesu akaondoka Mbele yao** na akauacha mji wa Nazaleti.

### **mahali pa kuabudia**

Hii ni, "nyumba ambayo wayahudi walikusanyika kumwabudu Mungu." hii pia inaweza kutafsiriwa kama " Nyumba ya ibada."

### **Lakini Yesu akaondoka Mbele yao**

"Lakini" inaweza kutafsiriwa kwa neno zito la kukanusha au sentensi kam vile "Lakini badala yake" au, "Hata hivyo" kuonesha kwamba watu hawakuweza kufanya lolote walilolipanga kumfanyia Yesu.

### **translationWords**

- Nazarethi, Nazarini
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Abudu



## 26:08



Tena Yesu **alienda mpaka mkoa wa Galilaya** na mkutano mkubwa wakaja kwake. wakaweleta watu wengi waliokuwa wagonjwa, au walemavu, kama wasioona, kutembea, kusikia au kuongea, na Yesu akawaponya.

### **alienda mpaka mkoa wa Galilaya**

Hii ni kwamba, "Sehemu zote katika galilaya" au, kutoka mali hadi mahali pengine katika Galilaya

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Galilaya, Mgalilaya
- Ponya, tibu



**26:09**

Watu wengi **waliokuwa na mapepo ndani yao** waliletwa kwa Yesu. Kwa amri ya Yesu aliwaamuru wawatoke watu hao, na waliendelea kupiga kelele "Wewe ni mwana wa Mungu!" Umati wa watu walishangaa na walimwabudu Mungu.

**waliokuwa na mapepo ndani yao**

Hii ni, "ambao walitawaliwa na roho za kiovu."


**Yesu alipo waamuru.**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " wakati Yesu aipotoa amri kwao."

**translationWords**

- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Abudu
- Mungu

## 26:10



Tena Yesu akachagua watu kumi na wawili ambao aliwaita mitume. Mitume walizunguka na Yesu tena **walijifunza kutoka kwake.**

### **walijifunza kutoka kwake.**

Hii ni kwamba, "walijifunza kutoka katika yale aliyowafundisha" au, "walijifunza katika yote aliyosema na kutenda."

Simulizi ya Biblia kutoka: Matahayo 4:12-25; Marko 1:14-15; 35-39; 3:13-21; Luka 4:14-30, 38-44

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mtume, utume

## 27. Simulizi ya Msamaria Mwema

27:01



**Siku moja** Mwalimu wa mambo ya sheria ya Kiyahudi alimwendea Yesu na kumuuliza kwa kumjaribu akisema, "Mwalimu nifanyeje ili ni urithi uzima wa milele?" Yesu akamjibu " sheria ya Mungu imeandikwaje?"

### Siku moja

Hii sentensi inatoa utangulizi wa tukio ambalo lilitokea wakati ulio pita, ingawa halizungumzi muda maalumu. Lugha nyingi zinz nzmnz hii ya kuanza kusimulia simulizi ambayo ni kweli.

### Mwalimu wa mambo ya sheria ya kiyahudi

Huyu ni mtu aliye fundishwa na kujifunza sheria za kiyahudi ambazo Mungu aliwapatia Israel paoja na zile sheria za kiyahudi.

### Kumjaribu

Hii ni kuona kama, Yesu angeliweza kutoa jibu zuri."

### Kurithi uzima wa milele

Hii ni "kuwa na maisha pamoja na Mungu milele" au , "ili kwamba Mungu anipatie maisha pamoja naye milele" au, kupokea uzima wa milele kutoka kwa Mungu." Mwalimu wa mambo ya sheria alikuwa anauliza jinsi gani angelistahili kupokea uzima wa milele kama urithi kutoka kwa Mungu baba.

## Uzima wa milele

Hii inamaanisha maisha ya milele pamoja na Mungu baada ya mwili wa kuharibika kufa.


## Nini kimeandikwa katika sheria ya Mungu?

Hii ni. "Nini kimeandikwa katika sheria ya Mungu kuhusu hili?Yesu aliuliza swali hili kwa sababu alitaka mtu huyu afikiri kuhusu nini hasa sheria ya Mungu inafundisha.

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mwalimu,Mwalimu
- rithi, urithi, mrithi
- milele
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe



**27:02**

**Mwalimu wa mambo ya sheria** ya Kiyahudi alimjibu Yesu na kusema, sheria ya Mungu inasema "**Mpende Bwana Mungu wako** kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote. Na pia inasema "Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe. Yesu akamwambia "uko sahihi. Fanya hivyo na utaurithi uzima wa milele."

**Mwalimu wa mambo ya sheria**

Huyu ni mtu aliye soma na kufundishwa sheria za Mungu walizopewa waisrael pamoja na sheia zingine za kiyahudi.

**Mpende Bwana Mungu wako**

Unaweza kuchagua kusema, "Tunapaswakumpenda Bwana Mungu wetu," Hakikisha kuwa haita someka kuwa mtu yule alikuwa amamwamrisha Yesu. Badala yake ananukuu nini ambacho sheria ya Mungu inawataka watu wafanye.

**Kwa moyo wako, nafsi, nguvu, na akili**

Hii ni kumaanisha "utu wote wa mtu" kila sehemu ya utu wako" katika baadhi ya lugha hii inaweza kutafsiriwa kama, "kwa ini lako, kwa pumzi zako kwa nguvu zako, na kwa mawazo yako." mtazamo si katika kila sehemu hizi, isipokuwa sisi katika utu wetu wote. tumia dhana katika lugha yako ambayo itafanya ieleweke kuwa ni mtu kwa ujumla wake.

**Moyo**

Hii ni sehemu ya mtu ambayo ina utashi na hisia

## **Nafsi**

Nafsi inamaanisha ile sehemu isiyo na mwili, sehemu ya kiroho ya mtu.

## **Nguvu**

Nguvu inamaanisha mwili halisi pamoja na uwezo wake wote.

## **Akili**

Akili inamaanisha sehemu ya mtu ambayo hufikiri, hupanga, na kutengeneza mawazo.

## **Jirani**

Neno "jirani" kwa kawaida humaanisha mtu anayeishi karibu nasi. Kwa wayahudi walitumia neno hili si tu kwa mtu aliye karibu, bali kwa ndugu, mgeni au adui.

## **Mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe**

Hii inamaana, "mpende jirani yako kwa kiwango kilekile unachojipenda wewe mwenyewe."

## **translationWords**

- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe
- upendo
- bwana, mkuu
- Mungu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

## 27:03



Lakini huyu **Mwalimu wa mambo ya sheria** ya Kiyahudi akitaka kujionyesha kwamba yeye ni mwenye haki, alimuuliza Yesu; "**Jirani yangu ni nani?**"

### **Mwalimu wa mambo ya sheria**

Huyu ni mtu aliye soma na kufundishwa sheria za Mungu walizopewa waisrael pamoja na sheia zingine za kiyahudi.

### **Jirani yangu ni nani?**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "unamaana gani unaposema jirani?" au. "ni watu gani ni majirani zangu?" Alijua kuwa hakuwapenda kila mtu, naalikuwa anauliza ni watu gani alihitajika kuwapenda.

### **translationWords**

- Adili, uadilifu

## 27:04



Yesu alimjibu huyu Mwalimu wa mambo ya sheria ya Kiyahudi kwa kumpa simulizi. " Kulikuwa na Myahudi mmoja aliyekuwa anasafiri kwa barabara kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko.

### **Mtaalam wa sheria**

Huyu ni mtu aliye soma na kufundishwa sheria za Mungu walizopewa waisrael pamoja na sheia zingine za kiyahudi.

### **Kutoka Yerusalem kwenda Yeriko**

Kwa baadhi ya lugha unaweza kutafsiri hii kama, "kutoka katika mji wa Yerusalem kwenda mjiwa Yeriko" au, "kutoka mji wa Yerusalem hadi mji wa Yeriko."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Yerusalemu
- Yeriko




**27:05**



"Wakati Myahudi huyu alipokuwa akisafiri kikundi cha wezi kilimvamia na kumwibia kila kitu na kumpiga sana karibu ya kufa. Walipokuwa wamempiga sana karibu ya kufa, walimwacha hapo barabarani na kuondoka zao."

### **kilakitu alichokuwa nacho**

Hii ni kwamba, " kilakitu alichokuwa nacho, pamoja na nguo alizokuwa amevaa."

**27:06**

"Muda mfupi baada ya tukio hilo Kuhani wa Kiyahudi alikuwa akisafiri na kupitia katika barabara hii ambayo Myahudi yule alikuwa amepigwa na kuachwa pale. Alipomuona alipita upande mwingine wa barabara mbali na alipokuwepo mtu huyo na kuendelea na safari yake wala asimjali na kumsaidia mtu yule."

**Alipita katika barabara hiyo**

Hii ni kwamba, "ilitokea akipita katika njia ile." kwa lugha zingine inaweza kulazimika kutumia neno kama, "kusafiri" badala ya kupita au kutembea kwa kuwa kuhani alikuwa hatembezi tu barabarani lakini alikuwa anasafiri kwenda mji mwingine.

**Hakumjali**

Hii ni kwamba, "Hakumsaidia mtu yule" au alionesha kutohusika kwa shida ya mtu yule."

**Aliendelea kwenda**

Hii ni kwamba, "Aliendelea kusafiri barabarani."

**translationWords**

- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Kuhani, ukuhani
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini

**27:07**

"Baada ya muda mfupi Mlawi (**Walawi walikuwa kabila la Wayahudi** ambao lilikuwa linawasadia makuhani katika huduma hekaluni) naye **alipita barabara hiyohiyo** na alipomuona mtu yule aliyekuwa amepigwa na kuumizwa na wezi alipita upande mwingine wa barabara na kuendelea na safari yake bila kumjali."

**alipita barabara hiyohiyo**

Hii ni kwamba, Alikuwa anasafiri kwenye barabara hiyo hiyo

**Walawi walikuwa kabila la Wayahudi**


Hii ni, "Walawi walikuwa wanatokana nakabila ya Waisrael ya Lawi" au, Walawi walikuwa wanatokana na waisrael katika ukoo wa Lawi."

**Bila kujali**

Hii ni kwamba, "Hakumsaidia."

**translationWords**

- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Kuhani, ukuhani
- hekalu

**27:08**

"Mtu mwingine aliyepita barabara hiyo alikuwa ni Msamaria (Wasamaria walikuwa wa uzao wa Wayahudi na ni watu waliooa na kuolewa na watu wa mataifa mengine. Wasamaria walikuwa wanachukiana sana na Wayahudi). Huyo Msamaria alipomuona Myahudi yule aliyekuwa amepigwa na kuumizwa sana na wezi, alimuonea sana huruma. Alimchukua na kuyahudumia majeraha yake na kumfunga pandeji."

**pita barabara**

Hii ni, kusafiri" Hawa watu walikuwa wanasafiri kutoka katika mji mmoja kwenda mwingine. hakikisha kwamba isionekane kwamba walikuwa wanazungukazunguka tu.

**translationWords**

- Samaria, Msamaria
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi



## 27:09



"Msamaria baada ya hapo alimchukua huyo Myahudi na kumpandisha kwenye **Punda wake** na kumpeleka kwenye nyumba ya wageni iliyokuwa karibu na barabara na kumuhudumia zaidi."

### **Punda wake**

Hakikisha kuwa neno wake inamaanisha Msamaria.

### **Nyumba ya wageni**


Hii ni, "Mahali wageni wanafika kulala" hii ni sehemu ambayo wasafiri wangeweza kupata chakula na kupumzika usiku.

### **Mahali ambapo alimuhudumia**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "Mahali ambapo aliendelea kumuhudumia."

### **translationWords**

- [Samaria, Msamaria](#)

**27:10**

"Siku iliyofuata Msamaria huyu alihitaji kuendelea na safari yake na hivyo alimkabidhi yule muangalizi wa nyumba ya wageni na kumwambia " Mhudumie Myahudi huyu aliyepigwa na wezi. Akampa fedha yule muangalizi na kumwambia, kama utatumia fedha zaidi katika kumhudumia Myahudi huyu basi nikirudi kutoka safari yangu nitakuja nilipe kiasi kilichoongezeka."

**aliendelea na safari yake**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Aliendelea kuafiri na kufika mwisho wa safari yake."

**Mwangelizi**

Huyu ni mtu "ambaye alisimamia." Inaweza kuwa kwamba mtu huyu pia alikuwa anamiliki sehemu ya kulala wageni.

**Kumtunza**


Kwa lugha zingine ingependelewa kusema, "Tafadhari mtunze" ili kwamba ijulikane wazi kuwa hili mlilikwa ni ombi la kumsihi, na si amri.

**Kulipa zaidi gharama hizo**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "kukulipa tena" au, "kulipa tena fedha hiyo" au, "kuilipa"

**translationWords**

- [Samaria, Msamaria](#)

**27:11**

Baada ya hadithi hiyo, Yesu alimuuliza yule Mwalimu wa mambo ya sheria ya Kiyahudi, kwamba "Unafikiri katika watu hao watatu, ni nani aliyekuwa jirani yake yule Myahudi aliyepigwa na wezi?" Yule Mwalimu wa mambo ya sheria ya Kiyahudi alijibu na kumwambia Yesu "ni yule aliyemuonea huruma". Yesu akamwambia "Wewe nawe nenda kafanye vivyo hivyo."

**Mwalimu wa sheria**

Huyu ni "mtaalamu wa sheria katika sheria ya kiyahudi."

**Watu watatu**

watu watatu walikuwa ni, Kuhani, Mlawi, na Msamalia.

**Jirani**

Yesu anatumia neno "Jirani" katikaile maana pana, "Jirani" inamaanisha mtu yeyote tunayekutana naye akiwa anahitaji msaada wetu.

**Alikuwa jirani**

Hii inweza pia kutafsiriwa kama, "Aliye kuwa na tabia za jirani" au, "Alikuwa rafiki" au, "alifanya kwa upendo".

**Nenda na ufanye**

Hii ni kwamba,, "wewe pia nenda ukafanye hivyo" au, "sasa lazima ufanye." Yesu alikuwa anamwamrisha mtaalamu wa sheria kufanya kama msamalia alivyo fanya.

## Fanya hivyo

Hii ni kwamba, "Wapende wengine hata wale ambao ni adui zako." hakikisha tu kwamba isomeke kuwa inamaanisha kumsaidia mtu aliye umizwa.

Simulizi ya Biblia kutoka: Luka 10:25-37

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- rehema



## 28. Kijana Tajiri Kiongozi

28:01



Siku moja, kiongozi kijana tajiri alimwendea Yesu na kumuuliza, "mwalimu mwema nifanye kitu gani cha lazima ili niwe na uzima wa milele?" Yesu akamwambia, "kwanini unaniita mwema?" Kuna mmoja tu aliye mwema naye ni Mungu. Lakini ukitaka kuwa na uzima wa milele, tii sheria za Mungu.

### Sikumoya

Sentensi hii inatoa utangulizi wa jambao ambalo lilitokea nyakati za nyuma, lakini halielezi muda maalumu. Lugha nyingi zina namja hii ya kuanza kueleza simulizi ya kweli.

### Kiongozi kijana tajiri

Huyu kijana alikuwa tayari ni tajiri na kiongozi mwanasiasa mwenye nguvu, ingawa alikuwa bado ni kijana.

### Alimwendea Yesu

Hii ni kwamba alimfuata Yesu

### Mwalimu Mwema

Hii inamaanisha "Mwalimu mwenye haki" Alikuwa hamaanishi kuwa Yesu alikuwa tu ni mwalimu aliye pitia mafunzo.

## **Kuwa na uzima wa milele**

Hii ni kwamba, "Kupokea uzima wa milele" au. "Kuishi na Mungu milele na milele."

## **Kwa nini kuniita "mwema"**

Yesu hakatai kuwa yeye ni Mungu, isipokuwa anamuomba mtawala kuelewa kuwa Yesu ni Mungu.


## **Kuna mmoja tu aliye mwema, na huyo ni Mungu**

Njia nyingine ya kusema hili ingelikuwa, "Aliye mwema kweli kweli ni mmoja tu ambaye ni Mungu." au, "Mungu ndiy pekee aliye mwema kweli kweli."

## **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- wema, uzuri
- mwalimu, Mwalimu
- milele
- Mungu
- tii, mtiifu, utiifu
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe

## 28:02



"Ni mambo gani nahitaji kutii?" Aliuliza. Yesu akajibu, "usiuwe. Usizini. Usiibe. Usidanganye. Mheshimu baba yako na mama yako, na umpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.

### Ni mambo gani nahitaji kutii?

Hii ni kwamba, "Ni sheria gani zitakazo tosheleza mimi kupokea uzima wa milele?"

### Kama unavyo jipenda mwenyewe

Hii ni kwamba, "kadiri unavyo jipenda mwenyewe" au, "kiwango kile kile unacho jipenda mwenyewe,"

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi
- upendo

**28:03**

Lakini kijana akasema, "Nimezitii sheria hizo zote tangu nikiwa kijana. Je, nahitaji kufanya nini bado ili niishi milele? Yesu alimwalia na akampenda.

**Tangu nikiwa kijana**

Njia nyingine ya kusema hili ingekuwa, "kuanzia wakati nilipo kuwa mtoto hadi sasa."

**Jambo gani ambalo bado napaswa kulifanya?**

Hii ni kwamba, "Nini zaidiambacho nahitajika kukifanya" au, Nahitaji kufanya nini kama nyongeza ya haya niliyokwisha fanya?"

**Akampenda**

Yesu alimuhurumia. chagua nenolinalo maanisha upendo ambao unalingana na ule upendo ambao Mungu anao kwa watu.

**translationWords**

- tii, mtiifu, utiifu
- sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- upendo



## 28:04



Yesu akajibu, kama unataka kuwa mkamilifu, nenda ukauze kila kitu ulichonacho na utoe pesa kwa maskini, na utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuata.

### **Wewe**

Kama lugha yako ina neno tofauti na "wewe" kutegemeana na idadi ya watu waliokusudiwa, tumia hali ya umoja. Yesu alikuwa anasema amri hii kwa mtu huyu mmoja.

### **Mkamilifu**

Hii inamaana, "mtu wa haki kabisa."

### **Kila kitu unachomiliki**

Hii ina maana, "kilakitu ambacho ni mali yako."

### **Hazina**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "utajiri" au, utajiri mwingi"


### **Mbinguni**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "iliyo mbinguni wakati utakapofika pale," kinyume na utajiri ambao Yesu alimwambia kijana kuutoa "hapa na sasa."

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mbingu, anga, mbinguni

## 28:05



Yule kijana aliposikia alichokisema Yesu, alihuzunika sana, kwa sababu alikuwa tajiri sana na hakutaka kutoa vitu vyote alivyomiliki. Akageuka na akaenda mbali na Yesu.

### **Aliposikia alicho kisema Yesu**

Hii ni kwamba, aliposikia Yesu akimwambia kutoa alivyo kuwa navyo."

### **translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)

**28:06**

Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Ni vigumu sana kwa watu matajiri kuingia katika ufalme wa Mungu! Ndiyo, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu

**Kuingia katika ufalme wa Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kufanyika raia katika ufalme wa Mungu."

**Ngamia**

Ngamia ni wanyama wakubwa ambao maranyingi wanatumika kubeba mizigo mizito. ikiwa ngamia hawajulikani katika lugha ya eneo lako, sentensi kama, "Mnyama mkubwa sana" au, "Mnyama wa mzungu" linaweza kutumika. ikiwa utachagua kutumia mnyama mkubwa badala ya ngamia, hakikisha kuwa mnyama unaye mtumia anajulikana na watu kama vile watu ambao Yesu alizungumza nao walivyo mjua mnyama. kama vile , "Punda."

**Tundu la sindano**


Hii inarejea kwenye tundu dogo mwishoni mwa sindano ya kushonea nguo. Wazo la kitu kikubwa kama ngamia kupita katika tundu la sindano imekusudiwa kuwakilisha jambo ambalo haliwezekani.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni



## 28:07



Wanafunzi waliposikia alichosema Yesu, walishikwa na mshangao na kusema, "Ni nani basi anaweza kuokolewa?"

### **Shikwa na mshangao**

Hii ni hali ya, "kustajabisha"

### **Nani anaweza kuokoka**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "ikiwa watu matajiri hawezi kuokoka, nji jinsi gani mtu wingine yeyote anaweza kuokoka?" Watu wengi waliamini kuwa kuwa tajiri ni dalili ya kupata upendeleo wa Mungu.


### **Okoka**

Hapa inarejea katika hali ya kuokoka katika hukumu ya Mungu na hukumu ya dhambi na kuruhusiwa kuwa raia katika ufalme wa Mungu.

### **translationWords**

- mfuasi
- okoa, salama

## 28:08



Yesu akawatazama wanafunzi na kusema, "**Kwa watu mambo haya hayawezekani, lakini kwa Mungu mambo yote yanawezekana**".

### **"Kwa watu mambo haya hayawezekani**

Hii ni kwamba, haiwezekani kwa watu kufanya hivi" au, watu wenyewe hawawezi kujiokoa wenyewe."


### **kwa Mungu mambo yote yanawezekana".**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "Mungu anaweza kufanya jambo lolote, hata kuokoa mtu tajiri" au, Mungu anaweza kufanya mambo yasiyowezekana, kwa hiyo anaweza kuokoa hata mtu tajiri."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Mungu

## 28:09



Petro akamwambia Yesu, "**Tumeacha kila kitu** na kukufuata wewe. **Je, tutapata thawabu gani?**"

### **Tumeacha kila kitu**

Hii ni kwamba, kuachana na mambo yote" , au, kuachilia vitu vyote tulivyo miliki."


### **Je, tutapata thawabu gani?"**

Njia nyingine ya kusema hivi ni, " ni zawadi gani tutapokea" au, Ni jinsigani tutazawadiwa?" inaweza pia kuwa muhimu kuongeza, kwa sababu tumefanya hivi?"

### **translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

## 28:10



Yesu akajibu, "Kila mmoja aliyeacha nyumba, kaka, dada yake, baba, mama, watoto, au mali kwa ajili yangu atapokea mara 100 zaidi na pia atapokea uzima wa milele. Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na wengi walio wa mwisho watakuwa wa kwanza."

### **Aliye acha**

Hii ni mtu "aliye acha" au, " aliye achana " au,"aliye hesabu jambo kutokuwa la muhimu kuliko Mungu.

### **Kwa ajili yangu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kwa sababu yangu" au, kwa ajili yangu."

### **Mara 100 zaidi**

Hii inamaan, "zaidi sana kuliko alivyo kuwa navyo mwanzoni."

### **Wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho**

Hii ni, " watu ambao ni wa muhimu sasa, hawata kuwa wa muhimu baadaye."

### **Wengi wa mwisho watakuwa wa kwanza**

Hii ni kwamba, wale wanaofikiriwa kuwa si wa muhimu duniani watafikiriwa kuwa wa muhimu mbinguni" au, "watu wengi ambao wanadhaniwa sasa kuwa na thamani ndogo hapa duniani watathaminiwa zaidi mbinguni."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 19:16-30; Marko 10:17-31; Luka 18:18-30



## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- milele

## 29. Simulizi ya Mtumishi Asiye na Huruma.

29:01



**Siku moja**, Petro alimuuliza Yesu "Bwana, ni mara ngapi inanipasa kumsamehe ndugu yangu akinikosea? Hadi mara saba?" Yesu akasema, "Sio mara saba, bali sabini mara saba!" Kwa hili, Yesu alimaanisha inatupasa kusamehe kila wakati. Yesu akawaambia habari hii.

### Siku moja

Sentensi hii inatoa utangulizi wa tukio lililo tokea wakati ulio pita, ingawa halielezi muda maalumu. Lugha zilizo nyingi zinanamna hii hii ya kueleza simulizi iliyo ya kweli.

### Ndugu yangu

Neno hili mara nyingine lilihusisha watu amabo hawakuwa ndugu wa damu, lakini ambao walikuwa na mahusiano thabiti kama vile mahusio ya ki dini, kabila, n.k.

### Ndugu yangu akinikosea

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, ambaye amefanya jambo baya kwangu."

### Si maa saba, bali sabini mara saba!

Hii inaweza kutafsiriwa kama, " hupaswi kusamehe mara saba tu, bali unapaswa kusamehe sabini mara saba." Yesu alikuwa hamaanishi idadi kamili ya matukio ya kusamehe. alimaanisha kuwa lazima kuwasamehe watu mara kwa mara wanaotukosea.

## **Kwa hili Yesu alimaanisha**

Hii ni, "wakati Yesu aliposema hili alimaanisha."

### **translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- bwana, mkuu
- samehe, kusamehe
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

29:02



Yesu akasema, " **Ufalme wa Mungu unafananishwa** na **mfalme alie** taka kukusanya madeni yake kutoka kwa watumishi wake. Mmoja wa watumishi wake alikua anadaiwa deni kubwa lenye thamani ya mshahara wa miaka 200,000."

### **Ufalme wa Mungu unafananishwa**

Njia nyingine ya kusema hivi ingekuwa, " utawala wa Mungu kwa watu wake unafanana"au, " Jinsi Mungu anavyotawala watu inafananishwa na."

### **mfalme alie**

Hii kutafsiriwa kama, "Ni kama ufalme wa mfalme ambaye" au, "unaweza kulinganishwa na utawala wa mfalme ambaye."

### **Tengeneza hesabu pamoja na mtumwa wake**

Hii ni kwamba, "kusanya madeni yote ya watumwa wanayodaiwa" au, "kusanya fedha kutoka kwa watumwa ambazo waliazima.

### **translationWords**

- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- mfalme
- mtumishi, mtumwa, utumwa



## 29:03



"Kwaku yule mtuishi hakuweza **kulipa deni**, mfalme alisema, 'muuzeni huyu mtu na familia yake kama watumwa ili **kulipa deni lake**."

### **kulipa deni,**

Hii ni, "lipa pesa alizodaiwa na mfalme."

### **kulipa deni lake.**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, tumia pesa uliyopokea kutokana na mauzo na ulipe sehemu ya deni ninalokudai."

### **translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- mfalme
- mtumishi, mtumwa, utumwa

**29:04**

"Yule mtumishi **alianguka na kupiga magoti** mbele ya mfalme na kusema, ' naomba nivumilie, na nitalipa deni loote unalonidai.' Mfalme alimuonea huruma yule mtumishi, ndipo **akafuta deni lake lote** na kumuacha aende zake."

**alianguka na kupiga magoti**

Hii kwamba, " kwa haraka alipiga magoti chini juu ya ardhi."hii ilikuwa ni njia ya kuonesha unyenyekevu na haja yake kwa mfalme kumsaidia. Hakikisha kwamba isije ikaonekana kana kwamba alianguka chini kwa bahati mbaya.

**Mbele ya mfalme**

Hii ina maana. " mbele ya mfalme"

**Alimuonea huruma**

Hii inamaana, "kuwa na huruma" Kujisikia kuumia. Mfalme alijua kuwa mtumwa pamoja na familia yake watateseka sana iwapo wangeuzwa utumwani.


**akafuta deni lake lote**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "alisema kuwa mtumwa hakuhitaji kulipa pesa yoyote aliyokuwa anadaiwa na mfalme."

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- mfalme

29:05



"Ila baada ya mtumishi kutoka kwa mfalme, alimpata **mtumishi mwenzake** aliekua akimdai deni lenye thamani ya mshahara wa miezi minne. Alimkamata yule mtumishi mwenzake na kusema, ' Nilipe hela ninayo kudai!'"

### **mtumishi mwenzake**

Hii inarejea kwa mtu mwingine ambaye pia alikuwa mtumishi wa mfalme.

### **translationWords**

- [mtumishi](#), [mtumwa](#), [utumwa](#)

## 29:06



"Yule **mtumishi mwenzake** alianguka na **kupiga magoti** na kumwambia, 'Tafadhali nivumilie, nitakulipa kiasi chote unachonidai.' Ila, yule mtumishi **alimtupa mtumishi mwenzake ndani ya gereza** hadi atakapo lipa deni lake."

### **mtumishi mwenzake**

Tafsiri sentensi hii sawa sawa na 29:5.

### **kupiga magoti**

Sentensi hii inamaana sawa na 29: 4.

### **alimtupa mtumishi mwenzake ndani ya gereza**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "alitaka yule mtu atiwe gerezani." "Neno tupa" ni mfano unao maanisha ilifanyika kwa njiaya ulazima.

### **translationWords**

- [mtumishi](#), [mtumwa](#), [utumwa](#)



## 29:07



"Baadhi ya watumishi wengine walioona **kilicho tokea walifadhaika sana**. Wakaenda kwa mfalme na kumuambia kila kitu."

### **kilicho tokea**

Hii ni kwamba, " mtumishi alikataa kufuta deni la mtumwa mwingine na akamuweka kifungoni."

### **walifadhaika sana**

Hii ni kwamba , " walifadhaika sana."

### **translationWords**

- [mtumishi](#), [mtumwa](#), [utumwa](#)
- [mfalme](#)

29:08



"Mfalme **alimwita yule mtumishi** nakumuambia, 'Ewe mtumishi muovu! Nilikusamehe deni lako kwasababu ulinisihi. Ungefanya vivyo hivyo.' Mfalme alikasirika sana na kumtupa yule mtumishi muovu gerezani mpaka atakapo lipa deni lake lote."

### **alimwita yule mtumishi**

Hii ni kwamba, " alimuamru mtumwa kuja kwake" au aliwaamuru walinzi wake kumleta mtumishi kwake."

### **Ulinisihi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "alinihihi" au, kwa haraka aliniomba niwe mwenye rehema."

### **ungefanya vivyo hivyo**

Hii ni kwamba, "ungelimsamehe yule mtu aliye kudai kama vile mimi nilivyo kusamehe wewe."

### **Kumtupa**

Hii ni kwamba, "alimuamuru mlinzi wake kumweka."

### **translationWords**

- mfalme
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- samehe, kusamehe
- kuomba
- baya, ovu, uovu

## 29:09



**Ndipo Yesu akasema** " Hivi ndivyo baba yangu wa mbinguni atakavyo fanya kwa kila mmoja wenu kama hamtawasamehe ndugu zenu kutoka moyoni".

### **Ndipo Yesu akasema**

Lugha zingine zingeongeza, " kwa wanafunzi wake."

### **Hivi**

"Hivi" inarejea katika namna mfalme alivyo muadhibu mtumwa asiye samehe.

### **Baba yangu wa mbinguni**

Hii ni, " Baba yangu aliye mbinguni."Yesu anaeleza uhusiano wake wa kipekee kwa Mungu baba.

### **Ndugu zenu**

Hii inafanana na neno lililo tumika katika 29:1

### **Kutoka moyoni**

Hii ni kwamba, "kwa dhati" au, "kweli" au, "halisi" au, "kwa uaminifu."

Simulizi ya Biblia kutoka: Matayo18:21-35

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- samehe, kusamehe



## 30. Yesu Anawalisha Watu Eifu Tano

30:01



Yesu aliwatuma mitume kuwahubiri na kuwafundisha watu vijiji tofauti, nao waliporudi kwa Yesu, waka mueleza kile walicho fanya, Yesu akawaalika kwenda faragha ng'ambo ya mto kwa mapunziko, nao wakapanda mashua kuelekea ng'ambo ya mto.


### Faragha

Hii inamaanisha mahali palipo na watu wachache ambapo wangelikuwa wao pekeyao.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mtume, utume
- Kuhubiri

## 30:02



Lakini walikuwako watu wengi waliomuona Yesu na wanafunzi wakaondoka kwenye mashua, Watu walipita pembezoni mwa ziwa kuelekea upande wa pili mbele yao, hivyo Yesu na wanafunzi wake walipowasili, tayari kundi kubwa la watu walikuwako huko wakiwasubili.

### Walipowasili

Hii ni kwamba, "walifika ng'ambo ya pili ya ziwa" au, "walifika pale."

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi

**30:03**

Umati ulikuwa zaidi ya wanaume 5000 **bila kuhesabu wanawake na watoto**, Yesu aliona mkutano mkubwa mbele yake nao walikuwa kama kondoo waliokosa mchungaji, kwa hiyo akawafundisha na kuwaponya watu miongoni mwao ambavyo walikuwa wagonjwa.

**bila kuhesabu wanawake na watoto**

Hii ni kwamba, "bila kuhesabu wanawake na watoto waliokuwa nao" au "na pia walikuwepo wanawake na watoto zaidi kama ongezeko la idadi ya wanaume." Njia nyingine ya kutafsiri hii inaweza pia kuwa, zaidi ya wanaume, kulikuwa na wanawake na watoto."

**Kwa Yesu**

Hii ni kwamba, "Yesu alifahamu kwamba" au, Yesu alijua kwamba."

**Kama kondoo wasio na mchungaji**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "waliohatarini na waliopotea, kama vile kondoo wanavyokuwa wanapokuwa hawana mchungaji wa kuwaangalia."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kondoo, kondoo dume, kondoo jike
- mchungaji, kuchunga
- Ponya, tibu

## 30:04



na ilipokuwa jion wanafunzi walimwambia Yesu, tumechelewa na hakuna mji karibu, basi uwaage watu ili waweza kwenda kujitafutia kitu wale.

### **Baadaye mchana**

Hiiinaweza pia kutafsiliwa kama, "Wakati ilipokuwa karibu na jioni."

### **Watume watu waende zao**


Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Tafadhali waambie watu waende mjini" au kwa nini usiwambie watu kwenda mahali fulani?" au "Waache watu waende mjini." Hakikisha kwamba itasikika kama ombi la kumsihi mtu, si amri.

### **translationWords**

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



## 30:05



Yesu akawaambia wanafunzi, "mnaweza kuwapatia chochote wale!" wakamjibu ni vipi tunaweza kufanya hivyo? sisi tuna vipande vitano vya mkate na samaki wawili

### **Ni jinsi gani tunaweza kufanya hivyo?**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Hatuwezi kufanya hivyo!" au "Haiwezekani kufanya hivyo!" Wanafunzi hawakuwa wanauliza swali halisi. Isipokuwa, walikuwa wanaeleza kwamba hawakudhani hili kuwa linawezekana.

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi

**30:06**



Yesu akawaambia wanafunzi wa waambie watu kwenye umati wakae chini kwenye nyasi kwa makundi ya watu 50

**30:07**



Na Yesu akachukua vile vipande vitano vya mikate na samaki wawili, akatazama mbinguni akamshukuru Mungu kwa Chakula.

## 30:08



Kisha Yesu akaigawa mikate na samaki vipande, akawapatia vile vipande wanafunzi wawagawie watu. Wanafunzi wakaendelea kupita nje na chakura, wala hakikuisha, watu wote wakala na kutosheka.

### Vunja mkate na samaki

Hiyo ni, "kuvunja mkate na samaki."

### Haikumalizika

Njia nyingine ya kusema hii ingelikuwa, kulikuwa daima na ziada iliyosalia."

### Alitosheka

Hii ni kwamba, "Hawakuwa na njaa tena" au, "hawakuwa na njaa kabisa,"

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi



## 30:09



Baada ya hapo wanafunzi walikusanya mabaki ya chakula, navyo vilikuwa vikapu kumi na mbili, nacho chakula chote kilitokana na Mikate mitano na Samaki wawili.


Simulizi ya Biblia kutoka: Matayo 14:13-21; Marko 6:31-44; Luka 9:10-17; Yohana 6:5-15

## translationWords

- mfuasi

## 31. Yesu Atembea Juu ya Maji

31:01



Kisha Yesu aliwaambia wanafunzi wapande kwenye mtumbwi na wasafiri hadi ng'ambo ya ziwa wakati alipokuwa akiyaaga makutano. Baada ya Yesu kuyaaga makutano kwenda zao, alipanda mlimani ili aombe huko. Yesu alibaki huko pekee yake, na aliomba mpaka usiku wa manane.

### Aliwaaga makutano.

Hii ni namna nyingine ya kusema, "aliwaruhusu waende zao"

### Mlimani

Hii ni, "Upande wa Mlimani"

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Kuomba, maombi

**31:02**

**Wakati huo huo**, wanafunzi walikuwa wakipiga kasia kwa mtumbi wao, lakini wakati wa usiku wa manane walikuwa pekee yao katikati ya ziwa. Walikuwa wakipiga kasia kwa shida kwa sababu upepo ulikuwa ukivuma kinyume chao.

**Wakati huo huo**

Hii ni kwamba "Wakati Yesu alipokuwa akiomba juu Mlimani"

**wakapiga kasia za Mtumbwi wao**

Mtumbwi ulikuwa na tanga (Nguo inayofungwa kwenye mtumbwi ili upepo unapokuja ipate kuuendesha), lakini mtumbwi usingeweza kufanya kazi upepo unapobadilisha uelekeo." "upepo unapovuma kinyume chao"

**ngumu sana**

Hii ni "ngumu zaidi" au " ngumu zaidi"

**translationWords**

- mfuasi
- Kuomba, maombi



**31:03**



Kisha Yesu alimaliza kuomba na akaenda kwa wanafunzi. Alitembea juu ya maji akivuka ziwa mbele ya mtumbwi wao!



## 31:04



Wanafunzi walijawa na hofu kuu walipomwona Yesu, sababu walidhani walikuwa wakiona **roho**. Yesu hali akijua kuwa wanafunzi wake wameogopa, alipaza sauti kwao kusema, "**Msiogope**. Ni mimi!

### **roho**

Hii ni "roho" walidhani Kuwa Yesu ni roho, maana mtu wa kawaida hawezi kutembea juu ya Maji.

### **Msiogope**

Kwa baadhi ya Lugha inaweza kuwa kiasili zaidi kusema "acha kuendelea kuwa na uoga"

### **Mimi ndiye!**

Kwa baadhi, inaweza ikawa zaidi ya kawaida kutafsiri kuwa " mimi ndiye, Yesu"

### **translationWords**

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

## 31:05



Kisha Petro akamwambia Yesu, "Bwana, **kama ni wewe** niruhusu nije kwako juu ya maji". Yesu akamwambia Petro "Njoo!"

### **kama ni wewe**

Hii ni "Kama kweli ni wewe, na kama siyo roho."

### **Njoo!**

Hii ni, "Njoo hapa" au "Njoo kwangu" au "Njoo, Tembea uje kwangu"

### **translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- bwana, mkuu

## 31:06



Hivyo, Petro akatoka kwenye mtumbwi na kuanza kutembea kwenda kwa Yesu juu ya uso wa maji. Lakini baada ya kwenda mwendo mfupi, aliyaondoa macho yake kwa Yesu na kuanza kutazama mawimbi na kuhisi nguvu ya upepo.

### alipoangalia kwingine

Hii inaeleza maana, "Aliangalia mbali na". inaweza pia kutafsiriwa kama "Kuacha kuangalia kwa".

### translationWords

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



**31:07**

Kisha Petro akashikwa na woga na kuanza kuzama ndami ya maji. Akapaza sauti kwake, "Bwana, niokoe!" Yesu alimwendea na kumnyakua. Kisha akamwambia Petro, "Wewe mwenye imani haba, kwa nini umeona shaka?"

**Wewe mtu mwenye imani ndogo**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "Una imani ndogo sana juu yangu!" au, "Hauniamini mimi sana!"

**kwa nini una mashaka?**

Hii ni kwamba, "Hupaswi kuwa na mashaka juu yangu! au, "Unapaswa kuniamini mimi kabisa." Hili si swali la kweli lakini ni njia katika lugha hii ili kufanya wazo imara. Katika lugha nyingi, ina faa zaidi kufafanua hii kama maelezo au taarifa.

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- bwana, mkuu
- okoa, salama
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- imani



**31:08**

Wakati Yesu na Petro walipopanda ndani ya mtumbwi, mara upepo ulikoma kuvuma na maji yakatulia. Wanafunzi wakashangaa. Wakamwabudu Yesu wakisema, "Hakika, wewe ni Mwana wa Mungu".

*Simulizi ya Biblia Kutoka: Mathayo 14:22-33;*

**Wakati Yesu na Petro walipoingia kwenye mtumbwi, Upepo**

Ingekuwa vizuri zaidi kusema "Petro na Yesu wakaingia kwenye mtumbwi, na baadaye upepo."

**Walimwabudu Yesu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Wakainama chini kumwabudu Yesu." Hili ni neno ni wazo ni kuinama kimwili mbele ya mtu fulani kutokana na heshima na unyenyekevu

**Hakika wewe ni mwana wa Mungu.**

Njia nyingine ya kusema hii ni, "Wewe kweli ni mwana wa Mungu" au "Ni hakika na ni kweli kuwa wewe ni mwana wa Mungu.


Marko 6:45-52; Yohana 6:16-21.

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Abudu
- kweli, ukweli, kuwa kweli
- Mwana wa Mungu, Mwana

## 32. Yesu Amponya Mwanamume Aliyepagawa - pepo na Mwanamke Mgojwa

32:01



**Siku moja** Yesu na wanafunzi wake walipanda mashua kuelekea mjini, ambako waliishi watu wa Gerasini.

### Siku moja

Aya hii inatambulisha Tukio ambalo lilitokea wakati wa Nyuma, Lakini haisemi wakati maalumu. Lugha nyingi zina namna moja ya kuanza kusimulia habari ya kweli.

### Watu wa Gerasi

Wagerasi waliishi eneo la pwani upande wa mashariki mwa Bahari ya Galilaya. Walikuwa ni ukoo wa kiyahudi, Lakini tunajua habari chache tu kuwahusu wao.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi

## 32:02



Na walipofika upande wa pili wa ziwa, na alikuwako mtu mwenye mapepo alimkimbilia Yesu.

### **Mtu mwenye mapepo**

Hii ni, "Mtu aliyekuwa na mapepo ndani yake" au, Mtu aliyeongozwa na roho chafu."

### **Akaja anakimbilia kwa**


Hii ni kuwa, "Kimbilia kwa" au "Kimbilia na kusimama mbele ya"

### **translationWords**

- [Kuwa na mapepo](#)
- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)



### 32:03



Mtu huyu alikuwa mwenye nguvu na hapukuwa na mtu yeyote wa kumdhibiti. watu walimfunga kamba mikonon na miguuni mwake lakini bado aliweza kuzikata.

#### **Alifungwa miguu na mikono yake**

Hii ni kwamba, "Kuzuia" au, "Kufungwa"

#### **Aliendelea kuzikata.**

Lugha zingine zinaweza kusema, "Aliendelea kuvunja minyororo"



## 32:04



Mtu huyo aliishi maeneo ya makaburi na mtu huyu alitetemeka mchana na usiku kwa sababu hakuvaa nguo zozote na mwili wake alijikata kwa mawe.

### Katakati ya Makaburi

Hii ni, "Karibu na makaburi" au, Kuzunguka makaburi"

### translationWords

- [kaburi](#)

## 32:05




Mtu huyo alipokuja kwa Yesu, alianguka mbele ya magoti yake. Na Yesu akaliaamuru lile pepo "limtoke mtu huyo".

### **akapiga magoti.**

Hii ni, "Haraka alipiga magoti chini kwenye ardhi"

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu

**32:06**

mtu huyo mwenye pepo akalia kwa sauti " unataka nini kwangu Yesu, mwana wa Mungu aliyetukuzwa juu? tafadhali usinitese" ndipo Yesu akaliuliza lile pepo " je unaitwa nani"? akajibu " jina langu ni legionni" na kwa sababu tupo wengi ( " legionni" kikundi cha wanajeshi maelfu katika vikosi vya rumi).

**Alilia**

Hii ni, "Kupiga kelele" au, "toa sauti"

**Unataka nini kwangu**

Hii tafsiri ina maanisha, "Unaenda kufanya nini kwangu? au, "Unataka kunifanya nini?"

**Mungu aliye juu.**

Hii ni, "Mungu mkuu" au, "Mungu mwenye Enzi" Maana ya "Juu" hapa linahusika na ukuu wa Mungu. haimaanishi urefu au kuwa mrefu.

**kundi**

Hili lilikuwa ni jina la kikundi cha mapepo, Lakini pia imetafsiriwa kwamba roho chafu walikuwa wanatofautiana. Tumia jina hili kwa kuzingatia ili kwamba lilete maana iliyo wazi kwa lugha yako. kama sivyo unahitaji kutafsiri neno kama, "Jeshi" au, "Umati wa watu" au, Maelfu

**Tuko wengi**

Tuko wengi- Hii ni, "Wako wengi kati" Tuko mapepo wengi"

## translationWords

- Kuwa na mapepo
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Mungu



**32:07**

Yale mapepo yakamwomba Yesu " tafadhali usituondoe katika mji huu", na hapo palikuwa na kundi la nguruwe karibu na kilima, yale mapepo yakamwomba Yesu " tuamuru twende kwenye nguruwe hao" na Yesu akajibu "nendeni".

**usitufukuze**

Hii ni, "Usitufanye tuondoke." au, "Usituondoe"

**tafadhali tuamuru**

hii ni, "Tafadhali Turuhusu twende"

**Badala yake.**

Hii ni, "Badala ya kutuacha twende mbali"

**Nenda!**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "nendeni mkaingie kwa Nguruwe!" au, "mnaweza kwenda kwa wale Nguruwe"

**translationWords**

- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu
- kuomba
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

**32:08**

yale mapepo yakamtoka yule mtu na kuwaingia wale nguruwe, Na wale nguruwe wakakimbilia huko chini bondeni kwenye ziwa..... na palikuwako na nguruwe 2000 kundini.

**Kundi**

Hii ni, "Kundi la nguruwe" au, "Au kikundi cha nguruwe" Lugha nyingi zina majina maalumu kwa makundi ya wanyama, "Kundi la kundoo" "Kundi la mifugo" "kundi la Mbwa" na "Kundi la samaki." Tumia neno ambalo linaweza kuwa sahihi linaloweza kutumika katika kundi la nguruwe.

**translationWords**

- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu

**32:09**

Na watu wale waliokuwa wakiwaangalia wale nguruwe walipoona hayo yakitokea, walikimbia na kuelekea mjini na huko wakamwambia kila mmoja yakuwa wamemkuta Yesu na aliyokuwa akitenda. Na watu wa mjini wakaenda na kumwona yule mtu aliekuwa na mapepo. Alikuwa amekaa kwa utulivu,amevaa nguo na alikuwa anaonekana kama mtu wa kawaida.

**Nini Kimetokea**

Hii ni, "Jinsi Yesu alivyowatoa pepo nje ya huyo mtu na akwaagiza kwenda kuingia kwa nguruwe."

**Aliyekuwa na mapepo**

Hii ni, "Ambaye mapepo yalika ndani yake" au, "Aliyekuwa akiongozwa na roho chafu"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu

**32:10**

watu waliogopa na wakamuomba Yesu aondoke, ndipo Yesu akapanda ndani ya mashua na akijiandaa kwa ajili ya kuondoka. na mtu yule aliekuwa na mapepo akamusihhi Yesu aondoke pamoja naye.

**Watu**

Lugha zingine zingependekeza kusema, "Watu kutoka katika mkoa ule" au, "Watu wa Gerasini"

**Ogopa**

Itakuwa vizuri kusema, "Ogopa kwa sababu ya kile Yesu alifanya"

**Andaliwa**

Hii ni, "Alikuwa anajitayarisha"

**Alisihhi kwenda pamoja na Yesu**


Hii ni, "alimsihhi Yesu kwenda pamoja naye" au, "alimuuliza Yesu kwa Bidii kama anaweza kwenda naye"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kuomba



## 32:11



Yesu akajibu " hapana, ondoka uende nyumbani na uwaeleze marafiki na familia yako kuhusu yote alivyokutendea Mungu na alivyokufanyia huruma yake kwako.

### **alivyokuwa na huruma juu yako**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Namna alivyoonyesha huruma kwako" au, "Hivyo ndivyo alivyokuwa na huruma kwako"

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- rehema

**32:12**

ndipo mtu yule akaondoka na kumweleza kila mtu yale yote Yesu aliyomtendea. Na kila mtu aliye sikia simulizi hizi alishangaa na kusitaajabishwa.

**aliyesikia habari yake**

hii ni, "Kusikia mtu anasema kilichotokea kwake"

**alistaajabishwa na kushangazwa**

Maneno "Mshangao" na "Ajabu" yana maana sawa. Walikuwa wakiyatumia pamoja ili kuisitiza namna watu wa walivyokuwa wakifanyiwa. Hii inaweza kutasriwa kama, "Kushangazwa kabisa kuhusiana na kile alichowaambia"

**translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)

**32:13**

ndipo Yesu akarudi upande mwingine wa ziwa, na lipofika lilikuwako kundi kubwa la watu waliokusanyika wakimzunguka. na hapo alikuwapo mwanamke aliegua na kutokwa damu miaka kumi na miwili. Alilipa pesa yake yote kwa waganga ili wamponye lakini hali ilizidi kuwa ngumu.

**Kumsonga sana**

Hii ni, "kumkandamiza zaidi" au, "Makutano walimbana wakimzunguka"

**Hali iliendelea kuwa mbaya**

Hii ni, "Hali yake iliendelea kuwa mbaya," au, "Afya yake ilikuwa mbaya badala ya kuwa nzuri" au, "Badala yake alizidi kuwa Mgonjwa."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Ponya, tibu

**32:14**



Alisikia ya kuwa Yesu aliponya watu wengi na akafikiri" hakika kama nitagusa vazi la Yesu na mimi nitapona pia". hivyo akaja karibu na Yesu akamgusa vazi lake. na baada ya kumgusa tu, alipona na hakutokwa damu kwake kukaisha.



**32:15**

na ndipo Yesu akagundua yakuwa nguvu zimemuishia, hivyo akageuka nyuma na kuuliza " je ni nani aliye nigusa", wanafunzi wakamjibu " kuna kundi kubwa la watu limekuzunguka na wakikugusa je ni kwa nini umeuliza "ni nani aliyenigusa"

**Nguvu zimemtoka**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Nguvu ya uponyaji imehama kutoka kwake kwenda kwa mtu mwingine" au, "Nguvu yake imemponya mtu fulani." Yesu hakupoteza nguvu yeyote kwa sababu ya hili

**kwa nini uliuliza, nani amenigusa?'**

kwa lugha nyingine ni nzuri kutumia nukuu isiyo ya moja kwa moja hapa kama, "Kwa nini uliuliza nani alikuwa anakugusa?" au, "Kwa nini unashangaa aliyekugusa?"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Nguvu
- mfuasi

**32:16**

kisha yule mwanamke akaanguka magotini pa Yesu akitetemeka na kuogopa, akamwambia yale yote aliyo yatenda na alivyopokea uponyaji. Yesu akamwambia " enenda kwa amani, imani yako imekuponya.

**alipiga magoti**

Hii ni, "Akapiga magoti haraka"

**kumwelekea Yesu**

Hii ni, "mbele zaYesu."

**akitetemeka na uoga mwingi**

Hii ni, "Kutetemeka kwa hofu" au,"alitetemeka kwa sababu alikuwa ameogopa"

**Imani yako imekuponya**

hii ingeweza kutafsiriwa kama, "Umeponywa kwa sababu ya Imani yako."

**Enenda kwa amani.**

Watu husema kama baraka za kimila pale wanapoachana kila mtu. Lugha zingine zingesema mambo ya kufanana kama," Nenda vizuri" "Enenda na Mungu" au "amani." Njia nyingine ya kutafsiri hii ingekuwa, Uwe na amani unapoenda" au, "Nenda ukijua kuwa kila kitu kiko sawa kati yetu."


Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 8:28-34; 9:20-22; Marko 5:1-20; 5:24b-34; Luka 8:26-39; 8:42b-48.

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- imani
- Ponya, tibu
- Amani

## 33. Simulizi ya Mkulima

### 33:01



**Siku moja**, Yesu alikuwa akifundisha makutano wengi katika pwani ya ziwa. Na watu wengi walimfuata wapate kumsikiliza. Yesu aliingia ndani ya mashua mahali pa juu apate nafasi nzuri ya kuzungumza nao. Yesu alikaa kwenye mashua akawafundisha watu.

### Siku moja

hii aya, inatambulisha tukio lililotokea wakati wa nyuma, lakini haioneshi wakati maalumu. Lugha nyingi zina namna moja ya kusimulia habari ya kweli.

### translationWords

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)



## 33:02



Yesu aliwasimulia hadithi, "Mpanzi alikwenda kupanda mbegu shambani, alipokuwa akimwaga mbegu kwa kutumia mikono yake. Mbegu zingine ziliangukia kwenye njia, ndege wakazila zote."

### **Kumwaga mbegu kwa mkono**

Hii ni, "Kutupa mbegu kwenye udongo" au, "kufunika mbegu zake zote kwa udongo." Hii ndiyo njia kwa wakulima wa kale Mashariki ya kati walivyopanda nafaka zao kuzalisha mazao.

### **translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)

### 33:03



"Mbegu zingine zilianguka kwenye **ardhi yenye mawe**, nazo zikachipuka haraka. Lakini jua lilipowaka zote zika unguwa, kwa sababu mizizi haikuweza kustawi vizuri katika ule udongo mchache, hivyo miche ile ikafa."

### **ardhi yenye mawe**

hii ni, "ardhi ambayo imejaa miamba."

## 33:04



"Mbegu zingine zilianguka kwenye miiba, nazo zikamea lakini zikasongwa na miiba. Kwa hiyo mbengu hizo hazikuweza kuzaa matunda."

### **Miiba**

Hii ni, "Miti ya miiba" au, "Kichaka cha miiba."

### **ikaisonga**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "ikazifunikana na kivuli" au, "Kuibana."

### **Ardhi ya miiba**

hii ni, "Ardhi ambayo imefunikwa na kichaka la miiba."



**33:05**

"Mbegu zingine ziliangukia penye **udongo mzuri**. Mbengu hizo ziliweza kustawi na kuzaa 30, 60 na 100 zaidi kadri ya wingi wake katika kupandwa. Aliye na masikio, na asikie."

**udongo mzuri**

Hii ni, "udongo wenye rutuba" au, "udongo ambao ni mzuri kuotesha mmea."

**mwenye masikio, na asikie!**

msemo huu unamaanisha, "Kila mmoja anayesikia ninachosema anapaswa kunisikiliza kwa makini" au, "kama kila mmoja amesikia nilichosema anapaswa kuwa makini kwa kile nilichomanisha." hii pia inaweza kutafsiriwa kama amri. "Ikiwa una masikio ya kusikia, sikiliza kwa makini kwa kile ninachomanisha."

**translationWords**

- wema, uzuri



**33:06**

Hadithi iliwachanganya watu. Naye Yesu akawafafanulia akasema, "mbegu ni neno la Mungu. Mbegu zilizoanguka kwenye njia, ni yule mtu anaye lisikia neno la Mungu, lakini halielewi. Shetani huja na kulichukua neno kwa mtu huyo."

**Habari hii iliwachanganya wale wanafunzi.**

Hii ni, "wanafunzi hawakuelewa habari hii."

**Ni mtu**

Huu mlinganisho unaweza kutafsiriwa kama, "ni kama mtu" au, "Inawakilisha mtu" au, "Inahusiana na mtu" au "anaongelea kuhusu mtu."

**hulichua neno kutoka kwake**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, Huchukua neno la Mungu, anasababisha kulisahau" au, "huiba neno kutoka moyoni mwake ili kwamba hawezi kuliadini neno na kuokolewa." unaweza kuongeza pia haya yafuatayo: ndege walikula mbegu zilizoanguka kwenye njia."

**translationWords**

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Shetani, ibilisi, yule muovu

## 33:07



"ile ardhi ya udongo wa mawe, ni yule mtu anayelisikia neno na kulipokea kwa furaha. Lakini yajapotokea mateso na majaribu, hushindwa kustahimili na huanguka dhambini."

### **ardhi yenye miamba**

Onyesha ni jinsi gani unaweza kutafsili

### **ni mtu**

Angalia jinsi unaweza kutafsili maelezo haya

### **analipokea kwa furaha**

Hiyo ni, "Wanaamini kwa furaha" au Kukubali kwa furaha kuwa ni kweli."

### **huangukia mbali**

Hiyo ni, "Hamfuati Mungu au kumtii yeye" au, "Kuacha kumfuata au kumtii Mungu"

### **translationWords**

- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- furaha, mwenye furaha
- Kuwatesa, mateso

## 33:08



"Ardhi yenye miiba, ni yule mtu anayelisikia neno la Mungu, lakini kwa kadri siku zinavyoendelea, **utajiri**, anasa za maisha humtenga na upendo wa Mungu. Matokeo yake, lile neno la Mungu alilolisikia halizai matunda."

### **ardhi ya miiba**

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii

### **ni mtu**

Ona jinsi gani unaweza kutafsili hii

### **kujali**

hiyo ni, "Wasiwasi" au "Mahitaji" au Matatizo."

### **utajiri**

hiyo ni, "Tamaa ya utajiri."

### **Anasa za maisha**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama "Kufanya vitu flani ili kupata anasa" au "Kushughulika na vitu ambavyo zitakupa anasa."

## **hulisonga**

hii ni, "Vuruga" au, "Haribu" au kushinda." haya maneno yanaweza pia kutafsiriwa kama, "Humsababisha kuacha kumpenda Mungu."

## **haikuweza kuzaa matunda**

Hii ni, "Hawezi kuzaa matunda ya kiroho" au, "haonyeshi hali ya Roho wa Mungu ambaye anafanya kazi ndani yake."

## **translationWords**

- [Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko](#)
- [upendo](#)
- [Mungu](#)



## 33:09



"ule **udongo mzuri** ni yule mtu anaye lisikia neno la Mungu na kuliaminii hivyo huzaa matunda.

### **udongo mzuri**

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii

### **ni mtu**

Angalia jinsi unaweza kutafsili maelezo haya

### **zaa matunda**

...Angalia jinsi unaweza kutafsili kipengele hiki

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 13:1-8, 18-23; Marko 4:1-8, 13-20; Luka 8:4-15

### **translationWords**

- wema, uzuri
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Kuamini, kuamini katika

## 34. Yesu Anafundisha Mambo Mengine

### 34:01



Yesu aliwaambia masilimuzi mengi kuhusu ufalme wa Mungu .Kwa mfano,alisema,"Ufalme wa Mungu ni kama **punje ya haradali** ambayo mtu aliipanda shambani mwake.Unajua kwamba punje ya haradali ni ndogo kuliko punje zote."

### Habari

Yesu alitumia habari hizi kufundisha ukweli wa ufalme wa Mungu. haiko wazi kama tukio lilitukia au hakuna. Kama lugha yako ina neno linalounganisha vyote habari za kutunga na za kweli, unaweza kuitumia hapa.

### **punje ya haradali**

Hii pengine inatoakana na mbegu ya haradali Nyeusi, ambayo ina vimbegu vidogo ambavyo vinakua haraka na kuwa mti mkubwa . kama kuna neno katika mti huu kwa Lugha yako, unaweza kutumia. kama hakuna unahitaji mbala wa jina la mti huo wenye sifa zinazofanana.

### **mbegu ndogo kuliko zote**

Hiyo ni, ni mbegu ndogo kuliko zote ambazo watu wanapanda."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni

## 34:02



"Lakini wakati punje ya haradali inapokuwa, inakuwa kubwa kuliko mimea yote bustanini, inakuwa na ukubwa wa kutosha hata ndege huja na kutua kwenye matawi yake,"

### **Punje ya haradali**

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii

### **kukua**

Unaweza kuongeza, "mmea uliokua."

### **Mimea ya Bustanini**

Hii pia inaweza kuytafsiriwa kama, "mmea unaopandwa kwenye bustani."

### **Kupumzika ndani yako**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "Kukaa juu, "Kutua juu yake."

### 34:03



Yesu akawaambia simulizi nyingine , "Ufalme wa Mungu ni kama amira aliyoichanganya mwanamke kwenye baadhi ya donge la mkate na mpaka kusambaa kwenye donge lote."

### Habari

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii

### hamira

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "chachu" au, "chachu kidogo" inawekwa kwenye unga wa mkate ili kutengeza Donge. mara chache hamira inaweza kuchanganywa na unga mwingi na kuufanya unga wote kuumka.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni



## 34:04



"Ufalme wa Mungu pia unafanana kama hazina ambayo mtu ameificha shambani. Mtu mwingine akaikuta hazina hiyo na kuifukia tena. Alijawa na furaha kiasi kwamba akaenda kuuza kila kitu alichonacho na akatumia fedha hiyo kununua shamba hilo."

### **Hazina**

hiyo ni, "Ni kitu ambacho ni cha thamani."

### **kuizika tena**

Inawezekana pia kuongeza, Ili kwamba hakuna mwingine anaweza kuipata."

### **akijawa na furaha**

Njia nyingine ya kusema hii ni kwamba, "Furaha kuu" au, "Msisimko"

### **nunua shamba lile**

watu wengine wanaweza kuongeza. "Ili kwamba hazina iwe yake."

### **translationWords**

- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- furaha, mwenye furaha

## 34:05



"Ufalme wa Mungu pia ni kama lulu kamili ya thamani kubwa .Mfanyabiashara wa lulu alipoipata, aliua vitu vyote alivyokuwanavyo na kutumia fedha hiyo kununua hiyo lulu.

### **Lulu Kamili**

Hii ni, "lulu isiyokuwa na kasoro."

### **Lulu**

Kama lulu haijulikani, hii inaweza kutafsiriwa kama, "Jiwe zuri" au, "kama aina fulani ya jiwe."

### **yenye thamani kubwa**

Hii ni, "hiyo ni ya thamani kubwa" au, "hii ilikuwa thamni ya pesa nyingi."

### **Mfanya Biashara wa Lulu**

Hii ni, "Muuzaji wa lulu" au, "Mchuuzi wa lulu."Hii inatokana na mtu ambaye biashara yake ni kununua na kuuza.

### **translationWords**

- [ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni](#)

**34:06**

Tena Yesu akawaambia simulizi ya baadhi ya watu ambao wameweka tumaini katika matendo yao mema na kudharau watu wengine .Akasema. "Watu wawili walikwenda hekaluni kusali .Mmoja alikuwa mtoza ushuru na mwingine kiongozi wa dini."

**habari**

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii

**wanatumaini matendo yao mema.**

Hii ni, "waliamini kuwa matendo yao mema yanawafanya kuwa wenye haki" au, "walijivunia kuwa wakamilifu kwa kushika sheria" au, "Waliamini kuwa matendo yao mema yanamfanya Mungu awafurahi kikamilifu."

**Dharau watu wengine**

Hii ni "inahusisha watu wengine ambao wana waudhi " au " kuonekana chini kwa watu wengine"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- imani, aminifu,
- hekalu
- Kuomba, maombi
- ushuru
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini

**34:07**

"Kiongozi wa dini aliomba hivi. 'Asante, Mungu kwamba mimi siyo mwenye dhambi kama watu wengine - mfano wanyanganyi, **wasio haki**, wazinzi, au hata kama huyu mtoza ushuru'".

**Viongozi wa dini waliomba hivi**

Njia nyingine ya kusema hii ingekuwa, "Hivi ndivyo viongozi wa dini waliomba" au, "viongozi wa dini waliomba kwa njia hii."

**mimi simenye dhambi kama**

Hii ni, "Mimi si mwenye dhambi kama" au, "mimi ni mwenye haki , si kama."

**wasio haki**

hiyo ni, "watu wasio haki " au, "Watu wanaofanya mambo maovu" au, "Wajunja sheria"

**translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Mungu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi
- ushuru



## 34:08



"Kwa mfano, nafunga mara mbili kwa wiki na kukutolea moja ya kumi ya pesa zote na mali zote nzipatazo."

### **Ninafunga**

watawala wa kidini waliamini kuwa kwa kufanya hivi kunaweza kupata Neema kwa Mungu.

### **Asilimia kumi**

Hii ni, "Moja ya Kumi." au "zaka."

### **translationWords**

- funga

**34:09**

"Lakini mtoza ushuru alisimama mbali na kiongozi wa dini hata hakuelekeza uso wake mbinguni. Badala yake alijipiga ngumi kifua chake na akaomba, "Mungu, tafadhali unirehemu mimi kwa sababu ni mwenye dhambi."

**simama mbali**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "Simama kwa umbali" au, "Kukaa umejitenga."

**Hakutazama hata juu mbinguni**

Neno "hata" linaashiria kuwa watu kawaida huangalia juu wanapokuwa wanaomba kwa Mungu, lakini huyu mtu hakufanya hivyo kwa sababu alikuwa anaona aibu kwa ajili ya dhambi zake.

**alijipigapiga juu ya kifua chake kwa ngumi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kwa sababu ya huzuni, alipigapiga kifua chake kwa ngumi" au, "alipigapiga kifua kwa huzuni" kama watu watagundua kuwa hii kuwa ni ngumu kuelewa kwa sababu huwanapiga vifua vyao kwa sababu nyingine, unaweza kutafsiri hii kama, "Alionyesha kukata tamaa."

**translationWords**

- ushuru
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- mbingu, anga, mbinguni
- Kuomba, maombi
- Mungu
- rehema
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**34:10**

"Kisha Yesu akasema, "Lakini nawaambieni ukweli, Mungu alisikia maombi ya mtoza ushuru na **kumtangaza kuwa mwenye haki**. Lakini hakuyapenda maombi ya kiongozi wa dini. Mungu humshusha kila ajikwezae na humpandisha kila ajinyenyekezaye,"

**kumtangaza kuwa mwenye haki**

hii ni, "kumfikiria kuwa ni mwenye haki." hata hivyo watoza ushuru walikuwa wenye dhambi, Mungu alikuwa mwaminifu kwake kwa sababu ya utu wake na toba yake.

**kunyenyekoa**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "alijishusha" au, "itakufanya kutokuwa wa muhimu." inaweza kutafsiriwa pia lugha ya mafumbo, "atakushusha"

**atakuinua**

hiyo ni, "atakupa nafasi ya juu" au, "atakuheshimu."

**kujishusha mwenyewe**

Hii ni, "Kuchagua kuishi kwa kujishusha" au, "ana tabia za kujishusha yeye mwenyewe."

Simuliziya Biblia kutoka: Mathayo 13:31-33; 44-46; Marko 4:30-32,; Luka 13:18-21; 18:9-14

**translationWords**


- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kweli, ukweli, kuwa kweli

- Mungu
- ushuru
- Kuomba, maombi
- Adili, uadilifu
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- nyenyekea, unyenyekevu
- Kiburi



## 35. Habari za Baba mwenye Huruma

### 35:01



Siku moja, Yesu alikuwa akiwafundisha watoza ushuru wengi na watu wenye dhambi waliokusanyika kumsikiliza.

#### siku moja

Hii aya inatambulisha tukio ambalo lilitokea kipindi cha nyuma, lakini haisemi muda kamili. lugha nyingi zina namna moja ya kuanza kutoa habari ya kweli.

#### Watoza Ushuru

Watoza ushuru walidhaniwa kuwa wenye dhambi kabisa waliiba pesa kwa watuykwa kukusanya ushuru kwa hali ya juu kuliko walivyoagizwa na serikali.

#### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ushuru
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

## 35:02



Viongozi wa dini waliokuwepo pale walimshutumu Yesu, kwa vile walimuona akiongea na wale wenye dhambi kama rafiki zake. Yesu akawaambia hadidhi hii.

### habari

Yesu alitumia habari hii ili kufundisha ukweli kuhusu ufalme wa Mungu. haiko wazi kama tukio lilitokea kweli au hakuna. kama lugha yako ina habari kama hiyo ya kufikirika au kweli, unaweza kuitumia hapa.

### translationWords

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

## 35:03



"Kulikuwa na mtu mwenye watoto wawili wa kiume, Mdogo alimuambia Baba yake, Baba nipe sehemu ya uridhi wangu! Baba yake akagawa mali zake kwa watoto wake wawilii.

### Urithi wangu

hii ingetafsiriwa kama, "Sehemu ya mali yako ambayo itakuwa haki yangu ya halali unapokufa"


### Mali

Hii ni "Mali" au, "milki." Hii mali inaweza pia kuwa ardhi, wanyama, na pesa"

### translationWords

- mwana, mwana wa
- rithi, urithi, mrithi

## 35:04



Baada ya muda mfupi, yule kijana mdogo alikusanya uridhi wake wote , kisha akaenda nchi ya mbali na kuanza kutapanya fedha zake kwa njia ya anasa.

### **Alitapanya pesa zake**

hiyo ni, "kutumia pesa bila kupata chochote cha thamani kwa kubadilisha." Kwa lugha zingine inaweza kutafsiriwa kama, "Kutupa pesa" au, "Kula pesa zote."

### **Maisha ya dhambi**

hii ni, "kutenda vitu viovu."

### **translationWords**

- [dhambi](#), [yenye dhambi](#), [mwenye dhambi](#), [kufanya dhambi](#)



**35:05**

Baada ya muda, njaa kali ikatokea katika nchi alikokwenda huyo kijana mdogo, akawa hana fedha ya kununulia chakula. Akatafuta **kazi** aliyoweza kufanya ambayo ni kulisha nguruwe. Hali yake ya maisha ikawa mbaya kiasi kwamba alitamani kula chakula kile cha nguruwe.

**Njaa kali ilitokea**

Hii ni, "kulikuwa na chakula kidogo." kwa lugha zingine hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kulikuwa na njaa kali."

**hakuna pesa kununua chakula**

kwa sababu ya njaa, chakula kilikuwa na gharama kubwa, na tayari alishatumia pesa zake zote.

**kazi**

hii inalenga kazi ambayo unaweza ukafanya kwa ajili ya mtu mwingine ili akulipe pesa. kama hii haiko wazi, hii sentensi inaweza kuanza hivi, "Ili kujipatia pesa, alipata kazi."

**Kulisha nguruwe**

Hii ni, "kutoa chakula kwa nguruwe." hii pia inaweza kudhaniwa kuwa ni kazi ya hali ya chini katika jamii kwa kipindi hiki. kama lugha yako ina badhi ya maneno kwa kazi ya hali ya chini, tumia neno hili.

## 35:06



Mwishowe, yule kijana mdogo akajiambia moyoni, ninafanya nini hapa? Watumishi nyumbani mwa Baba yangu wanakula vizuri wakati mimi nakufa na njaa hapa. Nitakwenda na kumuomba Baba anifanye mmoja wa watumishi wake.

### Nafanya nini?

Hii ni, "kwa nini ninaishi hivi?" au, "sipaswi kuishi hivi!" au, "haileti maana kwangu kuishi namna hii." kijana alikuwa haulizi maswali, kwa hiyo lugha zingine zinaweza kutafsiri hii kama maelezo.

### translationWords

- [mtumishi](#), [mtumwa](#), [utumwa](#)

**35:07**

Hivyo, kijana mdogo akaanza safari ya kurudi nyumbani, akiwa bado mbali na nyumbani, Baba yake alimuona na kumuonea huruma kisha akamkimbilia na kumkumbatia na kumbusu mtoto wake.

**akiwa mbali**

hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "Ndani ya maeneo ya nyumba ya babaye, lakini bado ni mbali kidogo." kijana alipokuwa akikaribia kwenye nyumba ya baba yake, lakini alikuwa mbali na hata watu wa nyumbani hawakuweza kumwona. Hakikisha isije ikajulikana kuwa alikuwa bado katika nchi tofauti.


**akuhurumia**

Hii ni, "Alipenda kwa upendo wa dhati na huruma"

**translationWords**

- mwana, mwana wa

## 35:08



Kijana mdogo akasema, "Baba, nimemtenda Mungu dhambi na wewe pia, sistahili kuitwa mwanao tena."

### **nimekosa mbele za Mungu na mbele zako**

hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kuasi kinyume na Mungu, na pia nimeasi mbele zako."

### **Sisitahili**

inawezekana pia kusema, kwa hiyo sisitahili" au, "kama matokeo, sisitahili."

### **translationWords**

- mwana, mwana wa
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu



**35:09**

Lakini Baba yake akamwambia mmoja wa Watumishi wake, harakisha kachukue nguo nzuri na kumvisha mwanangu, mvisheni pete kwenye kidole chake, mvalisheni viatu miguuni mwake. Kisha mchinjeni ndama aliyenona ili tule na kusheherekea, kwasababu mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai, alikuwa amepotea na sasa kapatikana.

**Ndama mzuri**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Ndama mnene." huyu alikuwa ndama aliyenenepeshwa ili kwamba akipikwa alete radha nzuri.

**Mwanangu alikuwa amekufa, lakini sasa ni mzima!**

hii ni, "Hii ni kama mwanangu alikuwa amekufa na sasa ni mzima!" au, "niliomboleza kana kwamba " Mwanangu alikufa, na sasa nafurahi kwa sababu ni kama amerudi kuwa hai tena! Baba alitumia maelezo haya ili kueleza furaha aliyonayo kuwa mtoto wake amerudi nyumbani.

**alikuwa amepotea na sasa amepatikana**

hiyo ni, " ni kama nilikuwa nimempoteza lakini sasa nimepata."

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- mwana, mwana wa
- kifo, kufa, mfu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

## 35:10



Watu wakaanza kusherehekea, na kabla mda mwingi haujapita, kaka yake mkubwa akarudi toka shambani. Alipofika nyumbani alisikia sauti ya muziki na watu wakicheza , akashangaa juu ya kilichokuwa kinaendelea.

### Muda mfupi

hii inaweza kutafsiriwa kama, "muda si muda" au, "Baada ya muda kitambo."

**35:11**



Baada ya kutambua kuwa watu wanasheherekea kwasababu ya kurudi kwa mdogo wake, alikasirika sana na kukataa kuingia nyumbani. Baba yake alikuja kumbembeleza na kumsihi aingie nyumbani ili washerehekee pamoja lakini alikataa.

**35:12**

"Kijana mkubwa akamuambia Baba yake, mimi nimefanya kazi kwa uaminifu miaka yote , nimekutii kwa wakati wote, na hujawahi hata kunipa mbuzi mdogo wa kumchinja ili kusheherekea na rafiki zangu, ila alipokuja huyo kijana wako aliyetapanya na kutumia mali zako vibaya ulimchinjia ndama aliyenona."

**Mbuzi mmoja mdogo**

Mbuzi mdogo anaweza kuliwa na watu wachache kuliko ndama aliyenona, na asingeweza kuthaminiwa sana. kaka mkubwa analalamika kuwa baba yake anamwona mtoto mwenye dhambi ni mhimu kuliko yeye.

**Mtoto huyu ni wako**

fafanuzi hii inaonyesha kuwa mtoto mkubwa alikuwa na hasira. inaonyesha kumkataa mdogo wake na kumkasirikia baba yake kwa kumkaribisha nyumbani tena mtoto mpotevu. lugha zingine pia zina njia ambayo si ya moja kwa moja ya mawasiliano ya vitu hivi.

**kutumia pesa zako**

hii ni, "aliponda pesa ulizompa" au, "alikula mali yako" kama inawezekana tumia maelezo ambayo yanaonyesha hasira za kaka mkubwa.

**kuchinja ndama aliyenona**

Hii ni, "Kuuu ndama aliyenona kwa ajili ya kukla kwenye sikukuu."

**translationWords**

- mwaminifu, uaminifu
- totii, mkaidi, kutotii



- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**35:13**

Baba yake akamjibu kuwa, wewe uko pamoja nami siku zote, na kila nilicho nacho ni cha kwako. Imetupasa kusherehekea kwa kuwa, Mdogo wako alikuwa amekufa na sasa yu hai, alikuwa amepotea na sasa amepatikana.

**ni haki kwetu**

Hii ni, "Ni kitu sahihi kwetu kufanya" au, "Ni kitu sahihi kwetu"

**Ndugu yako**

baba alirejea kwa mwana wake mdogo kama, "Ndugu yako" kumkumbusha mwana mkubwa mahusiano yake kwa mdogo wake na alivyopaswa kumpenda mdogo wake.

**alikuwa amekufa, lakini sasa yuko hai**

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii

**alikuwa amepotea, lakini sasa amepatikana!**

Angalia jinsi unaweza kutafsili hii


Simulizi ya Biblia kutoka: Luka 15:11-32

**translationWords**

- mwana, mwana wa
- kifo, kufa, mfu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

## 37. Kubadilika Sura

36:01



**Siku moja**, Yesu aliwachukua wanafunzi wake watatu **Yakobo**, Petro na Yohana. ( Mwanafunzi aitwae Yohana sio yule aliyembatiza Yesu.) Walipanda juu ya mlima mrefu kuomba pekeyao.

### Siku moja

Kipengele hiki kinatambulisha tukio ambalo lilitokea kipindi kilichopita, lakini halielezi muda maalumu. Lugha nyingi huanza kuelezea habari ya kweli kwa njia inayofanana.

### Yakobo

Huyu ni Yakobo tofauti na yule aliyehandika Kitabu cha Yakobo kwenye Biblia. Kwa kuweka wazi hili, baadhi ya lugha zinaweza kuhitaji kidogo kutumia majina tofauti mawili au kutofautisha kulitamka.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yohana (mtume)
- Batiza, ubatizo

## 36:02



Yesu akiwa anaomba uso wake ulibadilika na kung'aa kama jua na mavazi yake yakawa meupe kama mwanga, yalikua meupe sana zaidi awezavyo mtu duniani kuyafanya yang'ae.


### **Kitu cheupe**

Hiki ni , "cheupe zaidi" pia kinaweza kutafsiriwa kama nuru (chanzo cha mwanga) au angavu

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuomba, maombi



**36:03**

Ndipo Musa na nabii Eliya wakawatokea. Watu hawa waliishi duniani miaka mingi kabla. Waliongea na Yesu juu ya kifo chake ambacho kitatokea Yerusalemu siku chache baadae.

**iliyoonekana**

Vilevile inawezekana kusema, "ilionekana bila kujua ilikotokea." Ghafla walikuwa pale au, walitokea kwa ghafla.

**kifo chake, ambacho kingetokea karibuni**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "jinsi atakavyo kufa karibuni" au, "jinsi ambavyo wangemuua muda si mrefu"

**ndani ya Yerusalemu**

Baadhi ya lungha zinaweza kupendelea kusema, "katika jiji la Yerusalemu."

**translationWords**

- Musa
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Eliya
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kifo, kufa, mfu
- Yerusalemu

**36:04**

Wakati Musa na Eliya wanaongea na Yesu, Petro akamwambia Yesu, "Ni vizuri sisi kuwa hapa, hivyo naomba tutengeneze nyumba tatu moja ya kwako, nyingine ya Eliya na nyingine ya Musa". Lakini Petro hakujua alinenalo.

**vibanda**

Hii vilevile inaweza kutafasiriwa kama, "kivuli" au vibanda vya bustanini" au, hema. Hii inarejea kwenye baadhi ya vibanda vidogo vya muda, kama walivyovitengeneza wayahudi kutokana na matawi wakati wa sikuu ya kiyahudi.

**hakujua ambacho alikuwa akisema**

Ni kwamba "alikuwa anazungumza bila kuelewa kilichokuwa kinatokea" au, " alizungumza bila kufikiria vizuri kwa sababu alikuwa na furaha sana."

**translationWords**

- Musa
- Eliya
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Petro, Simoni Petro, Kefa
- wema, uzuri

**36:05**

Wakati Petro anaongea wingu jeupe lilishuka na kuwazunguka na sauti ikatoka katika lile wingu ikisema " Huyu ni Mwanagu nimpendaye. Ninayependezwa naye msikilizeni yeye".Wale wanafunzi watatu waliogopa na kuanguka chini.

**Sauti toka mawinguni ikisema**

Vilevile hii inaweza kutafasiriwa kama, "sauti ilizungumza kutoka mawinguni inasema, "au, Mungu alisikika kutoka mawinguni na kusema."

**Msikilizeni Yeye**

Hii inaweza kutafasiriwa kama, "ni Yeye pekee ambaye mnapaswa kumsikiliza."

**Anguka chini**

Huku ni, "kuinama chini kwa haraka" au, "kufika chini ghafla." yaani kusujudu. Hakikisha kwamba tafasiri ya "anguka" haimaanishi ajali. Huenda walifanya hili kwa unyenyekevu na hofu bila kutegemea.

**translationWords**

- [Petro, Simoni Petro, Kefa](#)
- [Mwana wa Mungu, Mwana](#)
- [upendo](#)
- [mfuasi](#)



**36:06**

Ndipo Yesu akawagusa na kuwaambia "**Msiogope** inukeni". walipotazama pembeni ni Yesu pekee ndiye aliyebaki pale.

**Aliwagusa**

Hii ni "akaweka mkono wake juu yao."Lugha zingine zinaweza kupendelea kuonesha aliwagusa wapi. Kama hivyo, hii ingetafasiriwa kama, "aliwagusa kwenye bega" au, "aliweka mkono wake kwa kila mtu begani."

**Msiogope**

Hii pia ingelitafasiriwa kwamba, "acha kuogopa"

**Inuka**

Hii inaweza kutafasiriwa kwamba, "inuka" au, "Tafadhali nakuomba inuka." Hakikisha inaleta maana kwamba Yesu alisema hili kwa upole.

**Yesu pekee ndiye alibakia pale**


Pia inawezekana kuongeza, Musa na Eliya tayari walishaondoka" yaani hawakuwepo pale.

**translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)



## 36:07



Yesu pamoja na wanafunzi wake watatu wakashuka kutoka mlimani. Yesu akawaambia "Msimwambie mtu yeyote yale yaliyotokea, siku chache baadae nitakufa kisha nitakua hai tena. Baada ya hapo mtawaambia watu."


Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 17: 1-9; Marko 9:2-8; Luka 9:28-36

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- kifo, kufa, mfu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

## 37. Yesu Amfufua Lazaro kutoka Wafu

### 37:01



**Siku moja**, Yesu alipata habari kuwa Lazaro ni mgonjwa sana. Lazaro na dada zake wawili- Martha na Maria walikuwa marafiki wa karibu wa Yesu. Yesu alipopata habari hizi alisema, "Huu si ugonjwa wa kifo, bali ni ugonjwa wa kumtukuza Mungu." Yesu aliwapenda marafiki zake, lakini alisubiri hadi siku mbili.

### Siku moja

Maneno haya yanaonesha tukio lililotukia kipindi kilichopita, lakini hayaelezi muda maalumu. Lugha nyingi zinanjia inayofanana katika kuanza kusimulia habari ya kweli.

### Mariamamu

Mama yake Yesu pia aliitwa Mariamamu. Huyu alikuwa ni mwanamke mwingine tofauti na mama yake Yesu.

### Ugonjwa huu siyo wa kifo

Hii inaweza kutafsirika kwamba, "matokeo ya ugonjwa huu siyo kifo" au, Lazaro ni mgonjwa, lakini kifo hayatakuwa matokeo kwenye ugonjwa huu." Huenda wanafunzi wa Yesu walifikiri inamaanisha kwamba Lazaro asingelikufa. Lakini Yesu alijua kwamba, ingawaje Lazaro atakufa kutokana na ugonjwa wake mwisho wake atakuwa hai.

### Ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu

Hii ni, "hii itawasababisha watu kumtukuza Mungu kwa jinsi alivyo mkuu."

## Lakini alisubiri mahali alipokuwa kwa siku mbili

Hii ingelitafasiriwa kuwa, "lakini alibaki mahali alipokuwa kwa siku mbili, hata kama walitaka aende na amponye Lazaro.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Lazaro
- kifo, kufa, mfu
- utukufu, fahari
- Mungu
- upendo

**37:02**

Baada ya siku mbili, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Twendeni tena **Uyahudi**." "Lakini mwalimu." Wanafunzi wake walisema, "Muda mfupi tu uliopita watu walitaka kukuuu!" Yesu alisema "Rafiki yetu Lazaro amelala usingizi na ni lazima nimwamshe."

**Uyahudi**

Hii inarejea sehemu ya kusini mwa Israeli, ambako waliishi kabila la Yuda. Lugha nyingine itapendelea kusema, "mkoa wa uyahudi."

**Amelala usingizi, na lazima nimwamshe**

Tafasiri kipengele hiki kwa maneno ya kawaida kwenye lugha yako yaani "kulala" na "amka." Ingawa Yesu alikuwa akitumia maneno haya akiwa na maana nyingine, bado wanafunzi hawakumwelewa.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- mwalimu, Mwalimu
- Lazaro



### 37:03



Wanafunzi wa Yesu walijibu, "Bwana, kama Lazaro amelala, basi atapata nafuu." Yesu aliwaambia wazi, "Lazaro amekufa, nafurahi kuwa sikuwepo ili mpate kuniamini."

### Atapata nafuu

Wanafunzi walidhani, "hakuna sababu ya sisi kwenda kwake sasa, sababu atapata nafuu."

### Nafurahi

Inaweza kutafasiriwa kuwa, "mimi ninafuraha" au, "hiyo ni nzuri." haina maana alikuwa na alifurahia kifo cha Lazaro, lakini zaidi kwamba alikuwa na furaha kwamba Mungu alikuwa aoneshe jinsi alivyo mkuu.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- bwana, mkuu
- Lazaro
- kifo, kufa, mfu
- Kuamini, kuamini katika

**37:04**

Yesu alipofika katika mji wa Lazaro, Lazaro alikuwa tayari amekufa kwa siku nne. **Martha** alikwenda kumwona Yesu akasema, "Bwana, kama ungekuwa hapa, kaka yangu asingekufa . Lakini ninaamini kuwa Mungu atakupa chochote umwombacho."

**Martha**

Martha alikuwa dada wa Lazaro na Mariamu.

**Alikwenda kukutana na Yesu**

Hii ni kwamba, "alikuwenda kumwona Yesu alipokuwa anakuja mjini."

**Kaka yangu asingelikufa.**

Hii ni, "ungelimponya kaka yangu na asingelikufa" au, "ungelizuia kufa kwa kaka yangu."

**Lolote uombalo toka kwake atakupa**

Hii ni, "atanfanya lolote unalomwomba toka kwake."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Lazaro
- kifo, kufa, mfu
- bwana, mkuu
- Kuamini, kuamini katika
- Mungu

**37:05**

Yesu akajibu akasema, "Mimi ni Ufufuo na Uzima, yeyote aniaminiye ataishi, hata kama akifa. Kila aniaminiye hatakufa. Unaamini hivyo?" **Martha** akajibu, "Ndiyo Bwana ninaamini kuwa wewe ni Masihi, Mwanawa Mungu."

**Mimi ni ufufuo na uzima**

Hii, "mimi" iliyotumika hapa ni kauli mojawapo yenye nguvu sana kati ya kauli zake Yesu anazosema kuhusu uasili wake. Hapa Yesu anaashiria kwamba yeye ni "mpaji" au "chanzo" cha ufufuo na uzima. Ikiwezekana tafasiri maneno haya kwa namna ambayo inaweka wazi umhimu wa asili. Hii inaweza kutafasirika kwamba, "Mimi ndiye hufufua watu na huwapa uzima"

**Ataishi hata kama akifa**

Hii ni, "hata kama atakufa, ataishi milele." Neno la kiingereza "Yeye" si kwamba linarejea kwa wanaume tu pia wanawake wanaoamini wataishi milele.

**Martha**

Martha alikuwa dada yake Lazaro na Mariamu.

**Hatakufa**

Hii inaweza kutafasiriwa kwamba, "ataishi milele."

**translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)
- [Ufufuo](#)
- [maisha, uhai, kuishi, kuwa hai](#)

- Kuamini, kuamini katika
- kifo, kufa, mfu
- bwana, mkuu
- Kristo, Masihi
- Mwana wa Mungu, Mwana



**37:06**

Maria alipofika. **Alianguka miguuni pa Yesu** akasema, "Bwana, kama wewe tu ungekuwepo kaka yangu asingekufa." Yesu akawauliza, "Mmemuweka wapi Lazaro?" Walimjibu " Kaburini, njoo uone." Yesu alilia.

**Mariam**

Huyu ni mwanamke ambaye siyo mama yake Yesu.

**Alianguka miguuni pa Yesu**

Hii ni, "alipiga magoti miguuni pa Yesu" ikiwa ishara ya heshima.


**Kaka yangu hangelikufa**

Ni kwamba, "ungelifanya kaka yangu asife" au, "ungalizuia kifo cha kaka yangu" au, "kaka yangu angelikuwa hai."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- bwana, mkuu
- kifo, kufa, mfu
- Lazaro
- kaburi

## 37:07



Kaburi lilikuwa pango limefunikwa na jiwe. Yesu alipofika kaburini aliwaambia, "Liondoeni jiwe." Lakini **Martha** alisema, "Amekuwa kaburini sasa siku nne, ananuka!"

### Yeye aliwaambia

Hii ni, "Aliwaambia watu pale." Huenda alikuwa hawaambii Martha na Mariamu kuliiondoa jiwe.

### Ondoa jiwe

Baadhi ya lugha zitapendelea kusema, "ondoa jiwe kutoka kwenye kaburi."

### Martha

Martha alikuwa dada yake Lazaro na Mariamu.

### Amekufa kwa siku nne

Hii pia inatafsirika kama, "Alikufa siku nne zilizopita na mwili wake umelazwa pale."

### translationWords

- kaburi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kifo, kufa, mfu

## 37:08



Yesu alijibu, "Je, sikusema kuwa kama ukiniamini utaona utukufu wa Mungu?" Ndipo wakaliondoa jiwe.

### Mimi sikuwaambia ninyi?

Hili, "kumbukeni kwamba niliwaambia." Si kwamba Yesu anawauliza swali ili apate jibu, hivyo lugha zingine zitatafsiri hii kama amri.

### Ona utukufu wa Mungu


Hii ni, "tazama utukufu wa Mungu uliyodhihilishwa" au "tazama Mungu anavyoonesha ukuu wake."

### Liondoe jiwe

Baadhi ya lugha zitasema, "liondoeni jiwe mahali pa mlango wa kaburi."

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- utukufu, fahari
- Kuamini, kuamini katika

**37:09**

Basi Yesu alitazama juu mbinguni akasema, "Baba, asante kwa kuwa unanisikia. Tena najua wewe hunisikia siku zote. Lakini nimesema haya kwa ajili ya watu hawa waliosimama hapa, kwa kuwa wataamini kuwa ulinituma." Kisha Yesu akapaza sauti, "Lazaro, njoo nje."

**Unanisikia**

Hii ni, ""unanisikiliza." Inaweza kusaidia kuongoza, "kama niombavyo kwako" au, "nizungumzapo kwako."

**Njoo nje**

Baadhi ya lugha zinaweza kupendelea kusema, "toka nje kaburini"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mbingu, anga, mbinguni
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- Kuamini, kuamini katika
- Lazaro



## 37:10



Ndipo Lazaro alitoka nje! Alikuwa bado amefungwa sanda, Yesu akawaambia, "Msaidieni kuondoa sanda na mwacheni huru!." Wayahudi wengi walimwamini Yesu kwa sababu ya muujiza huu.

### Lazaro alikuja kutoka nje

Baadhi ya lugha zitasema, "Lazaro toka kaburini."

### Sanda

Hii ni, "nguo za kuzikia" Hii inaweza kutafsirika kama, "sanda" au, "vazi maalumu."


### Sababu ya muujiza huu

Hii ni, "kwasababu Mungu alishafanya muujiza huu wa kushangaza" au, "kwasababu Yesu tayari alishamfufua Lazaro."

### translationWords

- Lazaro
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Kuamini, kuamini katika
- muujiza, ajabu, ishara

## 37:11



Lakini viongozi wa dini ya kiyahudi waliona wivu, ndipo wakakusanyika pamoja kupanga watakavyoweza kumuua Yesu na Lazaro.

### Wivu

Huo ni "wivu wa Yesu wa nguvu na mashuhuri " au "wivu ambao wayahudi walikuwa wanauamini kwa Yesu."

### Kusanyika pamoja

Hiyo ni, "kutana pamoja" au, "unganisha pamoja." huu haukuwa mkutano wa kawaida, lakini ni mkutano maalumu kwa lengo la kupanga jinsi ya kumuua Yesu.


Simulizi ya Biblia kutoka: Yohana 11:1-46

### translationWords

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Lazaro

## 38. Yesu Anasalitiwa

38:01



Kila mwaka wayahudi walisherehekea sikukuu ya Pasaka. Hii ilikuwa sherehe ya kukumbuka jinsi Mungu alivyowatoa mababu zao toka utumwani Misri karne nyingi zilizopita. Yapata miaka mitatu baada ya Yesu kuanza kuhubiri na kufundisha hadharani, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa alitaka kusherehekea Pasaka huko Yerusalem pamoja nao, na kwamba angeuawa huko.


### Karne nyingi zilizopita

Hii ni, "mamia ya miaka iliyopita" au, "muda mrefu kabla."

### translationWords

- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Pasaka
- Mungu
- okoa, salama
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Misri, Mmisri
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuhubiri
- mfuasi
- Yerusalemu



**38:02**

Mmoja wa wanafunzi wa Yesu alitwa Yuda. Yuda alikuwa mtunza mfuko wa fedha wa mitume, lakini alikuwa mpenda fedha na mara nyingi aliiba fedha kutoka mfuko huo. Baada ya Yesu na wanafunzi wake kufika Yerusalemu, Yuda alikwenda kwa viongozi wa Kiyahudi na kumsaliti kwa kupewa fedha. Alijua kwamba viongozi wa Kiyahudi walikataa kwamba Yesu ni Masihi na walikuwa wanapanga kumuua.

**Mtunza mfuko wa fedha za mitume**

Hii ni, "wajibika kutunza fedha za mitume" au, "kuwajibika kusimamia mfuko ambao ulikuwa na fedha za mitume na matumizi yake."


**Alipenda fedha**

Hii ni, "alithamini sana fedha" au, alitaka pesa." Baadhi ya lugha zisingelitumia neno lililo sawa na linaloweza kutumika kwa "kupenda watu."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Yuda Iskariote
- Mtume, utume
- Yerusalemu
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- kusaliti
- Kristo, Masihi



**38:03**

Viongozi wa Wayahudi, wakiongozwa na Kuhani mkuu, wakamlipa Yuda vipande thelathini vya fedha ili amsaliti Yesu. Hii ilitokea kama manabii walivyotabiri. Yuda akakubali, akachukua fedha, na kuondoka. Akaanza kutafuta nafasi ya kuwasaidia kumkamata Yesu.

**Vipande thelathini vya fedha**

Kila kipande au sarafu ilikuwa na thamani ya posho ya siku nne.

**translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- kuhani mkuu
- Yuda Iskariote
- kusaliti
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

**38:04**

Huko Yerusalem, Yesu alisherehekea Pasaka pamoja na wanafunzi wake. Wakati wa chakula cha Pasaka, Yesu alichukua mkate na kuuvunja. Na kusema "Chukueni na kuleni. Huu ni mwili wangu, uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi." Kwa jinsi hii, Yesu alimaanisha kuwa mwili wake utatolewa sadaka kwa ajili yao.

**Alisherekea**

Hii ni, "alikuwa akisherehe"

**Alichukua mkate**

Hii ingelikuwa inatafsirika kama, "alichukua kipande cha mkate." au " akachukua mkate."

**Akauvunja**

Baadhi ya lugha zitasema, "akaugawanya vipande" au, "akaugawa nusu yake" au, "akaugawa sehemu yake"

**Umetolewa kwa ajili yenu**


Hii inaweza kutafsiriwa kwamba, "ambao umetolewa kwaajili yenu"

**Fanya hivyo kwa kunikumbuka mimi**

Hii ni, "Fanya hivi ikiwa ni njia ya kukukumbusha ambayo Mimi nafanya kwaajili yako." Yesu alikuwa anarejelea kuhusu kifo chake, ambacho kingelitokea karibuni.

## translationWords

- Yerusalemu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Pasaka
- mfuasi
- dhabihu, sadaka

**38:05**

Kisha Yesu akachukua **kikombe** na kusema, "Kunyweni. Hii ni damu ya Agano Jipya iliyotolewa kwa ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi kila mnapokunywa."

**kikombe**

Hiki ni, "kikombe cha mvinyo" au, "kikombe kilichojaa kinywaji kilichotengenezwa kwa mzabibu"

**Kunywa hiki**

Hii ni, "kunywa ambacho kimo katika kikombe hiki" au, "kunywa kutoka katika kikombe hiki." Kunywa katika kikombe chenye zabibu iliyokuwa imetengenezwa ikiwa na rangi nyekundu sana.

**Damu ya agano jipya**

Hii ingelitafsiriwa kama, "damu inayofanya agano liwezekane." au "damu ambayo ni msingi wa agano jipya."

**Imemwagwa**

Hii ingelitafsiriwa kama, "itatoka mwilini mwangu" au, "nitatokwa damu."

**Kwaajili ya msamaha wa dhambi**

Hii ni, "kusudi kwamba Mungu aweze kusamehe dhambi zote za watu kikamilifu."




## Nikumbuke

Hii ni, "sherehekea kwa ajili yangu" au, "niadhimisheni." Inaweza pia kutafsiriwa kama, "hasa inayolenga kwangu" au, "jikumbusheni kuhusu mimi."

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- damu
- Agano
- samehe, kusamehe
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi

**38:06**

Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Mmoja wenu atanisaliti." Wanafunzi walishituka, na wakauliza nani atafanya jambo kama hili. Yesu akasema, "Nitakayempa kipande cha mkate huu ndiye msaliti." Kisha akampa Yuda mkate.

**Kumpa kipande cha mkate**

Hii ni, "kukabidhi kipande cha mkate"

**Ni msaliti**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "atanisaliti" au, "yeye ndiye atakaye nisaliti."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- kusaliti
- Yuda Iskariote

## 38:07



Baada ya Yuda kupokea mkate, akaingiwa na Shetani. Yuda akaondoka na kwenda kuwasaidia viongozi wa Kiyahudi kumkamata Yesu. Wakati huo ilikuwa usiku.

### **Shetani alimwingia**


Hii ni, "shetani alimwingia" au, "akajawa na shetani."

### **Yuda aliondoka na akaenda**

Lugha nyingine inaweza kupendelea kusema, "Yuda alikiacha chakula na akaenda." au, "Yuda aliondoka ndani na akaenda nje."

### **translationWords**

- Yuda Iskariote
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi

**38:08**

Baada ya chakula, Yesu na wanafunzi wake wakaenda mlima wa Mizeituni. Yesu akasema, "Wote mtaniacha usiku huu. **Imeandikwa**, 'Nitamshambulia **mchungaji na kondoo wote watatawanyika.**'"

**Mlima wa Mizeituni**

Hili ni jina mlima uliofunikwa na miti ya mizeituni, nje tu ya jiji la Yerusalemu. Pia inaweza kutafsiriwa kama, "mlima wenye miti ya mizeituni."

**kuniacha**

Hii ni, "kunitenga mimi" au, "kuniacha."

**Imeandikwa**

Hiyo ni, "Imeandikwa kwenye neno la Mungu" au, "imeandikwa katika maandiko" au, "Mmoja wa manabii aliandika." Pia inawezekana kusema, kilichoandikwa kitatokea." au, "itatimia kama ilivyoandikwa." Unabii huu unarejelea kifo cha Yesu na wafuasi wake kukimbia.

**Nitampiga**

Hii ni, "Nitaua"

**mchungaji na kondoo wote**

Usitumie jina la Yesu katika nukuu hii kwa sababu nabii aliyeandika mwanzoni hangelijua jina la mchungaji. Pia usirejeele wanafunzi kuwa ni wanafunzi. Inafaa sana kutumia maneno yenye maana ya "mchungaji" na "kondoo" unapotafsiri.



## **watatawanyika**

Hii ni, "kwenda huko na huko kwa uelekeo tofauti"

## **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- mchungaji, kuchunga
- kondoo, kondoo dume, kondoo jike

**38:09**

Petro akajibu, "Hata kama wengine wote watakuacha, mimi sitakuacha!" Kisha Yesu akamwambia Petro, "Shetani anawataka ninyi nyote, lakini nimekuombea, Petro, ya kwamba imani yako haitaisha. Hata hivyo usiku huu kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu kana kwamba hukunijua."

**Sitakuacha**

.....

**Kuwa nanyi wote**

Hii ni, "kuwatawala kikamilifu" au, "anataka ninyi mtumike kwake kikamilifu." Neno wewe au "ninyi" ni wingi katika kauli hii. Maneno haya "wewe" na "yako" yanayofuata yako katika umoja.

**Imani yako haitashindwa**

Hii ni, "kwamba hutaacha kuniamini"

**Kabla jogoo hajawika**

Kwa kawaida jogoo huwika kabla ya kuanza siku mpya. Kama hiyo haijaleweka, itasaidia kusema, "kabla ya kuwika jogoo mapema kesho" au, "kabla hajawika jogoo kesho asubuhi."

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Kuomba, maombi

- [imani](#)

## 38:10



Kisha Petro akamwambia Yesu, "Hata kama itanilazimu kufa, sitakukana." Wanafunzi wengine nao wakasema vile vile.

### Kukukana

Hii ni, "nakujua lakini nakana" au, "mimi mwanafunzi wako halafu nakana" au "nakukataa"

### translationWords

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kifo, kufa, mfu
- mfuasi



**38:11**

Kisha Yesu akaenda na wanafunzi wake sehemu inayoitwa Gethsemane. Yesu aliwaambia wanafunzi wake ombeni ili msiingie majaribuni. Kisha Yesu akaenda kuomba peke yake.

**Sehemu inayoitwa Gethmane**

Hii ingeliweza kutafsiriwa, "eneo jirani lililoitwa Gethsemane" au, au "sehemu iliyoitwa Gethsemane chini ya Mlima wa Mizeituni."

**Kuingia majaribuni**

Hii ni, "wasingetenda dhambi walipojaribiwa" au, "Wasingeliingia kwenye majaribu yaliyokuwa yanaelekea kuwapata."

**Peke yake**

Hii ingetafsiriwa kama "yeye tu."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Kuomba, maombi
- kujaribu, jaribu

**38:12**

Yesu aliomba mara tatu, "Baba yangu, kama inawezekana, tafadhali nisinywe kikombe hiki cha mateso. Lakini kama hakuna njia nyingine ya kuwasamehe watu dhambi zao, basi mapenzi yako yatimizwe." Yesu alihuzunika na jasho lake likawa kama matone ya damu. Mungu akatuma malaika akamtia nguvu.

**Kunywea kikombe cha mateso**

Hii ni, "kupitia amateso haya" au, "kuteseka kwa kinachokaribia kutokea" au, "kuvumilia haya mateso."


**Mapenzi yako yafanyike**

maelezo haya yanamaanisha, "fanya ambacho umepanga" au, "fanya unachohitaji kufanya."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuomba, maombi
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- teseka, kuteseka
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- samehe, kusamehe
- damu
- Mungu
- Malaika, Malaika mkuu

### 38:13



Kila mara anapomaliza kuomba, Yesu aliwarudia wanafunzi wake, lakini walikuwa wamelala. alipowarudia mara ya tatu, Yesu akasema, "Amkeni! msaliti wangu amefika."


### Kila baada ya maombi

Hii ni, "Kila wakati Yesu aliomba maombi hayo." Hii inarejelea zile mara tatu aliomba kama ilivyotajwa

### translationWords

- Kuomba, maombi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- kusaliti



**38:14**

Yuda akaja pamoja na viongozi wa Kiyahudi, askari, na umati mkubwa. Wakiwa na mapanga na marungu. Yuda akamjia Yesu akamwambia, "**Salaam**, mwalimu," na kumbusu. Hii ilikuwa ishara kwa viongozi wa Kiyahudi ili wajue watakayemkamata. Kisha Yesu akasema, "Yuda, unanisaliti kwa kunibusu?"

**Akaja**

Lugha zingine zitapendelea kusema, "akaenda"

**Salaam**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "habari" au, "amani" au, "Habari za mchana."

**Ishara**

Hiki ni, "kiashiria."

**Unanisaliti mimi kwa busu**

Hii ni, "ni hakika unakwenda kunisaliti mimi kwa busu?" Yesu hatafuti jibu kwenye swali hili. Hivyo lugha zingine zingelitafsiri kama ifuatavyo: "unanisaliti kwa kunibusu!" au, "unafanya usaliti mbaya wa kunibusu kabisa."

**translationWords**

- Yuda Iskariote
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mwalimu, Mwalimu
- kusaliti



**38:15**

Wakati askari walipomkamata Yesu, Petro akatoa upanga wake na kumkata sikio mmoja wa watumishi wa kuhani mkuu. Yesu akasema, "Weka upanga mbali! Ninaweza kumwambia Mungu Baba alete jeshi la malaika kunitetea. Lakini lazima nimtii Baba yangu." Kisha Yesu akamponya mtu aliyekatwa sikio. Baada ya Yesu kukamatwa, wanafunzi wote wakakimbia.

**Ikawa askari walimkamata Yesu**

Hii ni, "wakati askari walikuwa wakimkamata Yesu."

**Aliuvuta upanga wake**

Hii ni, "kutoa upanga kutoka mahali alipokuwa ameuweka."

**Lazima nimtii Baba yangu**

Hii ni, "Sitafanya hivyo kwa sababu lazima nitii mapenzi ya Baba yangu, niko tayari kukamatwa."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 26:14-56; Marko 14:10-50; Luka 22:1-53; Yohana 12:6; 18:1-11

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Petro, Simoni Petro, Kefa
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- kuhani mkuu
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- Malaika, Malaika mkuu
- tii, mtiifu, utiifu
- Ponya, tibu

- [mfuasi](#)

## 39. Yesu Anashitakiwa.

### 39:01



Ilikuwa **usiku wa manane** wakati huo. Askari wakampeleka kwenye nyumba ya kuhani mkuu ili **kumhoji**. Petro akawafuata kwa mbali nyuma yao. Wakati Yesu anachukuliwa kwenye nyumba, Petro alikuwa nje peke yake akiota moto.

### **usiku wa manane**

Kauli hii inamaanisha, "usiku ukiwa katikati" au, "usiku ukiwa umeendelea sana"

### **kumhoji**

Hii ni, "kumuuliza Yesu maswali kujaribu kutafuta jambo ambalo wangemtuhumu Yesu kuwa ni mkosaji "

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kuhani mkuu
- Petro, Simoni Petro, Kefa

**39:02**

Ndani ya Nyumba viongozi wa kiyahudi wakamshitaki Yesu. Wakaleta mashahidi wengi wa uongo walioshuhudia uongo dhidi ya Yake. vile vile hata maelezo yao yalitofautiana kila mmoja alisema tofauti. kwa hiyo viongozi wa kiyahudi hawakukubaliana kama alikuwa na hatia yeyote. Yesu hakusema chochote.

**Walimshitaki Yesu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "walishandaa kikao kumtuhumu Yesu kuwa anakosa." kwa kawaida mashitaka yanafanyika ili kubaini kama mtu anahatia au kosa kwenye uhalifu uliotokea. Katika hili viongozi walidhamiria kufanya Yesu aonekane anahatia.

**Walisema uongo juu ya mtu**

Hii ni, "shuhudia uongo dhidi yake" au, "kulazimisha mashitaka kwamba huyu anamakosa"

**Kauli zao hazikuoana**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "walisema mambo juu ya Yesu ambayo yalikuwa yanatofautiana" au "hoja za mashahidi walizosema juu ya Yesu zilipingana."

**Kuwa na hatia kwa kitu chochote**

Hii ni, "kwamba yeye alikuwa nakosa lolote."

**translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ushuhuda, shuhudia



- [hatia, mwenye hatia](#)

### 39:03




**Hatimaye** kuhani mkuu akamwalia Yesu na kusema "Tuambie wewe ni Masihi mwana wa Mungu aliye hai?"

### **Hatimaye**

Hii ni, "Baada ya kukosa uthibitisho wowote dhidi yake" au, "Baada ya kushindwa kuthibitisha kwamba alikuwa na hatia."

### **translationWords**

- kuhani mkuu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kristo, Masihi
- Mwana wa Mungu, Mwana

**39:04**

Yesu akamjibu, "**Mimi ndiye**, utaniona nimekaa na Mungu na pia nikishuka kutoka mbinguni" Kuhani mkuu akararua mavazi yake kwa hasira na akasema kwa sauti kuu kwa viongozi wa kidini wengine "Hatuhitaji mashahidi zaidi ya hawa! Mmesikia toka kwake mwenyewe, akisema yeye ni mwana wa Mungu. **Hukumu yenu ni ipi?**"

**Mimi ndiye**

Hii ni, "Mimi ndiye kama ulivyosema" au, "Mimi ndiye masihi na Mwana wa Mungu." "Mimi ndiye " pia ni jina la Mungu. Kwa kurahisisha, "Mimi ndiye" Pia Yesu alikuwa anasema kwamba yeye ni Mungu. Kama inawezekana tafsiri ili kwamba watu waone ulinganifu kati jibu la Yesu na jina la Mungu.

**Keti pamoja na Mungu**

Hii ingelitafsiriwa kama, "kutawala pamoja na Mungu." Kwa sababu Mungu ni mtawala wa vyote, Watu wanamzungumzia kama ameketi kwenye kiti cha enzi mbinguni. Kwa kusema hivyo atakuwa alikuwa pamoja na Mungu, Yesu alikiri kwamba alikuwa na mamlaka ya kutawala pamoja na Baba.

**Kaketi pamoja na Mungu na akishuka kutoka mbinguni**

Hii inatafsiriwa kama, "kaka karibu na Mungu halafu akishuka kutoka mbinguni"

**Alichana mavazi yake kwa hasira**

Wayahudi wangelichana nguo kuonesha huzuni au hasira. Ikiwa kuchana nguo inamaanisha kitu kingine kwenye lugha yako, unaweza kuweka sentensi mbadala kama vile, "alikuwa na hasira sana."

## Hukumu yenu ni ipi?

Hii ni, "Uamzi wenu ni upi?" au, "Tuambie umeamuaaje: Anahatia au kosa?" Kuhani mkuu alitaka viongozi wa dini wamhukumu Yesu kwa kukiri kuwa sawa na Mungu.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- mbingu, anga, mbinguni
- kuhani mkuu
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- ushuhuda, shuhudia
- Mwana wa Mungu, Mwana
- hukumu



## 39:05



Viongozi wa kiyahudi wote wakamjibu kuhani mkuu kuwa "Anastahili kufa" baadaye wakamfunika macho Yesu, wakamtemea mate, wakampiga, na kumdhihaki.

### **Walimfunika machon Yesu**

Hii ni, "Walimfunika macho Yesu ili kwamba asiweze kuona"

### **walimtemea mate**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kumtusi kwa kumtemea mate" au "Kumtemea mate kwa kusema alikwa hanafaida." Hii ilikuwa njia yakuonesha kumdharau mtu.

### **translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- kuhani mkuu
- kifo, kufa, mfu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- dhihaki

**39:06**

Na Petro alikuwa inje ya nyumba akisubiri. Mtumishi mmoja msichana akamwona na akamwambia "Na wewe pia ulikuwa na Yesu!" Petro akakana. baadaye binti mwingine akasema kitu hicho. Na petro akakataa tena. hatimaye watu wakasema "Tunajua wewe ulikuwa pamoja naye maana ninyi nyote ni wenyeji wa Galilaya.

**Alikana**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "alisema kwamba si kweli" au, "alisema kwamba hakuwa pamoja na Yesu" au, alisema, Hapana. "Hiyo siyo kweli"

**Petro akakana tena**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Petro alikana kumjua Yesu mara ya pili" au, "Petro akasema kwa mara nyingine hakuwa pamoja na Yesu"

**Mnatokea Galilaya**

Hii hii inaweza kutafsiriwa kama, "ni Wagalilaya." Watu wangelisema kutokana na Yesu na Petro walivyowaambia kwamba walitokea mkoa wa Galilaya.

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Galilaya, Mgalilaya

**39:07**

tena Petro akaapa, akisema, "Mungu wangu na anilaani kama mimi namjua mtu huyu!" Mara ghafla Jogoo akawika na Yesu akageuka kumwangukia Petro.

**Kaapa**

Hii ni, "kasema kwa msisitizo" au, "kasema kwa kukazia sana."

**Mungu anilaani kama namjua mtu huyu**

Hii ni laana inayoonesha kwamba, "Mungu alete au asababisha madhara kama unachosema ni kweli" au "Mungu anilaani kama ninawadanganya!" kwa namna hiyo Petro alikuwa anakazia alikuwa hamjui Yesu. Pia alikuwa anarejelea kwa Yesu kama, "mtu huyu" ili ieleweke kama hamjui.

**Akawika jogoo**

"Kuwika" ni sauti anayoitoa jogoo

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Mungu
- Laana, kulaaniwa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



**39:08**

Petro akaondoka na akilia kwa huzuni kubwa. Wakati huo huo, Yuda, mwenye kumsaliti Yesu, akaona kwamba viongozi wa kiyahudi wamemweka Yesu hatiani. Yuda akapatwa na huzuni kubwa sana na akaondoka mahali pale akaenda kujiua mwenyewe.

**Alilia kwa uchungu**

Hii ni, "kulia, kwa hisia kali sana" au, "kulia, kwa hisia na majuto"

**Msaliti**

Hii ni, "ambaye alimkana Yesu" au, "ambaye aliwasaidia viongozi wamkamate Yesu"


**Alimhukumu Yesu kufa**

Hii ni, "alisema kwamba Yesu alikuwa na hatia ni lazima afe"

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yuda Iskariote
- kusaliti
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



**39:09**

Asubuhi na mapema, viongozi wa kiyahudi wakamleta Yesu kwa Pilato liwali wa Kirumi. wakitumaini kuwa Pilato atamhukumu Yesu kama mtu mwenye hatia na wakamwambia auawe. Pilato akamuuliza Yesu "Wewe ni mfalme wa wayahudi?"

**Utawala wa Kirumi**


Hii ni, "afisa wa utawala wa Kirumi." Utawala wa Kirumi ulimteua Pilato kutawala mkoa wa uyahudi katika Israeli.

**Ahukumiwe kuuawa**

Kama mtawala, Pilato alikuwa na mamlaka kumhukumu Yesu kifo na kuidhinisha auawe msalabani, au kumwacha huru. Viongozi wa kidini wa Kiyahudi hawakuwa na mamlaka kuruhusu mtu afe.

**translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Pilato
- Rumi
- Mfalme wa Wayahudi

**39:10**

Yesu akamjibu "Wewe ndiye umesema hivyo, lakini ufalme wangu si ufalme wa dunia hii, kama ingekuwa hivyo watumishi wangu wangepigana kwa ajili yangu. Nimekuja ulimwenuni ili kuusema ukweli kuhusu Mungu. na kila mmoja anayependa huu ukweli hunisikiliza. Pilato akasema "**Ukweli ni nini?**"

**Umesema hivyo**

Hii ni, "Umesema sahihi kabisa" au, kweli umepatia

**Ufalme wangu siyo ufalme wa kidunia**

Hii ni, "Ufalme wangu siyo kama falme za kidunia.

**Watumishi wangu wangepigana kwaajili yangu**

Hii ni, "wanafunzi wangu wangepigana kunilinda" ili kwamba niimarisha ufalme wangu.

**Hunisikiliza**


Hii ingetafsiriwa kama, "husikia mafundisho yangu na hunitii." Siyo tu kusikiliza maneno ya Yesu lakini pia kufanya kile anachosema.

**Ukweli ni nini?**

Hii ni, "Inawezekana yeyote kujua ukweli ni nini?"

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- ufalme
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- kweli, ukweli, kuwa kweli
- Mungu
- upendo
- Pilato

**39:11**

Baada ya kuongea na Yesu Pilato alitoka nje katika umati wa Watu na kusema "Nimeona hakuna hatia juu ya mtu huyu" lakini viongozi wa kiyahudi na makutano wote wakapiga kelele "Msulubishe" pilato akajibu "**Hana hatia**" lakini waliendelea kupiga kelele tena kwa nguvu. na Pilato akasema kwa mara ya tatu "Hana hatia yeyote"

**Sioni hatia kwa mtu huyu**

Hii ni, "sijapata hatia kwa mtu huyu" au, "Nimefanya uchunguzi kwa mtu huyu na sioni kama kosa alilofanya."


**Hana hatia**

Hii ni, "Hajatenda kosa lolote!?"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Pilato
- hatia, mwenye hatia
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Sulubisha



**39:12**

Pilato akaogopa kwamba makutano wataanza kuleta **Ghasia**, kwa hiyo aliwaruhusu askari wake kumsulubisha Yesu. Askari wa Kirumi wakampiga Yesu huku wakimpa vazi la kifalme na kofia iliyotengenezwa na miiba wakamvika. pia wakamdhihaki kwa kusema "Mtazame mfalme wa wayahudi"

**Ghasia**

Hii ni, "wakafanya fujo wakiwa na hasira."

**Aliwakubalia**

Pilato hakutaka kumuua Yesu kwa sababu aliamini kwamba Yesu hakuwa na hatia. Lakini alilazimishwa kuwaambia askari kumsulubisha Yesu kwa sababu ya kuhofia makutano. Kama inawezekana, tafsiri kauli hii kwa namna ambayo itaonesha wasiwasi wake.

**Vazi la kifalme**

Hii ni, "vazi linalofanana na vazi la mfalme." Vazi hili lilikuwa na rangi ya kung'aa, hivyo lilionekana ni sawa na lile alilovaa mfalme.

**Taji lililotengenezwa kwa miiba**

Hii inamaana kwamba walifunga matawi kwa duara ionekane kama taji. Taji ni mapambo ambayo mfalme huvaa kichwani kuonesha mamlaka. Lakini taji walilomvisha Yesu lilichoma, likiwa na miiba mikali.

**Tazama**

Hii ni, "Tazama" au "Hapa ni"

## Mfalme wa Wayahudi

Kwa kuwa askari walimdhiki Yesu, hii inaweza kutafsiriwa kama, "anayeitwa Mfalme wa Wayahudi"

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 26:57 - 27:26; Marko14:53-15:15; Luka 22:54-23:23; Yohana 18:12-19:16

### translationWords

- Pilato
- Sulubisha
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Rumi
- dhihaki
- Mfalme wa Wayahudi

## 40. Yesu Anasulubiwa

40:01



Baada ya askari kumdhihaki Yesu, **walimpeleka** kumsulibisha. walimlazimisha aubebe msalaba ambao ungetumika kumuua.

### walimpeleka

Hii ni, " walimlazimisha kwenda naye." Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "walimchukua."

### Kumsulibisha

Hii ni, "Kumuua juu ya msalaba."

### translationWords

- dhihaki
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Sulubisha
- Msalaba

**40:02**

Askari walimpeleka Yesu eneo liitwalo "fuvu la kichwa" wakaipigilia miguu na mikono yake msalabani. Lakini Yesu akasema, "Baba wasamehe, kwa sababu hawajui wanalotenda." Pilato akaagiza waandike kwamba, "Mfalme wa Wayahudi" ikiwa ni ishara; na waweke msalabani, juu ya kichwa cha Yesu.

**Fuvu**

Mlima uliokaribu na Yerusalemambao una mawe meupe juu yaliyo mithili ya sehemu ya juu ya fuvu.

**Wasamehe, kwa sababu hawajui watendalo**

Hii ni, "Hawajui maana ya jambo ambalo wanalifanya, kwa hiyo tafadhali wasamehe." Maaskari walidhani kuwa Yesu alikuwa mharifu aliyestahili kufa. Hawakuelewa kuwa alikuwa mwana wa Mungu.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Msalaba
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- samehe, kusamehe
- Pilato
- Mfalme wa Wayahudi



**40:03**

Askari walipigia kura mavazi yake. Na kitendo hiki kinatimiza unabii usemao kwamba, " wakagawana nguo zangu na kucheza kamali."

**Wlipigia kura mavazi ya Yesu**


Hii inamaana, "walifanya mchezo wa bahati ya kushinda nafasi ya kuchukua mavazi ya Yesu." Hatujui jinsi gani walifanya haya, lakini katika baadhi ya tamaduni indeweza kutafsiriwa kama, "kutupa mawe kwenye ardhi kwa ajili ya kujishindia mavazi ya Yesu" au, "Kuchagua vijiti ili kuamua nani angeweza kushinda kuchukua mavazi ya Yesu."

**Walitimiliza unabii amabao ulisema**

Hii ni, "Walifanya kile ambacho maandiko yalitabiri muda mrefu uliopita kuhusu jambo ambalo lingetokea kwa Masihi." au, "Walifanya jambo ambalo nabii aliandika muda mrefu uliopita."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- timiza
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

**40:04**

Yesu alisulibiwa katikati ya wanyang'anyi wawili; mmojawapo alimdhiki Yesu, lakini mwingine alisema, "Humwogopi Mungu!? Sisi tunahatia, lakini huyu hana hatia" Ndipo yeye akamwambia Yesu "**Tafadhali unikumbuke** katika ufalme wako" Yesu akamjibu, leo, utakuwa nami **Paradiso.**"

**Wanyang'anyi wawili**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "majambazi wawili" hawa ni watu ambao ni wahalifu ambao walitumia nguvu kuiba vitu.

**Je huna hofu ya Mungu?**

Mwizi hategemei jibu la swali hili, ni njia ambayo baadhi ya lugha hutumia kuweka sentensi yenye mkazo. kama lugha yako haitumii maswali kama ilivyo hapa, hivyo tafsiri jambo hili kama, "Lazima uwe na hofu ya Mungu!"

**Sisi tunahatia lakini mtu huyu hana hatia**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "wewe na mimi tumefanya mambo maovu na tunastahili kufa, lakini mtu huyu, Yesu, hajafanya kitu chochote kibaya na hastahili kufa," "sisi" neno hili linajumuisha wezi, lakini halijumuishi Yesu.

**Mtu huyu**

Sentesi hii inamaanisha Yesu.

**Tafadhali unikumbuke**

Hii inamaanisha, "Tafadhali nipokee" au, Tafadhali nikaribishe" au, "niruhusu niwe pamoja na wewe." "Kumbuka" mahali hapa halimaanishi kukumbuka jambo baada ya kulisahau. Tafsiri jambo hili katika njia ambayo itawasilisha ombi la kumsihi mtu.

## **Katika ufalme wako**

Hii ni, Wakati utakapo simamisha ufalme wako" au, "wakati unatawala kama mfalme."

## **Paradiso**

Hili ni jina lingine la "Mbinguni"

## **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Sulubisha
- dhihaki
- Mungu
- hatia, mwenye hatia
- sio na hatia
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni

## 40:05



Viongozi wa wayahudi na baadhi ya wengine katika umati walimdhihaki Yesu. Wakisema, "kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka msalabani, jikoe mwenyewe, ndipo tutakuamini."

## Tutakuamini

Hii ni, "Tutakuamini" au, "Tutaamini kuwa wewe ni Masihi."

## translationWords

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- dhihaki
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Msalaba
- okoa, salama
- Kuamini, kuamini katika



**40:06**



Ndipo katika eneo hilo kukawa giza nene, ingawa ilikuwa mchana. Mchana huo kukawa giza kwa saa tatu.

**40:07**

Yesu akalia, "Baba imekwisha naweka mikononi mwako roho yangu." Ndipo akainama akajitoa mwenyewe roho yake. Alipokufa lilitokea tetemeko la ardhi na pazia la hekaluni lililowatenga watu na Mungu lilipasuka vipande viwili, tokea juu hadi chini.

**Imekwisha**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "imekwisha" au, imemalizika" au, "Nimeimaliza" au, "nimemaliza kazi." Hii inamaana kazi ya Yesu ya wokovu ilikuwa imemalizika.

**Mikonono mwako**

Hii inamaana, "chini ya uangalizi wako"

**Akainamisha kichwa**

Hii inamaana aliinama kichwa chake."

**Akaitoa roho yake**

Hii ni, " aliitoa roho yake kwa Mungu" au, "aliikabidhi roho yake kwa Mungu na akafa."

**Pazia kubwa**

Hii ilikuwa nguo ya kitambaa kubwa, imara imening'inizwa hekaluni. Ilikuwa kama ukuta uliotenganisha chumba kimoja na kingine. Inaweza pia kutafsiriwa kama, pazia nene" au, "nguo ya kitambaa iliyo ning'inizwa" au, " chandarua , ngao."

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- roho, kiroho
- kifo, kufa, mfu
- Mungu
- hekalu

**40:08**

Kifo chake Yesu kinafungua njia ili watu waje kwa Mungu. Askari aliyemlinda Yesu alipoona mambo haya yote yanatokea alisema, "Hakika mtu huyu hakuwa na hatia, alikuwa Mwana wa Mungu."

**Kupitia kifo chake**

Hii ni, "Kwa njia ya kifo chake" au, "kwa kufa kwake."

**Alifungua njia**

Hii ni, " alifanya iwezekane."

**Kuja kwa Mungu**

Hii ni, " kuja karibu na Mungu" au, " nenda karibu na Mungu" au, "karibia Mungu" au, "kumjua Mungu ki- binafsi." Kuchanika kwa pazia kulionesha kwamba kizuizi kati ya Mungu na watu kimeondolewa.

**translationWords**

- kifo, kufa, mfu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- sio na hatia
- Mwana wa Mungu, Mwana



**40:09**

Na ndipo **Yusufu** na Nikodemo viongozi wa Wayahudi walioamini Yesu kuwa ni Masihi wakuomba mwili wa Yesu na kuufunga kwenye sanda na kupeleka kwenye kaburi lililochongwa tayari mwambani na wakasogeza jiwe kubwa kulifunga kaburi.

**Yusufu**

Huyu hakuwa ni mume wa Mariam. Alikuwa ni mtu mwingine aliye itwa Yusufu.

**Alimuomba Pilato auchukuwe mwili wa Yesu**

Hii ni kwamba, "alimuomba Pilato awaruhusu kuuchukua mwili wa Yesu kutoka msalabani."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 27:27-61; Marko 15:16-47; Luka 23:26-56; Yohana 19: 17-42

**translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kristo, Masihi
- Pilato
- kaburi

## 41. Mungu Anamfufua Yesu kutoka katika Wafu

41:01



Baada ya askari kuwa wamemsulubisha Yesu, viongozi wa Kiyahudi wasioamini walimwambia Pilato, "**Yule Muongo, Yesu, alisema** angefufuka baada ya siku tatu. Mtu mmoja lazima alilinde kaburi ili kujihakikishia kwamba wanafunzi wake hawatauiba mwili wake na kusema **amefufuka kutoka katika wafu.**"

### viongozi wa Kiyahudi wasioamini

Hawa ni, "viongozi wa kiyahudi ambao hawakuamini."

### Yule Muongo, Yesu, alisema

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "huyo mwanaume Yesu , alidanganya na kusema," walikataa kuamini kwamba Yesu aliwaambia ukweli kuhusu yeye kuwa mwana wa Mungu.

### amefufuka kutoka katika wafu

Hii ni kwamba, " amerudi tena kuwa hai au kuishi, au, "amekuwa mzima tena."

### translationWords

- Sulubisha
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Pilato
- inua, inuka
- kifo, kufa, mfu

- kaburi
- mfuasi

**41:02**

Pilato alisema, "Chukueni baadhi ya askari na muhakikishe kaburi limelindwa ipasavyo." Hivyo **wakaweka** muhuri kwenye jiwe katika mlango wa kuingilia kaburini na kuweka maaskari ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote ambaye angeuiba mwili.

**wakaweka**

Hii ni kwamba, "viongozi wa dini na maaskari walimweka."

**Muhuri kwenye jiwe**

Waliweka kitu laini kama udongo mfinyanzi au nta kati ya jiwe na kaburi na wakalitia alama kwa kutumia muhuri maalumu. Kama mtu angelitoea jiwe, kile kitu laini kingelikatika na kuonesha kuwa mtu ameingia kaburini. Jambo hili pia linaweza kutafsiriwa pia kama, "alama katika jiwe kuzuia watu wasiliamishe."

**translationWords**

- Pilato
- kaburi



**41:03**

Siku iliyofuata baada ya Yesu kuzikwa ilikuwa ni Sabato, na wayahudi hawakuruhusiwa kwenda kaburini siku hiyo. Hivyo asubuhi na mapema baada ya Sabato, wanawake wengi walijiandaa kwenda kwenye kaburi la Yesu kuupaka mwili wa Yesu **marashi ya maziko**.

**Wayahudi hawakuruhusiwa**


Sheria za siku ya sabato hazikuruhusu myahudi kutembea umbali mrefu au kufanya aina nyingine ya kazi.

**marashi ya maziko.**

Hii inamaanisha vile viungo vyenye harufu nzuri , marashi ambavyo viliwekwa kwenye maiti ya mtu kuzuia harufu mbaya. Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "viungo vyenye marashi" au, "mafuta yenye manukato" au, "mimea yenye manukato, au harufu nzuri."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Sabato
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- kaburi

**41:04**

Ghafla, kulikuwa na **tetemeko kubwa**. Malaika **ambaye mng'ao wake ulikuwa kama mng'ao wa mwanga wa radi** alitokea kutoka mbinguni. Aliliviringisha mbali lile jiwe lilokuwa limeufunika mlango wa kaburi na kulikalia. Askari waliokuwa wanalilinda kaburi waliogopa sana na kuanguka chini na kuwa kama watu waliokufa.

**tetemeko kubwa**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "tetemeko lenye nguvu" au, "mtikisiko wa nguvu wa ardhi." Lugha zingine zingependelea kutumia neno hili kama, "ardhi ilianza kutetemeka kwa nguvu."

**ambaye mng'ao wake ulikuwa kama mng'ao wa mwanga wa radi**

Hii ni kwamba, " ambaye mwonekano wake ulikuwa unang'aa kama radi."

**Walianguka chini na kuwa kama watu waliokufa.**

Hawakuwa wamekufa, lakini hawakuweza kutembea, kama vile watu waliokufa wasivyoweza kutembea. Ili kufanya jambo hili lieleweke zaidi, ni kwamba jambo hili inaweza kutafsiriwa kama, " walianguka chini kwa ghafla na hawakuweza kutembea."

**translationWords**

- Malaika, Malaika mkuu
- mbingu, anga, mbinguni
- kaburi
- kifo, kufa, mfu

## 41:05



Wale wanawake walipofika kaburini, malaika aliwaambia. "**Msiogope**. Yesu hayupo hapa. **Amefufuka kutoka katika wafu**, kama alivyosema kwamba atafufuka! Angalieni kaburini na muone." Wale wanawake wakaangalia mle kaburini na kupaona mahali mwili wa Yesu ulipokuwa umelazwa. Mwili wake haukuwepo pale!

### Msiogope

Hii ni kwamba, "acheni kuogopa" malaika aliyeng'aa kama radi alikuwa na mwonekano wa kuogopesha!

### Amefufuka kutoka katika wafu

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "amerudi tena kuwa hai."

### translationWords

- Malaika, Malaika mkuu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- inua, inuka
- kifo, kufa, mfu
- kaburi



**41:06**



Malaika akawaambia wale wanawake, "Nendeni na mkawaambie wanafunzi, 'Kwamba Yesu amefufuka kutoka katika wafu na atawatangulia kwenda Galilaya."



## 41:07



Wanawake walijawa na hofu na furaha kuu. Wakakimbia kwenda kuwaambia wanafunzi **habari njema**.

### **Walijawa na hofu na furaha kuu**

Hii ni, kupata hisia za hofu pamoja na furaha kuu."

### **habari njema.**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, " Habari njema kuwa sasa Yesu yuko hai tena." Hii habari njema inamaanisha ukweli kwamba Yesu amefufuka katika wafu.

### **translationWords**

- furaha, mwenye furaha
- mfuasi

## 41:08



Wale wanawake walipokuwa wanaenda kuwaambia wanafunzi wake habari njema, Yesu aliwatokea wale wanawake, nao wakamuabudu. Yesu akasema, "Msiogope. Nendeni mkawaambie wanafunzi wangu waende Galilaya. Wataniona huko."

### Mtaniona

Hii ni kwamba, "mtaniona" au, "mtakutana na mimi."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mathayo 27:62-28:15; Marko 16:1-11; Luka 24:1-12; Yohana 20:1-18

### translationWords

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Abudu
- Galilaya, Mgalilaya

## 42. Yesu Anarudi Mbinguni

42:01



Siku ile Yesu alipofufuka, wanafunzi wake wawili walikuwa wanaenda mji jirani. Wakiendelea kutembea, walizungumza habari zilizotokea kumuhusu Yesu. Walitumaini kuwa alikuwa Masihi, lakini aliuawa. Wanawake waliwaambia yu hai anaishi tena. Nao hawakujua cha kuamini.

## 42:02



Yesu aliwakaribia na akaanza kutembea nao, lakini hawakumtambua. Aliwauliza juu ya mazungumzo yao, nao wakamueleza maajabu yote yaliyo tokea kumuhusu Yesu kwa siku chache zilizopita. Kwani walidhani wanaongea na mgeni asiyejua habari zilizotokea katika Yerusalemu.

### Hawakumtambua

Hii ni, " hawakujua kuwa alikuwa ndiye Yesu."

### Mambo ambayo yalikuwa yametokea

Hii inamaanisha mafundisho na miujiza ya Yesu, kifo chake, na taarifa za kufufuka kwake.

### translationWords

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)
- [Yerusalemu](#)



**42:03**

Ndipo Yesu akawaelezea jinsi neno la Mungu linavyo sema kumuhusu Masihi. Aliwakumbusha manabii walivyosema, kwamba Masihi atateswa na kuuawa, na atafufuka tena siku ya tatu. Nao walipofika katika mji waliokuwa wamepanga kufikia hawa wanaume wawili, ilikuwa imekaribia jioni.

**Siku ya Tatu**

Baadhi ya lugha zingeweza kusema, " siku ya tatu baada ya kifo chake."

**Ilikuwa imekaribia jioni**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "siku ilikuwa inaishiria" au, jua lilikuwa linazama" au, "ilikuwa inaanza kuwa usiku."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Kristo, Masihi
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- teseka, kuteseka
- inua, inuka

## 42:04




Hawa wanaume wawili walimkaribisha Yesu akae nao, naye akafanya hivyo. Walipokuwa tayari kula chakula cha jioni, Yesu alichukua kipande cha mkate, alimshukuru Mungu kwa mkate huo, akaumega. Ghafila, wakamtambua kuwa ni Yesu. Lakini wakati huo huo, Yesu akatoweka eneo hilo.

### Alitoweka mbele ya macho yao

Hii inawza kutafsiriwa pia kama, "alikuwa ameondoka" au, "alikuwa hayupo hapo."

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu

**42:05**

Hawa wanaume wawili waka ambiana, "Yule alikuwa ni Yesu! Ndiyo maana mioyo yetu ilikuwa inaungua wakati akielezea neno la Mungu kwetu." Punde, walirudi Yerusalemu. Nao walipofika, waliwaambia wanafunzi, "Yesu yu hai! tumemuona."

**Mioyo yetu ilikuwa inaungua**

Hii maana yake ni kwamba, "tulikuwa na shauku na shangwe ndani ya mioyo yetu" au, "tulikuwa tunaanza kupata tumaini" au, "tuliona furaha." Lugha zingine zina njia tofauti ya kueleza hali hii kama vile, "Mioyo yetu ilichochea" au, "mioyo yetu ilipashwa moto." Kama utatumia maneno yanayo eleza hali ya moyo kuungua, hakikisha isije ikamaanisha kuwa walikuwa wamekasirika.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Yerusalemu
- mfuasi
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai



**42:06**

Wakati wanafunzi wanaendelea kuongea, Yesu alijitokeza katikati yao kwenye kile chumba na kusema, "**Amani iwe kwenu!**" Wanafunzi walidhani kuwa ni mzimu, lakini Yesu akawaambia, "Mbona mnaogopa na kuwa na mashaka? Angalieni mikono yangu na miguu. Mizimu haina mwili kama mimi." Kuwahakikishia kuwa Yeye si mzimu, aliwaomba chakula. Walimpa kipande cha samaki kilichopikwa, naye akala.

**Amani iwe kwenu**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, " na muwe na amani" au, " amani iwe nayi."

**Mzimu**

Hii inamaanisha roho ya mtu aliye kufa.

**Mashaka**

Hii ni kwamba, "mashaka ya kuwa niko hai na niko hapa nanyi."

**Kuhakikisha**

Hii inamaana, kuthibitisha."

**translationWords**

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Amani



**42:07**

Yesu alisema, "Niliwaambia kila kitu kilicho andikwa katika neno la Mungu kunihusu mimi ni lazima kitimie." Ndipo alipofungua akili zao ili waweze kulielewa neno la Mungu. Akasema, "Iliandikwa muda mrefu uliopita yakuwa Masihi atateswa, atakufa na kufufuka kwa wafu siku ya tatu."

**Lazima itimie**

Hii inawza kutafsiriwa kama, lazima itokee."

**Fungua akili zao ili kwamba waweze kuelewa.**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "kuwawezesha kuelewa" au, "kuwafanya waweze kuelewa."

**Siku ya tatu**

Hii ni kwamba, "baada ya siku tatu" au, siku tatu baadaye."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- timiza
- Kristo, Masihi
- tseseka, kuteseka
- kifo, kufa, mfu
- inua, inuka

**42:08**

"Iliandikwa pia katika maandiko kwamba wanafunzi, wangu watatangaza kwa kila mtu katika makundi, kwamba lazima watubu ili wapate msamaha wa dhambi zao. Nao watafanya hivyo kuanzia Yerusalem, nao wataenda kwa watu wote mahali pote. **Ninyi ni mashahidi wa mambo haya.**"

**Tangaza**

Hii maana yake ni kwamba, julisha" au, "hubiri."

**Watafanya hivi wakianzia Yerusalem**

Hii ni kwamba watafanya hivi wakianzia Yerusalem" au, wataanza kutangaza mambo haya katika Yerusalem."

**Ninyi ni mashahidi wa mambo haya**

Hii ni kwamba, mmeona mambo haya yakitokea" au, "mtawaeleza watu wengine mambo ambayo mmeyaona yakitokea."

**translationWords**

- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- mfuasi
- Kutubu, toba
- Kupokea
- samehe, kusamehe
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Yerusalemu
- Kundi la watu, watu
- ushuhuda, shuhudia

**42:09**



Ndani ya siku arobaini zilizofuata, Yesu aliwatokea wanafunzi wake mara kwa mara. Wakati mwingine aliwatokea watu zaidi ya 500 kwa wakati mmoja! aliwadhibitishia wanafunzi wake kwa njia nyingi kuwa Yeye yu hai, na aliwafundisha kuhusu ufalme wa Mungu.



**42:10**

Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa hiyo nendeni mkawafanye watu wote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kuyatii yote niliyowaamuru. Kumbukeni kuwa nitakuwa pamoja nanyi siku zote."

**Mamlaka yote ya mbinguni na duniani yamekabidhiwa kwangu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "Mungu amenipatia mamlaka yote ya mbinguni na duniani" au, "Mungu amenipatia mamlaka kamili juu ya kila mtu aliye mbinguni na duniani" au, "ninamamlaka yote mbinguni na duniani."

**Fanya watu kuwa wanafunzi katika makundi yote ya watu**

Hii ni, saidia watu kutoka kila kundi la watu wawe wanafunzi wangu."

**Katika jina la**

Sentensi hii inamaanisha mambo yote mawili, "kwa mamlaka ya" na , "chini ya mamlaka ya ." ikiwa kwa hali halisi ikieleweka kwa jinsi hii katika lugha yako. Hii sentensi inaweza kurudiwa kama, kwa jina la Baba, kwa jina la mwana, na kwa jina la Roho mtakatifu."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- mbingu, anga, mbinguni
- Kundi la watu, watu
- Batiza, ubatizo
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- Mwana wa Mungu, Mwana



- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- tii, mtiifu, utiifu

**42:11**

Siku arobaini baada ya Yesu kufufuka kwa wafu, aliwaambia wanafunzi wake, "Kaeni Yerusalemu mpaka hapo Baba yangu atakapo wapa nguvu, pale Roho Mtakatifu atakapowajilia ninyi. Kisha Yesu akaenda mbinguni, nayo mawingu yakamfunika akatoweka kwao. Yesu alikaa mkono wa kuume wa Mungu kutawala vitu vyote.

**atawajilieni**

Hii in, " atawashukia chini" au, "atakuja kwenu."

**Wingu lilimfunika wasimuone**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "alipotelea kwenye wingu."

**Mkono wa kuume wa Mungu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " upande wa kulia wa Mungu."

**Juu ya mambo yote**

Hii ni, "juu ya kila kitu."

Simulizi ya Biblia kutoka: Matayo 28:16-20; Marko 16:12-20; Luka 24:13-53; Yohana 20:19-23; Matendo ya Mitume 1:1-11

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- Yerusalemu

- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- Nguvu
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- mbingu, anga, mbinguni
- Mungu

## 43. Kanisa Linaanza

43:01



Baada ya Yesu kurudi mbinguni, wanafunzi wake walibaki Yerusalem kama alivyowaagiza kufanya. Waumini wake walikuwa na utaratibu wa kukusanyika na kuomba pamoja.

### Alirudi mbinguni

Hii ni, "alirudi mbinguni."


### Walibakia Yerusalem

Hii ni kwamba, " walisalia Yerusalem kwa muda." hawakukaa pale kabisa.

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mbingu, anga, mbinguni
- mfuasi
- Yerusalemu
- Kuamini, kuamini katika
- Kuomba, maombi



**43:02**

Kila mwaka baada ya siku 50 za Pasaka, Wayahudi walisherehekea siku muhimu ya Pentekosti. Pentekosti ni kipindi ambacho wayahudi walisherehekea mavuno ya ngano, Wayahudi walikwenda Yerusalemu wakitokea ulimwenguni kote kusherehekea kwa pamoja Pentekosti. **Mwaka huu** kipindi cha Pentekosti kilikuwa baada ya wiki moja Yesu aliporudi mbinguni.

**Pentekoste**

"Pentekoste" maana yake ni siku ya hamsini. " Unaweza kutumia neno "pentekoste " katika tafsiri yako na kuacha kifungu kieleze maana yake. au unaweza kutumia neno ambalo linamaanisha. "siku 50."

**Walisherehekea mavuno ya ngano**

Wayahudi walifikiri Mungu katika mavuno ya ngano kwa njia ya kuleta sadaka pamoja na kusherehekea kwa kula chakula maalumu. Ngano ni zao la nafaka; unaweza kutumia neno la jumla linalo maanisha nafaka. hii ilifanyika katika mwezi Mei; mazao mengine yalikuwa yamevunwa kwa kipindi kingine cha mwaka.

**Mwaka huu**

Hii ni mkwamba, katika mwaka ambao Yesu alikufa."

**translationWords**

- Pasaka
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Yerusalemu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mbingu, anga, mbinguni

**43:03**

Wakati waumini wakiwa pamoja, ghafla nyumba ilijawa na sauti kama upepo mkali. Kisha kitu kama mwali wa moto kikaonekana juu ya vichwa vya waumini wote. Wote walijazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena kwa lugha nyingine.

**Sauti kama ya upepo mkali**

Hii ni, "sauti ambayo upepo mkali unatengeneza" au, "sauti ambayo inatengenezwa na upepo wakati unapovuma kwa nguvu."

**Kujazwa na Roho Mtakatifu**


Hii ni, "hali ya kpewa nguvu na Roho Mtakatifu" au, nguvu itokayo kwa Roho Mtakatifu."

**Katika lugha zingine**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "katika lugha zingine zaidi ya ile ya kwao" au, "katika lugha ngeni" au, "waamini hawakujua lugha hizi hadi pale Roho Mtakatifu alipowapa uwezo wa kuziongea. Hakikisha kwamba neno lililo tumika kutafsiri "lugha" linamaanisha lugha ambazo watu wanazungumza na kuzielewa.

**translationWords**

- [Kuamini, kuamini katika](#)
- [Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.](#)

**43:04**

Watu wa Yerusalemu waliposikia kelele, kusanyiko la watu walikuja kushuhudia kilichotokea. Watu waliposikia waumini wakitangaza matendo ya ajabu ya kazi za Mungu, walishangaa sana kwa kuwa walisikia maneno hayo kwa lugha zao za asili.

**Umati**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kundi la watu au, "kundi kubwa la watu."

**Kazi za Mungu za kushangaza**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, " mambo ya ajabu ambayo Mungu amefanya."

**translationWords**

- [Yerusalemu](#)
- [Kuamini, kuamini katika](#)
- [Mungu](#)



**43:05**

Baadhi ya watu wakawashutumu wanafunzi kuwa wamelewa, lakini Petro akasimama akawaambia, nisikilizeni, hawa watu hawajalewa, bali unatimizwa unabii uliotolewa na **Yoeli** ambao Mungu alisema "Siku za mwisho nitamdhihirisha Roho"

**Waliwashutumu wanafunzi kuwa wamelewa**

Hii pia inaweza pia kutafsiriwa kama, " walisema kuwa wanafunzi walikuwa wamelewa."

**Yoeli**

Yoeli alikuwa nabii katika Israel ambaye aliishi miaka mamia kabla mambo haya hayajatokea.

**Sku za mwisho**

Hii inamaana , Siku za mwisho kabala ya mwisho wa dunia."

**Nitawamwagieni Roho wangu**

Hii inaweza kueleweka katika hali ya , " kutoa kwa ukarimu Roho wangu kwa watu"au, " kusababisha Roho wangu kuwajaza nguvu kwa ukamilifu watu."

**Roho wangu**

Hii ni, Roho Mtakatifu wangu."



## translationWords

- mfuasi
- Petro, Simoni Petro, Kefa
- timiza
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.

**43:06**

"Wanaume wa Israeli Yesu alikuwa mwanadamu alitenda miujiza na maajabu mengi kwa uwezo wa Mungu, nanyi mnajua na kuona lakini mlimsulubisha."

**Watu wa Israel**

Kwa lugha zingine ni vema kusema, Watu wa Israel" kwa kuwa ni wazi kuwa hiiinajumuisha wanaume na wanawake. hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "ndugu zangu waisrael" au, " ndugu zangu wayahudi" ili kuweka wazi kwamba Petro alikuwa pia myahudi na kwamba alikuwa miongoni mwa " watu wa Israel."

**Mlimsulubisha**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " mlisababisha asulibiwe" au, " kwa sababu yenu alisulibiwa." Kwa uhalisia, wayahudi hawa kumgongelea misumari Yesu pale msalabani. Ingawaje, viongozi wa wayahudi walisababisha ahukumiwe na watu wengi katika kusanyiko walipiga kelele asulibiwe.

**translationWords**

- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- muujiza, ajabu, ishara
- Nguvu
- Mungu
- Sulubisha

**43:07**

Ingawa Yesu alikufa, Mungu alimfufua kutoka kwa wafu na hii inatimiza unabii unaosema "Hutamwacha mtakatifu wako kuoza kaburini" Nasi tu mashahidi wa mambo hayo kuwa ukweli kwamba Mungu alimfufua Yesu.

**Hii inatimiliza unabii unaosema**

Njia nyingine ya kutafsiri hii inaweza kuwa, hii ilisababisha haya kutimilika kwa yale ambayo mmoja wa manabii alisema zamani za kale."

**Wewe hutamwacha mtakatifu wako**

"Wewe" na "wako" inamaanisha Mungu baba. ili kuweka wazi, hii inaweza kutafsiriwa kama, "wewe" Mungu hatakuacha." Lughu zingine zaweza kuwa na njia maalumu ya kueleza mtu, kama vile "wewe, Mungu"

**Kuoza kaburini**

Hii inamaanisha "kuoza ndani ya kaburi" hii dhihirisha ukweli kwamba Yesu hakubakia kaburini kwa muda mrefu na ni njia nyingine ya kusema kwamba hakubakia mfu, lakini alifufuka na kuwa hai tena.

**Alimfufua Yesu kuwa hai tena**


Hii ni kwamba, " alimfanya Yesu kuwa hai tena."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- inua, inuka
- kifo, kufa, mfu

- timiza
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- ushuhuda, shuhudia
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai



**43:08**

"Yesu anatumwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu baba, na Yesu amemtuma Roho Mtakatifu kama alivyoahidi kuwa angefanya. Roho Mtakatifu anasababisha mambo mnayoyaona na kuyasikia.

**Yesu sasa ametukuzwa**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "Yesu sasa ameinuliwa juu" au, " Yesu sasa amepandishwa juu" au, " Mungu amemtukuza Yesu."

**Mkono wa kuume/ mkono wa kulia wa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "nafasi ya muhimu sana" au, mali pa heshima ya juu baada ya."


**Sababisha**

Hii ni, " kuwezesha waamini kufanya" au, " kuwapatia watu hawa uwezo wa kufanya."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Ahadi

## 43:09



"Mlimsulubisha mtu huyu Yesu. Lakini mfahamu kwa uhakika Mungu amesababisha Yesukufanyika kuwa Bwana na Masihi."

### Lakini mfahamu kwa uhakika kwamba

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "lakini unaweza kujua kuwa ni kweli kwamba" au, "unaweza kuwa na uhakika kwamba."

### translationWords

- Sulubisha
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- bwana, mkuu
- Kristo, Masihi

## 43:10



Watu waliomsikiliza Petro walivutwa kwa undani na mafundisho aliyosema. Wakamwuliza Petro na wanafunzi. Je mnataka tufanye nini?

### Walivutiwa sana

Hii ni kwamba, "walihangaishwa" au, walijisikia huzuni wakati waliposikia." kuvutiwa ni kupata hisia kali.

### Ndugu/ kaka

Hii ilikuwa ni njia ya kawaida kwa myahudi kumwita myahudi mwenzake. Inaweza pia kutafsiriwa kama, "marafiki."

### translationWords

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- mfuasi

**43:11**

Petro akawajibu, "kila mtu anapaswa atubu na kubatizwa kwa Jina la **Yesu Kristo** na Mungu atawasamehe dhambi zenu. Kisha atawapa kipawa cha Roho Mtakatifu."

**Kwa jina la**

Sentensi hii inamaana mbili, " kwa mamlaka ya" na, " chini ya mamlaka ya" fikiri kutafsiri neno "jina" kwa uhalisia ikiwa itaeleweka kwa jinsi hii katika lugha yako.

**Kristo**

Hili ni jina ambalo maana yake ni "Masihi" inaweza kutafsiriwa kama, " mpakwa mafuta" au, "aliye teuliwa" badala ya kutoa maana, tafsiri zingine zinaweza kuchagua kuhifadhi neno "Kristo" na kuliandika kwa kutumia herufi ambazo zina sauti ya lugha yao.

**Yesu Kristo**


Kwa kuwa "Kristo" ni cheo mahali hapa, baadhi ya watafsiri wanaweza kuchagua kubadilisha mpangilio na kusema, " Kristo Yesu" na mipangilio yote miwili inatumika katika Biblia.

**translationWords**


- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Kutubu, toba
- Batiza, ubatizo
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- samehe, kusamehe
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.



**43:12**



Yapata Watu 3,000 wakaamini alichokisema Petro wakawa wanafunzi wa Yesu. Nao wakabatizwa wakawa washirika wa kanisa la Yerusalemu.

**43:13**

Wanafunzi waliendelea kusikiliza mafundisho ya mitume, walikaa pamoja na kula pamoja na kuomba pamoja. Walifurahi wakamsifu Mungu kwa pamoja na walishirikishana kila kitu walichokuwa nacho kwa pamoja. Kila mtu alikuwa na mtazamo mzuri juu yao. kila siku watu wengi waliendelea kuamini.

**Mtazamo mzuri juu yao**

Hii ni kwamba, " alikuwa na mtazamo chanya juu yao."

Simulizi ya Biblia Kutoka: Matendo ya Mitume 2

**translationWords**

- mfuasi
- Mtume, utume
- Kuomba, maombi
- Kusifu
- Mungu
- Kuamini, kuamini katika

## 44. Petro na Yohana Wamponya Ombaomba

### 44:01



**Siku moja**, Petro na Yohana walikuwa wakihudhuria Hekaluni. Na walipokaribia kwenye lango la hekalu, walimwona kiwete aliyeketi langoni na kuomba fedha.

### **Siku moja**

Hii sentensi inatoa utangulizi wa tukio amabalo limetokea wakati ulio pita, lakini halielezi muda maalumu. lugha nyingi zina usemi wa jinsi hii wakati wa kuanza kueleza simulizi ya kweli.

### **Mtu aliye kiwete**

Hii inaweza pia kutafasiriwa kama, " kilema." Hii inamaanisha mtu ambaye hawezi kutumia miguu yake kwa ukamilifu, na hawezi kusimama au kutembea.

### **translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yohana (mtume)
- hekalu
- kuomba



## 44:02



Petro akamtazama yule kiwete na kumwambia, "Sina fedha za kukupa. Japo nitakupa kile nilichonacho. Kwa jina la Yesu Kristo, simama na utembe!"

### **Katika jina la Yesu**

"Jina" hii inasimama badala ya mamlaka na nguvu za mtu. Kwa hiyo usemi huu unamaanisha, " Kwa mamlaka ya Yesu."

### **Simama**

Hii maana yake ni , "simama juu."

### **translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



## 44:03



Mara tu, Mungu akamponya yule kiwete akaamka na akaanza kutembea na kurukaruka hapa na pale na kumsifu Mungu. Watu wote waliokuwa kwenye ua wa Hekalu walishikwa na mshangao mkubwa.

### Ua wa hekalu

Ni makuhani pekeyao ndio ambao waliingia hekaluni, lakini wayahudi wa kawaida waliruhusiwa kuja katika eneo hili ambalo lilizunguka hekalu.


### translationWords

- Mungu
- Ponya, tibu
- Kusifu
- hekalu

**44:04**



Watu wengi wakakusanyika kwa haraka ili kumwona yule kiwete aliyeponywa. Petro akawaambia, "Kwa nini mnashangazwa na uponyaji ambao mtu huyu ameupata? Uponyaji huu haujafanyika kwa sababu ya wema na nguvu zetu. Bali ni kwa nguvu na imani itokayo kwa Yesu Kristo."

**44:05**

"Ninyi ndio mliomshawishi Mtawala kutoka Rumi kumuua Yesu. Mlimuua mwanzilishi wa uzima, lakini Mungu alimfufua katika wafu. Ingawa hamkujua kile mlichokuwa mkikifanya, Mungu alitumia matendo yenu maovu kwa kutimiza unabii wa kwamba Masihi atateswa na kufa. Kwa hiyo mnapaswa kutubuna kurudi kwa Mungu ili msamehewe dhambi zenu."

**Mwanzilishi wa uzima**

Hii ni kwamba, Yule aliye umbaa uzima" au, "yeye yule atupaye uzima" au, yeye ambaye anafanya watu waishi" hii inamaanisa Yesu.

**Matendo yako**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "mambo uliyofanya." Hii inamaanisha maswali yao juu ya Pilato kumuua Yesu.

**Mrudie Mungu**

Hii maana yake ni kwamba, "amua kumtii Mungu."

**Dhambi zako zitasafishwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Mungu ataosha dhambi zenu" au, Mungu ataondoa dhambi zenu ana kuwafanya muwe safi." hii inazungumzia Mungu kuwatakaswa watu katika roho zao kwa kuondoa dhambi zao kabisa. Hii haimaanishi tendo halisi la kuosha.

**translationWords**

- Rumi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- Mungu
- inua, inuka
- kifo, kufa, mfu
- timiza
- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi
- teseka, kuteseka
- Kutubu, toba
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi



## 44:06



Viongozi wengi wa Hekalu walisikitishwa sana na yale maneno ya Petro na Yohana. Kwa hiyo wakawakamata na kuwaweka gerezani. Pamoja na hayo, bado watu wengi walimwamini Yesu kwa ujumbe wa Petro, na idadi ya wanaume waliomwamini Yesu siku hiyo walikuwa 5,000.

### Ujumbe wa Petro

Hii ni, " ujumbe ambao Petro alikuwa amewahubiri."


### Idadi ya wanaume

Hii ilikuwa ni ongezeko la idadi ya wanawake na watoto ambao waliamini

### translationWords

- hekalu
- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yohana (mtume)
- Kuamini, kuamini katika

**44:07**



Siku iliyofuata, viongozi wa hekalu waliwaleta Petro na Yohana kwa kuhani mkuu na mbele ya viongozi wa kidini na kuwauliza, "Ni kwa nguzu gani mlimponya huyu kiwete?"

**44:08**

Petro akawajibu, " Mtu huyu asimamaye mbele yenu, aliponywa kwa nguzu za Yesu. Ambaye nyinyi mlimsulubisha, lakini Mungu alimfufua katika wafu. Hamkumkubali, ila hakuna njia jingine duniani inayoweza kuokoa isipokuwa kwa nguvu za Yesu Kristo!"

**Kuponywa**

Hii maana ya keni , " kuwa salama" au, "kuwa mwenye nguvu"

**Walimkataa**

Hii ni, " walikataa kumpokea" au, "walikataa kumwamini Yesu" au, walikataa kuamini kuwa Yesu ni mwokozi."

**Lakini hakuna njia nyingine ya kutuokoa isipokuwa kupitia uwezo wa Yesu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Lakini njia pekee ya kuokolewa ni kupitia uwezo wa Yesu Kristo" au, " lakini Yesu pekee anaweza kutuokoa, kwa uwezo wake."

**Kuokolewa**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kuokolewa kutoka dhambi zetu" au, "kwamba tunaweza kuokolewa kutoka katika dhambi zetu."

**translationWords**

- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Ponya, tibu
- Nguvu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

- Kristo, Masihi
- Sulubisha
- Mungu
- inua, inuka
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- okoa, salama



**44:09**

Wale viongozi wa dini walipowatazama na kuwasikiliza Petro na Yohana na ujasiri wa hotuba yao, na kuowaona kuwa walikuwa watu wa kawaida na wasio na elimu, walishitushwa. Walikumbuka kuwa walikuwa pamoja na Yesu Kristo. Baada ya kuwatisha waliwaruhusu waende zao.

**Walishangazwa**

Hii ni kwamba, "walistaajabu" au, walishangaa."

**Kawaida**

Hii ni ile "iliyozoeleka" ya hali ya chini." Petro na Yohana walikuwa wavuvi wa kawaida.

**Ambao hawakuwa na elimu**

Hii ni kwamba, "ambao hawakuwa na elimu ya darasani." hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "ambao hawajaenda kwenye shule ya dini."

**Kisha walikumbuka**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "lakini kisha walifikiri juu ya ukweli kwamba."

**Walikuwa pamoja na Yesu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "walitumia muda pamoja na Yesu" au, walikuwa wamefundishwa na Yesu."

## **Baada ya kutishwa**

Viongozi walisema wangemuadhibu Petro na Yohana kama wangeendelea kuwafundisha watu kuhusuYesu.

## **Waruhusu waende**

Hii ni kwamba, "waliwaruhusu waondoke."

Simulizi ya Biblia Kutoka: Matendo ya Mitume 3:1-4:22

## **translationWords**

- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- Petro, Simoni Petro, Kefa
- Yohana (mtume)
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

## 45. Stephano na Filipo

45:01



Mmoja wa viongozi wa **Kanisa la kwanza** aliyeitwa Stephano. **Alikuwa na tabia nzuri**, mwenye kujawa na Roho Mtakatifu na hekima. Stephano alifanya miujiza mingi na kutumia ushawishi mkubwa illi watu wapate kumwamini Yesu.

### Kanisa la kwanza

Hili ni, "Kanisa wakati lilipo anza."

### Alikuwa na tabia nzuri

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "aliye kuwa anatazamwe vizuri na watu." Lugha zingine zinaweza kutafsiri hii kama, "alikuwa na jina zuri."

### Alikuwa amejaa roho mtakatifu na hekima

Hii ninaweza pia kutafsiriwa kama, "alikuwa na nguvu na uwezo kutoka kwa Roho Mtakatifu na alikuwa na hekima nyingi" au, "alijaa Roho Mtakatifu na alikuwa mwerevu."

### Toa hoja kwa ushawishi

Hii ni, "kutoa sababu zenye kushawishi kwa nini."

### translationWords

- [Kanisa](#)

- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Busara, hekima
- muujiza, ajabu, ishara
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



**45:02**

**Siku moja** wakati Stephano anafundisha habari za Yesu, baadhi ya Wayahudi wasiomwamini Yesu walianza kubishana na Stephano. Walikasirika sana na kusema uongo kinyume cha Stephano kwa viongozi wa kidini. Wakasema, "Tumemsikia akisema vibaya juu ya Musa na Mungu!" Hivyo viongozi wa kidini walimkamata Stephano na kumpeleka kwa Kuhani Mkuu na viongozi wengine wa kiyahudi mahali ambapo mashahidi wengine zaidi walishuhudia uongo juu ya Stephano.

**Siku moja**

Hii sentensi inatoa utangulizi wa tukio ambalo limetokea wakati ulio pita, ingawa halielezi muda maalumu. Lugha nyingi zina njia kama hii ya kueleza simulizi ya kweli.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini
- baya, ovu, uovu
- Musa
- Mungu
- kuhani mkuu
- ushuhuda, shuhudia

**45:03**

Kuhani Mkuu akamwuliza Stephano, "Maneno hayo ni ya kweli?" Stephano aliwajibu kwa kuwakumbusha mambo mengi makuu ambayo Mungu ameyafanya kutoka Ibrahimu hata wakati wa Yesu, jinsi ambavyo watu wa Mungu waliendelea kutomtii Mungu. Ndipo aliposema, "Enyi watu wagumu na waasi kila mara mnamkataa Roho Mtakatifu, kama wazazi wenu walivyomkataa Mungu na kuwaua manabii wake. Na nyinyi mmefanya jambo baya zaidi kuliko wao! Mmemwua Masihi."

**Je mambo haya ni kweli?**

Hii maana yake ni kwamba, "je mashitaka haya juu yako ni ya kweli?" au, "je mambo haya wanayosema watu hawa juu yako ni ya kweli?" au, "je ni kweli kuwa ulisema mambo maovu kuhusu Musa na Mungu?"

**Kila mara mnamkataa Roho Mtakatifu**

Hii ni kwamba, "hamkumtii Roho Mtakatifu" au, "kila mara mlikataa kumsikiliza Roho Mtakatifu."


**Baba zenu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, " baba zenu, waisraeli."

**translationWords**

- kuhani mkuu
- kweli, ukweli, kuwa kweli
- Mungu
- Abrahamu, Abramu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- totii, mkaidi, kutotii
- Waasi, uasi.
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.

- Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.
- Kristo, Masihi

**45:04**

Viongozi wa kidini ya kiyahudi waliposikia hayo, walikasirika, **wakaziba masikio yao** na **kupaza sauti kubwa**. Walimburuta Stephano kwa nguvu na kumpeleka nje ya mji na kumponda kwa mawe ili kumwua.

**wakaziba masikio yao**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "waliweka mikono yao kwenye masikio yao." Hii ilikuwa kuonesha kuwa walikuwa hawataki kusikia kile alichokisema Stefano.

**kupaza sauti kubwa.**

Walipaza sauti kwa hasira. Tafsiri jambo hili kwa njia ambayo itaonesha kuwa walikuwa wamekasirika sana.

**translationWords**

- [viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini](#)



## 45:05



Stephano alipokaribia kufa, alilia kwa sauti, "Ee Yesu, pokea roho yangu." Ndipo alipopiga magoti na kusema tena, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii." Baadaye akafa.

### Wakati Stefano akifariki

Hii maana yake ni kwamba, "wakati Stefano akikata roho."

### Alilia kwa sauti


Hii maana yake ni kwamba, "alilia kwa sauti kuu" au, "alisema kwa sauti ya juu."

### Usiwahesabie dhambi hii."

Hii maana yake ni kwamba, "usiwaone kama watu wenye hatia kwa dhambi hii ya kuniua mimi."

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kupokea
- roho, kiroho
- bwana, mkuu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- kifo, kufa, mfu

**45:06**

Kijana mmoja aitwaye Sauli alikubaliana na watu waliomwua Stephano na akalinda nguo zao walipokuwa wanamponda mawe. Tangu siku hiyo, watu wa Yerusalemu wakaanza kuwatesa wafuasi wa Yesu, hivyo waamini wakakimbia kwenda sehemu zingine. Licha ya hayo, walihubiri habari za Yesu popote walipoenda.

**Akalinda nguo zake**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "aliyalinda makoti yake." inawezekana alikuwa anahakikisha kuwa hayaibiwi au kuharibiwa.

**Lakini licha ya hii**

Viongozi wa Wayahudi walidhani kuwa wangesimamisha kuenea kwa mafundisho ya Yesu kwa kuwatesa wafuasi wake. badala yake jambo hili liliwafanya watawanyike na kueneza ujumbe kwa upana zaidi.

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Yerusalemu
- Kuwatesa, mateso
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuamini, kuamini katika
- Kuhubiri

**45:07**

Mwanafunzi wa Yesu jina lake Filipo, alikuwa mmoja wa waumini waliokimbia kutoka Yerusalemu wakati wa mateso. Alienda Samaria alipohubiri habari za Yesu na watu wengi wakaokolewa. Ndipo siku moja malaika kutoka kwa Bwana akamwambia Filipo kwenda katika njia fulani jangwani. Alipokuwa akitembea barabarani, Filipo alimuona afisa mashuhuri kutoka nchi ya **Ethiopia** akiwa amepanda gari lake. Roho Mtakatifi alimwambia aende kukutana na kuzungumza na mtu huyo.

**Siku moja**

Hii sentensi inatoa utangulizi wa tukio ambalo limetokea wakati ulio pita, laki haisemi muda maalum. Lugha nyingi zina namna hii ya kueleza simulizi ambayo ni ya kweli.

**Ethiopia**

Ethiopia ni nhi katika Afrika ya Mashariki.

**translationWords**

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuamini, kuamini katika
- Yerusalemu
- Kuwatesa, mateso
- Samaria, Msamaria
- Kuhubiri
- okoa, salama
- Malaika, Malaika mkuu
- Mungu
- Gari
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.



**45:08**

Filipo alipolikaribia gari, alimsikia mu-Ethiopia akisoma kile ambacho nabii Isaya aliandika. Huyo mtu alisoma, "Walimwongoza kama mwanakondoo na kumwua, kama mwanakondoo, alikaa kimya bila kusema neno. Walimtendea vibaya na hata hawakumheshimu. Walitoa uhai wake na kumwua."

**Muethiopia**

Huyu ni, "mtu wa nchi ya Ethiopia.

**Alikaribia gari la farasi**

Hii maana yake ni kwamba "alikaaribia gari" au, "alisogelea gari."

**Kama mwanakondoo akaapo kimya**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "kama mwanakondoo anapokuwa kimya hata kama anakaribia kuuwawa

**translationWords**

- Gari
- Isaya
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai



## 45:09



Filipo alimwuliza huyo mtu wa Ethiopia, "Unaelewa kile unachokisoma?" Yule mtu akajibu, "Hapana. Siwezi kuelewa isipokuwa awepo mtu wa kunielezea. Tafadhali njoo ukae pamoja nami. Isaya aliandika kuhusu yeye au juu ya mtu mwingine?"

### **Alikuwa ni Isaya anaandika kuhusu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " Isaya alikuwa anamlenga nani."

### **translationWords**


- [Isaya](#)

**45:10**



Filipo alimuelezea Muethiopia kuwa Isaya aliandika juu ya Yesu. Vile vile Filipo alitumia maandiko mengine kumuelezea habari njema za Yesu.

## 45:11



Filipo na yule mtu wa Ethiopia walipokuwa wanasafiri, walifika kwenye maji. Muethiopia akasema, "Tazama! Kuna maji hapa! Je naweza kubatizwa?" Akamwambia dereva wake kusimamisha gari.

### Maji

Tumia neno ambalo linamaanisha maji mengi kama vile bwawa, ziwa, au kijito.

### Naweza kubatizwa?

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "je kuna sababu yoyote ya kunizuia nisibatizwe?"

### translationWords

- Batiza, ubatizo
- Gari

## 45:12



Kwa hiyo walienda kwenye maji, na Filipo akambatiza yule mtu wa Etheopia. Baada ya kutoka majini, ghafla Roho Mtakatifu alimwondoa Filipo na kumpeleka mahali pengine kuendelea kuwaambia watu habari za Yesu.

### **Alimpeleka Filipo pengine**

Hii ni kwamba, "alimchukua Filipo" au, "alimnyakua zake Filipo."

### **translationWords**

- Batiza, ubatizo
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



## 45:13



Yule mtu wa Ethiopia aliendelea na safari yake kwenda nyumbani akimfurahia za Mungu kuwa amemjua Kristo.

Simulizi ya Biblia kutoka: Matendo ya Mitume 6:8-8:5; 8:26-40

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

## 46. Paulo Anakuwa Mkristo

### 46:01



Kijana Sauli ndiye alitunza nguo za wanaume waliomuua Stefano. Yeye hakuwa mfuasi wa Yesu. Kazi yake ilikuwa kuwatesa wakristo. Alizungukia kila kaya mjini Yerusalemu akiwakamata watu wa jinsia zote waliomwamini Yesu na kuwaweka gerezani. Mkuu wa makuhani alimpa kibali kwenda **Dameski** kuwakamata wafuasi wa Yesu na kuwaleta Yerusalemu.

### Alitunza nguo za wanaume waliomuua Stefano

Angalia maelezo kutoka hadithi sehemu 45-6.

### Kutoka nyumba hadi nyumba

Hiyo ina maana ya kwamba "kwenye nyumba nyingi."

### Dameski

Dameski sasa ni makao makuu ya nchi ya Syria. Nyakati zile za Sauli, lilikuwa jiji lililokuwa linamilikiwa na Dola la Kirumi. Watu wengi huko hawakuwa Wayahudi, lakini kulikuwa na baadhi ya Wayahudi na pia baadhi ya Wakristo waliokuwa wakiishi huko.

### translationWords

- Paulo, Sauli
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuwatesa, mateso

- Kuamini, kuamini katika
- Yerusalemu
- kuhani mkuu

## 46:02



Sauli alipokuwa akienda Damesiki, nuru kuu kutoka mbinguni ilimwangaza pande zote na akaanguka chini. Sauli alisikia mtu akisema, "Sauli! Sauli! Kwa nini unaniudhi?" Sauli alimuuliza "Wewe ni nani Bwana?" Jibu la Yesu lilikuwa, "Mimi ni Yesu unayeniudhi."

### Alipokuwa akienda

Hiyo ina maana "akiwa katika safari yake"

### translationWords


- Paulo, Sauli
- Kuwatesa, mateso
- bwana, mkuu



**46:03**



Sauli alipoamuka, hakuweza kuona. Waliokuwa pamoja naye ilibidi wampeleke Dameski. Alikaa siku tatu bila kula wala kunywa.

**46:04**

Huko Dameski alikuwapo mwanafunzi wa Yesu aliyetwa Anania. Mungu alimwagiza, "Nenda katika nyumba ambamo anaishi Sauli. Weka mikono juu yake ili apate kuona tena." Bali Anania akajibu, "Bwana nimesikia jinsi mtu huyu anavyowaudhi wafuasi wa wako. "Mungu akamwambia, Nenda! Nimemchagua alitangaze jina langu kwa Wayahudi na kwa watu kutoka Mataifa mengine. Naye atateseka sana kwa ajili ya jina langu."

**Lakini Anania akasema**

Kama haiko wazi sana kwanini neno "Lakini" linatumika hapa, hili neno linaweza kutafsiriwa kama " Lakini Anania aliogopa, na hivyo akasema"

**Mungu akamjibu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama "Ili kumhakikishia Anania, Mungu alisema" ili kuweka wazi kwa nini Mungu alisema hili.

**Alitangaze jina langu**

Hii ni " kufundisha kuhusu mimi" au "kunifanya mimi nijulikane"


**Kwa ajili ya jina langu**

Hii ni "kwa ajili yangu" au "kwa sababu yangu" au "kwa sababu ananitemikia mimi" au "kwa sababu anawafundisha watu wengine kuhusu mimi"

**translationWords**

- mfuasi
- Mungu

- Paulo, Sauli
- bwana, mkuu
- Kuwatesa, mateso
- teseka, kuteseka

**46:05**

Ndipo Anania alikaenda kwa Sauli, akamwekea mikono, akasema, "Yesu uliyekutana naye njiani wakati unakuja **hapa**, amenituma kwako ili **upate kuona tena** na ujazwe na Roho Mtakatifu". Mara akaweza kuona tena. Kisha Anania akambatiza, akala chakula na **nguvu zake zikamrudia**.

**hapa**

Hiyo ina maana "Dameski"

**upate kuona tena**

Hii ingeweza kutafsiriwa pia kama "kuweza kuona tena"

**nguvu zake zikamrudia**

Hii ingeweza kutafsiriwa pia kama "akawa mwenye nguvu tena" au "akajisikia vizuri"

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Batiza, ubatizo



**46:06**

**Mara hiyo**, Sauli alianza kuhubiri Wayahudi katika Dameski akisema, "Yesu ni Mwana wa Mungu". Wayahudi walishangaa kuona mtu aliyekuwa akijitahidi kuwaangamiza wakristo amegeuka kuwa mfuasi wa Yesu! Sauli alibainisha kuwa Yesu ndiye Masihi.

**Mara hiyo**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama "Maramoja" au "Kisha"

**alijadiliana na Wayahudi**

Hii pia ingeweza kutafsiriwa kama "aliwapa Wayahudi sababu njema za kuamini katika Yesu" au , "aliongea kwa ushawishi pamoja na Wayahudi"

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Kuhubiri
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Kuamini, kuamini katika
- Kristo, Masihi

**46:07**

Siku nyingi baadaye, Wayahudi walipanga kumuua Sauli. Waliwatuma watu kumfuatilia katika **malango ya miji** kwa lengo la kumwangamiza. Lakini Sauli aligundua mpango huo, na rafiki zake walimsaidia kutoroka. Usiku mmoja aliteremshwa akiwa ndani ya kikapu ukutani, akishatoroka kutoka Dameski aliendelea tu kuhubiri habari za Yesu.

**malango ya miji**

Malango yalikuwa ndiyo njia pekee ya kawaida ya kuingia au kutoka kwenye miji iliyokuwa imezungushiwa ukuta.

**walimteremsha akiwa ndani ya kikapu ukutani**

Njia nyingine ya kusema hiki ingekuwa "walimsaidia kuingia ndani ya kikapu kikubwa na kukishusha hicho kikapu na yeye akiwa ndani yake juu ya ukuta wa miji"

**translationWords**

- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Paulo, Sauli
- Kuhubiri
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

**46:08**

Sauli alitembelea Yerusalemu, lakini wanafunzi wa Yesu walimhofu. Kisha muumuni aliyetitwa Barinaba alimpeleka kwa mitume kuwaeleza jinsi alivyo hubiri kwa ujasiri habari njema huko Dameski. Taarifa hiyo ilisababisha mitume **wamkubali Sauli**.

**wamkubali Sauli**

Hii ina maana "waliamini kwamba Sauli pia alikuwa muumini katika Yesu"

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Yerusalemu
- mfuasi
- Kuamini, kuamini katika
- Barnaba
- Mtume, utume
- Kuhubiri



**46:09**

Baadhi ya waumini waliokimbia mateso huko Yerusalemu na kwenda mbali huko Antiokia, walizidi kuhubiri kuhusu Yesu. Wenyaji wengi wa Antiokia hawakuwa Wayahudi, hicho ndicho kipindi ambacho watu wa mataifa kwa mara ya kwanza walipokea imani. Barnaba na Sauli walikwenda huko kuwafundisha hao waumini wachanga zaidi kuhusu Yesu na **kulikomaza kanisa**. Kwa mara ya kwanza wafuasi wa Yesu waliitwa Wakristo hapo Antiokia.

**mji wa Antiokia**

Huu ulikuwa mji wa zamani ambao unapatikana mahali ambapo hivi sasa ni sehemu ya kusini kabisa wa nchi ambayo sasa inajulikana kama Uturuki, karibu na mpaka wa Syria na karibu na Bahari ya Mediterania. Ni kama umbali wa maili 450 kaskazini magharibi mwa Yerusalemu.

**kulikomaza kanisa**

Hii ingeweza pia kutafsiriwa kama, "kulisaidia kanisa kukua imara kiroho" au "kuwasaidia waumini katika Yesu kukuwa imara katika imani yao" au, "kuwasaidia watu kuamini kwa uthabiti ndani ya Yesu"

**translationWords**

- Kuwatesa, mateso
- Yerusalemu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Myahudi, Yahudi, Wayahudi
- Barnaba
- Paulo, Sauli
- Kanisa
- Mkristo



**46:10**

Hapo Antiokia, **siku moja** wakristo walipo kuwa katika maombi ya kufunga, Roho Mtakatifu aliwaambia **nitengeeni** Sauli na Barinaba wafanye kazi niliyo waitia. Hivyo **kanisa** liliwaombea na kuwawekea mikono, kisha **wakawatuma waende** maeneo mengine mengi kuhubiri habari njema za Yesu. Barinaba na Sauli walifundisha makundi ya watu wa matifa mbalimbali, watu wengi wakamwamini Yesu.

**siku moja**

Hii sentensi inatambulisha tukio ambalo limetokea huko nyumba, lakini haisemi ni wakati gani hasa. Lugha nyingi zinanamna kama hiyo ya kuanza kuhadithia hadithi.

**nitengeeni**

Sentensi hii inaweza kutafsiriwa kama, "Kuwaoteuwa Paulo na Barnaba kufanya kazi maalumu ambayo nimewachagua kufanya."

**kanisa**

Hii ingeweza pia kutafsiriwa kama, "waumini" au, "wakristo."

**wakawawekea mikono juu yao**

Hii ingeweza pia kutafsiriwa kama, "waliwabarikia kwa nguvu na mamlaka ya Roho Mtakatifu kwa kuwawekea mikono juu yao" au, "waliweka mikono juu yao kama alama ya umoja wao katika Roho," Baadhi ya Lugha zingelizimika kusema ni wapi walipoweka mikono yao. Kama ni hivyo ungelisema waliweka mikono juu ya vichwa vyao, mabega au mgongo yao.

## wakawatuma waende

Hiyo ni ina maana ya kwamba, "wakawatuma waende huko" au, "wakawatuma waende katika sayari yao.


Simulizi ya Biblia Kutoka: Matendo ya Mitume 8:3; 9:1-31; 11:19-26;13:1-3

## translationWords

- funga
- Kuomba, maombi
- Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.
- Kanisa
- Barnaba
- Paulo, Sauli
- Kuhubiri
- habari njema, injili
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuamini, kuamini katika

## 47. Paulo na Sila wakiwa Filipi

47:01



Sauli alianza kujiita Paulo, kwa jina lake la Kirumi, alipofanya safari katika ufalme wote wa madola ya Kirumi. Paulo na mtu wake wa Karibu aitwaye Sila walienda kuhubiri habari njema kuhusu Yesu katika mji wa Filipi. Walienda nje ya mji, kando ya mto mahali ambapo watu walikutana kusali. Walipokuwa hapo walionana na mwanamke mfanya biashara aliyeitwa Lidia. Alimpenda na alimcha Mungu.

### kutangaza

Hiyo ina maana kwamba, "kufundisha" au, "kuhubiri."

### mfanyabiashara

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "muuzaji" au, "mmiliki wa biashara" au, "mwenye biashara."

### translationWords

- Rumi
- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu
- Filipi
- habari njema, injili
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- upendo
- Abudu
- Mungu

**47:02**

Mungu alimwongoza Lidia kuupokea ujumbe wa Yesu, yeye, wakiwemo watu wa nyumbani mwake, wote walibatizwa. Paulo na Sila walikaa kwake na watu wake, aliwakaribisha nyumbani.

**aliufungua moyo wa Lidia**

Hii ina maana kwamba, "alimwezesha Lidia"

**yeye na familia yake walibatizwa**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "walimbatiza Lidia na familia yake."

**hivyo wakakaa naye yeye na familia yake**

Hii ilikuwa desturi ya kawaida siku zile kwa watu kuwakarimu wageni nyumbani mwao. Kulikuwa hakuna nia mbaya kinyume cha maadili katika kufanya hivi.

**translationWords**

- Mungu
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Batiza, ubatizo
- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu



**47:03**

Kulikuwa na mahali ambapo watu walikuwa wakikutana na kusali. Hapo ndipo mahali Paulo na Sila mara nyingi walikutana na watu. Walipokuwa akienda mahali pale kila siku, mwanamke mmoja mwenye umri mdogo kabisa, akiwa mtumwa, na mwenye pepo, aliwafuata. Alikuwa akiwatabiria watu kwa kuongozwa na pepo, kutokana na uwezo kama huo aliwafaidisha **waliomtumikisha**, kwa kuwapatia fedha nyingi kwa kazi yake ya utambuzi.

**waliomtumikisha**


katika hili, hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "wamiliki wake" au, "watu wanaommiliki"

**kama mtambuzi**

Hiyo ina maana kwamba. "ni kama mtu anaye waambia watu yale ambayo yangewatokea katika siku zao za usoni."

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu
- Kuomba, maombi
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Kuwa na mapepo
- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu
- bwana, mkuu

**47:04**

Msichana mtumwa alikuwa akipaza sauti kila alipowaona wakitembea, na kusema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye hai." Wanawaelezeeni **njia ya kupata wokovu!** Alifanya hivyo bila ya kuchoka kiasi cha kumkera Paulo.

**njia ya kupata wokovu**

Hiyo ina maana kwamba, "ni jinsi unaweza kuokoka" au, "jinsi gani Mungu anaokoa watu" au. "Mpango wa Mungu kuwaokoa watu"

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Mungu
- okoa, salama
- Paulo, Sauli

**47:05**

Hatimaye **siku moja** msichana mtumwa alipoanza kupaza sauti, Paulo **aligeuka kwake** na kumkemea pepo aliyekuwa ndani yake, akisema, "kwa jina la Yesu toka," palepale pepo alimwacha.

**siku moja**

Hii sentensi inatambulisha tukio ambalo limetokea huko nyumba, lakini haisemi ni wakati gani hasa. Lugha nyingi zinanamna kama hiyo ya kuanza kuhadithia hadithi.

**aligeuka kwake**

Hii ina maana kwamba, "aligeuka na kumwangalia"

**kwa Jina la Yesu**

Hiyo ina maana kwamba, "kwa mamlaka ya Yesu." Kwa sababu ya mamlaka ya Yesu, Paulo aliweza kuamuru pepo kuondoka.

**toka ndani yake**

Hiyo ina maana kwamba, "muache" au, "nenda mbali naye"

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Paulo, Sauli
- pepo mbaya, roho ovu, roho chafu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

## 47:06



Watumikishaji wa msichana walipotambua kuwa **bila ya pepo** mtumwa wao alikuwa hawezi kuwatabiria watu, walikasirika. Kwa kuwa hangewaingizia kipato cha fedha tena, kwa kulipwa wao ili afanye utabiri kwa watu.

### **bila ya pepo**

Hiyo ina maana kwamba. "bila ya nguvu kutoka kwa pepo" au, "sasa kwamba hakuwa na pepo."

### **wakati ujao**

Hiyo ina maana kwamba, "mambo yatakayowatokea katika wakati ujao."

### **Hii ilimaanisha kwamba**

Hii ingeweza pia kutafsiriwa kama, "Kwa sababu ya hili" au, "Kwahiyo."

### **translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa



## 47:07




Kwa sababu hiyo Paulo na Sila walipelekwa kwenye vyombo vya dola vya serikali ya Kirumi na Watumikishaji wa msichana mtumwa, watu hawa waliwapiga na **kuwatia** gerezani.

### **kuwatia**

Hiyo ina maana kwamba, "kuwaweka."

### **translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu
- Rumi

**47:08**

Paulo na Sila waliwekwa katika chumba cha ndani kabisa sehemu mojawapo ya gereza, kwa usalama wasitoroke na hata kufungwa miguu yao. Usiku wa manane walikuwa **wakiimba nyimbo za kumsifu Mungu**.

**usiku wa manane**

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "usiku sana" au, "alfajiri mapema sana." Hii ilikuwa wakati ilipokuwa giza kabisa huko nje, ambapo watu kwa kawaida wanakuwa wamelala."

**wakiimba nyimbo za kumsifu Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kumsifu Mungu kwa kuimba" au, "kuimba nyimbo za kumsifu Mungu" au, "kuimba nyimbo ambazo zinampa Mungu sifa."

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu
- Kusifu
- Mungu

## 47:09



Kushtukia, kulitokea tetemeko kubwa lililosababisha milango ya gereza na pingu za minyororo ya wafungwa kufunguka na **kuanguka** kutoka mikononi.

### **kuwa wazi**

Hiyo ina maana kwamba, "kutokufungwa na ghafla kuwa wazi kabisa."

### **kuanguka**

Hiyo ni maana kwamba, "ghafla ilitoka" au, "ghafla ikajitenga hivyo wafungwa wakawa wamefunguliwa."

**47:10**

Askari mlinzi wa wa wafungwa aliamuka, alijawa na hofu kubwa sana baada ya kuona milango ya gereza iko wazi, akifikiri kuwa, wafungwa wote watakuwa wametoroka, alikusudia kujiangamiza. (Alijua serikali ya Kirumi ingemhukumu kifo endapo aliwaachia wafungwa kutoroka). Lakini Paulo alipaza sauti kumkataza "Acha kujiangamiza, sisi sote hatujatoroka.

**Askari mlinzi wa wafungwa**

Hiyo ina maana kwamba, "afisa mwangalizi wa gereza."

**Sisi**

Baadhi ya lugha zinaliangalia neno "sisi" kimaalum kabisa ambayo haimhusishi mtu anayeongelehwa. Hapa "sisi" haimhusishi askari mlinzi wa wafungwa, ni Paulo tu pamoja na wafungwa wengine.

**translationWords**

- Rumi
- Paulo, Sauli



**47:11**

Mlinzi wa wafungwa alienda kwa Paulo na Sila akitetemeka na kuwauliza, "Nifanye nini nipate **kusalimika**?" Paulo alimjibu, "mwamini Yesu, Bwana, **wewe na watu wa nyumbani mwako mtapata wokovu**. Hivyo mlinzi wa wafungwa aliwakaribisha Paulo na Sila nyumbani kwake na kuwaosha majeraha yao. Kila mtu katika nyumba yake alipata kuhubiriwa na Paulo habari njema za Yesu.

**kusalimika**

Hii ingeweza kutafsiriwa pia kama, "ili niweze kuokoka kutoka katika dhambi zangu" au "ili kwamba Mungu aniokoe kutoka katika dhambi zangu." Swali linahusu wokovu kutoka katika kuadhibiwa na Mungu aliyesababisha tetemeko.

**Mwamini Yesu, Bwana mkubwa.**

Hii inaelezwa kwa wote wawili yaani askari mlinzi wa gereza pamoja na familia yake, ambao wote walikuja kuamini na kubatizwa. Baadhi ya lugha zingetumika kuonyesha kwamba Paulo anaongea na kundi.

**wewe na watu wa nyumbani mwako mtapata wokovu.**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Mungu atawaokoa wewe na familia yako kutoka katika adhabu ya milele kwa sababu ya dhambi zenu." Hakikisha kwamba wokovu unaoongelewa hapa ni wakiroho, na si wa kimwili.

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu
- okoa, salama
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- bwana, mkuu

- [Kuhubiri](#)
- [habari njema, injili](#)

**47:12**



Mlinzi wa wafungwa na kila mtu katika nyumba yake walimwamini Yesu na kubatizwa. Mlinzi wa wafungwa aliwahudumia chakula Paulo na Sila na walifurahi pamoja.

**47:13**

Siku iliyofuata, Paulo na Sila waliachiliwa huru kutoka gerezani na waliambiwa kuondoka Filipi na **viongozi wa mji**. Paulo na Sila walipata nafasi kumtembelea Lidia na wpendwa wengine na ndipo walipoondoka katika mji. **Injili ya Yesu iliendelea kuenea na Kanisa liliendelea kukua.**

**viongozi wa mji**

Hii inaelezea juu ya, "maafisa wa mji" au, "mamlaka ya mji."

**Injili ya Yesu iliendelea kuenea**

Hiyo ina maana kwamba, "Watu katika maeneo mengi zaidi walikuwa wakisikiliza habari njema kuhusu Yesu."

**Kanisa liliendelea kukua**

Hiyo ina maana kwamba, "watu wengi zaidi walikuwa wanakuwa sehemu ya kanisa" au, "watu wengi zaidi na zaidi walikuwa wakimwamini Yesu."

**translationWords**

- Paulo, Sauli
- Sila, Silivanu
- Filipi
- habari njema, injili
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kanisa



## 47:14



Miji mingi ilifikiwa na Paulo pamoja na viongozi wengine wakristo waliosafiri kwenda katika miji hiyo wakihubiri na kufundisha habari njema za Yesu. Zaidi ya hapo waliandika barua nyingi za kuwatia moyo wakristo makanisani. Baadhi ya barua hizi ni sehemu ya vitabu vya Biblia.

Simulizi ya Biblia kutoka: Matendo ya Mitume 16:11-40

### translationWords

- Paulo, Sauli
- Mkristo
- Kuhubiri
- habari njema, injili
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuamini, kuamini katika
- Kanisa

## 48. Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa:

48:01



Mwenyezi Mungu alipoumba ulimwengu, vitu vyote vilikuwa sawa pasipo dosari yoyote. **Hapakuwa na dhambi**, wala magonjwa, wala kifo duniani. Adam na Mke, Eva, walipendana sana na walimpenda Mungu pia. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu alivyokusudia ulimwengu uwe.

### Mungu aliumba ulimwengu

Hiyo ina maana kwamba, "Mungu aliufanya ulimwengu kutoka katika utupu au katika hali ya kutokuwa na kitu."

### Pasipo dosari yoyote

Hiyo ina maana kwamba, "sahihi kabisa kama inavyotakiwa kuwa" kukamilisha yote yale ambayo Mungu alikusudia kwayo.

### Hapakuwa na dhambi

Kwa baadhi ya lugha siyo rahisi kuelezea "dhambi" kama kitu, badala yake dhambi inaelezewa kama kitendo. Katika mazingira hayo hii ingeweza kutafsiriwa kama, "Hakuna ambaye aliwa kutenda dhambi" au, "Watu hawakutenda dhambi" au, "Hakuna jambo ovu lililotokea."

### Hapakuwa na magonjwa wala kifo

Hiyo ina maana kwamba, "Hakuna aliyegua na hakuna aliyekufa" au, "Hawakuugua wala hawakufa."

## translationWords

- Mungu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Adamu
- Hawa
- upendo
- kifo, kufa, mfu

**48:02**

Katika bustani ya Edeni, Shetani alijitokeza kama nyoka. Akazungumza na Eva kwa lengo la kumdanganya. Kwa njia hiyo, Adam na Eva wakawa wamemtenda Mungu dhambi, na leo watu wote duniani tunaweza kuugua na kufa kama matokeo ya dhambi.

**Bustani**

Hii inaelezea juu ya bustani iliyotengenezwa na Mungu mahali alipowaweka watu wa kwanza mtu mume na mtu mke.

**Alimdanganya Eva**

Hiyo ina maana kwamba, "alimdanganya Eva." Shetani alimdanganya kwa kumuongoza Eva kutilia mashaka kile ambacho Mungu alikisema. Kwa kufanya hivi, alimlaghai Eva kwa kumuweka katika hali ya kutomtii Mungu.

**translationWords**

- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Hawa
- Adamu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- kifo, kufa, mfu



**48:03**

Jambo jingine **la hatari zaidi** likajitokeza kama matokeo ya dhambi ya Adam na Eva. Uhusiano wao na Mungu ukaharibika na toka wakati huo, kila mwanadamu anazaliwa akiwa na asili ya dhambi, akiwa hana mahusiano mazuri na Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu akawa na mpango wa kurejesha uhusiano ulioharibiwa na dhambi baina ya mwanadamu na Mungu.

**la hatari zaidi**

Hiyo ina maana kwamba, "mbaya zaidi" au, "bado mbaya"

**translationWords**

- Adamu
- Hawa
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu

**48:04**

kupitia mpango huo, Mwenyezi Mungu aliahidi kuwa mmoja wa wazaliwa katika uzao wa Eva **atakiponda kichwa cha shetani**, na shetani **atakigonga kisigino** chake. Maneno haya yana maana kwamba, shetani atamuua Masihi, lakini Mwenyezi Mungu **atamfufua tena**, na kisha huyo Masihi atazishinda nguvu za shetani milele. Baada ya miaka mingi kupita, Mwenyezi Mungu akaudhirishia ulimwengu kuwa Yesu ndiye Masihi.

**atakiponda kichwa cha shetani**

Hii ingeweza kutafsiriwa pia kama, "kukanyaga kwenye kichwa cha shetani na kukiharibu kabisa" au, "Kukivunja kichwa cha Shetani kwa kukikanyaga juu yake." Hii ni namna ya sura ya mtu anayekanyaga juu ya kichwa cha nyoka. Kichwa kinakuwa kimepondwa kabisa na nyoka anakuwa amekufa na kwa hiyo hawezi kudhuru.

**atakigonga kisigino**

Hii ni namna ya sura ya nyoka ardhini akiuuma mguu wa mtu. Katika habari hii, Shetani angesababisha Masihi kuteseka, lakini asingemharibu.

**atamfufua tena**

Hiyo ina maana kwamba, "kumfanya awe hai tena."

**translationWords**

- Mungu
- Ahadi
- Hawa
- uzao, kutokana na
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Kristo, Masihi
- inua, inuka

- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

**48:05**

Katika siku zile Mwenyezi Mungu alipouangamiza ulimwengu kwa mafuriko, aliandaa chombo cha kuwaokoa na gharika hilo watu wote waliokuwa wanamwamini. Kwa sababu ya dhambi, ni kwa namna iyo hiyo, watu wote duniani wanastahili kuangamizwa. Lakini ashukuriwe Muwenyezi Mungu aliyemtoa Yesu kumuokoa kila mtu anayemwamini.

**kuangamizwa kwa sababu ya dhambi zao**

Hii ingeweza kutafsiriwa pia kama, "kila mmoja anapaswa kuadhibiwa milele na Mungu kwa sababu wametenda dhambi."

**translationWords**

- Mungu
- okoa, salama
- Kuamini, kuamini katika
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



**48:06**

Katika kipindi cha mamia ya miaka, makuhani wakadumu katika kutoa sadaka za kuteketezwa, wakidhihirisha aina ya adhabu iliyowapasa kupewa kwa ajili ya dhambi zao. Hata hivyo, sadaka hizo hazikuweza kabisa kuwaondolea dhambi zao. Hivyo, Yesu ndiye kuhani mkuu asiyelingana na makuhani wengine. Yeye alijitoa nafsi yake mwenyewe ili awe sadaka ya pekee ya kuteketezwa kwa ajili ya kuziondoa dhambi za watu wote duniani. Yesu ndiye kuhani mkuu wa kweli maana **alibeba adhabu** ya dhambi iliyotendwa na watu wote.

**alijitoa mwenyewe**


Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "Yesu aliruhusu yeye mwenyewe auwawe."

**alibeba adhabu**

Hiyo ina maana kwamba, "alipokea adhabu katika mwili wake mwenyewe."

**translationWords**

- Kuhani, ukuhani
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- kuhani mkuu
- Kuadhibu, adhabu

**48:07**

Ndipo Mwenyezi Mungu akazungumza na Ibrahimu akamwambia, "Kupitia wewe Ibrahimu, watu wa kila kabila duniani wamebarikiwa." Naye Yesu alitokana na uzao wa Ibrahimu, na watu wa kila namna wanabarikiwa kupitia Ibrahimu. Hivyo, kila anayemwamini Yesu ameokolewa kutoka katika dhambi, na anafanyika kuwa **uzao wa Ibrahimu kwa jinsi ya kiroho**.

**watu wote wa duniani**

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "watu kutoka pande mbalimbali zote za dunia."

**uzao wa Ibrahimu kwa jinsi ya kiroho**

Hiyo ina maana kwamba, "kiroho anahusiana na Ibrahim, na mmoja wa watu wa Mungu."

**translationWords**

- Mungu
- Abrahamu, Abram
- Kundi la watu, watu
- Kubariki
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- uzao, kutokana na
- Kuamini, kuamini katika
- okoa, salama
- roho, kiroho

**48:08**

Mwenyezi Mungu alipomwagiza Ibrahimu kumtoa mwanae, Isaka, kama sadaka ya kuteketezwa na akatii, Bwana Mungu akampatia Ibrahimu mwana kondoo achinjwe na kutolewa sadaka badala ya mwanae, Isaka. Hii inatufundisha kuwa sisi sote tunastahili kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini Mwenyezi Mungu amemtoa Yesu, mwanakondoo wa Mungu ili atolewe kama sadaka na kisha **kufa badala yetu**.

**badala ya mwanawe Isaka**

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "mahali pa mwanawe Isaka" au, "Katika mahali pa mwanawe Isaka" au, "ili kwamba asimtoe sadaka mwanawe Isaka kuwa sadaka ya kuteketezwa."

**kustahili kufa**

Hiyo ina maana kwamba, "ilitupasa kufa."


**kufa badala yetu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "kufa mahali pa kila mmoja wetu" au, "ili kwamba asituuwe sisi."

**translationWords**

- Mungu
- Abrahamu, Abramu
- mwana, mwana wa
- Isaka
- dhabihu, sadaka
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu
- kifo, kufa, mfu
- dhambi, yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu



**48:09**

Hata Mwenyezi Mungu alipoamuru mapigo saba katika nchi ya Misri, aliagiza kila familia ya kiisraeli kuchinja mwana **kondoo asiye na kasoro** na kisha kunyunyiza damu ya kondoo juu na chini ya miimo ya milango yao. Na ndipo Mwenyezi Mungu alipoiona damu katika miimo ya milango yao, **aliziruka** nyumba zile na hakuwauwa watoto wao wa kiume wa kwanza. Tendo hilo linajulikana kama pasaka.

**alituma pigo la mwisho juu ya Misri**

Hiyo ina maana kwamba, "alisababisha maafa ya mwisho kuja juu ya Misri." Hili lilikuwa pigo la kumi pale Mungu aliposababisha mzaliwa wa kwanza wa kiume wa Wamisri kufa.

**kondoo asiye na kasoro**

Hiyo ina maana kwamba, "kondoo bila kuwa na kasoro yoyote"

**damu yake**

Hiyo ina maana kwamba, "damu ya mwana wa kondoo."

**miimo ya mlango**

Kama miimo ya milango haijulikani, hii inaweza kutafsiriwa kama, "milango."

**aliziruka**

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "kupita." Unaweza kutaka kulioanisha neno hili linavyotafsiriwa na jinsi neno "pasaka" linavyotafsiriwa.



## translationWords

- Mungu
- Misri, Mmisri
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu
- damu
- Pasaka

**48:10**

Yesu **hakuwa na kosa wala dhambi yoyote** na aliuawa katika kipindi cha maazimisho ya pasaka. Hakika Yesu ndiye mwanakondoo wetu wa pasaka. kwa yeyote anaemwamini Yesu, **damu yake Yesu** hulipia dhambi za mtu huyo na **adhabu ya Mungu humruka mtu huyo**.

**Mwanakondoo wetu wa Pasaka**

Hiyo ina maana kwamba, "Mwanakondoo wa pasaka aliyeuwawa kwa ajili yetu" au, "mwanakondoo aliyeuwawa ili Mungu apite juu yetu" au, "mwanakondoo aliyeuwawa ili kwamba Mungu asituuwe."

**hakuwa na kosa wala dhambi yoyote**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "hakuwahi kutenda dhambi."

**damu yake Yesu**

Hii ingeweza kutafsiriwa kama, "Sadaka ambayo Yesu alijitoa mwenyewe alipokufa kwa ajili ya wenye dhambi." Neno "damu" hapa linamaanisha pia "kifo."

**adhabu ya Mungu humruka mtu huyo**

Kauli hii inamaanisha, "Mungu hamuadhibu mtu." Itafsiri kutumia maneno yanayoonyesha uhusiano wake na neno "Pasaka" na "Mwanakondoo wa Pasaka." Kama neno "alituhifadhi" limetumika katika neno Pasaka, hii inaweza kutafsiriwa kama, "Mungu alimuacha huyo mtu bila kumuadhibu."

**translationWords**

- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)
- [Pasaka](#)

- mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu
- Kuamini, kuamini katika
- damu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu

**48:11**

Ni kweli kuwa Mwenyezi Mungu alifanya agano na watu wake, taifa la Israel. Bali sasa Mwenyezi Mungu anafanya agano lililo wazi kwa kila mtu. Kwa sababu ya agano hili jipya, watu wote wa kila mahali, wanaweza kuwa sehemu ya watu wa Mungu kwa kumwamini Yesu Kristo.

**Israel ambao ni wateule wake**

Hiyo ina maana kwamba, "Wanaisrael, watu aliowachagua" au, "watu wake aliowachagua, Wanaisrael."

**translationWords**

- Mungu
- Agano
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Agano
- Kundi la watu, watu
- Kuamini, kuamini katika



**48:12**

Japokuwa Musa pia alikuwa ni **nabii mkubwa** aliyetangaza neno la Mungu, Yesu ndiye **nabii mkuu zaidi** ya manabii wote. Kila jambo alilolifanya na kulisema Yesu lilikuwa ni tendo na neno la Mungu kwakuwa yeye ni Mungu. Ndio maana wakati mwingine Yesu anaitwa neno la Mungu.

**nabii mkubwa**

Hiyo ina maana kwamba, "nabii muhimu sana."

**nabii mkuu zaidi**

Hiyo ina maana kwamba, "nabii muhimu sana sana."


**Yeye ni Neno la Mungu**

Hiyo ina maana kwamba, "Anaitwa Neno la Mungu" kwa sababu anafunua tabia ya Mungu. Manabii wengine walihubiri ujumbe ambao Mungu aliwapa, lakini Yesu alimfunua Mungu katika mahubiri yake na matendo yake.

**translationWords**

- [Musa](#)
- [Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.](#)
- [Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko](#)
- [Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu](#)
- [Mungu](#)

**48:13**



Mungu alimuahidi mfalme Daudi kuwa mmoja ya wazaliwa wake atawatawala watu wa Mungu milele. Kwakuwa Yesu ni mwana wa Mungu na Masihi , yeye ndiye yule mzaliwa wa uzao wa Daudi atakayetawala milele.

## 48:14



Daudi alikuwa mfalme wa Israeli, lakini Yesu ni mfalme wa ulimwengu wote. Atarudi tena kuutawala ufalme wake kwa haki na amani milele.

### Mfalme wa ulimwengu wote

Hiyo ina maana kwamba, "Mfalme juu ya kila mmoja na kila kitu kila mahali."

Simulizi ya Biblia kutoka: Mwanzo 1-3, 6, 14, 22; Kutoka 12, 20; 2Samueli 7; Waebrania 3:1-6, 4:14-5:10, 7:1-8:13, 9:11-10:18; Ufunuo 21

### translationWords

- Daudi
- mfalme
- Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- haki, adilifu
- Amani

## 49. Agano Jipya la Mungu

49:01



Malaika akamwambia bikira alieitwa Mariamu kuwa atazaa mtoto atakaekua mwana wa Mungu. Sasa wakati alipoendelea kuwa bikira, Roho Mtakatifu akamfunika na akapata ujauzito. Nae akazaa mtoto mwanamume na kumwita jina lake Yesu. Kwa hiyo Yesu ni Mungu na binadamu.



## 49:02



Yesu alifanya miujiza mingi kuthibitisha yeye ni Mungu. Alitembea katika maji, alizuia mawimbi, aliponya watu wengi, akatoa mapepo, akafufua wafu kua hai na akabadilisha vipande vya mikate mitano na samaki wawili kuwa chakula cha kutosha kwa watu 5000.

### **kutoa mapepo**

Hii inamaanisha kwamba, "alitoa mapepo kwa watu."


### **Aliwafufua wafu**

Hii inaweza kutafsiriwa kwamba, "alisababisha watu waliokufa kuwa hai tena."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- muujiza, ajabu, ishara
- Mungu
- Ponya, tibu
- pepo mbaya, roho oву, roho chafu
- inua, inuka
- kifo, kufa, mfu

## 49:03



Pia Yesu alikua **mwalimu mkuu**, alizungumza kwa mamlaka kwa sababu alikua mwana wa Mungu. Alifundisha watu kua inahitajika kupenda watu wengine kama unavyojipenda mwenyewe.

### **mwalimu mkuu**

Hii ni sawa na kusema: "mwalimu muhimu" au "mwalimu bora."

### **Kwa njia hiyo hiyo**

Hii ni sawa na, "kama ilivyo" au, "kwa sawa kiasi kama kile" au, "kwa kiwango kama kile."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mwana wa Mungu, Mwana
- upendo

## 49:04



Pia alifundisha uhitaji wa kumpenda Mungu kuliko vitu vyote, pamoja na **mali zako**.

### **mali zako**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "fedha yako" au "milki yako."

### **translationWords**

- upendo
- Mungu



## 49:05



Yesu alisema ufalme wa Mungu ni wa thamani kuliko kitu chochote duniani. Kitu cha msingi ni kila mtu kuwemo kwenye Ufalme wa Mungu. Kuingia kwenye Ufalme wa Mungu, ni lazima uweze kuokolewa kutoka kwenye dhambi zako.

### **kuokolewa kutoka katika dhambi zenu**

Hii ni sawa kusema kwamba, "kuokolewa kutoka kwenye hali ya kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zenu" au "kwamba Mungu ataweza kuwasamehe dhambi zenu" au, "kupokea wokovu ili mtoke katika dhambi zenu."

### **translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- okoa, salama
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi



**49:06**

Yesu alifundisha kua baadhi ya watu watampokea na kuokolewa, lakini **wengine hawataokolewa**. Akasema baadhi ya watu ni kama udongo mzuri. Wamepokea habari njema ya Yesu na wameokolewa. Lakini watu wengine ni udongo mgumu wa njiani, ambapo **mbegu ya neno la Mungu** haiwezi kuingia na kutengeneza mavuno yoyote. Watu hawa wamekataa ujumbe kumuhusu Yesu na hawataingia katika ufalme wake.

**wengine hawata**

Hii ni kusema kwamba, "watu wengine hawatampokea na kwa hiyo hawataokolewa."

**mbegu ya neno la Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "mbegu, ambayo inaweza kulinganishwa na neno la Mungu." Kipengele hiki kinaleta mlinganisho kati ya mbegu na neno la Mungu.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kupokea
- okoa, salama
- habari njema, injili
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni

**49:07**



Yesu alifundisha kuwa Mungu anawapenda wenye dhambi sana. Anataka kuwasamehe wenye dhambi na kuwafanya kuwa watoto wake.

**49:08**

Yesu alituambia kuwa Mungu anachukia dhambi. Wakati Adamu na Hawa walivyofanya dhambi, iliharibu uzao wao wote. Na matokeo yake kila mtu duniani ana dhambi na ametenganishwa na Mungu. Na hata sasa, kila mtu amekua adui wa Mungu.

**ametengwa na Mungu**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kuwa, "hawezi kuishi na Mungu" au "hawezi kuwa karibu na Mungu" au "hawezi kuwa na uhusiano na Mungu."

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Adamu
- Hawa
- uzao, kutokana na

**49:09**

Lakini Mungu alimpenda kila mtu sana katika ulimwengu hata akamtoa mwanae wa pekee ili kila mtu amwaminiye Yesu hatahukumiwa kwa dhambi zake, lakini ataishi na Mungu milele.

**alimtoa Mwanawe wa pekee**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "alitoa Mwanawe wa pekee kwa ulimwengu kama dhabihu kwa dhambi" au, "alitupatia Mwanawe pekee awe dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu."

**kila aaminiye**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kuwa, "yeyote aaminiye."

**kila aaminiye katika Yesu hatahukumiwa kwa dhambi zake bali ataishi na Mungu milele**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kwamba, "Wakati yeyote akimwamini Yesu, Mungu hatamhukumu mtu huyo kwa ajili ya dhambi zake, lakini atamruhusu kuishi na Mungu milele."

**translationWords**

- Mungu
- upendo
- Mwana wa Mungu, Mwana
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuadhibu, adhabu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai



**49:10**

Kwa sababu ya dhambi yako, una hatia na unastahili kufa. **Mungu anapaswa kuwa na hasira** nawe, lakini alimwaga hasira yake kwa Yesu badala yetu. Wakati Yesu alipokufa msalabani, alipokea hukumu yako.

**Kwa sababu ya dhambi zenu**

Inaweza kutafsiriwa kwamba, "Kwa sababu mmetenda dhambi." Kuiweka vizuri hii ni kwamba anaongea kuhusu watu wote, kwa baadhi ya lugha inaweza kuwa sawa kama hii itatafsiriwa kwamba, "Kwa sababu watu wote wametenda dhambi, wana hatia, kwa hiyo wanastahili kifo."

**Mungu anapaswa kuwa na hasira**

Hii yaweza kutafsiriwa kwamba, "Itakuwa sawa kwa Mungu kuwa na hasira."

**Alimwaga hasira yake kwa**

Hii ni kusema kwamba, "alielekeza hasira yake kwa" au, "aliweka hasira yake yote juu" au "alimkasirikia tu."


**alipokea hukumu yenu**

Hii inaweza kutafsiriwa kwamba, "alihukumiwa badala yenu" au, "alihukumiwa kwa ajili ya dhambi yako." Kuiweka sawa ni kwamba hii hutumika kwa kila mtu, inaweza pia kutafsiriwa pia kwamba, "alihukumiwa kwa dhambi ya kila mtu."

**translationWords**

- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- hatia, mwenye hatia
- kifo, kufa, mfu

- Mungu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Msalaba
- Kupokea
- Kuadhibu, adhabu

**49:11**


Yesu hakuwai kufanya dhambi, lakini alikubali kuadhibiwa na kufa akiwa sadaka kamilifu kuondoa dhambi zako na dhambi za kila mtu katika ulimwengu. Kwa sababu Yesu alijitoa dhabihu mwenyewe. Mungu anaweza kusamehe dhambi yoyote, hata dhambi zenye kutisha.

**chukua**

Hii ni sawa na kusema, "ondoa adhabu ya" au, ondoa hukumu kwa." Dhabihu ya Yesu husababisha Mungu kutazama dhambi zetu kama kwamba hazijwahi kuwepo.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kuadhibu, adhabu
- kifo, kufa, mfu
- dhabihu, sadaka
- Mungu
- samehe, kusamehe

**49:12**

Matendo mema hayawezi kukuokoa. Hivyo hakuna chochote unachoweza kufanya kwa ajili ya mahusiano yako na Mungu. Yesu pekee awezae kuosha dhambi zako. Unapaswa kumuamini Yesu kuwa ni mwana wa Mungu, alikufa msalabani badala yako, na Mungu alimfufua tena na kumpa uhai.

**Matendo mema hayawezi kuwaokoa**

Hii inamaanisha kuwa, "Kufanya mambo mazuri hakuwezi kuwaokoa ninyi kutoka katika dhambi zetu" au "Hamuwezi kufanua kitu chochote chema cha kutosha ninyi wenyewe kuwaokoa kutoka katika hukumu yenu ya dhambi zenu."

**Mungu huosha dhambi zenu**

Sawa na, " huondoa dhambi zenu kikamilifu" au, "huchukua dhambi zenu na kuwafanya ninyi safi." Hii inazungumzia kuhusu Mungu kutakasa roho za watu kwa kuondoa kikamilifu dhambi zao. Haimaanishi kuoshwa kimwili.

**badala yenu**

Hii ni kusema kwamba, "kwa niaba yenu."

**alimrudisha katika uhai tena**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kwamba, "alimfanya kuwa hai tena."

**translationWords**

- [okoa, salama](#)
- [Mungu](#)



- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Kuamini, kuamini katika
- Mwana wa Mungu, Mwana
- kifo, kufa, mfu
- Msalaba
- inua, inuka
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

**49:13**

Mungu atamuokoa kila mtu amwaminiye Yesu na kumpokea kama Bwana wake. Lakini hatamuokoa mtu yeyote asiyemuamini yeye. Haijalishi wewe ni tajiri au maskini, mwanaume au mwanamke, mzee au kijana au mahali unapoishi. Mungu anakupenda wewe na anataka umuamini Yesu ili aweze kuwa na mahusiano ya karibu na wewe.

**anaweza kuwa na uhusiano wa karibu na ninyi**

Hii inaweza kutafsiriwa hivi, "ili kwamba uweze kuwa mtoto wake" au, "ili kwamba uweze kuwa rafiki yake" au, "ili uweze kumilikiwa naye."

**translationWords**

- Mungu
- okoa, salama
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kupokea
- bwana, mkuu
- upendo

**49:14**

Yesu anakualika umuamini yeye na uweze kubatizwa. Je unaamini Yesu ni Masiya, mwana wa pekee wa Mungu? Je unaamini wewe ni mwenye dhambi na unastahili Mungu akuhukumu? Je unaamini Yesu alikufa msalabani kuondoa mbali dhambi zako?

**amini katika yeye**

Hii inaweza kutafsiriwa kwamba, "amini katika yeye" au, au amini katika yeye ili akuokoe" au, "weka tumaini la maisha yako yote kwake."

**mmebatizwa**

Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, "muwe na mtu fulani wabatize" au, "muwaache wawabatize ninyi."

**amini kwamba**

Hii inaweza kutafsiriwa kwamba, "kiri kwamba" au, "kubali kwamba."

**chukua**


Hii ni sawa na kusema, "ondoa adhabu ya" au, ondoa hukumu kwa." Dhabihu ya Yesu husababisha Mungu kutazama dhambi zetu kama kwamba hazijwahi kuwepo.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kuamini, kuamini katika
- Batiza, ubatizo
- Kristo, Masihi

- Mwana wa Mungu, Mwana
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Mungu
- Kuadhibu, adhabu
- kifo, kufa, mfu
- Msalaba



**49:15**

Ikiwa unaamini katika Yesu na nini amefanya kwa ajili yako, wewe ni mkristo! Mungu amekutoa kwenye **ufalme wa giza wa Shetani** na amekuweka kwenye ufalme wa nuru wa Mungu. Mungu amechukua ukale wako, amechukua njia zako za kufanya dhambi na amekupa upya, njia ya ufanyaji haki kwa mambo.

**ufalme wa giza wa Shetani**

"Giza" imetumika hapa kurejea kwenye dhambi na kila kitu ambacho ni kiovu. Hii inaweza kutafsiriwa hivi. "Uovu wa Shetani, ambao ni kama giza hutawala juu ya watu."


**Ufalme wa Mwanga wa Mungu**

"Mwanga" hapa unarejea kwa utakatifu na uzuri wa Mungu. Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Haki ya Mungu, ambayo ni kama mwanga hutawala juu ya watu." Biblia mara kwa mara hulinganisha uovu na giza, na wema na mwanga.

**translationWords**

- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mkristo
- Mungu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- ufalme
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni

## 49:16




Ikiwa ni mkristo, Mungu ameshakusamehe dhambi zako kwa sababu ya kile alichofanya Yesu kwa ajili yako. Sasa, angalia Mungu anakuona kuwa rafiki wa karibu badala ya adui.

### **anakuchukulia kama**

Hii ni sawa na, "hukufikiri wewe kama umekuwa" au, "akuangalia wewe kama" au "akuita kama."

### **translationWords**

- Mkristo
- Mungu
- samehe, kusamehe
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

**49:17**

Ikiwa ni rafiki wa Mungu na mtumishi wa Yesu, Bwana, unatakiwa kutii kile Yesu alichokufundisha wewe. Hata kama, umkristo, unaweza **jaribiwa kutenda dhambi**. Lakini Mungu **ni mwaminifu** na anasema ikiwa utakiri dhambi zako, atakusamehe. Atakupa nguvu ya kupambana dhidi ya dhambi.

**jaribiwa kutenda dhambi**

Hii ni kusema, "kujaribiwa kutenda dhambi ingawa unajua dhambi ni mbaya."

**ni mwaminifu**

Katika muktadha huu ina maana kwamba Mungu, "hutunza ahadi zake."

**ungama dhambi zenu**

Hii inaweza kutafsiriwa hivi, "kiri kwa Mungu kile ulichokosa."

**Atawapa nguvu ya kupambana dhidi ya dhambi**

Maana yake ni, "Atawapa nguvu ya kiroho ya kukataa kufanya dhambi."

**translationWords**

- Mungu
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- bwana, mkuu
- tii, mtiifu, utiifu
- Mkristo

- kujaribu, jaribu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- mwaminifu, uaminifu
- samehe, kusamehe



## 49:18



Mungu anasema uombe, usome neno lake, umuabudu yeye na wakristo wengine, na kuwaambia wengine nini amefanya ndani yako. Mambo yote haya yanatusaidia kuwa na uwezo mpana wa ushirikiano na Mungu.

### kuwa na uhusiano wa kina zaidi naye

Hii pia inaweza kutafsiriwa kuwa, "kumpenda yeye zaidi" au, "kumjua yeye zaidi" au, "kuwa mwaminifu zaidi kwake."

Simulizi ya Biblia kutoka: Warumi 3:21-26; 5:1-11; Yohana 3:16; Marko 16:16; Wakolosai 1:13-14; 2Wakorintho 5:17-21; 1Yohana 1:5-10

### translationWords

- Mungu
- Kuomba, maombi
- Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko
- Abudu
- Mkristo

## 50. Yesu Anarudi

### 50:01



Kwa zaidi ya miaka 2,000, zaidi na zaidi watu ulimwenguni kote wamekuwa wakisikia habari njema kuhusu Yesu Masihi. **Kanisa limekuwa likikua.** Yesu aliahidi angerudi mwisho wa dunia. Ingawa bado hajarudi, ataitimiza ahadi yake.

### **Kanisa limekuwa likikua**


Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " Idadi ya watu kanisani duniani kote imekuwa ikiongezeka" au, " Idadi ya waamini katika Yesu imekuwa ikiongezeka."

### **Wakati wa mwisho wa dunia**

Sentensi hii inamaanisha, "kabla tu ya mwisho wa dunia kufika" au, "katika siku za mwisho za dunia hii."

### **translationWords**

- habari njema, injili
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Kristo, Masihi
- Kanisa
- Ahadi

**50:02**

Wakati tunamsubiri Yesu kurudi, Mungu anataka tuishi maisha ya utakatifu na ya kumweshimu. Tena anataka tuwaambie wengine habari za ufalme wake. Wakati Yesu alipokuwa akiishi duniani alisema, "Wanafunzi wangu watahubiri habari njema ya ufalme wa Mungu kwa watu wote ulimwenguni na ndipo mwisho utawadia."

**Mwisho utakuja**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "Mwisho wa dunia hii utakuja" au, "mwisho wa dunia hii utatokea" au, "dunia hii ya sasa itafikia mwisho"

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mungu
- takatifu, utakatifu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- mfuasi
- Kuhubiri
- habari njema, injili



**50:03**

Makundi ya watu wengi bado hawajasikia habari za Yesu. Kabla hajarudi mbinguni, Yesu aliwaambia wakristo kuitangaza habari njema kwa watu ambao kamwe hawajasikia. Alisema, "Enendeni na kufanya wanafunzi kwa watu wa makundi yote!" na "**Mashamba yamekomaa kwa mavuno!**"

**Kufanya wanafunzi**

Hii inamaana, wasaidie watu wafanyike wanafunzi wangu."

**Mashamba yamekomaa kwa mavuno**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "wako tayari kuletwa kwa Mungu kama vile mashamba yalivyotayari kwa mavuno" au, "wako tayari kukusanywa na kuletwa kwa Mungu kama vile mashamba ambayo mazao yake yameiva na kuwa tayari kukusanywa."

**Mashamba**

Katika maelezo , "Mashamba" yanawakilisha watu wa duniani.

**Kuiva**

"Iva" Hii inawakilisha jambo la kuwa tayari kumwamini Yesu.


**Mavuno**

"Mavuno" Hii inawakilisha kazi ya kuwaleta watu kwa Mungu kw kuwafundisha kuhusu Yesu.



## translationWords

- Kundi la watu, watu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mbingu, anga, mbinguni
- Mkristo
- habari njema, injili
- mfuasi

**50:04**

Pia Yesu alisema, "Mtumwa si mkuu juu ya bwana wake. Kama ilivyo mamlaka ya dunia hii inavyonichukia mimi, watawatesa na kuwaua kwa sababu yangu. Ingawaje katika dunia hii mtateswa, iweni na ujasiri kwa sababu nimemshinda Shetani, ambaye anatawala dunia hii. Ikiwa mtabaki waaminifu kwangu hadi mwisho, kisha Mungu atawaokoa!"

**Si mkuu kuliko**

Hii ni, "si wa muhimu kuliko" au, "katika hali hii, "si kutendewa vizuri zaidi kuliko."

**Kwa sababu yangu**

Hii ni, " kwasababu mnanitii mimi" au, kwa sababu mnawafundisha watu kuhusu mimi" au, " kwasababu ninyi ni watu wa miliki yangu."

**Katika dunia hii**

Hii ninaweza pia kutafsiriwa kama, "katika wakati huu wa kuishi."

**Baki mwaminifu kwangu**

Hii ni, "Endelea kuwa mtiifu kwangu."

**Hadi mwisho**

Hii ni, "mpaka mwisho wa maisha yako."

## Atawaokoa

Hii inamaanisha wokovu wa ki roho zaidi zsana kuliko kuokolewa ki mwili kutokakatika hali ya kudhurika. imekwisha semwa kwamba waamini wengi watauwawa au kuteswa.

## translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mtumishi, mtumwa, utumwa
- bwana, mkuu
- teseka, kuteseka
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- mwaminifu, uaminifu
- okoa, salama

**50:05**

Yesu aliwaambia wanafunzi wake simlizi juu ya namna itakavyotokea kwa watu wakati dunia itakapokwisha. Alisema, "Mtu alipanda mbegu njema katika shamba lake. Wakati alipokuwa amelala, adui yake alikuja na kupanda mbegu za magugu sambamba na ngano na kisha akaenda zake."

**Mbegu njema**

Mbegu hizi zilikuwa ni mbegu za ngano. Kama aina hii ya mbegu haijulikani katika lugha ya eneo lako ni vema kutumia neno la jumla lenye kumaanisha "mbegu." Kama hakuna neno la jumla, itakuwa lazima kuchagua aina ya mbegu inayo fahamika na kusema, kwa mfano, "mbegu njema kama mpunga."

**Mbegu za magugu**

Mbegu za magugu ambazo zilipandwa zingelikua na kuwa kama nyasi marefu lakini zisingeweza kuliwa. zilikuwa hazifai.

**Ngano**

Hii ni, "mbegu za ngano." Ngano ni aina ya mbegu ambazo hukua na kuwa kama nyasi ndefu. Zina mbegu ambazo watu huzitumia kwa chakula.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- mfuasi
- wema, uzuri



**50:06**

"Wakati mimea ilipoota, watumishi wa bwana walisema, 'Bwana, ulipanda mbegu njema katika shamba lile, Je, kwanini kuna magugu ndani yake?' Bwana akajibu, 'Lazima adui ameyapanda.'"

**Adui atakuwa lazima amepanda**

Kama ikiwezekana tafsiri jambo hili kwa njia ambayo itaonesha msemaji hakuona hili likitendeka.

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- bwana, mkuu
- wema, uzuri

**50:07**

"Watumishi wakamjibu bwana wao, 'Je, tunaweza kuyang'oa magugu?' Bwana akasema, 'Hapana. Mkifanya hivyo, mtang'oa na ngano pamoja. Subirini hadi mavuno kisha mkusanye magugu katika matita na kuyateketeza kwa moto, bali muilete ngano gharani mwangu.'"

**Mtang'oa na ngano pamoja**

Hii ni kwamba, "mnaweza kung'oa ngano kwa bahati mbaya pia." Itakuwa jambo gumu kutofautisha ngano ambayo haijakomaa na magugu, na kung'oa magugu bila kung'oa ngano.

**Hadi mavuno**

Hii ni, "Hadi wakati ambao ngano itakuwa tayari kuvunwa" au, "hadi pale ambapo ngano imekomaa vya kutosha kuvunwa."

**Ngano**

Hii ni, "mbegu za ngano zilizo vunwa."

**Galani**

Hii inamaanisha nyumba ambayo mbegu za ngano zinapovunwa zinahifadhiwa na kutunzwa. inaweza pia kuitwa gala.

**translationWords**

- mtumishi, mtumwa, utumwa
- bwana, mkuu

**50:08**

Wanafunzi hawakufahamu maana ya simulizi, hivyo walimwomba Yesu awafafanulie. Yesu alisema, "Mtu aliyepanda mbegu njema anawakilisha Masihi. Na shamba linawakilisha ulimwengu. Mbegu njema inawakilisha watu wa ufalme wa Mungu."


**Watu wa ufalme wa Mungu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, " watu wanaoishi chini ya mamlaka ya Mungu" au, "watu ambao wametii mamlaka ya utawala wa Mungu" au, "watu ambao wataishi pamoja na Mungu katika ufalme wake."

**translationWords**

- mfuasi
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- wema, uzuri
- Kristo, Masihi
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni



**50:09**

"Magugu yanawakilisha watu wa milki ya mwovu. Adui aliyepanda magugu anamwakilisha **Ibilisi**. Mavuno yanawakilisha mwisho wa dunia, na wavunaji wanawakilisha Malaika wa Mungu."

**Watu wa milikiya mwovu**

Hii ni, Ambao wanamtii mwovu" au, "ambao wanatawaliwa na mwovu."

**Mwovu**

Hili ni jina lingine la shetani. Linaweza kutafsiriwa kama,"shetani" ingawa jina mwovu linaeleza hasa tabia yake.

**Ibilisi**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " shetani"

**Inawakilisha mwisho wa dunia**

Hii ni, " inawakilisha jambo ambalo litatokea kwa watu mwisho wa dunia."

**Wavunaji**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " watua ambao wanavuna mbegu zilizo komaa au zilizo iva" au, "wafanyakazi ambao wanakusanya mbegu zilizo iva."

**translationWords**

• baya, ovu, uovu



- Shetani, ibilisi, yule muovu
- Mungu
- Malaika, Malaika mkuu

**50:10**

Wakati wa mwisho wa dunia, malaika watawakusanya pamoja watu wote walio wa milki ya Ibilisi na kuwatupa katika moto, mahali watakapolia na kusaga meno katika mateso ya kutisha. Kisha wenye haki watang'aa kama jua katika ufalme wa Mungu Baba yao."

**Wa miliki ya ibilisi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "anaye mtii shetani, au, "anaye tawaliwa na shetani," hawa ni wale wasio mwamini Yesu ila wakifuata njia mbaya za ibilisi.

**Moto wa hasira**

Huu ni moto ambao ni mkali sana, "moto unao unguza," au, " moto mkubwa.

**Wenye haki**

Hawa ni wale watu ambao ni miliki ya Masihi

**Wata ng'aa kama jua**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, " hali ya kuwa katika utukufu kama jua" au, " kuonesha wema usio na waa kama jua linavyo oneshwa mwanga mkali."

**translationWords**

- Malaika, Malaika mkuu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- teseka, kuteseka
- Adili, uadilifu

- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba

**50:11**

Pia Yesu aliwaambia kwamba angerudi duniani kabla ya mwisho wa dunia. Atarudi kwa namna ilie ile alivyoondoka, kwa hali hiyo, atakuwa na mwili na atakuja na mawingu katika anga. Wakati Yesu akirudi, kila mkristo aliye kufa atafufuka kutoka wafu na kukutana naye mawinguni.

**aliondoka**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, "aliiacha dunia" au, "aliondoka kurudi mbinguni."

**Atakuja katika mawingu katika anga**

Hii ni, " Mawingu katika anga yatamzunguka wakati atakapo kuja" au, "Mawingu ya angani yata mbeba."

**Wakati Yesu atakaporudi**

Hii ni, " Wakati Yesu atakapo rudi duniani."

**Kutana naye angani**

Hii ni, "Kuungana naye katika anga." wale ambao wameamini watapaa juu kuwa karibu na Yesu wakati atakapokuwa angani.

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Mkristo
- kifo, kufa, mfu
- inua, inuka



**50:12**

Kisha wakristo watakaosalia hai watanyakuliwa juu katika mawingu na kuungana pamoja na wakristo waliofufuka kutoka wafu. Wote watakuwa pamoja na Yesu huko. Baada ya hapo, Yesu atakaa na watu wake katika amani timilifu na umoja wa milele.

**Salia hai**

Hii ni, "ambao watakuwa hai wakati Yesu atakaporudi,"

**translationWords**

- Mkristo
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- inua, inuka
- kifo, kufa, mfu
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

## 50:13



Yesu aliahidi kuwapa taji kwa kila mtu amwaminiye yeye. Watakaa na kutawala pamoja na Mungu katika amani timilifu ya milele.

### Taji

Taji hii inawakilisha zawadi yetu kwa kumwamini Yesu na kumtumikia katika maisha haya

### Timilifu

Hii, "iliyo kamilifu" au "Jumla"

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Ahadi
- Kuamini, kuamini katika
- maisha, uhai, kuishi, kuwa hai
- Mungu
- Amani

## 50:14



Lakini Mungu atamhukumu kila mmoja ambaye hakumwamini Yesu. Atawatupa wote jehanamu, mahali watakapolia na kusaga meno katika mateso ya milele. Moto usioweza kuzimika utaendelea kuwaanguza, na funza hawatakoma kuwatafuna.

### **Kulia na kusaga meno katika mateso**

Tazama tafsiri ya simulizi ya 50 -10

### **translationWords**

- Mungu
- hukumu
- Kuamini, kuamini katika
- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Jehanamu, ziwa la moto



## 50:15



Wakati Yesu akirudi, atamwangamiza kabisa Shetani na ufalme wake. Atamtupa Shetani Jehanamu ambapo atachomwa milele, pamoja na kila mmoja aliyechagua kumfuata yeye badala ya kumtii Mungu.

### Ufalme wake

Hiiinaweza pia kutafsiriwa kama, "utawala wa kiovu wa shetani kwa watu" au, "mambo yote maovu afanyayo ana watu waovu anao wadhibiti."

### Badala ya

Hii ni, "badala ya."

### translationWords

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- Shetani, ibilisi, yule muovu
- ufalme
- Jehanamu, ziwa la moto
- tii, mtiifu, utiifu
- Mungu



**50:16**

Kwa sababu Adamu na Eva walimwasi Mungu na kuleta dhambi humu ulimwenguni, Mungu aliilaani na kukusudia kuingamiza. Lakini kuna siku Mungu ataumba mbingu mpya na nchi mpya itakayokuwa kamilifu.

**Kuleta dhambi humu**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "alisababisha dhambi kuingia."

**Mbingu mpya**

Hii inaweza pia kutafsiriwa kama, mbingu mpya, au, nchi mpya," Inarejea katika mfumo mpya wa nyota na kila kitu katika anga.

**Nchi mpya**

Nchi hii ya sasa ambayo tunakaa itatoweshwa nakuwekwa nyingine mpya iliyoboreshwa.

**translationWords**

- Adamu
- Hawa
- totii, mkaidi, kutotii
- Mungu
- dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi
- Laana, kulaaniwa
- mbingu, anga, mbinguni

**50:17**

Yesu na watu wake wataishi katika nchi mpya, na atatawala milele juu ya kila kitu kilichopo. **Atafuta kila chozi** na hapatakuwa tena na mateso, huzuni, kilio, uovu, maumivu, au kifo. Yesu atatawala katika ufalme wake kwa haki na amani, na atakuwa na watu wake milele.

**Atafuta kila chozi**

Hii inaweza kutafsiriwa kama, "kukomesha huzuni zote" au, "kufanya matatizo yote kuisha" au, " kuondoa huzuni zote watu walizo nazo."

**Hakutakuwa na mateso, huzuni, kilio, uovu, maumivu, au, kifo."**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "watu hawatapata mateso tena, huzuni, kilio, mambo mauvu, kuhisi maumivu, au, kufa."

**Atatawala katika ufalme wake kwa amani na haki**

Hii pia inaweza kutafsiriwa kama, "utawala wa haki juu ya watu wake, kwa njia ambayo inaleta amani."

Simulizi ya Biblia Kutoka: Mathayo 24:14; 28:18; Yohana 15:20; 16:33; Ufunuo 2:10; Mathayo 13:24-30, 36-42; 1Wathesolanike 4:13-5:11; Yakobo 1:12; Mathayo 22:13; Ufunuo 20:10, 21:1-22:21

**translationWords**

- Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu
- teseka, kuteseka
- baya, ovu, uovu
- kifo, kufa, mfu
- ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni
- Amani

- haki, adilifu



# **translationWords**

**Toleo. 7.3**



## Abrahamu, Abram

### Ufafanuzi

Abramu alikuwa Mkalidayo toka mji wa Urialiyechaguliwa na Mungu kuwa baba wa Waisraeli. Mungu alibadilisha jina lake na kuwa "Abrahamu."

- Jina "Abramu" lina maana ya "baba aliyeinuliwa."
- "Abrahamu" lina maana ya "baba wa wengi."
- Mungu alimuahidi Abrahamu kuwa atakuwa na uzao mwingi, na atakuwa taifa kubwa.
- Abrahamu alimuaminina kumtii Mungu. Mungu alimuongoza Abrahamu toka Kaldayo mpaka nchi ya Kaanani.
- Alipokuwa akiishi katika nchi ya Kaanani, walipokuwa wazee sana Abrahamu na mke wake Sara walipata mtoto, Isaka.

(Rudi tena: 04:04; 04:05; 04:06; 04:07; 04:08; 04:09; 05:01; 05:02; 05:03; 05:04; 05:05; 05:06; 05:07; 05:08; 05:09; 05:10; 06:01; 06:02; 06:04; 07:10; 08:15; 09:13; 09:14; 14:12; 19:10; 21:02; 45:03; 48:07; 48:08)

## Abudu

### Ufafanuzi

"Kuabudu" ni kuheshimu, kusifu na kumtii mtu hasa Mungu.

- Neno hili lina maana ya kawaida ya kuinama kumnyenyekea mtu.
- Tunamwabudu Mungu tunapo muheshimu, kumsifu na kumtii yeye.
- Waisraeli walimwabudu Mungu kwa kutoa sadaka ya wanyama kwenye madhabahu.
- Watu wengine wanaabudu miungu ya uongo.

(Rudi tena: 13:04; 13:05; 13:10; 13:12; 14:03; 16:01; 16:03; 16:11; 16:16; 17:06; 18:02; 18:03; 18:09; 18:12; 18:13; 19:02; 19:05; 19:16; 20:01; 20:05; 20:13; 23:10; 25:06; 25:07; 26:02; 26:07; 26:09; 31:08; 41:08; 47:01; 49:18)

# Adamu

## Ufafanuzi

Adamu alikuwa binadamu wa kwanza aliyeumbwa na Mungu. Yeye na mke wake Hawa walitengenezwa kwa mfano wa Mungu.

- Mungu alitengeneza Adamu toka kwenye mavumbi na kumpulizia pumzi ya uhai.
- Jina la Adamu linafanana naneno la Kiebrania linalomaanisha "udongo mwekundu"
- Jina "Adamu" ni sawa na neno kwenye Agano la kale linalomaanisha "mwanadamu" au binadamu."
- Watu wote ni uzao wa Adamu na Hawa.
- Adamu na Hawa walimuasi Mungu. Mungu alijitenga nao hivyo dhambi na mauti vikaingia duniani.

(Rudi tena: [01:10](#); [01:11](#); [01:12](#); [01:13](#); [01:14](#); [02:01](#); [02:07](#); [02:11](#); [02:12](#); [21:01](#); [48:01](#); [48:02](#); [48:03](#); [49:08](#); [50:16](#))

## Adili, uadilifu

### Ufafanuzi

Adili au uadilifu ni wema wa Mungu, haki, uaminifu na upendo. Kwa sababu Mungu ni wa adili hukemea dhambi.

- Maneno haya pia hutumika kumuelezea mtu anayemtii Mungu na mwenye maadili mema. Kwa sababu wote wametenda dhambi Mungu pekee ndiye mwenye adili.
- Mfano wa watu waliokuwa waadilifu kwenye Biblia walikuwa Nuhu, Ayubu, Abrahamu, Zakaria na Elizabeti.
- Watu wakimwamini Mungu awaokoe, Mungu anawasafisha na kuwafanya kuwa waadilifu katika uadilifu wa Yesu.

(Rudi tena: [03:02](#); [04:08](#); [17:02](#); [23:01](#); [27:03](#); [34:10](#); [50:10](#))



# Agano

## Ufafanuzi

Agano ni makubaliano kati ya pande mbili kuwa upande mmoja au zote unapaswa kutekeleza.

- Makubaliano haya yanaweza kuwa ya mmoja mmoja, kati ya makundi ya watu au kati ya Mungu na watu.
- Watu wanapoweka agano kati yao wanaahidi kufanya jambpo fulani ambalo wanapaswa wafanye.
- Mfano wa maagano ya wanadamu ni maagano ya ndoa, makubaliano ya biashara na mikataba kati ya nchi.
- Katika Biblia Mungu ameweka maagano mbalimbali na watu wake.
- Katika baadhi ya maagano Mungu aliahidi kutekeleza bila masharti yoyote. Kwa mfano Mungu alipoweka agano na mwanadamu kuwa hataiangamiza duinia kwa mafuriko.
- Katika maagano mengine Mungu ameahidi kutekeleza kama watu watamtii yeye.

(Rudi tena: [04:09](#); [05:03](#); [05:04](#); [06:04](#); [07:10](#); [08:15](#); [13:02](#); [13:04](#); [14:01](#); [15:13](#); [20:01](#); [21:05](#); [21:14](#); [38:05](#); [48:11](#))

# Ahabu

## Ufafanuzi

Ahabu alikuwa mfalme muovu sana katika ufalme wa Kaskazini mwa Israeli toka 875-854 BC.

- Mfalme Ahabu aliwashawishi watu wa Israeli kuabudu miungu.
- Nabii Eliya alimkabidi Ahabu na kumwambiakuwa kutakuwa na ukame mkubwa kwa miaka mitatu na nusu kwa dhambi ambazo Ahabu alisababisha wana wa Israeli wafanye.

Ahabu na mkewe walifanya mambo mengi maovu ikiwemu kutumia nguvu zao kuwaua watu wasio na hatia.

(Rudi tena: [19:02](#); [19:03](#); [19:05](#); [19:13](#))

# Ahadi

## Ufafanuzi

Ahadi ni hali ya kuahidi kufanya jambo fulani. Mtu anapokuahidi kitu inamaana yupo tayari kufanya jambo hilo.

- Biblia imeandika ahadi nyingi ambazo Mungu aliahidi watu wake.
- Ahadi ni sehemu muhimu ya makubaliano kama maagano.
- Ahadi mara nyingi huambatana na kiapo cha kuthibitisha kuwa itafanyika.

(Rudi tena: 03:15; 03:16; 04:08; 05:04; 05:10; 06:04; 07:10; 08:15; 09:13; 13:07; 13:10; 14:12; 14:14; 15:01; 15:07; 15:13; 17:08; 17:14; 18:04; 19:18; 20:10; 21:01; 21:03; 21:04; 21:05; 43:08; 48:04; 50:01; 50:13)

# Amani

## Ufafanuzi

Amani ni kitendo cha kutokuwa na migogoro au hofu. Mtu mwenye amani anahisi shwari na ana uhakika wa kuwa salama.

- Amani pia inaweza kuelezewa kama kipindi ambacho kundi la watu au nchi hawapo katika vita na watu wengine. Watu hawa wanasemwa kuwa na "mahusiano ya amani.
- "Kutengeneza amani" na watu au kundi la watu linamaanisha kuchukua hatua ya kusababisha ugonvi uishe.
- "mtengeneza amani" ni mtu anayefanya kitu au kusema kitu ili kuwashawishi watu waishi kwa amani na watu wengine.
- Kuwa na amani na watu wengine inamaanisha kuwa katika hali ya kutogombana na watu hao.
- Uhusiano mzuri kati ya Mungu na wanadamu hutokea pale ambapo Mungu aliwaokoa watu toka kwenye dhambi zao. Hii inaitwa kuwa na amani na Mungu.
- Salamu "neema na amani" ilitumiwa na mitume katika barua zao kwa waamini aka baraka.
- Amani pia inaweza kuonesha kuwa katika mahusiano mazuri na watu wengine au na Mungu.

(Rudi tena: [07:10](#); [14:03](#); [15:06](#); [15:07](#); [15:12](#); [16:03](#); [21:13](#); [23:07](#); [32:16](#); [42:06](#); [48:14](#); [50:13](#); [50:17](#))



## Amri kumi

### Ufafanuzi

"Amri Kumi" zilikuwa amri ambazo Mungu alimpa Musa Mlima Sinai wakati Waisraeli waliishi jangwani wakiwa njiani kwenda nchi ya Kanani. Mungu aliandika hizi amri kwenye mawe makubwa mawili.

- Mungu aliwapa Waisraeli amri nyingi za kutii, lakini Amri Kumi zilikuwa maalumu kuwasaidia Waisraeli kumpenda na kumuabudu Mungu na kupenda watu wengine.
- Hizi amri pia zilikuwa sehemu ya agano la Mungu na watu wake. Kwa kumtii Mungu na aliyo waamuru kufanya, watu wa Israeli walionyesha kuwa wana mpenda Mungu na kuwa ni wao.
- Amri kwenye mawe zilihifadhiwa katika Agano lililo kuwa pa takatifu zaidi mwa maskani na baadae, hekalu.

(Rudi tena: [13:07](#); [13:13](#); [13:15](#))

## Ashuru, Waashuru, Dola ya Waashuru

### Ufafanuzi

Ashuru lilikuwa taifa lenye nguvu kipindi ambacho wana wa Israeli walikuwa wakiishi Kaanani. Ngome ya waashuru ilikuwa ni kundi la mataifa waliotawaliwa na mfalme wa Ashuru.

- Taifa la Ashuru lilikuwa sehemu ambayo kwa sasa ni nchi ya Iraq.
- Mwaka 722 BC Waashuru waliuteka ufalme wa Israeli na kuwalazimisha Waisraeli wengi kwenda Ashuru.
- Waisraeli waliobaki waliwaoa wageni walioletwa na Waashuru toka Samaria. Kizazi cha watu hao waliotokana na mwingiliano huo wa kuoana waliitwa Wasamaria.

(Rudi tena: [20:02](#); [20:03](#); [20:04](#); [20:06](#))

## Baali

### Ufafanuzi

"Baali" maana yake "bwana" lilikuwa jina la mungu wa kwanza wa uongo aliyekuwa akiabudiwa na Wakanaani.

- Pia kulikuwa na miungu mingine ya uongo yenye jina "Baali, kama vile "Baali wa Peori." Wakati mwingine miungu hii kwa pamoja inarejerewa kama "Mabaali."
- Baadhi ya watu walikuwa na majina yenye jina "Baali" ndani yake.
- Ibada ya Baali ilihusisha matendo maovu kama vile kutoa watoto kama sadaka na ukahaba.
- Kwa nyakati tofauti katika historia, Waisraeli pia walijiingiza katika ibada ya Baali, kwa kufuata mfano wa mataifa ya kipagani yaliyowazunguka.
- Wakati wa utawala wa Mfalme Ahabu, Eliya nabii wa Mungu aliweka jaribio la kuwathibitishia watu kwamba Baali si mungu wa kweli na kwamba Yahwe pekee ndiye aliyekuwa Mungu wa kweli. Matokeo yake, manabii wa Baali waliangamizwa na watu wakaanza kumwabudu Yahwe tena.

(Rudi tena: [19:02](#); [19:05](#); [19:06](#); [19:07](#); [19:08](#); [19:12](#))

## Bahari ya shamu

### Ufafanuzi

Bahari ya shamu ni jina la la bahari iliyokuwa Misri na Uarabbuni. Sasa inaitwa bahari ya Shamu.

- Bahari ya shamu ni ndefu na nyembamba. Ni kubwa zaidi ya ziwa au mto lakini ndogo kuliko bahari.
- Waisraeli walivuka bahari ya shamu walipotoka Misri. Mungu aliwafanyia muujiza na kusababisha maji kugawanyika na watu wapakita.
- Nchi ya Kanaani ilikuwa kaskazini mwa bahari hii.

(Rudi tena: [12:04](#); [12:05](#); [13:01](#))



## Barnaba

### Ufafanuzi

Barnaba ni miongoni mwa wakristo wa mwanzo aliyeishi wakati wa mitume.

- Barnaba alikuwa wa kabila ya Lawi na alikuwa mwenyeji wa kisiwa cha Mileto.
- Wakati Sauli (Paulo) anakuwa mkristo, Barnaba aliwasihi waamini wangine kumpokea kama mwamini mwenzao.
- Barnaba na Paulo walisafiri kwa pamoja katika miji mbalimbali ili kuhubiri injili.
- Jina lake lilikuwa Yusufu, lakini alitwa "Barnaba," jina linalomaanisha "mwana wa faraja."

(Rudi tena: [46:08](#); [46:09](#); [46:10](#))

## Bathsheba

### Ufafanuzi

Bathsheba alikuwa mke wa Uria, askari katika jeshi la Daudi. Baada ya kifo cha Uria, akawa mke wa Daudi, na mama wa Sulemani.

- Daudi alizini na Bethsheba akiwa mke wa Uria.
- Bathsheba alipokuwa mjamzito kwa Daudi, Daudi alisababisha Uria kuuawa vitani.
- Kisha Daudi alimwoa Bethsheba na akazaa mwana.
- Mungu alimwadhibu Daudi kwa dhambi yake kwa kufanya mtoto afe siku chache baada ya kuzaliwa.
- Baadaye, Bethsheba alizaa mwana mwingine, Sulemani, aliyekuja kuwa mfalme baada ya Daudi.

(Rudi tena: [17:10](#); [17:11](#); [17:12](#); [17:13](#); [17:14](#))

## Batiza, ubatizo

### Ufafanuzi

Katika Agano Jipya, maneno "batiza" na "ubatizo" kwa kawaida utaratibu wa kuoshwa kwa Mkiristo kwa kutumia maji kuonesha kwamba ameoshwa kutoka katika dhambi na ameungana na Kristo.

- Mbali na ubatizo wa maji, Biblia inazungumzia "kubatizwa kwa Roho Mtakatifu" na "kubatizwa kwa moto."
- Neno "ubatizo" katika Biblia limetumika pia kuonesha hali ya kupitia matiso makubwa.

### Maono ya Kutafasiri

- Wakristo wanamaoni tofauti jinsi mtu anavyopaswa kubatizwa kwa maji. Pengine inafaa zaidi kutafasiri neno hili kwa njia ya jumla inayoruhusu njia mbalimbali ya kutumia maji.
- Kwa kutegemea mazingira, neno "batiza" laweza kutafasiriwa kama "kutakasa," "kumimina juu," "kuzamisha"

(Rudi tena: [24:03](#); [24:06](#); [24:07](#); [24:08](#); [24:09](#); [25:01](#); [36:01](#); [42:10](#); [43:11](#); [45:11](#); [45:12](#); [46:05](#); [47:02](#); [49:14](#))

## **baya, ovu, uovu**

### **Ufafanuzi**

Msemu "baya" na "uovu" yote ina maana ya chochote ambacho kinapingana na tabia takatifu na mapenzi ya Mungu.

Wakati "ubaya" unaweza kuelezea tabia ya mtu, "ovu" unaweza kumaanisha zaidi ya tabia ya mtu. Hata hivyo, misemo yote inafanana maana.

Msemu "uovu" una maana ya hali ambayo watu hufanya maovu.

Matokeo ya uovu yanaonyweshwa kwa uwazi kwa jinsi watu wanavyotenda vibaya wengine kwa kuwaua, kuiba, kusengenya au kuwa katili na kutokuwa mwema.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, misemo "uovu" na "ovu" inaweza kutafsiriwa kama "ubaya" au "dhambi" au "kinyume na maadili".

Njia zingine za kutafsiri hii zinaweza kujumuisha "isiyo nzuri" au "sio takatifu" au "sio adilifu".

Hakikisha maneno au misemo ambayo inatumika kutafsiri misemo hii kutosha muktadha ambayo ni kawaida katika lugha husika.

(**Rudi tena:** [01:11](#); [02:03](#); [02:04](#); [02:12](#); [03:15](#); [04:02](#); [08:12](#); [17:13](#); [18:11](#); [18:13](#); [19:02](#); [19:16](#); [29:08](#); [45:02](#); [50:09](#); [50:17](#))



## Bethlehemu

### Ufafanuzi

Bethlehemu ulikuwa mji mdogo katika nchi ya Israeli, karibu na mji wa Yerusalemu. Ulijulikana pia kama "Efratha," ambalo pengine ndilo jina lake la awali.

- Bethlehemu umekuwa ukiitwa mji wa "Daudi," kwa kuwa Daudi alizaliwa pale.
- Nabii Mika alitabiri kuwa Masiya angekuja kutokea katika "Bethlehemu ya Efratha."
- Ili kutimiza unabii huo, Yesu alizaliwa Bethlehemu, miaka mingi baadaye.
- Jina "Bethlehemu" maana yake ni "nyumba ya mikate" au "nyumba ya chakula."

(Rudi tena: [17:02](#); [21:09](#); [23:04](#); [23:05](#); [23:06](#); [23:09](#))

## Bikira

### Ufafanuzi

Bikira ni mwanamke ambaye hajawahi kuwa na mahusiano ya ngono.

- Nabii Isaya alisema kuwa Masihi atazaliwa na bikira.
- Mariamu alikuwa Bikira alipokuwa na mimba ya Yesu. Yesu hakuwa na baba wa kibinadamu.
- Lugha nyingine zaweza kuwa na neno zuri badala ya neno bikira.

(Rudi tena: [21:09](#); [22:04](#); [22:05](#))

## Busara, hekima

### Ufafanuzi

Busara inamuelezea mtu anayeelewa jambo la haki na mambo ya maadili na akayafanya. Hekima ni uelewa na kutenda yaliyo sahihi na maadili ya haki.

- Kuwa na busara inajumuisha uwezo wa kufanya maamuzi mazuri hasa kuchagua kufanya yanayompendeza Mungu.
- Katika Biblia "busara za dunia" inamaanisha kitu ambacho watu wa dunia wanafikiri ni burasa lakini ni upuuzi.
- Watu huwa na busara wanapomsikiliza Mungu na kunyeyekea kutii mapenzi yake.
- Mtu mwenye busara ataonesha matunda ya roho mtakatifu kwenye maisha yake kama furaha, upendo na uvumilivu.

(Rudi tena: [02:05](#); [18:01](#); [23:09](#); [45:01](#))

## bwana, mkuu

### Ufafanuzi

Neno "bwana" linamaanisha mtu anayemiliki na mwenye mamlaka juu ya watu wengine.

Neno hili wakati mwingine linatafsiriwa kama "mkuu" wakati wakumuita Yesu au wakati wakumaanisha mtu anayemiliki watumwa.

(Rudi tena: 23:06; 25:05; 25:07; 26:03; 27:02; 29:01; 31:05; 31:07; 37:03; 37:04; 37:05; 37:06; 43:09; 45:05; 46:02; 46:04; 47:03; 47:11; 49:13; 49:17; 50:04; 50:06; 50:07)



## damu

### Ufafanuzi

Neno "damu" linamaanisha kimiminika chekundu kinachotoka katika ngozi ya mtu panapokuwa na jeraha au kidonda. Damu inaleta viini lische vya uhai katika mwili wote wa mtu.

- Damu inaashiria uhai na inapomwagwa, inaashiria kifo.
- Watu walipotoa sadaka kwa Mungu, walimwua mnyama na kumimina damu yake juu ya madhabahu. Hii inaashiria kutolewa kwa uhai wa mnyama kulipa dhambi za watu.
- Kupitia kifo chake msalabani, Damu ya Yesu hutakasa watu kutokana na dhambi zao na kulipa kwa ajili ya adhabu wanayostahili kwa ajili ya dhambi zao.
- Kifungu "mwili na damu" kinarejerea wanadamu.
- Kifungu "mwili wake na damu yake" inarejerea kwa watu wanaohusiana kibaolojia.

### Maoni ya Kutafasiri

- Neno hili litumika kwa kulingana na neno lifaalo katika lugha lengwa.
- Kielezi "mwili na damu" chaweza kutafasiriwa kama "watu" au "wanadamu".
- Kwa kutegemea mazingira, kifungu "mwili wangu na damu yangu mwenyewe" yaweza kutafasiriwa kama "familia yangu" au "ndugu zangu" au "watu wangu."
- Ikiwa kuna kionyeshi katika lugha lengwa kinachotumika kwa maana hii, kifungu hicho kitumike kutafasiri "mwili na damu"

(Rudi tena: [11:03](#); [11:05](#); [13:09](#); [38:05](#); [38:12](#); [48:09](#); [48:10](#))

## Daudi

### Ufafanuzi

Daudi alikuwa mfalme wa pili wa Israeli na alimpenda na kumtumikia Mungu. Alikuwa mwandishi mkuu wa kitabu cha Zaburi.

Daudi alipokuwa mvulana mdogo akichunga kondoo wa familia yake, Mungu alimchagua kuwa mfalme afuataye wa Israeli.

Daudi alikuwa mpiganaji hodari na aliongoza jeshi la Israeli katika vita dhidi ya maadui zake. Kumshinda kwake Goliati na Wafilisti kunajulikana sana.

Mfalme Sauli alijaribu kumuua Daudi, lakini Mungu alimlinda, na kumfanya awe mfalme baada ya kifo cha Sauli.

Daudi alitenda dhambi mbaya sana, lakini alitubu na Mungu alimsamehe.

Yesu, Masihi, anaitwa "Mwana wa Daudi" kwa sababu ni uzao wa Mfalme Daudi.

(Rudi tena: [17:02](#); [17:03](#); [17:04](#); [17:05](#); [17:06](#); [17:07](#); [17:08](#); [17:09](#); [17:10](#); [17:11](#); [17:12](#); [17:13](#); [17:14](#); [18:01](#); [18:02](#); [18:13](#); [21:04](#); [21:08](#); [23:04](#); [48:14](#))

## dhabihu, sadaka

### Ufafanuzi

Katika Biblia, maneno "dhabihu" na "sadaka" ya husu zawadi maalumu anazopewa Mungu kama kitendo cha kumuabudu. Watu pia walitoa sadaka kwa miungu ya uongo.

- Neno "sadaka" la husu chochote kinacho tolewa au kupewa. Neno "dhabihu" la husu kitu kinacho tolewa au kufanywa kwa gharama kubwa kwa mtoaji.
- Sadaka kwa Mungu zilikuwa vitu maalumu alizo waamuru Waisraeli kutoa ili kuonyesha upendo na utii kwake.
- Maneno ya sadaka tofauti, kama "sadaka ya kuteketeza" na "sadaka ya amani," ili hashiria aina gani ya sadaka ilitolewa.
- Dhabihu kwa Mungu kulihusisha kuuu mnyama.
- Dhabihu peke yake ya Yesu, Mwana mkamilifu, asiye na dhambi, wa Mungu, anaweza kutakasa watu na dhambi. Mnyama hakuweza kufanya hivyo.
- Mfano wa msemu "jitoeni kama dhabihu hai" ina maana, "ishi maisha yako kwa kumtii Mungu, kuacha kila kitu ili kuweza kumtumikia.

(Rudi tena: [03:06](#); [03:14](#); [05:06](#); [05:07](#); [05:08](#); [05:09](#); [13:09](#); [13:12](#); [16:06](#); [17:06](#); [18:02](#); [18:12](#); [18:13](#); [19:07](#); [21:07](#); [38:04](#); [48:06](#); [48:08](#); [49:11](#))

## **dhambi,yenye dhambi, mwenye dhambi, kufanya dhambi**

### **Ufafanuzi**

Neno "dhambi" la husu matendo, mawazo, na maneno yaliyo kinyume dhidi ya mapenzi ya Mungu na Sheria. Dhambi yaweza maanisha kutofanya kitu Mungu alichu tuambia tufanye.

- Dhambi ya jumuisa chochote tunacho fanya kisicho mtii au mpendeza Mungu, ata vitu watu wasivyo vijua.
- Mawazo na matendo yanayo kosea mapenzi ya Mungu yanaitwa "yenye dhambi"
- Kwasababu Adamu alitenda dhambi, wanadamu wote wanazaliwa na hasili ya dhambi inayo watawala.
- "mwenye dhambi" ni mtu anaye tenda dhambi, hivyo kila mwanadamu ni mwenye dhambi.
- Wakati mwingine neno "mwenye dhambi" lilitumika na watu wa dini kama Mafarisayo kueleza watu wasio shika sheria.

(Rudi tena: 02:01; 03:15; 04:02; 08:05; 10:08; 10:09; 13:09; 13:10; 13:12; 14:09; 16:17; 17:07; 17:09; 17:13; 17:14; 18:09; 20:01; 20:10; 21:05; 21:07; 21:13; 21:14; 22:07; 23:02; 24:03; 24:06; 24:07; 25:01; 29:01; 34:07; 34:09; 35:01; 35:02; 35:04; 35:08; 35:12; 38:05; 38:12; 42:08; 43:11; 44:05; 45:05; 48:01; 48:02; 48:03; 48:05; 48:06; 48:08; 48:10; 49:05; 49:08; 49:09; 49:10; 49:11; 49:12; 49:14; 49:16; 49:17; 50:16)



## **dhihaki**

### **Ufafanuzi**

Neno kudhihaki ni kumtania mtu, kwa namna mbaya.

- Kudhihaki mara kadha kuna husisha muingiza maneno ya watu au matendo kwa kusudi kuwaaibisha au kuonyesha kuchukizwa nao.
- Wanajeshi wa Kirumi walidhihaki Yesu walipo mvalisha joho na kujifanya kumheshimu kama mfalme.
- Kikundi cha vijana walimdhihaki Elisha walipo muita jina, wakimtania kichwa chake cha upara.

(Rudi tena: [39:05](#); [39:12](#); [40:01](#); [40:04](#); [40:05](#))

# Eliya

## Ufafanuzi

Eliya alikuwa mmoja wa manabii muhimu sana wa Yahwe. Eliya alitabiri katika wakati wa tawala za wafalme kadhaa wa Israeli au Yuda, akiwemo Mfalme Ahabu.

Mungu alifanya miujiza mingi kupitia Eliya, ikiwemo kumfufua mvulana mfu kurudi katika uhai.

Eliya alimkaripia Mfalme Ahabu kwa kuabudu mungu wa uongo Baali.

Aliwapa changamoto manabii wa Baali katika mtihani ambao ulithibitisha ya kwamba Yahwe ni Mungu mmoja wa kweli.

Katika mwisho wa maisha ya Eliya, Mungu alimchukua kimuujiza juu mbinguni angali bado yu hai.

Miaka mia moja baadaye, Eliya, pamoja na Musa, walijitokeza na Yesu juu ya mlima na waliongea pamoja juu ya kurudi, kuteseka na kufa kwa Yesu Yerusalemu.

**(Rudi tena: [19:02](#); [19:03](#); [19:04](#); [19:05](#); [19:06](#); [19:07](#); [19:10](#); [19:12](#); [19:13](#); [19:14](#); [26:05](#); [36:03](#); [36:04](#))**

## Esau

### Ufafanuzi

Esau alikuwa mmoja wa mapacha wana wa Isaka na Rebeka. Alikuwa mtoto wa kwanza kuzaliwa. Pacha ndugu yake alikuwa Yakobo.

Esau aliuza haki yake ya mzawa wa kwanza kwa kaka yake Yakobo kwa kubadilishana na bakuri la chakula.

Kwa kuwa Esau alizaliwa kwanza, baba yake Isaka alitakuwa kumpatia baraka maalumu. Lakini Yakobo alimdanganya Isaka kumpatia hiyo baraka badala yake. Mara ya kwanza Esau alikuwa na hasira sana hadi alitaka kumuua Yakobo, lakini baadaye alimsamehe.

Esau alikuwa na watoto wengi na wajukuu, na vizazi hivi viliunda kuni kubwa la watu walioishi katika nchi ya Kaanani.

(Rudi tena: [06:07](#); [07:01](#); [07:02](#); [07:03](#); [07:04](#); [07:05](#); [07:06](#); [07:09](#); [07:10](#))

## Farao, mfalme wa Misri.

### Ufafanuzi

Hapo nyakati za kale wafalme waliotawala nchi ya Misri waliitwa Mafarao.

- Kwa pamoja zaidi ya wafalme 300 walitawala Misri kwa miaka zaidi ya 2,000.
- Wafalme hawa wa Misri walikuwa na nguvu na utajiri.
- Baadhi ya Mafarao hawa wametajwa kwenye Biblia.
- Mara nyingi cheo hiki kimetajwa kama jina na sio cheo.

(Rudi tena: 08:06; 08:07; 08:08; 09:02; 09:04; 09:07; 09:10; 09:13; 09:15; 10:01; 10:02; 10:03; 10:04; 10:05; 10:06; 10:07; 10:08; 10:09; 10:12; 11:01; 11:07; 11:08; 12:03; 12:04)



## Filipi

### Ufafanuzi

Filipi ulikuwa mji muhimu na koloni la Rumi lililokuwa Makedonia kaskazini mwa Ugiriki ya kale.

- Paulo na Sila walisafiri kuhubiri kuhusu Yesu kwa watu wa huko.
- Wakiwa Filipi Paulo na Sila walikamatwa, lakini Mungu aliwaweka huru kwa muujiza.
- Katika agano jipya kitabu cha Wafilipi ni barua ya mtume Paulo aliyowaandikia Wakristo katika kanisa la Filipi.
- Kumbuka kuwa huu ni mji tofauti na Kaisaria Failipi ambayo ilikuwa kaskazini mashariki mwa Israeli karibu na mlima Hermoni.

(Rudi tena: [47:01](#); [47:13](#))

# funga

## Ufafanuzi

Msemo "kufunga" una maana ya kuacha kula chakula kwa kipindi fulani, kama vile siku moja au zaidi. Mara nyingi inajumulisha kutokunywa.

Kufunga kunaweza kusaidia watu kumlenga Mungu na kuomba bila kutolewa mawazo kwa kuandaa chakula na kula.

Yesu aliwalaani viongozi wa dini wa Kiyahudi kwa kufunga kwa sababu ambazo sio sahihi. Walifunga ili kwamba wengine wafikiri kuwa wao ni watakatifu.

Mara nyingi watu walifunga kwa sababu walikuwa na huzuni sana au majonzi juu ya jambo.

Kitenzi cha "kufunga" kinaweza kutafsiriwa kama "kujizuia kula" au "kutokula".

Nomino ya "funga" inaweza kutafsiriwa kama "muda wa kutokula" au "muda wa kujizuia na chakula"

(Rudi tena: [25:01](#); [34:08](#); [46:10](#))

## furaha, mwenye furaha

### Ufafanuzi

Furaha ni hisia ya kupendezwa au kuridhika inayotoka kwa Mungu. Maana inayokaribiana, "mwenye furaha" inaelezea mtu anayejisikia vizuri sana na mwenye furaha nyingi.

Mtu anasikia furaha anapokua anahisi kuwa anachopitia ni chema sana. Mungu ndiye anayegawa furaha ya kweli kwa watu. Kuwa na furaha hakutegemei hali nzuri. Mungu anaweza kuwapa watu furaha hata kama vitu vigumu kabisa vinatokea katika maisha yao. Sehemu zingine zinaelezwa kama za furaha, kama nyumba na miji. Hii inamaanisha kuwa watu waiishio humo ni wenye furaha.

(Rudi tena: [33:07](#); [34:04](#); [41:07](#))

## Galilaya, Mgalilaya

### Ufafanuzi

Galilaya ni eneo la kaskazini ya Israeli, kaskazini ya Samaria. "Mgalilaya" alikuwa mtu ambaye aliishi Galilaya.

Galilaya, Samaria, na Yudea ilikuwa miji mitatu ya msingi ya Israeli wakati wa Agano Jipya.

Galilaya imepakana upande wa mashariki na ziwa kubwa liitwalo "Ziwa la Galilaya".

Yesu alikua na kuishi katika mji wa Nazareti Galilaya.

Miujiza mingi na mafundisho ya Yesu yalifanyika katika eneo la Galilaya.

(Rudi tena: [21:10](#); [26:01](#); [26:08](#); [39:06](#); [41:08](#))



## Gari

### Ufafanuzi

Zamani za kale magari yalikuwa mepesi, yenye matairi mawili yalioendeshwa na farasi.

- Watu walikaa au kusimama katika magari, waliyatumia katika vita au safari.
- Katika vita jeshi lenye magari lilikuwa na faida ya kuwa na kasi na uwezo juu ya jeshi ambalo halikuwa na magari.
- Katika nyakati za Wamisri na Rumi walijulikana sana kwa kutumia farasi na magari.

(Rudi tena: [12:10](#); [45:07](#); [45:08](#); [45:11](#))

## Gibeoni. Wagibeoni

### Ufafanuzi

Gibeoni ilikuwa mji ambao ulikuwa kama kilomita 13 kaskazini magharibi mwa Yerusalemu. Watu walioishi Gibeoni walikuwa Wagibeoni.

Wagibeoni waliposikia jinsi Waisraeli wameangamiza miji ya Yeriko na Ai, waliogopa.

Kwa hiyo Wagibeoni walikuja kwa viongozi wa Israeli Gilgali na kuvunga kuwa watu kutoka nchi ya mbali.

Viongozi wa Israeli walidanganywa na kufanya makubaliano na Wagibeoni ya kwamba watawalinda na kutowaangamiza.

(Rudi tena: [15:06](#); [15:07](#); [15:08](#))

## Gideoni

### Ufafanuzi

Gideoni alikuwa mwanamume wa Kiisraeli ambaye aliinuliwa na Mungu kuwakomboa Waisraeli kutoka kwa adui zao.

Katika kipindi ambacho Gideoni aliishi, kundi la watu lijulikanalo kama Midiani waliendelea kuwashambulia Waisraeli na kuangamiza mazao yao.

Ingawa Gideoni aliogopa, Mungu alimtumia kuwaongoza Waisraeli kupigana dhidi ya Midiani na kuwashinda.

Gideoni pia alimtii Mungu kwa kuangusha madhabahu chini ya miungu wa uongo wa Baali na Ashera.

Hakuwaongoza tu watu katika kuwashinda adui zao lakini pia aliwatia moyo kutii na kumwabudu Yahwe, Mungu mmoja wa ukweli.

(Rudi tena: [16:05](#); [16:06](#); [16:07](#); [16:08](#); [16:09](#); [16:10](#); [16:11](#); [16:12](#); [16:13](#); [16:15](#); [16:16](#))

## habari njema, injili

### Ufafanuzi

Msemo "injili" una maana ya "habari njema" na una maana ya ujumbe au tangazo ambalo linawaambia watu jambo ambalo lina manufaa kwako na kuwapa furaha.

Katika Biblia, msemo huu humaanisha ujumbe kuhusu wokovu wa Mungu kwa watu kupitia sadaka ya Yesu msalabani.

Katika Biblia nyingi za Kiingereza, "habari njema" mara nyingi hutafsiriwa kama "injili" na pia hutumika katika misemo kama vile "injili ya Yesu Kristo" au "injili ya Mungu" na "injili ya ufalme".

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia tofauti za kutafsiri msemo huu zinaweza kujumuisha "jumbe mzuri" au "tangazo zuri" au "ujumbe wa Mungu wa wokovu" au "mambo mazuri Mungu anayofundisha kuhusu Yesu".

Kulingana na muktadha, njia za kutafsiri msemo "habari njema ya" inaweza kujumuisha "ujumbe/havbari njema" au "ujumbe mzuri kutoka" au "mambo mazuri Mungu husema juu ya" au "kile Mungu anasema kuhusu jinsi anavyookoa watu".

(Rudi tena: [26:03](#); [46:10](#); [47:01](#); [47:11](#); [47:13](#); [47:14](#); [49:06](#); [50:01](#); [50:02](#); [50:03](#))



## Hajiri

### Ufafanuzi

Hajiri alikuwa ni mwanamke wa Kimisri alikuwa mtumwa wa Sara. Sara alimtoa Hajiri kwa Ibrahimu ili aweze kuzaa naye, baada ya kuona kuwa yeye (Sara) hana uwezo wa kuzaa . Hajiri alipata mimba na akamzalia Ibrahim mwana, Ishmaeli. Mungu aliangalia taabu ya Hajiri katika jangwa na akaahidi kuubariki uzao wa Hajiri.

(Rudi tena: [05:01](#); [05:02](#))

## **haki, adilifu**

### **Ufafanuzi**

Maneno haya yanamaanisha kuwatendea watu vyema kulingana na sheria za Mungu. Sheria za binadamu zinazo oneshwa kiwango cha Mungu cha tabia sawa kwa watu wengine.

Kuwa wa "haki" ni kutenda ya haki na mema kwa mtu mwingine. Pia inaashiria uaminifu na msimamo kufanya kilicho adilifu machoni pa Mungu. Kutenda kwa "haki" inamaanisha kuwatendea watu kwa njia iliyo sawa, nzuri na ya kufaa kulingana na sheria za Mungu. Kupokea "haki" inamaanisha kutendewa vyema chini ya sheria, aidha kulindwa kwa sheria au kuadhibiwa kwa kuvunja sheria. Wakati mwingine neno "haki" lina maana pana ya "utakatifu" au "kufuata sheria za Mungu."

(Rudi tena: [17:09](#); [18:13](#); [19:16](#); [48:14](#); [50:17](#))

## Haruni

### Ufafanuzi

Haruni alikuwa kaka yake na Musa. Mungu alimchagua Haruni kuwa kuhani mkuu wa kwanza wa watu wa Israeli. Haruni alimsaidia Musa kuzungumza na Farao kuhusu kuwaachia huru wana wa Israeli. Wakati wana wa Israeli wanasafiri jangwani, Haruni alitenda dhambi kwa kutengeneza sanamu ili watu waiabudu. Pia Mungu alimchagua Haruni na uzao wake kuwa makuhani.

(Rudi tena: [09:15](#); [10:01](#); [10:05](#); [10:08](#); [11:08](#); [13:09](#); [13:11](#); [13:12](#); [14:07](#))

## hatia, mwenye hatia

### Ufafanuzi

Msemo "hatia" una maana ya ukweli wa kufanya dhambi au kutenda kosa.

Kuwa na "hatia" ina maana ya kuwa umefanya kitu kiouvu kimaadili, yaani, kutomtii Mungu.

Kinyume cha "mwenye hatia" ni "asiye na hatia".

Mapendekezo ya Tafsiri

Baadhi ya lugha zinaweza kutafsiri "hatia" kama "uzito wa dhambi" au "hesabu ya dhambi".

Njia za kutafsiri "kuwa na hatia" inaweza kujumuisha neno au msemo ambayo ina maana ya "kuwa katika kosa" au "kuwa umefanya jambo ovu kimaadili" au "kuwa umefanya dhambi".

(Rudi tena: [19:16](#); [39:02](#); [39:11](#); [40:04](#); [49:10](#))



## Hawa

### Ufafanuzi

Hili lilikuwa jina la mwanamke wa kwanza. Jina lake linamaanisha "uhai" au "kuishi".

Mungu alimuumba Hawa kutoka kwa ubavu ambao aliuchukua kutoka kwa Adamu.

Hawa aliumbwa kuwa "msaidizi" wa Adamu. Alikuwa kando ya Adamu kumsaidia katika kazi ambayo Mungu aliwapa kufanya.

Hawa alijaribiwa na Shetani (kwa mfano wa nyoka) na alikuwa wa kwanza kufanya dhambi kwa kula tunda ambalo Mungu aliwaambia kutokula.

(Rudi tena: [02:11](#); [02:12](#); [21:01](#); [48:01](#); [48:02](#); [48:03](#); [48:04](#); [49:08](#); [50:16](#))

## hekalu

### Ufafanuzi

Hekalu lilikuwa ni jengo lililo zungukwa na kuta za nyuani ambapo Waisraeli walikuja kuombaa na kutoa dhabihu kwa Mungu. Lilikuwa Mlima Moria katika mji wa Yerusalemu.

- Mara nyingi neno "hekalu" lina husu jengo zima, pamoja na nyuani iliyo zunguka jengo lote. Wakati mwingine lina husu tu jengo.
- Jengo la hekalu lilikuwa na vyumba viwili, Pa Takatifu na Pa Takatifu pa Pa Takatifu.
- Mungu alitaja hekalu kama sehemu yake ya kuishi.
- Wakati wa utawala wa Mfalme Sulemani alijenga Hekalu, ambalo lilikuwa sehemu ya kudumu ya kuabudu Yerusalemu.
- Katika Agano Jipya, neno "hakalu la Roho Mtakatifu" linatumika kuelezea waamini wa Yeu, kwasababu ya Roho Mtakatifu kuishi ndani yao.

(Rudi tena: [17:06](#); [17:07](#); [18:02](#); [18:09](#); [20:07](#); [20:12](#); [20:13](#); [25:04](#); [27:07](#); [34:06](#); [40:07](#); [44:01](#); [44:03](#); [44:06](#))

## hema la kukutania

### Ufafanuzi

Neno "hema la kukutania" la husu hema ambalo lilikuwa la muda mfupi Mungu alipo kutana na Musa kabla ya maskani kujengwa.

- Hema la kukutania lilikuwa nje ya kambi ya Waisraeli.
- Wakati Musa alipoenda kwenye hema ya kukutania kukutana na Mungu, nguzo ya wingu ilisimama katika mwingilio wa hema kama ishara ya uwepo wa Mungu hapo.
- Baada ya Waisraeli kujenga maskani, hema ya muda mfupi haiku hitajika tena na neno "hema la kukutania" lilitumika kueleza maskani.

(Rudi tena: [13:08](#); [13:09](#); [14:08](#); [17:06](#); [18:02](#))

## **hukumu**

### **Ufafanuzi**

Neno "hukumu" mara nyingi humaanisha kufanya maamuzi kama jambo liko sawa kimaadili au kama haliko sawa.

"Hukumu ya Mungu" mara nyingi humaanisha uamuzi wake kulaani kitu au mtu muovu. Hukumu ya Mungu mara nyingi huhusisha kuwaadhibu watu kwa dhambi zao. Neno "hukumu" inaweza pia kumaanisha "kulaani." Mungu anawaagiza watu wake kutowahukumu wengine kwa naamna hii. Maana nyingine ni "uamuzi kati ya" au "kuhukumu kati ya", yaani kuchagua ni mtu gani yuko sahihi katika ugomvi kati yao. Katika mazingira mengine, "hukumu" za Mungu ni yale aliyeamua ni mema na yenye haki. Zinafanana na amri, sheria na maagizo yake. "Hukumu" inaweza kumaanisha uwezo wa busara wa kufanya maamuzi. Mtu anayekosa "hukumu" hana hekima kufanya maamuzi ya busara.

(Rudi tena: [18:01](#); [19:16](#); [21:08](#); [39:04](#); [50:14](#))



# imani

## Ufafanuzi

Kwa ujumla, msembo "imani" una maana ya imani, au matumaini ndani ya mtu au jambo.

"Kuwa na imani" na mtu ni kuamini ya kwamba kile anachosema na kufanya ni kweli na kuaminika.

"Kuwa na imani na Yesu" ina maana ya kuamini mafundisho yote ya Mungu kuhusu Yesu. Ina maana haswa ya kwamba watu wanamuamini Yesu na sadaka yake kuwasafisha kutoka kwa dhambi zao na kuwakomboa kutoka na adhabu wanayostahili kwa sababu ya dhambi yao.

Imani ya kweli kwa Yesu itamsababisha mtu kuzaa matunda mazuri ya kiroho au tabia kwa sababu ya Roho Mtakatifu anayeishi ndani yake.

Mara kwa mara "imani" kwa ujumla ina maana ya mafundisho yote kuhusu Yesu, yaani kama msembo, "ukweli wa imani".

Katika muktadha kama wa "tunza imani" au "telekeza imani", msembo "imani" una maana ya hali ya kuamini mafundisho yote kuhusu Yesu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika baadhi ya muktadha, "imani" inaweza kutafsiriwa kama "imani" au "hatia" au "kujiamini" au "kuamini".

Kwa baadhi ya lugha misemo hii inaweza kutafsiriwa kutumia aina za kitenzi cha "imani".

(Rudi tena: [05:06](#); [31:07](#); [32:16](#); [38:09](#))

## imani, aminifu,

### Ufafanuzi

Neno "imani" la eleza kuamini kwamba kitu au mtu ni wa kweli au tegemeo. Mtu "mwaminifu" na weza kuwa tegemevu kufanya kitu na kusema kilicho sawa na kweli.

- Imani ni ina maana ya karibu na imani ya Mungu. Kama tuna mwamini mtu, tuna imani kwamba mtu huyo atafanya alichio ahidi.
- Kuwa na imani kwa mtu pia ina maana ya kumtegemea huyo mtu.
- Kumuamini Yesu ina maana ya kukubali kuwa yeye ni Mungu na kwamba alikufa kwenye msalaba kulipa dhambi zetu, na kumtegemea kutuokoa.
- "msemu aminifu" ni kitu kilicho semwa na kinaweza hesabiwa kuwa kweli.

(Rudi tena: [14:15](#); [17:02](#); [34:06](#))

## inua, inuka

### Ufafanuzi

Inua, inua juu inamaana ya kuinua kitu juu au kukuweka juu.

- Kuinua juu ni kusababisha kitu kionekane. Pia yaweza kuwa kumteua mtu afanye kitu fulani.
- "Inua" ina maan ya pekee katika "kuinuka toka kwenye kifo" ikiwa inamaanisha kusababisha mtu aliyekufa aishi tena.
- Mara nyingine "kuinua juu" inamaana ya "kupandisha" kitu au mtu.
- Mtu anapoinuka kwenda mahali fulani inamaana kuwa amenyanyuka na kwenda.
- Yesu alitabiri kuwa atainuka toka kwa wafu . Baada ya siku tatu malaika akasema "ameinuka"

(Rudi tena: [21:14](#); [41:01](#); [41:05](#); [42:03](#); [42:07](#); [43:07](#); [44:05](#); [44:08](#); [48:04](#); [49:02](#); [49:12](#); [50:11](#); [50:12](#))

# Isaka

## Ufafanuzi

Isaka alikuwa mwana pekee wa Abrahamu na Sara. Mungu aliwaahidi kuwapa mwana wa kiume ingiwa walikuwa wazee sana.

Jina "Isaka" linamaanisha "kicheko." Mungu alipomuambia Abrahamu kuwa Sara atazaa mwana wa kiume, Abrahamu alicheka kwa sababu wote walikuwa wazee sana. Baada ya muda, Sara pia alicheka aliposikia taarifa hii. Lakini Mungu alitimiza ahadi yake na Isaka alizaliwa kwa Abrahamu na Sara katika uzee wao. Mungu alimuambia Abrahamu kuwa agano alilofanya na Abrahamu itakuwa pia ya Isaka na vizazi vyake milele. Wakati Isaka alikuwa kijana, Mungu alijaribu imani ya Abrahamu kwa kumuamuru kumtoa Isaka kama sadaka. Mwana wa Isaka, Yakobo, alikuwa na wana kumi na mbili ambao uzao wao baadaye ukawa makabila kumi na mbili ya taifa la Israeli.

(Rudi tena: 05:04; 05:05; 05:06; 05:07; 05:08; 05:09; 06:01; 06:03; 06:04; 06:05; 07:01; 07:03; 07:04; 07:06; 07:10; 08:15; 09:13; 09:14; 14:12; 19:10; 48:08)



# Isaya

## Ufafanuzi

Isaya alikuwa nabii wa Mungu aliyetabiri wakati wa utawala wa wafalme wanne wa Yuda: Uzia, Yothamu, Ahazi, na Hezekia.

Aliishi Yerusalemu wakati Waashuri walipokuwa wakivamia mji, wakati wa utawala wa Hezekia. Kitabu cha Agano la Kale cha Isaya ni moja ya vitabu vikuu vya Biblia. Isaya aliandika unabii mwingi ulitokea wakati wa uhai wake. Isaya anajulikana zaidi kwa unabii alioandika kumhusu Masihi uliotimia miaka 700 baadaye wakati Yesu alipoishi duniani. Yesu na wanafunzi wake walinukuu utabiri wa Isaya kuwafundisha watu kuhusu Masihi.

(Rudi tena: [21:09](#); [21:10](#); [21:11](#); [21:12](#); [26:02](#); [45:08](#); [45:09](#))

## Ishmaeli

### Ufafanuzi

Ishmaeli alikuwa mwana wa Abrahamu na mtumwa wa Kimisri Hagai. Kuna wana kadhaa pia katika Agano la Kale wanaoitwa Ishmaeli.

Jina "Ishmaeli" linamaanisha, "Mungu husikia." Mungu aliahidi kumbariki mwana wa Abrahamu, Ishmaeli, lakini hakuwa mwana ambaye Mungu aliye ahidi kuweka agano lake naye. Mungu alimlinda Hagai na Ishmaeli walipotumwa jangwani. Wakati Ishmaeli alipokuwa akiishi katika jangwa la Parani, alimuoa mwanamke wa Misri. Ishmaeli mwana wa Nethania alikuwa afisa wa jeshi kutoka Yuda aliyeongoza kundi la wanaume kumua gavana aliyeteuliwa na mfalme wa Kibabeli, Nebukadreza. Pia kuna wanaume wengine wanne walioitwa Ishmaeli katika Agano la Kale.

(Rudi tena: [05:02](#); [05:04](#))

## Israeli, Waisraeli, taifa la Israeli

### Ufafanuzi

Neno "Israeli" ni jina ambalo Mungu alimpa Yakobo. Linamaanisha, "anashindana na Mungu."

Uzao wa Yakobo walijulikana kama "watu wa Israeli," "taifa la Israeli" au "Waisraeli." Mungu aliunda agano lake na watu wa Israeli. Walikuwa watu wake aliowachagua. Taifa la Israeli liliundwa na makabila kumi na mbili. Mara baada ya mfalme Sulemani kufa, Israeli iligawanyika katika falme mbili: ufalme wa kusini, uliitwa "Yuda" na ufalme wa kaskazini, uliitwa "Israeli."

(Rudi tena: 08:15; 09:01; 09:02; 09:03; 09:04; 09:05; 09:07; 09:08; 09:13; 10:01; 10:03; 10:04; 10:05; 10:06; 10:07; 10:09; 10:11; 10:12; 11:01; 11:03; 11:04; 11:05; 11:08; 12:01; 12:03; 12:04; 12:05; 12:06; 12:08; 12:10; 12:11; 12:12; 12:13; 12:14; 13:01; 13:02; 13:08; 13:15; 14:01; 14:03; 14:04; 14:10; 14:11; 14:12; 14:14; 14:15; 15:01; 15:02; 15:04; 15:05; 15:06; 15:07; 15:08; 15:09; 15:10; 15:11; 15:12; 15:13; 16:01; 16:02; 16:04; 16:05; 16:08; 16:09; 16:10; 16:14; 16:16; 16:17; 17:01; 17:02; 17:03; 17:05; 17:06; 17:07; 17:08; 18:01; 18:04; 18:05; 18:07; 18:08; 18:11; 19:01; 19:10; 20:03; 20:04; 20:11; 21:05; 21:07; 26:05; 26:06; 43:06; 48:09; 48:11; 48:14)

## Jehanamu, ziwa la moto

### Ufafanuzi

Jehanamu ni sehemu ya mwisho iliyo na maumivu na mateso yasiyokoma, mahali ambapo Mungu atamhukumu kila mmoja anayemwasi Yeye na kuukataa mpango wake wa kuwaokoa kupitia kwa sadaka ya Yesu. Pia inarejelewa kama 'ziwa la moto'. Jehanamu au Kuzimu kunatajwa kama sehemu ya moto na mateso makali. Shetani na roho chafu zinazomfuata zitatupwa katika Jehanamu kwa ajili ya hukumu ya milele. Watu wasioamini sadaka ya Yesu kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, na wasiomtumaini Yeye, watahukumiwa Jehanamu milele

Mapendekezo ya tafsiri Maneno haya yanapaswa kutafsiriwa tofauti tofauti kwasababu yanatokea tofauti katika muktadaha tofauti. Katika baadhi ya lugha haziwezi kutumia neno 'ziwa' kwa sababu kwao ziwa ni 'maji' Neno Jehanamu laweza kutafsiriwa kama 'sehemu ya mateso au sehemu yenye giza na maumivu' Maneno 'ziwa la moto' yanaweza pia kutafsiriwa kama 'bahari ya moto' au 'moto mkubwa.'

(Rudi tena: [50:14](#); [50:15](#))



## **kaburi**

### **Ufafanuzi**

Neno "kaburi" ni sehemu watu wanapo weka mwili wa mtu aliye kufa.

- Wayahudi wakati mwingine walitumia mapango ya asili na makaburi, na wakati mwingine walichimba mapango katika miamba ya vilima.
- Wakati wa Agano Jipya, ilikuwa ni kawaida kuviringisha, jiwe kubwa mbele ya uwazi wa kaburi ilikufunga.
- Neno "kaburi" utumika kwa mfano wa kumaanisha hali ya kufa au sehemu nafsi za watu waliyo kufa zipo.

(Rudi tena: [32:04](#); [37:06](#); [37:07](#); [40:09](#); [41:01](#); [41:02](#); [41:03](#); [41:04](#); [41:05](#))

## Kalebu

### Ufafanuzi

Kalebu alikuwa mmoja wa wapelelezi wa Israeli ambao walitumwa na Munsu kuipeleleza nchi ya Kanaani.

- Yeye na Yoshua waliwaambia watu wamwamini Mungu ili awasaidie wawashinde Wakanaani.
- Yoshua na Kalebu walikuwa watu pekee katika uzao wao waliokubaliwa kuingia katika nchi ya ahadi ya Kanaani.
- Kalebu aliomba kuwa nchi ya Hebroni apewe yeye na familia yake. Alijua kuwa Mungu atamsaidia kuwashinda watu wanaoishi huko.

(Rudi tena: [14:06](#); [14:07](#); [14:08](#))

## Kanaani, Mkanaani

### Ufafanuzi

Kanaani alikuwa mtoto wa Hamu, ambaye alikuwa moja ya watoto wa Nuhu. Wakanaani walikuwa vizazi vya Kanaani.

- Neno "Kanaani" au "nchi ya Kanaani" pia limerejelewa kwenye eneo la nchi kati ya Mto Yordani na Bahari ya Meditrenia. Iliendelea kusini mpaka kwenye mpaka wa Misri na kaskazini ya mpaka wa Siria.
- Hii nchi ilikuwa makazi kwa Wakanani, na makundi ya watu wengine wengi.
- Mungu aliahidi kumpa Ibrahim na uzo wake nchi ya Kanaani, Waisraeli.

(Rudi tena: 04:05; 04:06; 04:09; 05:01; 05:03; 07:08; 07:10; 08:10; 09:13; 14:01; 14:03; 14:04; 14:05; 14:06; 14:09; 14:10; 15:01; 15:05; 15:06; 15:07; 15:11; 16:01; 20:05)

# Kanisa

## Ufafanuzi

Katika agano jipya kanisa ni kundi la watu wanaomwamini Yesu wanaokutana na kuomba pamoja na kusikiliza mafundisho ya Mungu.

- Yaweza kuwa na maana ya watu walioitwa kukutana pamoja kwa ajili ya jambo la muhimu.
- Neno hili linapotumika linamaanisha waamini wote popote ni mwili wa Kristo, Baadhi ya Biblia zimeandika kwa kuanza na herufi kubwa ("Kanisa") Kutofautisha na kanisa la kawaida.
- Mara nyingine waamini wa mji fulani hukutana katika nyumba ya mtu. Makanisa haya yalipewa majina ya miji mfano "Kanisa la Efeso."
- Katika Biblia kanisa halimaanishi jengo.

(Rudi tena: [45:01](#); [46:09](#); [46:10](#); [47:13](#); [47:14](#); [50:01](#))

## Kiburi

### Ufafanuzi

Kiburi ni hali ya mtu kujifikiria mwenyewe na kudhani kuwa yeye ni bora kuliko wengine.

- Mtu mwenye kiburi huwa hakubali makosa yake. Sio mnyenyekevu.
- Kiburi kinaweza kusababisha usimtii Mungu katika njia nyingine.
- Pia kiburi kinaweza kuelezwa katika mtazamo chanya kwa mfano "kujivunia" kwa kitu ambacho mtu fulani amefanikiwa au "kujivunia" watoto wako.
- Mtu anaweza kujivunia kwa alichokifanya bila kuwa na kiburi juu ya hilo.

(Rudi tena: [04:02](#); [34:10](#))



## kifo, kufa, mfu

### Ufafanuzi

Msemo huu unatumika kumaanisha vyote kifo cha kimwili na kiroho. Kimwili, ina maana ya mwili wa kihalisia wa mtu kukoma kuishi. Kiroho, ina maana ya wenye dhambi kutengwa na Mungu mtakatifu kwa sababu ya dhambi yao.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kutafsiri msemo huu, ni vyema kutumia neno la kila siku au usemi ambao una maana ya kifo katika lugha husika.

Katika baadhi ya lugha, "kufa" inaweza kuelezwa kama "kutokuishi". Msemo "kufa" unaweza kutafsiriwa kama "kutokuwa hai" au "kutokuwa na uhai wowote" au "kutokuishi".

Lugha nyingi zinatumia msemo wa tamathali kuelezea kifo, kama "kuondoka" kwa Kiingereza. Ila katika Biblia ni bora kutumia msemo wa moja kwa moja kwa ajili ya kifo ambao unatumika kila siku katika lugha.

Katika Biblia, uhai na kifo wa kimwili mara kwa mara hulinganishwa na uhai na kifo cha kiroho. Ni muhimu katika tafsiri kutumia neno moja au msemo kwa ajili ya kifo cha kimwili na kifo cha kiroho.

Katika baadhi ya lugha inaweza kuwa wazi zaidi kusema, "kifo cha kiroho" ambapo muktadha unahitaji maana hiyo. Watafsiri wengine wanaweza kuhisi ni bora kusema, "kifo cha kimwili" katika muktadha ambapo unalinganishwa na kifo cha kiroho.

Msemo wa "wafu" ni kivumishi chenye maana ya watu waliokufa. Baadhi ya lugha zitatafsiri hili kama, "watu waliokufa" au "watu ambao wamekufa"

**(Rudi tena: 01:11; 02:03; 02:04; 02:11; 21:12; 21:13; 21:14; 35:09; 35:13; 36:03; 36:07; 37:01; 37:03; 37:04; 37:05; 37:06; 37:07; 38:10; 39:05; 40:07; 40:08; 41:01; 41:04; 41:05; 42:07; 43:07; 44:05; 45:05; 48:01; 48:02; 48:08; 49:02; 49:10; 49:11; 49:12; 49:14; 50:11; 50:12; 50:17)**

## **komboa, mkombozi, ukombozi**

### **Ufafanuzi**

"Kukomboza" mtu ina maana ya kumukokoa mtu huyo. Msmo "mkombozi" una maana ya mtu ambaye hukomboza au kuweka huru watu kutoka utumwani, mateso au hatari zingine. Msemu "ukombozi" una maana ya kile kinachotokea pale mtu anapookoa au kuweka watu huru kutoka utumwani, matesoni, au hatari zingine.

Katika Agano la Kale, Mungu aliwaweka wakombozi kuwalinda Waisraeli kwa kuwaongoza katika vita dhidi ya makundi ya watu wengine waliokuja kuwashambulia.

Wakombozi hawa pia walijulikana kama "waamuzi" na kitabu cha Agano la Kale cha Waamuzi kimeweka kumbukumbu ya kipindi katika historia ambapo waamuzi hawa walikuwa wakitawala Israeli.

Mungu pia anaitwa "mkombozi". Kote katika historia ya Israeli, aliwakomboza au kuwaokoa watu wake kutoka kwa maadui zao.

Msemu "kutoa kwa" ina maana tofauti kabisa ya kumtoa mtu kwa adui, kama pale Yuda alipomtoa Yesu kwa viongozi wa Kiyahudi.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika muktadha wa kusaidia watu kutoroka kutoka kwa adui zao, msemu "komboa" unaweza kutafsiriwa kama "okoa" au "kuweka huru" au "nusuru".

Pale inapomaanisha kukabidhi mtu kwa adui, "kukabidhi" inaweza kutafsiriwa kama "kusaliti" au "kumpatia" au "kutoa kwa".

Neno "mkombozi" linaweza kutafsiriwa kama, "mkombozi" au "mweka huru".

Pale ambapo msemu "mkombozi" una maana ya waamuzi waliongoza Israeli, inaweza pia kutafsiriwa kama "bosi" au "mwamuzi" au "kiongozi"

**(Rudi tena: [16:03](#); [16:16](#); [16:17](#))**

## **kondoo, kondoo dume, kondoo jike**

### **Ufafanuzi**

"kondoo" ni mnyama wa saizi ya kati wa miguu minne mwenye manyoya mwili mzima.

- Waisraeli mara kadhaa walitumia kondoo kwa dhabihu, hususani dume na kondoo mdogo.
- Watu ula nyama ya kondoo na kutumia manyoya yake kufanya nguo na vitu vingine.
- Kondoo ni wa piole, dhahifu, na waoga. Wanashawishika haraka kupotea. Wanaitaji mchungaji kuwaongoza, kuwalinda, na kuwapa chakula, maji, na hifadhi.
- Katika Biblia, watu wanalinganishwa na kondoo waliyo na Mungu kama mchungaji wao.

(Rudi tena: [09:12](#); [16:09](#); [17:02](#); [30:03](#); [38:08](#))

## Kristo, Masihi

### Ufafanuzi

Masihi na Kristo inamaana ya mpakwa mafuta na inamuelezea Yesu mwana wa Mungu.

- Masihi na Kristo vimetumika katika agano jipya kumuelezea mwana wa Mungu ambaye Mungu baba alimpaka mafuta kutawala kama mfalme juu ya watu wake na kuwaokoa toka kwenye dhambi.
- Katika agano la kale manabii waliandika unabii juu ya Masihi miaka mia kabla ya kuja kwake duniani.
- Neno mpakwa mafuta limetumika katika agano la kale kumuelezea Masihi atakayekuja.
- Yesu alitimiza unabii huo na alifanya miujiza mingi iliyothibitisha kuwa yeye ni Masihi, unabii uliobaki utatimia atakaporudi.
- Neno Kristo hutumika kama jina "Kristo Yesu."

(Rudi tena: 17:07; 17:08; 19:18; 21:01; 21:02; 21:03; 21:04; 21:05; 21:06; 21:07; 21:08; 21:09; 21:10; 21:11; 21:12; 21:13; 21:14; 21:15; 22:02; 23:06; 24:05; 26:04; 37:05; 38:02; 39:03; 40:09; 42:03; 42:07; 43:07; 43:09; 44:05; 44:08; 45:03; 46:06; 48:04; 49:14; 50:01; 50:08)

## Kuadhibu, adhabu

### Ufafanuzi

"Kuadhibu" inamaana ya kusababisha mtu ateseke baada ya kufanya makosa. Adhabu ni matokeo hasi anayopewa mtu baada ya kufanya jambo baya.

- Adhabu hutumika kumfanya mtu aache dhambi.
- Mungu aliwaadhibu Waisraeli walipomuasi hasa walipoabudu miungu ya uongo, Mungu aliruhusu adui zao kuwavamia na kuwateka.
- Mungu ni wa haki hivyo huadhibu wenye dhambi. Kila binadamu ametenda dhambi na anastahili adhabu.
- Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya makosa ya kila mtu. Alipokea adhabu ya kila mtu japokuwa yeye hakuwa na kosa lolote.
- Maneno kama "bila kuadhibiwa" au "kuacha kuadhibiwa" yanamaana kuamua kutokuadhibu watu kwa matendo yao maovu. Mungu mara nyingine anawaacha wenye dhambi bila kuwaadhibu akisubiria watubu.

(Rudi tena: [13:07](#); [16:02](#); [16:16](#); [16:17](#); [17:14](#); [18:04](#); [18:06](#); [19:16](#); [20:02](#); [20:05](#); [20:08](#); [20:10](#); [21:07](#); [21:13](#); [48:06](#); [48:10](#); [49:09](#); [49:10](#); [49:11](#); [49:14](#))



## **Kuamini, kuamini katika**

### **Ufafanuzi**

**Neno "kuamini" na "kuamini katika" yanahusiana kwa karibu, lakini yana maana tofauti:**

### **Maoni ya Kutafasiri**

- "Kuamini" laweza kutafasiriwa kama "kujua kuwa ni kweli" au "Jua kuwa sawa."
- "Kuwa na imani" laweza kufasiriwa kama "kuamini kikamilifu" au "kuamini na Kutii" au "kutegemea kwa ukamilifu na kufuata."

(Rudi tena: 04:08; 11:01; 11:02; 11:06; 12:01; 12:12; 15:01; 20:05; 22:03; 22:05; 33:09; 37:03; 37:04; 37:05; 37:08; 37:09; 37:10; 40:05; 40:09; 43:01; 43:03; 43:04; 43:13; 44:06; 45:01; 45:06; 45:07; 46:01; 46:06; 46:08; 46:10; 47:02; 47:11; 47:14; 48:05; 48:07; 48:10; 48:11; 49:09; 49:12; 49:13; 49:14; 49:15; 50:13; 50:14)

## Kubariki

### Ufafanuzi

"kubariki" mtu au kitu maana yake ni kusababisha mema na mambo ya manufaa kufanyika kwa mtu au kitu kinachobarikiwa.

- Kumbariki mtu pia inamaanisha kuonesha nia chanya na vitu vyenye manufaa kumpata mtu huyo.
- Katika nyakati za Biblia, kwa kawaida baba alitamka baraka maalumu kwa wanawe.
- Watu "wanapombariki" Mungu au kuonesha hamu ya kuwa Mungu abarikiwe, inamaanisha wanamwinua.
- Neno "baraka" wakati mwingine linatumika kwa kukitakasa chakula kabla hakijaliwa, au kwa kumshukuru na kumsifu Mungu kwa ajili ya chakula.

//kutokana na maoni hapa chini: Ni mhimu kutoa maana, lengo, au kuzingatia matumizi ya mzizi wa neno "bariki" ambalo kimsingi linapendekeza kustawi au kuwa na wingi wa vitu au utajiri. Kwa kuzingatia wingi wa mafundisho ya kimaandiko juu ya upendo wa Mungu, rehema na neema ambayo siyo ya kale tu bali hata sasa. Kwa kuzingatia uangelizi, ulinzi, na uwepo wa Roho wa Mungu. Na kwa ajili yetu kumbariki Mungu, kwa kutoa shukurani, kuthamini, na kuelewa kama tunavyojifunza na kumfuata(kumtii)//

### Maoni ya Kutafasiri

- "Kubariki" kwaweza kutafasiriwa kama "kuandaa kwa wingi" au "kuwa mwema ."
- "Mungu ameleta baraka kuu" ifasiriwe kama "Mungu ametoa mambo mengi mema kwa" au "Mungu ametoa kwa wingi kwa ajiri" au "Mungu amesababisha Mambo mema kutokea kwa".
- "Amebarikiwa" ifasiriwe kama "atanufaika sana" au "atapitia mambo mema" au "Mungu atamfanya kustawi".
- "Amebarikiwa mtu yule" yaweza kutafasiriwa kama "Ni vema kiasi gani kwa mtu ambaye".
- Vioneshi kama vile, "abarikiwe Bwana" yaweza kutafasiriwa kama, "na asifiwe Bwana" au "Bwana asifiwe" au "Ninamtukuza Bwana".
- Katika mazingira ya kubariki chakula, hii yaweza kutafasiriwa kama, "alimshukuru Mungu kwa ajili ya chakula" au "alimshukuru Mungu kwa kuwapa chakula" au "alikitakasa chakula kwa kumsifu Mungu.

(Rudi tena: 01:07; 01:15; 01:16; 03:14; 04:04; 04:07; 05:10; 07:03; 07:04; 07:05; 08:04; 08:05; 08:14; 09:03; 13:07; 17:05; 17:07; 17:08; 17:09; 21:02; 48:07)

## kuhani mkuu

### Ufafanuzi

Neno 'kuhani mkuu' hurejelea kuhani maalumu aliyekuwa ameteuliwa kutumika kwa mwaka mmoja kama kiongozi wa makuhani wote wa Wayahudi. Kuhani mkuu alikuwa na majukuu mahususi. Alikuwa ni mtu pekee aliyeruhusiwa kuingia mahali patakatifu sana katika hekalu ili kutoa sadaka maalumu mara moja kwa mwaka. Waisraeli walikuwa na makuhani wengi sana, lakini walikuwa na kuhani mkuu mmoja kwa muda fulani. Kipindi alichokamatwa Yesu, Kayafa alikuwa kuhani mkuu. Anasi, Baba mkwe wa Kayafa anatajwa mara kadhaa kwasababu alikuwa kuhani mkuu hapo awali, huenda alikuwa bado na mamlaka na nguvu fulani juu ya watu.

Mapendekezo ya tafsiri 'Kuhani mkuu' tunaweza kutafsiri kama "kuhani wa daraja la juu"

(Rudi tena: [13:08](#); [16:16](#); [21:07](#); [38:03](#); [38:15](#); [39:01](#); [39:03](#); [39:04](#); [39:05](#); [45:02](#); [45:03](#); [46:01](#); [48:06](#))

## Kuhani, ukuhani

### Ufafanuzi

Katika Biblia Kuhani alikuwa mtu aliyechaguliwa kutoa sadaka ya kuteketezwa kwa Mungu kwa niaba ya watu wa Mungu. Ukuhani lilikuwa jina au masharti ya kuwa kuhani.

- Katika agano la kale Mungu alimchagua Haruni na uzao wake kuwa makuhani wa Israeli.
- Ukuhani ilikuwa haki na majukumu yaliyorithishwa toka kwa baba kwenda kwa mtoto katika kabila ka Lawi.
- Makuhani wa Israeli walikuwa na jukumu la kutoa sadaka za watu kwa Mungu pamoja na kazi nyingine katika hekalu.
- Makuhani pia walitoa maombi kwa Mungu kawa niaba ya watu wake na kufanya kazi nyingine za kidini.
- Makuhani walitangaza baraka kwa watu na kuwafundisha sheria za Mungu.
- Katika wakati wa Yesu kulikuwa na ngazi mbalimbali za makuhani kama Makuhani Wakuu na Kuhani mkuu.
- Yesu ni kuhani wetu mkuu anayetuomba mbele za Mungu. Alijitoa mwenyewe kama sadaka kwa dhambi zetu.
- Katika agano jipya hata anayemwamini Mungu ni kuhani ambaye anaweza kwenda moja kwa moja kwa Mungu kwa njia ya maombi kujiomba mwenyewe na kuomba watu wengine.
- Hapo kale kulikuwa pia na makuhani wa kipagani walioleta sadaka kwa miungu ya uongo kama Baali.

(Rudi tena: [04:07](#); [13:02](#); [13:09](#); [15:02](#); [15:03](#); [15:04](#); [19:07](#); [21:06](#); [21:07](#); [22:01](#); [27:06](#); [27:07](#); [48:06](#))

## Kuhubiri

### Ufafanuzi

Kuzungumza na kundi la watu kuwafundisha kuhusu Mungu na kuwasihi wamtii Mungu.

- Mara nyingi kuhubiri hufanywa na mtu mmoja kwa kundi kubwa la watu. Mara nyingi huzungumzwa na sio kuandikwa.
- "kuhubiri" na "kufundisha" ni sawa japo haifanani sana.
- "Kuhubiri" ni kitendo cha kutangaza hadharani ukweli wa kiroho na kuwasihi wasikilizaji watekeleze. "Kufundisha" ni kitendo cha kusisitiza maelekezo yanayotolewa kwa watu au kuwafundisha kitu cha kufanya.
- Neno "kuhubiri" mara nyingi kunaambatana na neno "injili."

(Rudi tena: [24:02](#); [30:01](#); [38:01](#); [45:06](#); [45:07](#); [46:06](#); [46:07](#); [46:08](#); [46:10](#); [47:11](#); [47:14](#); [50:02](#))



## kujaribu, jaribu

### Ufafanuzi

Kumjaribu mtu ni kufanya huyo mtu kufanya kitu kibaya.

- Jaribu ni kitu kinacho sababisha mtu kutaka kufanya kitu kibaya.
- Watu wanajaribiwa kwa dhambi zao na kwa watu wengine.
- Shetani pia anajaribu watu kutomtii Mungu na kufanya dhambi dhidi ya Mungu na kwa kufanya vitu vibaya.
- Shetani alimjaribu Yesu na kumtaka afanye kitu kibaya, lakini Yesu alizuia majaribu yote ya Shetani na hakutenda dhambi.

(Rudi tena: [25:01](#); [25:02](#); [25:08](#); [26:01](#); [38:11](#); [49:17](#))

## Kundi la watu, watu

### Ufafanuzi

"Watu" au "kundi la watu" linamaanisha makundi ya watu wenye lugha moja na utamaduni mmoja. Pia yaweza kuwa na maana ya watu waliokusanyika sehemu fulani au kwa ajili ya tukio fulani.

- Mungu alipotenga "watu" kwa ajili yake inamaanisha aliwachagua watu wawe wake na wamtumikie yeye.
- Katika nyakati za Biblia kundi la watu mara nyingi lilikuwa na mababu na waliishi pamoja katika nchi fulani au eneo fulani la nchi.
- Inategemea na lengo katika kifungu fulani "watu wako" inaweza kuwa na maana ya "kundi lako la watu" au "famila yako" au "ndugu zako"
- Neno "Watu" mara nyingi hutumika kuelezea watu wa makundi yote duniani.

(Rudi tena: [21:02](#); [42:08](#); [42:10](#); [48:07](#); [48:11](#); [50:03](#))

## kuomba

### Ufafanuzi

Neno "kuomba" lamaanisha kumwomba mtu kitu fulani kwa umuhimu. Mara kwa mara inamaanisha kuomba pesa, lakini pia limetumika kuonesha kuombeza jambo fulani.

- Mara kwa mara watu wanaomba wakati wanapoitaji jambo fulani kwa uzito, lakini wasijue kwamba kuna mtu atawapa waombacho.
- "Mwombaji" ni mtu ambaye mara kwa mara hukaa au kusimama katika maeneo ya wazi kuomba pesa kwa watu.
- Kwa kutegemea mazingira, neno hili lingetafsiriwa kama "kusihi" "omba kwa uzito" "kudai pesa" au "kuomba pesa mara kwa mara."

(Rudi tena: [10:04](#); [29:08](#); [32:07](#); [32:10](#); [44:01](#))

## Kuomba, maombi

### Ufafanuzi

"Maombi" au "kuomba" ni kitendo cha kuongea na Mungu. Neno hili pia laweza kutumika kama kitendo cha watu kujaribu kuongea na miungu ya uongo.

- Mtu anaweza kuomba taratibu, kuzungumza na Mungu katika mawazo au kuomba kwa nguvu kuzungunza na Mungu kwa sauti. Mra nyingine maombi huandikwa mfano kama Daudi alipoandika maombi yake katika kitabu cha Zaburi.
- Mambi yanaweza kujumuisha kumuomba Mungu rehema, msaada kwa tatizo fulani au hekima ya kufanya maamuzi.
- Mara nyingine watu humuomba Mungu awaponye wagonjwa au wanaohitaji msaada wake.
- Pia watu hushukuru na kumsifu Mungu katika maombi.
- Maombi yanajumuisha kukiri dhambi zetu na kumuomba Mungu atusamehe.
- Kuongea na Mungu huitwa kunong'onezana naye roho zetu zikiwa na mazungumzo na roho yake na kufurahia uwepo wake.
- Hii inaweza kutafsiriwa kama kuzungumza na Mungu au kuwasiliana na Mungu.

(Rudi tena: 10:08; 13:12; 13:15; 19:08; 19:10; 21:07; 31:01; 31:02; 34:06; 34:09; 34:10; 36:02; 38:09; 38:11; 38:12; 38:13; 43:01; 43:13; 46:10; 47:03; 49:18)

## Kupokea

### Ufafanuzi

Kupokea ni kupata au kukubali kitu unachopewa au kuletewa.

- "Kupokea" pia yaweza kumaanisha kuteseka au kupitia jambo fulani kama "alipokea adhabu kwa alichokifanya."
- Pia kuna namna ya pekee ya kumpokea mtu. Kwa mfano kumpokea mgeni inamaanisha kumkaribisha na kumfanyia jambo la heshima ili kujenga mahusiano naye.
- "Kupokea zawadi ya roho mtakatifu" inamaanisha tumepewa roho mtakatifu na kumkaribisha afanye kazi kwenye maisha yetu.
- Kumpokea Yesu inamaana kukubali wokovu wa Yesu kwa njia ya Yesu Kristo.
- Yule kipofu alipopokea uponyaji inamaana kuwa Mungu alimponya na kumuwezesha kuona tena.

(Rudi tena: [21:13](#); [42:08](#); [45:05](#); [49:06](#); [49:10](#); [49:13](#))



## kusaliti

### Ufafanuzi

Neno "kusaliti" lamaanisha tendo la kumdanganya na kumdhuru mwingine. "Msaliti" ni mtu amsalitiye rafiki yake mwenye kumwamini.

- Yuda alikuwa "msaliti" kwa sababu aliwaeleza viongozi wa Kiyahudi jinsi ya kumkamata Yesu.
- Tendo la Yesu kuwalitiwa na Yuda ulikuwa uovu kwa sababu alikuwa mwanafunzi wake aliyepokea pesa kama malipo juu ya habari aliyowapa ya kumkamata Yesu kwa kifo kisicho cha haki.

### Maoni ya Tafasiri

- Kwa kutegemea mazingira, neno "kusaliti" laweza kutafasiriwa kama "kudanganya na kusababisha madhara" au "kumsaidia adui" au "kufanya uhaini."
- Neno "msaliti" laweza kutafasiriwa kama "mtu asalitiye" au "mfanya biashara mbili" au "msaliti."

(Rudi tena: [21:11](#); [38:02](#); [38:03](#); [38:06](#); [38:13](#); [38:14](#); [39:08](#))

## Kusifu

### Ufafanuzi

Kumsifu mtu ni kuonesha pongezi au heshima kwa mtu yule.

- Watu wanamsifu Mungu kwa namna alivyo mkuu na kwa sababu ya mambo ya ajabu anayoyafanya kama muumbaji na mwokozi wa dunia.
- Kumsifu Mungu kunajumuisha kumshukuru kwa aliyoyafanya.
- Muziki na kuimba hutumiwa kama njia ya kumsifu Mungu.
- Kumsifu Mungu ni sehemu ya kumwabudu.
- Neno "kusifu" yaweza kutafsiriwa kama "kusema mazuri" au "kusifia kwa maneno."

(Rudi tena: [12:13](#); [17:03](#); [17:08](#); [22:07](#); [23:08](#); [43:13](#); [44:03](#); [47:08](#))

## Kutubu, toba

### Ufafanuzi

Kutubu na toba ni hali ya kuacha dhambi na kumrudia Mungu.

- "Kutubu" ni hali ya kubadili nia ya mtu.
- Katika Biblia "kutubu" inamaanisha kuacha dhambi, namna ya kufikiri kibinadamu na kutenda na kumrudia Mungu na njia zake na matendo yake.
- Watu wanapotubu kabisa dhambi zao, Mungu anawasamehe na kuwasaidia kuanza kumtii.

(Rudi tena: [16:02](#); [16:17](#); [17:13](#); [19:18](#); [20:01](#); [24:02](#); [24:03](#); [24:04](#); [42:08](#); [43:11](#); [44:05](#))

## Kuwa na mapepo

### Ufafanuzi

Mtu ambaye ana mapepo ana pepo au roho chafu ambalo humuongoza kile afanyacho au kufikiri.

Mara kwa mara mtu mwenye pepo hujiumiza mwenyewe au watu wengine kwa sababu peopo husababisha afanye hivyo.

Yesu aliponya watu waliokuwa na mapepo kwa kuwaamuru mapeopo kuwatoka . Hii mara kwa mara hujulikana kama "kutoa" mapepo.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri msemu huu zinaweza kujumuisha, "kutawaliwa na pepo" au "kutawaliwa na roho mchafu" au "kuwa na roho mchafu aishiye ndani".

(Rudi tena: [32:02](#); [32:06](#); [47:03](#))

## Kuwatesa, mateso

### Ufafanuzi

"Kuwatesa" au "mateso" ni kitendo endelevu cha kumfanyia mtu au kundi la watu kitu katika namna mbaya ya kuwasababishia madhara.

- Mateso yanaweza kuwa dhidi ya mtu mmoja au watu wengi na mara nyingi huhusisha mashambulizi ya kuendelea.
- Waisraeli waliteswa na makundi mbalimbali ya watu waliowavamia, wakawakamata na kuwaibia vitu vyao.
- Mara nyingi watu huwatesa watu wengine wenye dini tofauti na wao au wanyinge.
- Dini ya Kiyahudi walimtesa Yesu kwa sababu hawakupenda alichokuwa akifundisha.
- Baada ya Yesu kurudi mbinguni viongozi wa kidini wa Kiyahudi na serikali ya Rumi iliwatesa wafuasi wake.
- "Mateso" pia yanaweza kutafsiriwa kama "manyanyaso."

(Rudi tena: [33:07](#); [45:06](#); [45:07](#); [46:01](#); [46:02](#); [46:04](#); [46:09](#))



## kweli, ukweli, kuwa kweli

### Ufafanuzi

Maneno "kweli" na "ukweli" yana eleza mambo ambyo ni halisi, matukio yaliyo tukia, na maneno yaliyo semwa.

- Vitu vya kweli ni halisi, thabiti, uhakika, sawasawa, halali.
- Ukweli ni ufahamu, uamini, uhalisia, au maneno yaliyo kweli.
- Msemo kuwa "kuwa kweli" au "kuja kuwa kweli" ni msemo unao maanisha kuwa unabii ulitokea hakika kama iliyo tabirika kuwa itakuwa.
- Ukweli una jumuisha maelezo ya kutenda kwa namna iliyo tegemevu na aminifu.
- Yesu alidhihirisha ukweli wa Mungu katika maneno aliyo zungumza.
- Neno la Mungu ni kweli. Lina eleza vitu vilivyo tokea na kufundisha yaliyo kweli kuhusu Mungu na kuhusu kila kitu alichofanya.

(Rudi tena: [02:04](#); [16:01](#); [19:10](#); [26:05](#); [31:08](#); [34:10](#); [39:10](#); [45:03](#))

## Laana, kulaaniwa

### Ufafanuzi

Laana ni kusababisha mambo mabaya yatokee kwa mtu au kitu kilicholaaniwa.

- Laana yaweza kuwa kauli ya kusababisha madhara yatokee kwa mtu au vitu.
- Kumlaani mtu ni kutamani mabaya yatokee kwake.
- Pia inaweza kuwa adhabu au mambo mabaya ambayo mtu amesababisha yatokee kwa mtu.

(Rudi tena: [02:09](#); [02:11](#); [03:15](#); [04:04](#); [39:07](#); [50:16](#))

## Lazaro

### Ufafanuzi

Lazaro na dada zake, Mariamu na Martha, walikuwa marafika wa karibu wa Yesu. Mara nyingi alikaa nao katika nyumba yao Bethania.

Lazaro anajulikana zaidi kwa kufufuliwa na Yesu kutoka wafu baada ya kuzikwa kaburini kwa siku kadhaa. Viongozi wa Kiyahudi walikasirika na kuwa na wivu kuwa Yesu alifanya mujiza huu na wakatafuta njia ya kumua Yesu na Lazaro. Yesu pia alitoa fumbo kuhusu maskini ombaomba na mtu tajiri ambapo ombaomba aliitwa "Lazaro."

(Rudi tena: [37:01](#); [37:02](#); [37:03](#); [37:04](#); [37:06](#); [37:09](#); [37:10](#); [37:11](#))

## Madhabahu

### Ufafanuzi

Madhabahu ilikuwa sehemu yenye muundo ulioinuka ambao wana wa Israeli walichoma wanyama na mazao kama sadaka kwa Mungu.

- Katika nyakati za Biblia madhabahu rahisi zilikuwa zinatengenezwa kwa kilima chenye udongo au mawe makubwa yaliyopangwa na kupafanya pawe imara.
- Madhabahu nyingine zilitengenezwa kwa mbao pamoja na dhahabu na shaba.
- Watu wengine walioishi karibu na Israeli walitengeneza pia madhabahu na kutoa sadaka kwa miungu yao.

(Rudi tena: [03:14](#); [05:08](#); [13:09](#); [16:06](#); [16:07](#); [19:11](#))

## maisha, uhai, kuishi, kuwa hai

### Ufafanuzi

Maneno haya yote yanamaanisha kuwa hai kimwili, sio kufa. Yanatumika pia kimaumbo kumaanisha kuwa hai kiroho. Yanayofuata yanaelezea nini kinamaanishwa na "maisha ya kimwili" na "maisha ya kiroho."

Kulingana na mazingira, "maisha" inaweza kuetafsiriwa kama "kuwepo" au "mtu" au "roho" au "kuwa" au "kupitia." Neno "uhai" inaweza kutafsiriwa kama "kuishi" au "kukaa" au "kuwepo." Msemu "mwisho wa maisha yake" inaweza kutafsiriwa kama, "alipoacha kuishi." Msemu "alinusuru maisha yao" unaweza kutafsiriwa kama, "aliwaruhusu waishi" au "hakuwaua." Msemu "walihatarisha maisha yao" unaweza kutafsiriwa kama, "walijiweka hatarini" au "walifanya kitu ambacho kingiweza kuwaua." Bibilia inapozungumzia kuwa hai kiroho, "maisha" yanaweza kutafsiriwa kama "maisha ya kiroho" au "maisha ya milele," kulingana na mazingira. Wazo la "maisha ya kiroho" linaweza pia kutafsiriwa kama, "Mungu kutufanya kuwa hai katika roho zetu" au "maisha mapya kwa Roho wa Mungu" au "kufanywa hai ndani yetu." Kulingana na mazingira, msemu "toa maisha" unaweza kutafsiriwa kama, "kusababisha kuishi" au "kutoa uzima wa milele" au "kusababisha kuishi milele."

(Rudi tena: [01:10](#); [01:11](#); [02:12](#); [27:02](#); [35:09](#); [35:13](#); [36:07](#); [37:05](#); [42:05](#); [43:07](#); [44:05](#); [44:08](#); [45:08](#); [48:04](#); [49:09](#); [49:12](#); [50:12](#); [50:13](#))



## Malaika, Malaika mkuu

### Ufafanuzi

Malaika ni kiumbe chenye roho na chenye nguvu kilichoumbwa na Mungu. Malaika wanamtumikia Mungu kwa kufanya yale wanayoagizwa kuyafanya na Mungu. Malaika mkuu ni malaika anayewaongoza malaika wengine.

- Malaika maana yake ni mjumbe.
- Malaika mkuu maana yake ni mjumbe mkuu. Malaika pekee kwenye Biblia anayesemwa kama malaika mkuu ni Mikaeli.
- Katika Biblia malaika wanafikisha ujumbe kwa watu toka kwa Mungu. Ujumbe huu ni pamoja na maelekezo juu ya nini Mungu anataka watu wafanye.
- Malaika pia waliwaambia watu mambo yajayo.
- Malaika wana mamlaka ya Mungu katika kumuwakilisha na wakati mwingine kwenye Biblia wamezungumza kama vile Mungu anazungumza.
- Njia nyingine ambazo Malaika wanamtumikia Mungu ni kwa kuwalinda na kuwapa watu nguvu.
- Malaika wa Yahweh ina maana mbili 1) "malaika wanaomwakilisha Yahweh" au "wajumbe wanaomtumikia Yahweh." 2) Yaweza kuwa na maana ya Yahweh mwenyewe aliyeonekana kama malaika alipoongea na mtu.

(Rudi tena: [02:12](#); [16:05](#); [22:01](#); [22:02](#); [22:03](#); [22:04](#); [22:05](#); [22:06](#); [22:07](#); [23:01](#); [23:02](#); [23:06](#); [23:07](#); [23:08](#); [25:04](#); [25:08](#); [38:12](#); [38:15](#); [41:04](#); [41:05](#); [45:07](#); [50:09](#); [50:10](#))

## Mariam, mama yake Yesu

### Ufafanuzi

Mariam alikuwa mwanamke mdogo aliye ishi katika mji wa Nazarethi aliye poswa kuolewa na Yusufu. Mungu alimchagua Mariam kuwa mama wa Yesu Mesia, Mwana wa Mungu.

- Roho Mtakatifu kimiujiza alisababisha Mariam kuwa na mimba wakati akiwa bikra
- Malaika alimwambia Mariam kuwa mtoto atakaye zaliwa ni Mwana wa Mungu na kuwa amwite Yesu.
- Mariam alimpenda Mungu na akamsifu kwa kuwa na neema kwake.
- Yusufu alimuoa Mariam , lakini alibaki bikra mpaka mtoto kuzaliwa.
- Mariam alidhani kwa undani kuhusu vitu vya ajabu wachungaji na mamajusi alivyo visema kuhusu Yesu.
- Mariam na Yusufu walimchukuwa mtoto Yesu kuwekwa wakfu hekaluni. Baadae wakamchukuwa Misri kutoroka njama ya Farao kuuwa watoto. Hatimae wakarudi Nazarethi.

(Rudi tena: [22:04](#); [22:05](#); [22:06](#); [23:01](#); [23:02](#); [23:03](#); [23:04](#); [23:08](#))

## mbingu, anga, mbinguni

### Ufafanuzi

Neno linalotafsiriwa kama "mbingu" hurejelea mahali anapoishi Mungu. Neno hilo hilo laweza kumaanisha " anga" kwa kutegemea na muktadha. Neno 'mbingu' hurejelea kila kitu tunachokiona juu mawinguni kama vile jua, mwezi, na nyota. Inaweza pia kujumuisha vitu vingine vya anga la mbali kama vile sayari, vitu ambavyo hatuwezi kuviona tukiwa hapa duniani. Neno "anga" hurejelea anga la bluu lililo juu ya dunia ambalo lina mawingu na hewa tunayopumua. Mara kwa mara, jua na mwezi husemwa kuwa ziko 'juu angani. Neno 'mbingu' laweza kumaanisha 'anga' au sehemu ambako Mungu anaishi' hii hutegemea na muktadha mbalimbali. Wakati neno 'mbingu' linapotumika kama tamathali ya semi, humrejelea Mungu mwenyewe. Kwa mfano, Mathayo anapoandika juu ya 'ufalme wa mbinguni' anarejelea ufalme wa Mungu.

Mapendekezo ya tafsiri Wakati neno 'mbingu' linapotumika kimfano laweza kutafsiriwa kama 'Mungu' Maneno 'mbingu' au " vitu vya kimbingu' yaweza kutafsiriwa kama 'jua, mwezi na nyota. Kirai "nyota za mbinguni" chaweza kutafsiriwa kama " nyota za angani."

(Rudi tena: 04:02; 04:07; 23:07; 24:08; 28:04; 34:09; 37:09; 39:04; 41:04; 42:10; 42:11; 43:01; 43:02; 50:03; 50:16)

## mchungaji, kuchunga

### Ufafanuzi

Mchungaji ni mtu anaye linda kondoo. Kitenzi "kuchunga" ina maana ya kulinda kondoo na kuwapa chakula na maji.

- Wachungaji wanachunga kondoo, kuwa ongoza sehemu yenye chakula kizuri na maji. Wachungaji pia wana chungu kondoo wasipotee na kuwalinda na wanyama hatari.
- Hili neno linatumika kifumbo kwenye Biblia kueleza kutunza maitaji ya kiroho ya watu. Hii ni pamoja na kuwa fundisha nini Mungu alichwa waambia kwenye Biblia na kuwa ongoza kwenye njia ya kuishi.
- Katika Agano la Kale, Mungu amewaita "wachingaji" wa watu wake kwasababu ana watunza na maitaji yao yote na kuwalinda. Pia uwaongoza na kuwa elekeza.
- Musa alikuwa mchungaji wa Waisraeli alipo waongoza kiroho katika kumuabudu Yahweh na kuwa ongoza kimwili katika safari yao kwenye nchi ya Kanani.
- Katika Agano Jipya, Yesu anajitaja "mchungaji mwema." Mtume Paulo pia anamtaja kama "mchungaji mkuu" juu ya Kanisa.

(Rudi tena: [09:11](#); [17:02](#); [23:06](#); [23:08](#); [30:03](#); [38:08](#))

## mfalme

### Ufafanuzi

Neno "mfalme" linamaanisha mwanamme ambaye ni mtawala mkuu wa mji, jimbo, au nchi.

Mfalme kawaida huchaguliwa kutawala kwa sababu ya uhsiano wake kifamilia na wafalme wa nyuma. Mfalme anapokufa, kawaida mwana wake mkubwa ndiye anayekuwa mfalme mpya. Katika nyakati za zamani, mfalme alikuwa na mamlaka yote juu ya watu katika ufalme wake. Neno "mfalme" halitumiki sana kwa mtu asiye mfalme wa kweli, kama "mfalme Herode" katika Agano Jipya. Katika Biblia, Mungu anajulikana kama mfalme anaye tawala juu ya watu wake. "Ufalme wa Mungu" unamaanisha utawala wa Mungu juu ya watu wake. Yesu alitwa "Mfalme wa Wayahudi," "mfalme wa Israeli," na "mfalme wa wafalme." Yesu atakaporudi, atatawala kama mfalme wa dunia. Neno hili linaweza kutafsiriwa kama, "mkuu" au "kiongozi kamili" au "mtawala mwenye nguvu." Usemi "mfalme wa wafalme" unaweza kutasiriwa kama "mfalme anayetawala juu ya wafalme wengine wote" au "kiongozi mkuu aliye na mamlaka juu ya viongozi wengine wote."

(Rudi tena: 08:06; 15:07; 16:01; 16:15; 16:18; 17:01; 17:02; 17:04; 17:05; 17:07; 18:05; 18:08; 18:11; 18:12; 18:13; 19:02; 19:13; 19:17; 20:06; 20:08; 20:11; 21:06; 21:08; 29:02; 29:03; 29:04; 29:07; 29:08; 48:14)



## Mfalme wa Wayahudi

### Ufafanuzi

Usemi, "Mfalme wa Wayahudi" ni jina linalomaanisha Yesu, Masihi.

Mara ya kwanza Biblia inaandika hili jina wakati linapotumika na wanaume wenye hekima waliosafiri kwenda Bethlehemu wakimtafuta mtoto aliye "Mfalme wa Wayahudi." Malaika alimfunulia Mariamu kuwa mwanaye, mzawa wa mfalme Daudi, atakuwa mfalme ambaye ufalme wake utadumu milele. Kabla Yesu hajasulibishwa, askari Wakirumi walimdhaki Yesu kwa kumuita "Mfalme wa Wayahudi." Jina hili liliandikwa pia katika kipande cha mbao na kupigwa msumari juu ya msalaba wa Yesu. Yesu kweli ni Mfalme wa Wayahudi na mfalme wa viumbe vyote.

(Rudi tena: [23:09](#); [39:09](#); [39:12](#); [40:02](#))

## mfuasi

### Ufafanuzi

Msemo wa "mfuasi" una maana ya mtu anayetumia muda mwingi na mwalimu, akijifunza kutoka kwa tabia na mafunzo ya mwalimu huyo.

Watu waliomfuata Yesu, wakimsikiliza mafundisho yake na kuyatii, walijulikana kama "wanafunzi" wake.

Yohana Mbatizaji pia alikuwa na wanafunzi.

Katika kipindi cha huduma ya Yesu, kulikuwa na wanafunzi wengi waliomfuata na kusikiliza mafunzo yake.

Yesu alichagua watume kumi na wawili wawe wafuasi wake wa karibu; wanamume hawa wakaja kujulikana kama "mitume" wake.

Watume kumi na wawili waliendelea kujulikana kama "wanafunzi" wake au "wale kumi na wawili".

Kabla tu ya Yesu kwenda juu mbinguni, aliwaamuru wanafunzi wake kuwafundisha watu wengine juu ya kuwa wafuasi wa Yesu pia.

Yeyote anayemwamini Yesu na kumtii mafunzo yake anaitwa mfuasi wa Yesu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo "mwanafunzi" unaweza kutafsiriwa kwa neno au msemo wenye maana ya "mfuasi" au "mwanafunzi".

Hakikisha ya kwamba tafsiri ya msemo huu haimaanishi mwanafunzi anayejifunza darasani.

Tafsiri ya msemo huu unatakiwa kuwa tofauti na tafsiri ya "mtume".

(**Rudi tena:** 28:06; 28:07; 28:08; 30:02; 30:04; 30:05; 30:08; 30:09; 31:01; 31:02; 31:04; 31:08; 32:01; 32:15; 33:06; 36:01; 36:05; 36:07; 37:02; 37:03; 38:01; 38:02; 38:04; 38:06; 38:08; 38:10; 38:11; 38:13; 38:15; 41:01; 41:07; 41:08; 42:05; 42:06; 42:08; 42:10; 42:11; 43:01; 43:05; 43:10; 43:13; 45:07; 46:04; 46:08; 50:02; 50:03; 50:05; 50:08)

## Midiani, Wamidiani

### Ufafanuzi

Midiani alikuwa mwana wa Ibrahimu na mkewe Ketura. Pia ni jina la kundi la watu na eneo upande wa kaskazini mwa Jangwa la Kiarabu sehemu ya kusini mwa nchi ya Kanani. Kundi la watu liliitwa "Wamidiani."

- Musa alipo ondoka Misri, alienda eneo la Midiani alipo kutana na binti wa Yethro na kuwasaidia kunyeshwa maji mifugo yao. Baadae Musa alimuoa mmoja wa binti wa Yethro.
- Yusufu alichukuliwa Misri na kundi la wanfanya biashara ya watumwa Wamidiani.
- Miaka mingi baadae Wamidiani alishambulia na kuvamia Waisraeli katika nchi ya Kanani. Gidioni aliongoza Waisraeli katika ushindi wao.
- Waarabu wengi wa leo ni wa kabila la uzao wa hili kundi.

(Rudi tena: [16:03](#); [16:04](#); [16:05](#); [16:08](#); [16:09](#); [16:11](#); [16:12](#); [16:14](#); [16:15](#))

# **milele**

## **Ufafanuzi**

Msemu huu "milele" una maana ya kitu ambacho kitaendelea kuwepo au kutadumu daima.

Msemu "milele" una maana ya hali ya kutokuwa na mwanzo au mwisho. Pia inaweza kumaanisha maisha ambayo hayana mwisho.

Baada ya maisha haya ya sasa ya duniani, binadamu wataishi milele aidha mbinguni na Mungu au jehanamu kutengana na Mungu.

Misemo "maisha ya milele" inatumika katika Agano Jipya kumaanisha kuishi milele pamoja na Mungu mbinguni.

Msemu "milele na milele" ina wazo la muda ambao hauna mwisho na huelezea nini milele au maisha ya milele yakoje.

Mapendekezo ya Tafsiri

Njia zingine za kutafsiri "milele" zinaweza kujumuisha "kutokuwa na mwisho" au "kuendelea siku zote".

Msemu "maisha ya milele" unaweza kutafsiriwa kama "maisha ambayo hayana mwisho" au "maisha ambayo yanaendelea bila kikomo" au "kufufua miili yetu kuishi milele".

Kulingana na muktadha, njia tofauti za kutafsiri "milele" zinaweza kujumuisha "kuwepo nje ya muda" au "maisha yasiyo na mwisho" au "maisha mbinguni".

Pia fikiria namna neno hili linatafsiriwa katika Biblia katika lugha ya taifa.

**(Rudi tena: [27:01](#); [28:01](#); [28:10](#))**

## Misri, Mmisri

### Ufafanuzi

Misri ni nchi katika sehemu ya kaskazini ya Afrika, kusini mashariki mwa nchi ya Kaanani. Mmisri ni mtu ambaye anatoka katika nchi ya Misri.

Katika miaka ya zamani, Misri ilikuwa nchi yenye nguvu na utajiri.

Misri ya zamani iligawanyika katika sehemu mbili, Misri ya Chini (sehemu ya kaskazini ambapo mto hutiririka chini kuelekea baharini) na Misri ya Juu (sehemu ya kusini). Katika Agano la Kale, sehemu hizi zinajulikana kama "Misri" na "Pathrosi" katika lugha ya maandishi asili.

Wakati mwingine ambapo kuna chakula kichache Kaanani, wakuu wa koo walisafiri kwenda Misri kununua chakula kwa ajili ya familia zao.

Kwa miaka mia moja hivi, Waisraeli walikuwa watumwa Misri.

Yusufu na Mariamu walishuka chini Misri na mtoto mdogo Yesu kutoroka kwa Herode Mkuu.

**(Rudi tena: 08:04; 08:06; 08:08; 08:10; 08:11; 08:12; 08:14; 09:01; 09:02; 09:03; 09:08; 09:10; 09:11; 09:13; 10:02; 10:04; 10:05; 10:06; 10:07; 10:08; 10:10; 10:11; 11:03; 11:04; 11:06; 11:07; 11:08; 12:01; 12:04; 12:06; 12:10; 12:11; 12:12; 12:13; 12:14; 13:04; 14:07; 38:01; 48:09)**



## Mji wa Babeli

### Ufafanuzi

Mji wa Babeli ulikuwa makao makuu wa jimbo la Babeli ya kale, ambao pia ulikuwa sehemu ya Himaya ya Babeli.

- Babeli ulikuwa kandokando ya Mto Frati, katika eneo ambalo mnara wa Babeli ulikuwa umejengwa mamia ya miaka iliyokuwa imepeita.
- Wakati mwingine jina "Babeli" linarejerea Himaya yote ya Babeli. Kwa mfano, "mfalme wa Babeli alitawala himaya yote ya Babeli, siyo mji tu.
- Watu wa Babeli walikuwa wenye nguvu walioishambuli Yuda na kuwapeleka watu katika uhamisho huko Babeli kwa miaka 70.
- Sehemu yake iliitwa "Ukalidayo" na watu walioishi pale waliitwa "Wakalidayo." Matokeo yake neno "Ukalidayo mara kwa mara lilitumika kurejerea Babeli.
- Katika Agano Jipya, neno "Babeli" wakati mwingine linatumika kama sitiari kurejerea maeneo, watu, na vitu vya kufikirika viusianishwavyo na ibada ya sanamu na tabia nyingine za dhambi.
- Kirai "Babeli Mkuu" au "Babeli mji mkuu" kisitiari inarejerea kwa mji au taifa kubwa, tajiri, na lenye dhambi, kama ulivyokuwa mji wa kale wa Babeli.

(Rudi tena: [20:06](#); [20:07](#); [20:08](#); [20:09](#); [20:11](#))

## Mkristo

### Ufafanuzi

Baada ya Yesu kurudi mbinguni watu wakaanza kuitwa Wakristo ikiwa na maana ya wafuasi wa Kristo.

- Ilikuwa katika mji wa Antiokia ambapo wafuasi wa Yesu waliitwa Wakristo kwa mara ya kwanza.
- Mkristo ni mtu anayeamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na anayeamini kuwa Yesu anaweza kumuokoa toka kwenye dhambi.
- Katika wakati wa sasa Mkristo ni mtu anayetambulishwa na dini ya Kikristo lakini sio mfuasi wa Yesu kabisa. Hii sio maana ya Mkristo ki Biblia.
- Kwa sababu Mkristo kwenye Biblia inamaanisha mtu anayemwamini Yesu kabisa Mkristo pia anaitwa mwamini.

(Rudi tena: [46:09](#); [47:14](#); [49:15](#); [49:16](#); [49:17](#); [49:18](#); [50:03](#); [50:11](#); [50:12](#))

## Msalaba

### Ufafanuzi

Katika Biblia msalaba ni mbao iliyosimama wima inayochimbiwa kwenye ardhi na yenye mbao nyingine inayopita kwa mlalo na inayoshikizwa karibu na juu.

- Katika wanyati wa utawala wa Rumi serikali ya Rumi ilimhukumu mhalifu kwa kumgongelea msalabani na kumuacha afe hapo.
- Yesu alihukumuwa bila kosa na walimua msalabani.

(Rudi tena: [40:01](#); [40:02](#); [40:05](#); [49:10](#); [49:12](#); [49:14](#))

## Mto Nili, Mto wa Misri

### Ufafanuzi

Nili ni mto mrefu na mpana katika kaskazini mashariki mwa Africa. Unajulikana kama mto rasmi wa Misri.

- Mto Nili unapita kaskazini kupita Misri na kwenda Bahari ya Medetarenia.
- Mimea ina kua kwenye nchi ya rotuba pande zote mbili za Mto Nili.
- Wamisri wengi wanaishi karibu na Mto Nili maan ni muhimu kwa maji na mazao ya chakula.
- Waisraeli waliishi nchi ya Gosheni iliyo kuwa na rotuba kwababu ilikuwa upande wa Mto Nile

(Rudi tena: [08:04](#); [09:04](#); [09:06](#); [10:03](#))

## Mto Yordani, Yordani

### Ufafanuzi

Mto Yordani ni mto unaotiririka toka kaskazini hadi kusini, na inaunda mpaka wa mashariki wa nchi iliyokuwa inaitwa Kanaani.

Leo, mto Yordani unatenganisha Israeli magharibi kutoka Yordani mashariki. Mto Yordani unatiririka katikati ya Bahari ya Galilaya na kuishia katika Bahari iliyo Kufa. Wakati Yoshua anawaongoza Waisraeli kuelekea Kanaani, ilibidi wavuke mto Yordani. Kwa sababu palikuwa parefu sana, Mungu alisimamisha maji kutembea kwa miujiza ili watu wavuke. Mara nyingi Biblia katika Biblia Mto Yordani unajulikana ka "Yordani."

(Rudi tena: [15:02](#); [15:03](#); [19:14](#); [19:15](#))



## Mtume, utume

### Ufafanuzi

Mitume walikuwa watu waliotumwa na Yesu kuhubiri kuhusu ufalme wa Mungu. Utume ni nafasi au mamlaka ya wale waliochaguliwa kuwa mitume.

- "Mtume" maana yake ni mtu aliyetumwa kwa ajili ya lengo maalumu. Mtume ana mamlaka sawa na ya yule aliyemtuma.
- Kwa nguvu za Mungu, Mitume waliweza kuhubiri injili na kuonya watu na kuwatoa watu mapepo.

(Rudi tena: [26:10](#); [30:01](#); [38:02](#); [43:13](#); [46:08](#))

## mtumishi, mtumwa, utumwa

### Ufafanuzi

Neno "mtumishi" la weza pia maanisha "mtumwa" na kumueleza mtu anaye mfanyia mtu mwingine kazi, iwe kwa uwamuzi au kwa lazima. Muktaadha wa maneno yaliyo zunguka yanaweka dhahiri kuwa kama mtumishi au mtumwa ndiye anaye tajwa.

- Katika nyakati za Biblia, kulikuwa na tofauti ndogo katika ya mtumishi na mtumwa kuliko ilivyo leo. Wote watumishi na watumwa walikuwa sehemu muhimu ya nyumba ya bwana wao na wengi walichukuliwa kama ndugu wa familia.
- Mtumwa ni aina ya mtumishi ambaye ni mali ya mtu anaye mfanyia kazi. Mtu anaye nunua mtumwa anaitwa "mmiliki" au "bwana." Mabwana wengine wanawatendea watumwa wao kwa ukatili sana, wakati wengine wana watendea vizuri.
- Zamani za kale, watu wengine kwa hiari walikuwa watumwa kwa mtu aliye wadai ilikulipa deni lao.
- Katika Biblia, maneno "mimi ni mtumishi wako" yalitumika kama alama ya heshima na huduma kwa mtu wa ngazi ya juu, kama mfalme. Haimanishi kwamba mtu anaye zungumza alikuwa mtumishi halisi.
- Katika Agano la Kale, manabii wa Mungu na watu wengine waliyo muabudu Mungu mara nyingi waliitwa "watumishi."
- Wakristo pia wanaitwa "watumwa wa haki," ambayo ni mfano unao linganisha uwaminifu wa kumtii Mungu kama mtu anavyo mtii bwana wake.

(Rudi tena: 04:05; 05:01; 06:01; 06:02; 06:03; 07:08; 07:09; 08:02; 08:04; 08:12; 09:02; 09:08; 09:13; 12:01; 12:03; 12:04; 12:13; 12:14; 13:04; 14:07; 19:10; 20:06; 29:02; 29:03; 29:04; 29:05; 29:06; 29:07; 29:08; 35:06; 35:09; 38:01; 38:15; 39:06; 39:10; 47:03; 47:04; 47:05; 47:06; 47:07; 49:17; 50:04; 50:06; 50:07)

# Mungu

## Ufafanuzi

Katika Biblia, msembo "Mungu" una maana ya kiumbe wa milele ambaye aliumba ulimwengu bila chochote. Mungu alikuwepo kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Jina binafsi la Mungu ni "Yahwe".

Mungu mara zote alikuwepo; alikuwepo kabla ya kitu chochote kuwepo, na ataendelea kuwepo milele.

Yeye ni Mungu mmoja wa kweli na ana mamlaka juu ya kila kitu ulimwenguni.

Mungu ana haki timilifu, hekima isiyo na mwisho, mtakatifu, bila dhambi, wa haki, wa rehema, na upendo.

Ni Mungu wa kutunza agano, ambaye hutimiza ahadi zake daima.

Watu waliumvwa kumwabudu Mungu na ni yeye pekee wanaopaswa kumwabudu.

Mungu alifunua jina lake kama "Yahwe" ambayo ina maana ya "yeye ni" au "Mimi ni" au "Yule anayekuwepo daima".

Biblia pia hufundisha kuhusu "miungu" wa uongo ambao ni sanamu wasioishi ambao watu huabudu kwa makosa.

(Rudi tena: 01:01; 01:02; 01:03; 01:04; 01:05; 01:06; 01:07; 01:08; 01:09; 01:10; 01:11; 01:12; 01:13; 01:15; 01:16; 02:01; 02:02; 02:03; 02:04; 02:07; 02:08; 02:09; 02:10; 02:11; 02:12; 03:01; 03:02; 03:03; 03:04; 03:06; 03:13; 03:14; 03:15; 03:16; 04:01; 04:02; 04:03; 04:04; 04:05; 04:06; 04:07; 04:08; 04:09; 05:01; 05:02; 05:03; 05:04; 05:05; 05:06; 05:07; 05:08; 05:09; 05:10; 06:02; 06:04; 06:05; 06:06; 07:07; 07:10; 08:04; 08:05; 08:07; 08:12; 08:15; 09:03; 09:12; 09:13; 09:14; 09:15; 10:01; 10:02; 10:03; 10:04; 10:05; 10:06; 10:07; 10:08; 10:10; 10:11; 10:12; 11:01; 11:02; 11:03; 11:04; 11:05; 11:06; 12:01; 12:02; 12:03; 12:05; 12:06; 12:07; 12:10; 12:11; 12:12; 12:13; 12:14; 13:01; 13:02; 13:03; 13:04; 13:05; 13:07; 13:08; 13:09; 13:10; 13:11; 13:12; 13:13; 13:14; 13:15; 14:01; 14:03; 14:06; 14:08; 14:09; 14:10; 14:11; 14:12; 14:13; 14:14; 14:15; 15:01; 15:02; 15:03; 15:05; 15:06; 15:07; 15:09; 15:10; 15:12; 15:13; 16:01; 16:02; 16:03; 16:04; 16:05; 16:06; 16:08; 16:09; 16:10; 16:11; 16:14; 16:16; 16:17; 16:18; 17:01; 17:02; 17:03; 17:05; 17:06; 17:07; 17:08; 17:09; 17:13; 17:14; 18:01; 18:02; 18:03; 18:04; 18:09; 18:13; 19:01; 19:03; 19:04; 19:05; 19:06; 19:07; 19:10; 19:11; 19:13; 19:14; 19:15; 19:16; 19:17; 19:18; 20:01; 20:02; 20:05; 20:06; 20:09; 20:10; 21:01; 21:02; 21:03; 21:04; 21:05; 21:06; 21:07; 21:09; 21:13; 21:14; 21:15; 22:01; 22:03; 22:05; 22:06; 22:07; 23:07; 23:08; 24:06; 24:09; 25:03; 25:04; 25:05; 25:07; 26:03; 26:05; 26:09; 27:02; 28:01; 28:08; 32:06; 32:11; 33:08; 34:07; 34:09; 34:10; 35:08; 37:01; 37:04; 37:08; 38:01; 38:12; 39:04; 39:07; 39:10; 40:04; 40:07; 40:08; 42:04; 42:11; 43:04; 43:06; 43:07; 43:09; 43:11; 43:13; 44:03; 44:05; 44:08; 45:02; 45:03; 45:07; 46:04; 47:01; 47:02; 47:04; 47:08; 48:01; 48:02; 48:03; 48:04; 48:05; 48:06; 48:07; 48:08; 48:09; 48:10; 48:11; 48:12; 49:02; 49:04; 49:08; 49:09; 49:10; 49:11; 49:12; 49:13; 49:14; 49:15; 49:16; 49:17; 49:18; 50:02; 50:09; 50:13; 50:14; 50:15; 50:16)

## Mungu Baba, Baba wa mbinguni, Baba

### Ufafanuzi

Misemo, "Mungu Baba" na "Baba wa mbinguni" ina maana ya Yahwe, Mungu mmoja wa kweli. Msemo huu hujitokeza kama "Baba" haswa pale Yesu anamaan ya yeye.

Mungu alikuwepo kama Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Kila mmoja ni Mungu kamili, na bado wote ni Mungu mmoja. Hii ni siri ambayo binadamu wa kawaia hawezi kuelewa kikamilifu.

Mungu Baba alimtuma Mungu Mwana (Yesu) duniani na yeye humtuma Roho Mtakatifu kwa watu wake.

Yeyote anayemwamini Mungu Mwana anakuwa mtoto wa Mungu Baba, na Mungu Roho Mtakatifu huja kuishi ndani ya mtu huyo. Hii ni siri nyingine ambayo binadamu hawawezi kuelewa kikamilifu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika msemo "Mungu Baba" ni bora kutafsiri "Baba" na neno sawa ambalo lugha hutumia kikawaida kumaanisha baba wa kimwili.

Msemo "Baba wa mbinguni" unaweza kutafsiriwa na "Baba anayeishi mbinguni" au "Baba Mungu ambaye anaishi mbinguni" au "Mungu Baba kutoka mbinguni".

Kawaida "Baba" inaandikwa kwa herufi kubwa, kuonyesha ya kwamba hii inamaanisha Mungu.

(Rudi tena: [22:04](#); [24:09](#); [29:09](#); [37:09](#); [38:12](#); [38:15](#); [40:02](#); [40:07](#); [42:10](#); [42:11](#); [43:08](#); [50:10](#))

## mungu wa uongo, mungu mgeni, mungu, mungu wa kike

### Ufafanuzi

Mungu wa uongo ni kitu ambacho watu huabudu badala ya Mungu mmoja wa ukweli. Msemu "mungu wa kike" una maana haswa kwa mungu wa uongo wa kike.

Miungu hawa wa uongo hawapo. Yahwe ni Mumungu wa pekee.

Watu mara kwa mara hutengeneza vitu kuwa sanamu ili kuabudu kama ishara ya miungu yao ya uongo.

Katika Biblia, watu wa Mungu mara kwa mara waligeuka kutoka kumtii yeye ili kuabudu miungu ya uongo.

Mapepo mara kwa mara hudanganya watu kuamini ya kwamba miungu ya uongo na sanamu wanazoabudu ina nguvu.

Baali, Dagoni, na Moleki walikuwa miungu watatu wa uongo ambao waliabudiwa na watu katika kipindi cha Biblia.

Ashera na Artemi (Diana) walikuwa miungu wa kike wawili ambao watu wa zamani waliwaabudu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kunaweza kuwa tayari na neno kwa ajili ya "mungu" au "mungu wa uongo" katika lugha yako.

Msemu "sanamu" unaweza kutumika kumaanisha miungu wa uongo.

Katika Kiingereza, herufi ndogo ya "m" inatumika kumaanisha miungu wa uongo, na herufi kubwa ya "M" hutumika kwa ajili ya Mungu wa ukweli. Lugha zingine pia hufanya hivi.

Njia nyingine inakuwa kutumia neno tofauti kabisa kumaanisha miungu wa uongo.

Baadhi ya lugha zinaweza kuongeza neno kuelezea kama mungu wa uongo ni wa kiume au wa kike.

(Rudi tena: [10:02](#); [12:03](#); [13:04](#); [13:05](#); [13:11](#); [13:12](#); [13:13](#); [13:14](#); [14:03](#); [16:01](#); [16:03](#); [16:06](#); [16:07](#); [16:16](#); [18:03](#); [18:09](#); [18:12](#); [18:13](#); [19:02](#); [19:16](#); [20:05](#))



# Musa

## Ufafanuzi

Musa alikuwa nabii na kiongozi wa watu wa Israeli kwa miaka 40.

- Musa alipo kuwa mtoto, wazazi wa Musa walimueka kwenye kikapu Mto Nile kumficha na Farao wa Misri. Dada wa Miriamu alimwalia hapo. Maisha ya Musa yalinusurika binti wa Farao alipo mkuta na kumchukuwa kama mwanae.
- Mungu alimchagua Musa kuwa toa Waisraeli utumwani Misri na kuwaongoza Nchi ya Ahadi.
- Baada ya Waisraeli kutoka Misri na walipo kuwa jangwani wakitanga, Mungu alipa Musa mawe mawili ya mbao yenye Amri Kumi.
- Mwisho wa maisha yake, Musa aliona Nchi ya Ahadi, lakini hakuishi sababu hakumtii Mungu.

(Rudi tena: 09:07; 09:08; 09:10; 09:11; 09:12; 09:14; 09:15; 10:01; 10:04; 10:05; 10:07; 10:08; 11:08; 12:05; 12:07; 12:11; 12:12; 13:01; 13:02; 13:03; 13:07; 13:09; 13:11; 13:12; 13:13; 13:14; 13:15; 14:04; 14:07; 14:09; 14:12; 14:13; 14:14; 14:15; 17:06; 21:03; 36:03; 36:04; 45:02; 48:12)

## muujiza, ajabu, ishara

### Ufafanuzi

"Muujiza" ni kitu kinacho shangaza ambacho hakiwezekani pasipo Mungu kusababisha kitokee.

- Mifano ya miujiza Yesu aliyo fanya ni kutuliza dhoruba na kumponya kipofu.
- Miujiza wakati mwingine inaitwa "maajabu" kwasababu ina sababisha watu kujawa na mshangao au kustaaajabika.
- Neno "ajabu" pia laweza kwa ujumla kueleza nguvu za Mungu, kama alivyo umba mbingu na nchi.
- Miujiza pia ya weza itwa "ishara" kwasababu inatumika kama kiashiria au ushaidi kwamba Mungu ni mwenye nguvu kamilifu juu ya ulimwengu.
- Miujiza mingine ilikuwa matendo ya urejesho wa Mungu, kama vile alipo waokoa Waisraeli kutoka utumwani Misri na alipo mlinda Danieli kuto umizwa na simba.
- Maajabu mengine yalikuwa matendo ya hukumu ya Mungu, kama alivyo tuma garika ulimwenguni kote kipindi cha Nuhu na alipo leta mapigo katika nchi ya Misri kipindi cha Musa.
- Miujiza mingi ya Mungu ilikuwa uponyaji wa mwili wa wagonjwa au kuleta wafu kuwa hai.

(Rudi tena: [19:14](#); [37:10](#); [43:06](#); [45:01](#); [49:02](#))

## **mwalimu,Mwalimu**

### **Ufafanuzi**

Mwalimu ni mtu anaye toa taarifa mpya. Waalimu wanasaidiana kupata na kutumia maarifa na ujuzi.

- Katika Biblia, neno "mwalimu" linatumika kwa namna maalumu kumueleza mtu anaye fundisha kuhusu Mungu. Haimuelezi mwalimu wa shule.
- Watu wanao jifunza kutoka kwa mwalimu wanaitwa "wanafunzi."
- Katika baadhi ya fasiri za Biblia, hili jina limewekwa herufi kubwa ("Mwalimu") wakati linapo tumika kama jina la Yesu.

(Rudi tena: [27:01](#); [28:01](#); [37:02](#); [38:14](#))

## **mwaminifu, uaminifu**

### **Ufafanuzi**

Kuwa "mwaminifu" kwa Mungu ina maana kuwa na desturi ya kuishi kulingana na mafunzo ya Mungu. Ina maana ya kuwa mwaminifu kwake na kumuamini. Hali ya kuwa mwaminifu ni "uaminifu".

Mtu ambaye ni mwaminifu anaweza kuaminiwa kuweza kushika ahadi zake na kutimiza majukumu yake daima kwa watu wengine.

Mtu mwaminifu huvumilia katika kutenda kazi, hata pale ambapo ni ndefu au ngumu.

Uaminifu kwa Mungu ni matendo ya daima ya kutenda ambacho Mungu anatutaka kufanya.

Mapendekezo ya Tafsiri

Katika muktadha nyingi, "mwaminifu" inaweza kutafsiriwa kama "uaminifu" au "kujitolea" au "kutegemea".

Katika muktadha zingine, "mwaminifu" inaweza kutafsiriwa kwa neno au msembo ambao una maana ya "kuendelea kuamini" au "kuvumilia katika kuamini na kumtii Mungu".

Njia ambazo "uaminifu" inaweza kutafsiriwa inaweza kumaanisha "kuvumilia katika kuamini" au "uaminifu" au "kuamini na kumtii Mungu".

**(Rudi tena: [08:05](#); [14:12](#); [15:13](#); [17:09](#); [17:14](#); [18:07](#); [35:12](#); [49:17](#); [50:04](#))**

## Mwamori

### Ufafanuzi

Waamori walikuwa watu wenye nguvu sana ambao ni uzao wa mjukuu wa Nuhu Kanani.

- Jina lao lilikuwa na maana ya "aliye juu" ambalo lilimaanisha miji ya milima ambapo walikuwa wakiishi au kwa sababu walijulikana kuwa ni watu warefu kwa kimo.
- Waamori waliishi katika majimbo yote yaliyokuwa kandokando ya mto Yordani. Mji wa Ai ulikaliwa na Waamori.
- Mungu alisema "dhambi za waamori" akiwa anajumuisha waliabudu miungu ya uongo na walitenda dhambi.
- Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuwaangamiza Waamori kama ambavyo Mungu alimuamuru afanye.

(Rudi tena: [15:07](#); [15:08](#); [15:09](#); [15:10](#))



## Mwana wa Mungu, Mwana

### Ufafanuzi

Neno "Mwana wa Mungu la husu Yesu, Neno la Mungu aliye kuja duniani kama binadamu. Anajulikana kama "Mwana."

- Mwana wa Mungu ana tabia moja na Mungu Baba, na ni Mungu timilifu.
- Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu yote ni maana moja.
- Tofauti na wana wa binadamu, Mwana wa Mungu alikuwepo siku zote.
- Mwanzo, Mwana wa Mungu alikuwepo katika uumbaji wa ulimwengu, pamoja na Baba na Roho Mtakatifu.
- Kwasababu Yesu ni Mwana wa Mungu, na penda na kumtii Baba yake, na Baba yake anampenda.

(Rudi tena: 22:04; 22:05; 24:08; 24:09; 25:02; 25:04; 26:09; 31:08; 32:06; 36:05; 37:05; 39:03; 39:04; 40:05; 40:08; 42:10; 46:06; 49:03; 49:09; 49:12; 49:14)

## **mwana, mwana wa**

### **Ufafanuzi**

Neno "mwana" la husu mvulana au mwanaume na wazazi wake. La weza eleza mzao wa kiume wa mwanaume au mwana aliye pangwa.

- "Mwana" ni linatumika sana kifumbo katika Biblia kueleza mzao wa kiume, kama mjukuu au kitukuu.
- Neno "mwana" pia la weza kama rasmi ya kumtaja mvulana au mwanaume aliye mdogo.
- Wakati mwingine "wana wa Mungu" lina tumika katika Agano Jipya kueleza waamini wa Yesu.
- Mungu anamuita Israeli "mwana wake wa kwanza." Hii yaeleza Mungu kuchagua taifa la Israeli kuwa watu wake maalumu. Ni kupitia wao kuwa ujumbe wa Mungu wa wokovu ulikuja, kwa matokeo kwamba wengi wamekuwa wana wake wa kiroho.
- Maneno "mwana wa" mara nyingi ina maana ya kimaafumbo, "kuwa na tabia ya."
- Maneno "mwana wa" pia linatumika kueleza baba wa mtu. Hili neno linatumika katika vizazi na sehemu nyingine.

(Rudi tena: [04:08](#); [04:09](#); [05:04](#); [05:05](#); [05:06](#); [05:08](#); [05:10](#); [06:01](#); [06:06](#); [06:07](#); [09:07](#); [11:02](#); [17:07](#); [20:08](#); [23:02](#); [35:03](#); [35:07](#); [35:08](#); [35:09](#); [35:13](#); [48:08](#))

## **mwanakondoo, Mwanakondoo wa Mungu**

### **Ufafanuzi**

Neno "mwanakondoo" linamaanisha kondoo mchanga. Kondoo ni wanyama wenye miguu minne na wana nywele nene ya sufu, waliotumika kwa sadaka kwa Mungu. Yesu anaitwa "Mwanakondoo wa Mungu" kwa sababu alitolewa kulipia dhambi za watu.

Wanyama hawa huongozwa nje ya mstari kirahisi na wanahitaji ulinzi. Mungu anawafananisha binadamu na kondoo. Mungu anawaagiza watu wake kutoa sadaka kimwili kama kondoo na wanakondoo kamili kwake. Yesu anaitwa "Mwanakondoo wa Mungu" aliyetolewa sadaka kwa ajili ya dhambi za watu. Alikuwa sadaka kamili, bila kasoro kwa sababu alikuwa hata dhambi kabisa.

(Rudi tena: 05:07; 11:02; 11:03; 11:05; 12:14; 24:06; 45:08; 48:08; 48:09; 48:10)

## Myahudi, Yahudi, Wayahudi

### Ufafanuzi

Wayahudi ni watu ambao ni uzao wa mjukuu wa Abrahamu, Yakobo. Neno "Yahudi" linatoka katika neno "Yuda"

Watu walianza kuwaita Waisraeli "Wayahudi" baada ya kurudi Yuda kutoka katika uhamisho kutoka Babeli. Yesu Masihi alikuwa Myahudi. Isipokuwa, viongozi wa dini wa Kiyahudi walitaka kwamba auliwe. Mara nyingi msemu "Wayahudi" inamaanisha viongozi wa Wayahudi, sio watu wote Wayahudi. Kwa mazingira hayo, tafsiri zingine huongeza "viongozi wa" kuiweka wazi.

(Rudi tena: [20:11](#); [20:12](#); [24:05](#); [26:06](#); [27:04](#); [27:06](#); [27:07](#); [27:08](#); [37:10](#); [37:11](#); [38:01](#); [38:07](#); [41:03](#); [43:02](#); [45:02](#); [46:06](#); [46:07](#); [46:09](#))

## Naamani

### Ufafanuzi

Katika Agano la Kale, Naamani alikuwa mkuu wa jeshi wa mfalme Aramu.

- Naamani alikuwa na ungonjwa mbaya wa ngozi uitwao ukoma usiyo tibika.
- Myahudi mtumwa katika nyumba ya Naamani alimwambia aende kwa nabii Elisha apone.
- Elisha alimwambia Naamani ajisafishe mara saba katika Mto Yordani. Naamani alipo tii, Mungu akamponya ungonjwa wake.
- Baada ya matokeo, Naamani alikuja kuamini kuwa Mungu ndiye wa kweli, Yahweh.
- Wanaume wengine wawili waliitwa Naamani walikuwa uzao wa mjukuu wa Yakobo Benjamini.

(Rudi tena: [19:14](#); [19:15](#); [26:06](#))



## Nabii, unabii, mwonaji, nabii mwanamke.

### Ufafanuzi

"Nabii ni mtu anayesema ujumbe wa Mungu kwa watu. Mwanamke anayefanya hivi anaitwa "nabii mwanamke."

- Mara nyingi manabii waliwaonya watu kuacha dhambi zao na kumtii Mungu.
- Unabii ni ujumbe unaozungumzwa na nabii.
- Ujumbe wa unabii mara nyingi ulikuwa unahusu mambo yatakayotokea hapo baadae.
- Unabii mwingi wa agano la kale umeshatimia.
- Katika Biblia mkusanyiko wa vitabu vilivyoandikwa na manabii mara nyingine vinajulikana kama "manabii."
- Kwa mfano maneno "sheria na manabii" ni namna ya kuelezea maandiko ya kiebrania ambayo yanajulikana kama "agano la kale"
- Jina la zamani la nabii lilikuwa "mwonaji" au "mtu anayeona."
- Mara nyingine "mwonaji" inamana ya nabii wa uongo au mtu anayefanya uganga.

(Rudi tena: 12:12; 14:14; 17:07; 17:13; 19:01; 19:02; 19:06; 19:07; 19:08; 19:12; 19:14; 19:16; 19:17; 19:18; 20:01; 20:05; 20:10; 21:03; 21:05; 21:06; 21:09; 21:10; 21:11; 21:12; 21:13; 21:14; 21:15; 22:01; 22:07; 24:01; 24:04; 26:02; 26:05; 26:06; 36:03; 38:03; 40:03; 42:03; 43:05; 43:07; 44:05; 45:03; 48:12)

## Nathani

### Ufafanuzi

Nathani alikuwa nabii mwaminifu wa Mungu aliye ishi kipindi cha Daudi akiwa mfalme wa Israeli.

- Mungu alimtuma Nathani kumuona Daudi alipo tenda dhambi dhidi ya Uria.
- Nathani alimkemea Daudi, japo kuwa Daudi alikuwa mfalme.
- Daudi alitubu dhambi yake baada ya Nathani kumfuata.

(Rudi tena: [17:07](#); [17:13](#))

## Nazarethi, Nazarini

### Ufafanuzi

Nazarethi ni mji katika mji wa Galilaya kusini mwa Israeli. Ilikuwa kama kilomita 100 kaskazini mwa Yerusalemu, iliyo chukuwa kam siku tatu hadi tano kufika kwa miguu.

- Yusufu na Maria walitoka Nazarethi, na hapo ndipo walipo mlelea Yesu.
- Ndio maana Yesu alijulikana kama "Mnazarini"
- Wayahudi wengi wanao ishi Nazarethi hawaku muheshimu Yesu na mafundisho yake, kwasababu alikulia miongoni mwao na wakadhani alikuwa mtu tu wa kawaida.
- Wakati Yesu alipo kuwa anafundisha sinagogi la Nazarethi, Wayahudi walijaribu kumuua kwasababu alidai kuwa Mesia na akawakemea kwa kumkataa.

(Rudi tena: [23:04](#); [26:02](#); [26:07](#))

## Nchi ya ahadi

### Ufafanuzi

"Nchi ya ahadi" imaonekana tuu katika simulizi za Biblis. Ni namna ya kuelezea nchi ya Kanaani ambayo Mungu aliahidi kumpa Abrahamu na uzao wake.

- Abramam alipokuwa akiishi katika nchi ya Uru Mungu aliwamuri kwenda kuishi katika nchi ya Kanaani. Yeye na uzao wake, Waisraeli waliishi huko kwa miaka mingi.
- Wakata njaa kuu iliposababisha uhaba wa chakula Waisraeli wakahamia Misri.
- Miaka mia nne baadae Mungu akawaokoa Israeli kutoka utumwani Misri na kuwarudisha katika nchi yao ya Kanaani nchi ambayo aliahidi atawapa.

(Rudi tena: [12:01](#); [13:15](#); [14:01](#); [14:03](#); [14:08](#); [14:13](#); [14:14](#); [14:15](#); [15:01](#); [15:02](#); [15:12](#); [20:09](#); [20:10](#); [20:13](#))

## ndoto

### Ufafanuzi

Ndoto ni kitu ambacho watu huna au kupitia akilini mwao wanapokuwa wamelala.

Ndoto mara kwa mara huonekana kama zinatokea kihalisia, lakini haziko hivyo.

Mara nyingine Mungu husababisha watu kuota juu ya kitu ili waweze kujifunza kutoka na hicho kitu. Pia anaweza kuzungumza moja kwa moja na watu ndani ya ndoto zao.

Katika Biblia, Mungu alitoa ndoto maalumu kwa baadhi ya watu kuwapa ujumbe, mara nyingi kuhusu jambo ambalo lingetoke hapo baadaye.

Ndoto ni tofauti na maono. Ndoto hutokea wakati mtu amelala, lakini maono mara kwa mara hutokea wakati mtu yupo macho.

(Rudi tena: [08:02](#); [08:06](#); [08:07](#); [16:11](#); [23:01](#))



# Nebukadneza

## Ufafanuzi

Nebukadneza alikuwa mfalme wa Utawala wa Babiloni ambaye jeshi lake kuu liliwashinda makundi ya watu na mataifa.

- Chini ya uongozi wa Nebukadneza, jeshi la Wababiloni walishambulia na kuishinda Yuda, na kuchukuwa watu wa Yuda kwenda Babiloni. Hii ndio "Mateka ya Babiloni" kwa miaka 70.
- Mmoja wa mateka, Danieli, alitafsiri ndoto ambazo Nebukadneza alikuwa nazo.
- Waisraeli wengine wa tatu, Hanania, Meshaeli, na Azaria, walitupwa katika tanuru kali walipo kataa kuinama kwa sanamu kubwa Nebukadneza alilo tengeneza.
- Mfalme Nebukadneza alikuwa na kiburi na kuabudu miungu ya uongo. Alipo shinda Yuda, aliiba dhahabu nyingi na fedha kutoka hekaluni Yerusalemu.
- Kwasababu Nebukadneza alikuwa na kiburi na kukataa kugeuka pembeni asiabudu miungu ya uongo, Yahweh alimsababisha kuwa na uwitaji kwa miaka saba, akiishi kama mnyama. Baada ya miaka saba Mungu alimrejsha Nebukadneza alipo jinyenyekesha na kumuabudu Mungu wa kweli, Yahweh.

(Rudi tena: [20:06](#); [20:08](#); [20:09](#))

## Neno la Mungu, Neno la Yaweh, Neno la Bwana, maandiko

### Ufafanuzi

Katika Biblia neno la Mungu ni kitu chochote ambacho Mungu anawaambia wanadamu. Hii ni pamoja na lililoandikwa au kutamkwa. Yesu pia anaitwa "neni la Mungu.

- "Maandiko" ni maandishi . Imetumika tuu katika agano jipya na imeelezea maandiko ya Kiebrania au agano la kale. Maandishi haya yalikuwa ujumbe toka kwa Mungu aliowaambia watu kuandika ili miaka ya baadae watu waweze kuyasoma.
- Neno la Yaweh au neno la Bwana ni ujumbe toka kwa Mungu aliopewa nabii au mtu mwingine katika Biblia.
- Mara nyingine neno hili hutokea kama "neni" au "neni langu" au "neni la Mungu.
- Katika agano jipya Yesu anaitwa "neni" na "neni la Mungu." Cheo hiki kinamaanisha kuwa Yesu alidhihiridha Mungu ni nani kwa sababu yeye ni Mungu.

(Rudi tena: 25:03; 25:05; 25:07; 26:04; 33:06; 33:07; 33:08; 33:09; 42:03; 42:05; 42:07; 42:08; 48:12; 49:06; 49:18)

# Nguvu

## Ufafanuzi

"Nguvu" ni uwezo wa kufanya jambo au kusababisha mambo yatokee mara nyingi hutumia nguvu. Pia nguvu yaweza kumaanisha watu au roho zenye uwezo wa kusababisha mambo yatokee.

- "Nguvu ya Mungu ni uweza wa Mungu kufanya jambo hasa ambalo ni ngumu kufanywa na mwanadamu.
- Mungu ana nguvu juu ya vyote alivyoviumba.
- Mungu huwapa watu wake nguvuza kufanya anayoyataka ili kwamba wakiponya watu au kufanya miujiza wafanye kwa nguvu za Mungu.
- Kwa sababu Yesu na Roho mtakatifu ni Mungu wana hizi nguvu.

(Rudi tena: [22:05](#); [26:01](#); [32:15](#); [42:11](#); [43:06](#); [44:08](#))

# Nuhu

## Ufafanuzi

Nuhu alikuwa mwanaume aliye ishi miaka 4,000 iliyo pita, kipindi ambacho Mungu alipotuma garika duniani kuharibu watu waovu. Mungu alimwambia Nuhu ajenge meli kubwa ambayo yeye na familia yake waliweza kuishi wakati mafuriko yalipo funika dunia.

- Nuhu alikuwa mwenye haki aliye mtii Mungu kwa kila kitu.
- Wakati Mungu alipo mwambia Nuhu kujenga meli kubwa, Nuhu alijenga kama Mungu alivyo mweleza.
- Ndani ya hiyo meli, Nuhu na familia yake walihifadhiwa salama na baadae watoto wao na wajukuu wao walijaza dunia na watu tena.
- Kila mtu aliye zaliwa kipindi cha garika ni mzao wa Nuhu.

(Rudi tena: [03:02](#); [03:03](#); [03:04](#); [03:06](#); [03:10](#); [03:11](#); [03:12](#); [03:13](#); [03:14](#))

## nyenyekea, unyenyekevu

### Ufafanuzi

Neno 'nyenyekea' humwelezea mtu ambaye hufikirii kuwa ni bora kuliko watu wengine. Ni mtu asiye na kiburi au majivuno. Unyenyekevu ni sifa au hali ya kuwa mnyenyekevu. Kuwa mnyenyekevu mbele za Mungu ina maana ya kujua udhaifu na hali ya kutokamilika, huku ukilinganisha na ukuu, hekima na ukamilifu wa Mungu. Mtu anapojinyenyesha, hujiweka katika daraja la chini. 'Unyenyekevu' ni hali ya kujali mahitaji ya watu wengi kuliko mahitaji yako binafsi. Kirai 'uwe mnyenyekevu' kinaweza kutafsiriwa kama "usiwe mwenye kiburi/majivuno." "Nyenyekea mbele za Mungu" ina maana ya "wasilisha utashi wako kwa Mungu, kwa kuutambua ukuu wake.

(Rudi tena: [17:02](#); [34:10](#))



## okoa, salama

### Ufafanuzi

Neno "okoa" la husu kumzuia mtu kutopitia kitu kibaya au cha hatari. Kuwa "salama" ya maanisha kulindwa na hatari au majanga.

- Kwa hali ya kawaida, watu wanaweza okolewa au kombolewa kutoka kwenye hatari, au kifo.
- Katika hali ya kiroho, kama mtu ameokolewa ina maana kupitia kifo cha Yesu msalabani, Mungu amemsamehe na kumkomboa kutoadhibiwa jehanamu kwa dhambi zake.
- Watu wanaweza okoa au kukomboa watu na hatari, lakini Mungu tu anaweza okoa watu kutoadhibiwa milele kwa dhambi zao.

(Rudi tena: 09:08; 11:02; 11:05; 12:05; 12:13; 13:04; 16:04; 16:08; 16:09; 16:14; 16:17; 21:02; 21:14; 23:02; 28:07; 31:07; 38:01; 40:05; 44:08; 45:07; 47:04; 47:11; 48:05; 48:07; 49:05; 49:06; 49:12; 49:13; 50:04)

## Pasaka

### Ufafanuzi

"Pasaka " ni jina la sherehe ya kidini ambayo Wayahudi walisherehekea kila mwaka kukumbuka mi kwa namna gani Mungu aliwaokoa mababu zao Waisraeli toka utumwani Misri.

- Jina la sikukuu hii lilitokana na namna ambayo Mungu "alizipita" nyumba za Waisraeli na hakuwaua watoto wake pale alipowaua wazaliwa wa kwanza wa Misri.
- Sikukuu ya pasaka inajumuisha chakula maalumu yaani kondoo mzuri waliomuua na kumpika, pia mkate usio na amira. Vyakula hivi vinawakumbusha chakula walichokula Waisraeli usiku ule kabla ya kuondoka Mirsi.
- Mungu aliwaambia Waisraeli wale chakula hiki kila mwaka kama kumbukumbu na kusherehekea namna ambavyo Mungu "alizipita" nyumba zao na namna alivyowaweka huru toka utumwa nchini Misri.

(Rudi tena: [12:14](#); [38:01](#); [38:04](#); [43:02](#); [48:09](#); [48:10](#))

## Paulo, Sauli

### Ufafanuzi

Paulo alikuwa kiongozi wa kanisa la kwanza aliyetumwa na Mungu kupeleka habari njema kwa makundi mengi ya watu.

- Paulo alikuwa Myahudi aliyezaliwa Rumi kwenye mji wa Tarso hivyo alikuwa raia wa Rumi.
- Paulo kwa jina la Kiyahudi aliitwa Sauli.
- Sauli alikuwa kiongozi wa dini ya Kiyahudi na aliwafunga Wayahudi waliokuwa Wakristo kwa sababu alifikiri kuwa hawakumuheshimu Mungu kwa kumwamini Yesu.
- Yesu alijidhihirisha mwenyewe kwa Sauli kwa kutumia mwanga unaopofua na kumwambia aache kuwatesa Wakristo.
- Sauli alimwamini Yesu na akaanza kuwahubiria Wayahudi wenzake kuhusu Yesu.
- Baadaye Mungu akamtuma Sauli kwenda kuwahubiria wasio Wayahudi kuhusu Yesu na kuanzisha makanisa katika miji na vijiji mbalimbali. Wakati huu sasa akaanza kuitwa Paulo.
- Paulo pia aliandika barua ili kuwatia moyo Wakristo katika makanisa kwenye miji hiyo. Barua hizi zipo katika agano jipya.

(Rudi tena: [45:06](#); [46:01](#); [46:02](#); [46:04](#); [46:05](#); [46:06](#); [46:07](#); [46:08](#); [46:09](#); [46:10](#); [47:01](#); [47:02](#); [47:03](#); [47:04](#); [47:05](#); [47:07](#); [47:08](#); [47:10](#); [47:11](#); [47:13](#); [47:14](#))

## pepo mbaya, roho ovu, roho chafu

### Ufafanuzi

Misemo hii yote ina maana ya mapepo, ambayo ni viumbe vya roho vinavyopingana na mapenzi ya Mungu.

Mungu aliwaumba malaika kumtumikia. Shetani alipomwasi Mungu, baadhi ya malaika pia waliasi na kutupwa kutoka mbinguni. Inaaminika ya kwamba mapepo na roho mbaya ndio hawa "mailak walioanguka".

Mara kwa mara haya mapepo yanajulikana kama "roho chafu". Msemo "chafu" una maana ya "isiyo safi" au "uovu" au "isiyo takatifu".

Kwa sababu mapepo humtumikia shetani, wanafanya mambo maovu. Mara kwa mara wanaishi ndani ya watu na kuwaendesha.

Mapepo wana nguvu kuliko wanadamu, lakini hawana nguvu kama ya Mungu.

Mapendekezo ya Tafsiri

Msemo wa "pepo" unaweza kutafsiriwa kama "roho mchafu".

Msemo wa "roho mchafu" unaweza kutafsiriwa kama "roho chafu" au "roho iliyoharibika" au "roho mchafu".

Hakikisha ya kwamba neno au msemo unaotumika kutafsiri msemo huu ni tofauti na msemo unaotumika kumaanisha shetani.

Pia fikiria jinsi msemo wa "pepo" unaweza kutafsiriwa katika lugha ya kawaida au ya taifa.

(Rudi tena: [26:09](#); [32:05](#); [32:07](#); [32:08](#); [32:09](#); [47:03](#); [47:05](#); [49:02](#))

## Petro, Simoni Petro, Kefa

### Ufafanuzi

Petro alikuwa mmoja wa mitume wa Yesu. Alikuwa kiongozi wa muhimu katika kanisa la kwanza.

- Kabla Yesu hajamuita kuwa mwanafunzi wake aliitwa Simoni.
- Baadae Yesu akamuita Kefa yenye maana ya "jiwe" au "mwamba." Jina Petro pia linamaana ya "jiwe" au "mwamba" kwa lugha ya Kigiriki.
- Mungu alifanya kazi kupitia Petro kwa kuwaponya watu na kuhubiri habari njema kuhusu Yesu.
- Vitabu viwili vya agano jipya ni barua ambazo Petro aliandika kuwatia moyo na kuwafundisha waamini wenzake.

(Rudi tena: 28:09; 29:01; 31:05; 31:06; 31:07; 31:08; 36:01; 36:04; 36:05; 38:09; 38:10; 38:15; 39:01; 39:06; 39:07; 39:08; 43:05; 43:10; 43:11; 44:01; 44:02; 44:06; 44:08; 44:09)



## Pilato

### Ufafanuzi

Pilato alikuwa kiongozi wa serikali ya Rumi katika Yudea aliyumuhukumu Yesu kifo.

- Kwa sababu Pilato alikuwa gavana alikuwa na mamlaka ya kuamua hukumu ya kifo kwa watu wenye hatia.
- Viongozi wa dini ya Kiyahudi walimtaka Pilato amsulubishe Yesu hivyo wakadanganya na kusema Yesu alikuwa mhalifu.
- Pilato aligundua kuwa Yesu hakuwa na makosa lakini aliwaogopa makutano na akataka kuwaridhisha hivyo akawaamuru askari wake wamsulubishe Yesu.

(Rudi tena: [39:09](#); [39:10](#); [39:11](#); [39:12](#); [40:02](#); [40:09](#); [41:01](#); [41:02](#))

## Ponya, tibu

### Ufafanuzi

Maneno 'ponya' na 'tibu' yote mawili yana maana ya kumfanya mtu aliye mgonjwa, aliyejeruhika na asiyekiweza (mlemavu) kuwa na afya nzuri tena. Mtu aliyeponya au kutibiwa amekuwa amefanywa mzima na mwenye afya nzuri tena. Uponyaji waweza kutokea tu kiuasilia bila kutumia kitu chochote, hii ni kwasababu Mungu alitupa miili yenye uwezo wa kupona na kurudia hali yake ya kawaida hata kama ina vidonda au magonjwa ya aina mbalimbali. Aina hii ya uponyaji hutokea polepole. Hata hivyo hali zingine kama kuwa upofu au ulemavu, na magonjwa mengine kama ukoma hayawezi kupona menyewe tu. Wakati watu wenye magonjwa kama haya wanapoponywa huwa ni muujiza ambao hautokei mara kwa mara. Kwa mfano, Yesu aliponya watu wengi walikuwa vipofu, vilema na wagonjwa na wakapona hapo hapo. Mitume pia waliponya watu kwa miujiza, kwa mfano Petro alimfanya mlevu aweze kutembea mara hiyo.

(Rudi tena: [19:14](#); [19:15](#); [21:10](#); [26:06](#); [26:08](#); [30:03](#); [32:13](#); [32:16](#); [38:15](#); [44:03](#); [44:08](#); [49:02](#))

## Rahabu

### Ufafanuzi

Rahabu alikuwa mwanamke aliyeishi Yeriko Waisraeli walipovamia mji. Alikuwa kahaba.

- Rahabu aliwaficha Waisraeli wawili waliokuja kupeleleza Yeriko kabla ya Waisraeli kuvamia. Aliwasaidia wapelelezi kurudi kwenye kambi ya Israeli.
- Rahabu akamwamini Bwana.
- Yeye na familia yake hawakudhuriwa Yeriko ilipoharibiwa na wakaenda kuishi Israeli.

(Rudi tena: [15:01](#); [15:05](#))

## Rebeka

### Ufafanuzi

Rebeka alikuwa mjukuu wa kaka yake na Abrahamu yaani Nuhu.

- Mungu alimchagua Rebeka kuwa mke wa mtoto wa Abrahamu, Isaka.
- Rebeka alitoka mjia wa Aramu alipokuwa akiishi na kwenda na mtumishi wa Abrahamu katika mji wa Negevu ambapo Isaka aliishi.
- Kwa muda mrefu Rebeka hakuwa na mtoto lakini baadaye Mungu akambariki na mapacha Esau na Yakobo.

(Rudi tena: [06:02](#); [06:03](#); [06:04](#); [06:05](#); [06:06](#); [06:07](#); [07:01](#); [07:03](#); [07:06](#); [07:07](#))

## rehema

### Ufafanuzi

Neno "rehema" lina husu kusaidia mtu waliyo na shida, hususani wanapo kuwa chini au hali ngumu.

- Neno "rehema" linaweza maanisha maana yakuto adhibu watu kitu walicho kosea.
- Mtu mwenye nguvu kama mfalme anaelezwa kama mwenye "rehema" anapo tendea watu wema badala ya kuwaua.
- Kuwa mwenye Rehema ina maana ya kusamehe mtu aliye kukosea.
- Tuna onyesha rehema tunapo saidia watu mwenye shida kubwa.
- Mungu ni wa rehema kwetu, na anataka tuwe na rehema kwa wengine.

(Rudi tena: [19:16](#); [19:17](#); [20:12](#); [27:11](#); [32:11](#); [34:09](#))



## Rehoboamu

### Ufafanuzi

Rehoboamu alikuwa mmoja wa wana wa mfalme Sulemani na alikuja kuwa mfalme baada ya Sulemani kufa.

- Katika mwanzo wa utawala wake Rehoboamu alikuwa mkali sana kwa watu wake hivyo makabila kumi ya Israeli waliasi dhidi yake na kuunda ufalme wa Israeli huko Kaskazini.
- Rehoboamu aliendelea kuwa mfalme wa ufalme wa Kusini wa Yuda ambapo kulikuwa na makabila mawili Yuda na Benyamini.
- Rehoboamu alikuwa kiongozi mbaya asiyemtii Mungu na kuabudu miungu ya uongo.

(Rudi tena: [18:05](#); [18:06](#); [18:07](#); [18:08](#))

## rithi, urithi, mrithi

### Ufafanuzi

Maneno "rithi" na "urithi" zinamaanisha kupokea kitu cha dhamani kutoka kwa mzazi au mtu mwingine kwa sababu ya uhusiano maalumu na huyo mtu. "Mrithi" ni mtu ambaye anapokea urithi.

Urithi wa halisia ambao unapokelewa unaweza kuwa fedha, ardhi, au aina zingine za mali. Urithi wa kiroho ni vyote ambavyo Mungu huwapa watu wanaomuamini Yesu, zikiwemo baraka za maisha ya sasa pamoja na maisha ya milele pamoja naye. Biblia pia inawaiita watu wa Mungu urithi wake, kinachomaanisha kuwa ni wake, ni mali yake ya dhamani. Mungu alimuahidi Abrahamu na uzao wake kuwa watarithi nchi ya Kanaani, kwamba itakuwa yao milele. Kuna maana ya kitamathali na kiroho ya jinsi watu walio wa Mungu wanasemwa "kurithi nchi." Hii inamaanisha kuwa watafanikiwa na kubarikiwa na Mungu kwa mambo ya kimwili na kiroho. Katika Agano Jipya, Mungu anaahidi kuwa wale wanaomuamini Yesu "watarithi wokovu" na "kurithi uzima wa milele." Pia inaelezwa kama, "kurithi ufalme wa Mungu." Huu ni urithi wa milele unaodumu milele. Kuna maana zingine za kitamathali za haya maneno: Biblia inasema kuwa watu wenye hekima "watarithi utukufu" na watakatifu "watarithi vitu vizuri." "Kurithi ahadi" inamaanisha kupokea vitu vizuri ambavyo Mungu ameahidi kuwapa watu wake. Msemo huu pia unatumika kwa njia ya uhasi kumaanisha watu wapumbavu au wasiotii ambao "wanarithi upepo" au "kurithi upumbavu." Hii inamaanisha wanapokea matokeo ya matendo yao ya dhambi, ikiwemo adhabu na maisha yasiyo na maana.

(Rudi tena: [04:06](#); [27:01](#); [35:03](#))

## **Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho wa Bwana.**

### **Ufafanuzi**

Maneno haya yote humrejelea Roho Mtakatifu ambaye ni Mungu. Mungu mmoja na wa kweli aishiye milele katika nafsi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu mara zingine hutajwa kama 'Roho' na 'Roho ya Yahweh' au 'Roho wa ukweli' Roho Mtakatifu ni mtakatifu kwa sababu yeye ni Mungu. Yeye yuko kamili na mwadilifu katika kila jambo alifanyalo. Roho Mtakatifu alishiriki kikamilifu katika uumbaji wa ulimwengu pamoja na Baba na Mwana. Wakati Mwana wa Mungu, Yesu aliporudi mbinguni, Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kwa watu ili awaongoze, kuwafundisha, kuwafariji na kuwawezesha kufunya mapenzi ya Mungu. Roho Mtakatifu alimwongoza Yesu na pia anawaongoza wale wanaomwamini Yesu.

Mapendekezo ya tafsiri Neno hili laweza kutafsiriwa tu kwa kutumia maneno yenye kumaanisha 'roho' na 'mtakatifu' Lakini maneno mengine ambayo yaweza kutumika ni kama 'Roho Safi' au 'Roho aliye Mtakatifu' au 'Mungu Roho.'

(Rudi tena: 01:01; 22:02; 22:05; 23:02; 24:08; 24:09; 25:01; 26:01; 26:03; 42:10; 42:11; 43:03; 43:05; 43:08; 43:11; 45:01; 45:03; 45:07; 45:12; 46:05; 46:10)

## roho, kiroho

### Ufafanuzi

Neno "roho" la eleza sehemu isiyo ya kimwili ya watu isiyo onekana. Mtu anapo kufa, roho yake inaacha mwili wake. "Roho" inaweza eleza tabia au hali ya kihisia ya mtu.

- Neno "roho" la eleza kiumbe kisicho kuwa na mwili, hususani roho chafu.
- Roho ya mtu ni sehemu yake inayo weza mjua Mungu na kumuamini.
- Kwa ujumla, neno "kiroho" la eleza chochote kisicho katika dunia ya mwili.
- Katika Biblia, sana ueleza chochote kinacho muhusu Mungu, sana Roho Mtakatifu.
- Mungu ni roho na ameumba roho za viumbe wengine wasiyo na miili.
- Malaika ni roho, pamoja na hao waliyo hasi dhidi ya Mungu na kuwa roho chafu.
- Neno "roho ya" la weza maanisha "kuwa na tabia za," kama vile, "roho ya hekima" au "katika roho ya Eliya."
- Mifano ya "roho" kama tabia au hisia itahusisha "roho ya hofu" au "roho ya wivu"

(Rudi tena: [40:07](#); [45:05](#); [48:07](#))

## Rumi

### Ufafanuzi

Katika agano jipya mji wa Rumi ulikuwa mji muhimu wa himaya ya Warumi. Sasa ni mji kuu wa Itali.

- Himaya ya Warumi ilitawala miji yote kuzunguka bahari ya Mediteraniani pamoja na Israeli.
- Rumi ni neno linaloelezea chochote kinachozungumzia miji iliyotawaliwa na serikali ya Rumi.
- Mtume Paulo alipelekwa mji wa Rumi kama mfungwa kwa sababu alihubiri habari njema kuhusu Yesu. Kitabu cha Warumi ni barua ya Paulo kwa Wakristo waliokuwa Rumi.

(Rudi tena: [23:04](#); [39:09](#); [39:12](#); [44:05](#); [47:01](#); [47:07](#); [47:10](#))



## Sabato

### Ufafanuzi

Neno "Sabato" la husu siku ya saba ya wiki, ambayo Mungu aliwaamuru Waisraeli waitenge kama siku ya kupumzika na kutofanya kazi.

- Baada ya Mungu kumaliza kuumba dunia kwa siku sita, alipumzika siku ya saba. Kwa namna hiyo hiyo, Mungu aliwaamuru Waisraeli kutenga siku ya saba kama siku maalumu ya kupumzika na kumuabudu.
- Amri "kutakasa Sabato" ni moja ya amri kumi Mungu alizo andika katika jiwe alilo mpa Musa kwa ajili ya Waisraeli.
- Kwa kufuata kanuni ya Wayahudi ya kuhesabu siku, Sabato ya anza Ijumaa jua linapo zama na kudumu hadi Juma Mosi jua linapo zama.
- Wakati mwingine katika Biblia Sabato yaitwa "siku ya Sabato" kuliko tu Sabato.

(Rudi tena: [13:05](#); [26:02](#); [41:03](#))

## Samaria, Msamaria

### Ufafanuzi

Samaria ilikuwa jina la mji na maeneo yake jirani kaskazini mwa Israeli. Eneo hili lilikuwa katikati ya Milima ya Sharoni magharibi na Mto Yordani mashariki.

- Katika Agano la Kale, Samaria ulikuwa mji mkuu wa ufalme wa kaskazini wa Israeli. Baadae eneo lililo kuwa jirani liliitwa Samaria.
- Wakati Waassiria walipo chukuwa ufalme wa kaskazini wa Israeli, waliteka mji wa Samaria na kuwa lazimisha Waisraeli wa kaskazini kuondoka eneo hilo na kuwa hamisha maeneo tofauti katika miji ya Assiria.
- Waassiria pia walileta wageni wengi katika eneo la Samaria kuwaweka katika maeneo Waisraeli waliyo ondolewa.
- Baadhi ya Waisraeli waliyo baki eneo hilo walioa wageni waliyo hamia, na wazao wao waliitwa Wasamaria.
- Wayahudi waliwadharau Wasamaria kwasababu walikuwa nusu Wayahudi na kwasababu mababu zao waliabudu miungu ya wapagani.
- Katika kipindi cha Agano Jipya, eneo la Samaria lilipakana na Galilaya upande wa kaskazini na eneo la Yudea upande wa kusini.

(Rudi tena: [20:04](#); [27:08](#); [27:09](#); [27:10](#); [45:07](#))

## samehe, kusamehe

### Ufafanuzi

Kumsamehe mtu ina maana ya kutokaa na kinyongo dhidi ya mtu ambaye alifanya jambo la kuumiza. "Kusamehe" ni tendo la kumsamehe mtu.

Kumsamehe mtu mara nyingi humaanisha kutomuadhibu mtu huyo kwa jambo ambalo amekosa.

Msemo huu unaweza kutumika kitamathali kumaanisha, "katisha" kama msemo "kusamehe deni".

Watu wanapokiri dhambi zao, Mungu huwasamehe kutokana na sadaka ya kifo cha Yesu msalabani.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kusamehe wengine kama jinsi alivyowasamehe wao.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "samehe" inaweza kutafsiriwa kama "omba radhi" au "katisha" au "achilia" au "kutoshikilia dhidi ya"

(Rudi tena: [07:10](#); [13:15](#); [17:13](#); [21:05](#); [22:07](#); [29:01](#); [29:08](#); [29:09](#); [38:05](#); [38:12](#); [40:02](#); [42:08](#); [43:11](#); [49:11](#); [49:16](#); [49:17](#))

## Sara, Sarai

### Ufafanuzi

Sara alikuwa mke wa Ibrahimu.

- Jina lake awali lilikuwa "Sarai," lakini Mungu akalibadilisha kuwa "Sara"
- Sara alimza mwana Mungu aliyeye muahidi kumpa yeye na Ibrahimu.

(Rudi tena: [04:05](#); [04:08](#); [05:01](#); [05:02](#); [05:04](#); [05:05](#))

## Sauli (A K)

### Ufafanuzi

Sauli alikuwa mwanaume wa Kiisraeli ambaye Mungu alimchagua kuwa mfalme wa kwanza wa Israeli.

- Sauli alikuwa mrefu na mtanashati, na mwanajeshi mwenye nguvu. Alikuwa aina ya mwanaume Waisraeli walitaka awe mfalme wao.
- Japo kuwa alimtumikia Mungu mwanzoni, Sauli baadae alikuwa na kiburi na hakumtii Mungu. Matokeo yake, Mungu alimteua Daudi kuchukuwa nafasi ya mfalme na kumruhusu Sauli kuuawa katika pambano.
- Katika Agano Jipya, kulikuwa na Myahudi aliye itwa Sauli ambaye pia alijulikana kama Paulo na akawa mtume wa Yesu Kristo.

(Rudi tena: [17:01](#); [17:02](#); [17:04](#); [17:05](#))



## sheria, sheria ya Musa, sheria ya Mungu, sheria ya Yahwe

### Ufafanuzi

Misemo hii yote inamaanisha amri na maelekezo ambayo Mungu alimpa Musa kwa ajili ya Waisraeli kutii. Misemo "sheria" na "sheria ya Mungu" zinatumiwa pia kwa ujumla kumaanisha kila kitu Mungu anachotaka watu wake kutii.

Kulingana na mazingira, "sheria" inaweza kumaanisha: Amri kumi ambazo Mungu aliandika katika jiwe kwa ajili ya Waisraeli. sheria zote alizopewa Musa vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale. Agano lote la Kale (pia inajulikana kama "maandiko" katika Agano Jipya). maelekezo yote ya Mungu na mapenzi yake. Usemi "sheria na manabii" inatumika katika Agano Jipya kumaanisha maandiko ya Kihebrania (au "Agano la Kale").

(Rudi tena: [13:07](#); [13:09](#); [15:13](#); [16:01](#); [27:01](#); [27:02](#); [28:01](#); [28:03](#))

## Shetani, ibilisi, yule muovu

### Ufafanuzi

Ibilisi ni roho hai Mungu aliyo umba, lakini aliasi dhidi ya Mungu na kuwa adui wa Mungu. Ibilisi anaitwa "Shetani" na "yule muovu."

- Ibilisi ana

(Rudi tena: [21:01](#); [25:01](#); [25:02](#); [25:04](#); [25:05](#); [25:06](#); [25:07](#); [25:08](#); [26:01](#); [33:06](#); [38:07](#); [38:09](#); [48:02](#); [48:04](#); [49:15](#); [50:04](#); [50:09](#); [50:10](#); [50:15](#))

## Sila, Silivanu

### Ufafanuzi

Sila alikuwa kiongozi miongoni mwa waamini wa Yerusalemu.

- Wazee wa kanisa la Yerusalemu alichagua Sila na Paulo na Barnaba kuleta barua kwa mji wa Antioki.
- Sila baadae alisafiria na Paulo kwenye miji mingine kufundisha watu kuhusu Yesu.
- Paulo na Sila waliwekwa gerezani katika mji wa Filipi. Waliimba nyimbo kwa Mungu wakati walipo kuwa huko na Mungu akawafungua kutoka gerezani. Askari wa gereza akawa Mkristo sababu ya ushuhuda wao.

(Rudi tena: [47:01](#); [47:02](#); [47:03](#); [47:07](#); [47:08](#); [47:11](#); [47:13](#))

## Sinai, Mlima Sinai

### Ufafanuzi

Mlima Sinai ni jina la mlima uliyo upande wa kusini wa unaojulikana kama Sinai Peninsula kwa sasa. Pia ulijulikana kama "Mlima wa Horebu."

- Mlima Sinai ni sehemu kubwa ya jangwa la mawe.
- Waisraeli walikuja Mlima Sinai walipo kuwa wanasafiri kutoka Misri kwenda nchi ya ahadi.
- Mungu alimpa Musa amri kumi Mlima Sinai.

(Rudi tena: [13:01](#); [13:03](#); [13:11](#); [13:15](#); [14:01](#); [15:13](#); [20:01](#); [21:05](#))

## sio na hatia

### Ufafanuzi

Usemi "sio na hatia" unamaanisha kutokuwa na hatia la uhalifu au makosa mengine. Inaweza pia kumaanisha kwa ujumla watu ambayo hawahusiki na matendo maovu.

Mtu anayetuhumiwa kwa kufanya kitu kibaya hana hatia kama hataambatanishwa na hilo kosa. Wakati mwingine usemi "sio na hatia" unatumika kumaanisha watu ambao hawajafanya kosa kustahili ubaya wanaoupata, kama jeshi la adui kushambulia "watu wasio na hatia."

(Rudi tena: [08:06](#); [40:04](#); [40:08](#))



# Sulemani

## Ufafanuzi

Sulemani alikuwa mmoja wa wana wa Mfalme Daudi. Mama yake alikuwa ni Bathsheba.

- Sulemani alipo kuwa mfalme, Mungu alimwambia aulize chochote alichotaka. Hivyo Sulemani aliomba hekima kutawala watu wake kwa haki na kweli. Mungu alifurahishwa na Sulemani na kumpa hekima na utajiri.
- Sulemani ni al maarufu kwa kuwa na hekalu zuri Yerusalemu.
- Japo kuwa Sulemani alitawala kwa hekima mwanzoni mwa utawala wake, baadae alioa kijinga wanawake wengi wa kigeni na kuanza kuabudu miungu yao.
- Kwasababu ya kutokuwa mwaminifu, baada ya kifo chake Mungu aligawanya Waisraeli kwenye falme mbili: Israeli na Yuda. Hizi falme mara nyingi zilipigana.

(Rudi tena: [17:14](#); [18:01](#); [18:02](#); [18:03](#); [18:04](#); [18:05](#); [18:06](#))

## Sulubisha

### Ufafanuzi

Sulubisha inamaanisha kumuhukumu mtu kwa kumuweka msalabani na kumuacha ateseke mpaka afe.

- Mtu huyo anaweza kufungwa msalabani au kugongewa misumari. Watu wanaosulubishwa hufa kwa kupoteza damu nyingi.
- Huko Rumi walitumia sana njia hii kuwaadhibu watu na kuwaua wahalifu au watu walioasi dhidi ya serikali.
- Viongozi wa Kiyahudi walimuomba gavana wa Rumi kuwaamuru askari wake wamsulubishe Yesu. Askari walimweka Yesu msalabani. aliteseka masaa siti kisha akafa.

(Rudi tena: [39:11](#); [39:12](#); [40:01](#); [40:04](#); [41:01](#); [43:06](#); [43:09](#); [44:08](#))

## takatifu, utakatifu

### Ufafanuzi

Maneno 'takatifu' na 'utakatifu' hurejelea tabia ya Mungu ambayo imetengwa na kutofautishwa na kila kitu ambacho ni chenye dhambi na kisicho kamili. Mungu pekee ndiye mtakatifu kweli. Hufawafanya watu na vitu kuwa vitakatifu. Mtu aliye mtakatifu ni mali ya Mungu na ametengwa maalumu kwa kusudi la kumtumika Mungu na kumpa utukufu Yeye. Na kitu ambacho Mungu amekitangaza kuwa ni kitakatifu ni kile ambacho Mungu amekitenga kwa ajili ya utukufu wake na matumizi yake, kwa mfano madhabahu ambayo makusudi yake ni kumtolea Mungu sadaka. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu, hakuna mtu awezaye kumkaribia Mungu isipokuwa awe ameruhusiwa na Yeye kufanya hivyo, hii ni kwasababu wao ni watu tu, wenye dhambi na wasiokamili. katika Agano la Kale, Mungu alitenga makuhani kama watakatifu kwa huduma maalumu kwake. Walitakiwa kutakaswa kwa sherehe maalumu ili waweze kumkaribia Mungu. Mungu pia aliweza kutenga sehemu na vitu maalumu kuwa vitakatifu vilivyo mali yake au kupitia kwa vitu hivyo aweze kujifunua mwenyewe, vitu hivi ni kama hekalu.

Mapendekezo ya tafsiri Njia za kutafsiri neno 'takatifu' zinaweza kuwa 'kutengwa kwa ajili ya Mungu,' au "kuwa mali ya Mungu" au "hali ya kutokuwa na dhambi" au "kuwa safi." kufanya kitu/kuwa kuwa mtakatifu ina maana ya "kutakasa" au "kutenga"

(Rudi tena: [01:16](#); [09:12](#); [13:02](#); [13:05](#); [22:05](#); [50:02](#))

## teseka, kuteseka

### Ufafanuzi

Maneno "teseka" na "kuteseka" yanaeleza kupitia kitu kisicho pendeza, kama ugonjwa, maumivu, au magumu.

- Watu wanapo teswa au kuumwa, wana teseka.
- Wakati mwingine watu wana teseka kwasababu ya vitu vibaya walivyo fanya; wakati mwingine kwasababu ya dhambi na magonjwa duniani.
- Kuteseka kunaweza kuwa kimwili, kama maumivi au ugonjwa. Inaweza pia kuwa hisia kama hofu, kusunoneka, au upweke.

(Rudi tena: [09:13](#); [38:12](#); [42:03](#); [42:07](#); [44:05](#); [46:04](#); [50:04](#); [50:10](#); [50:17](#))

## tii, mtiifu, utiifu

### Ufafanuzi

Neno "tii" lina maana ya kufanya unachopaswa au kuamriwa. Neno "mtiifu" la eleza tabia ya mtu anaye tii. Wakati mwengine amri ni kuhusu kutofanya kitu, "usiibe"

- Mara kwa mara "tii" lina tumika katika muktadha wa kutii amri au sheria ya mtu mwenye mamlaka.
- Kwa mfano, watu wanatii sheria zinazo tengenezwa na viongozi wa nchi, ufalme, au taasisi ingine.
- Watoto wanatii wazazi wao, watumwa wanatii bwana zao, watu na mtii Mungu, na rahia wanatii sheria ya nchi.
- Wakati mtu katika mamlaka anapo amuru watu wasifanye kitu, wanatii kwa kutofanya.
- Neno "utiifu" la weza tafsiriwa kama, "kufanya kilicho amriwa" au "kufuata utaratibu"
- Neno "utiifu" la weza tafsiriwa kama, "kufanya kilicho amriwa" au "kufuata utaratibu"

(Rudi tena: 03:04; 04:05; 05:06; 05:10; 11:01; 13:02; 13:07; 13:10; 14:03; 14:15; 15:03; 15:13; 16:01; 17:01; 17:02; 17:13; 19:16; 19:17; 20:01; 20:05; 28:01; 28:03; 38:15; 42:10; 49:17; 50:15)



## timiza

### Ufafanuzi

Msemu "timiza" una maana ya kukamilisha au fanikisha jambo ambalo lilitarajiwa.

Pale ambapo unabii unatimizwa, ina maana ya kwamba Mungu alisababisha itokee kile kilichotabiriwa katika unabii.

Kama mtu anatumiza ahadi au kiapo, ina maana ya kwamba anafanya kile alichohadi kufanya.

Kutumiza jukumu ina maana kufanya kazi ambayo ulipangiwa au unapaswa kufanya.

Mapendekezo ya Tafsiri

Kulingana na muktadha, "timiza" unaweza kutafsiriwa kama "fanikisha" au "kamilisha" au "kusababisha kutokea" au "kutii" au "kutenda".

Msemu "imetimizwa" inaweza kutafsiriwa kama "imekuwa kweli" au "imetokea".

Njia za kutafsiri "timiza" kama vile "timiza huduma yako" inaweza kujumuisha, "maliza" au "fanya" au "mazoezi" au "tumikia watu wengine kama vile Mungu amekuita kufanya"

(Rudi tena: [21:02](#); [24:04](#); [40:03](#); [42:07](#); [43:05](#); [43:07](#); [44:05](#))

# Tohara

## Ufafanuzi

Tohara ni kitendo cha kukata govi la mwanaume au mtoto wa kiume. Sherehe ya tohara hufanyika pamoja na tendo hili.

- Mungu alimuamuru Abrahamu awatahiri wanaume wote katika familia yake na watumishi wake kama ishara ya agano lao na Mungu.
- Mungu aliamuru uzao wa Abrahamu waendeleo kufanya hivi kwa kila mtoto wa kiume katika nyumba hiyo.
- "Kutahiri moyo" ni mitendo cha kuondoa uovu wa mtu.
- Kwa namna ya kiroho "aliyetahiriwa" ni mtu ambaye ametakaswa na Mungu toka kwenye dhambi kupitia damu ya Yesu.
- "Wasiotairiwa" ni watu ambao hawajatahiriwa kimwili. Pia yaweza kuwa na maana ya ambao hawajatahiriwa kiroho wasiokuwa na mahusiano na Mungu.

(Rudi tena: [05:03](#); [05:05](#))

## **totii, mkaidi, kutotii**

### **Ufafanuzi**

Msemo wa "totii" una maana ya kutotii kile mtu mwenye mamlaka ameamuru au kuagiza. Mtu anayefanya hivi anakuwa "mkaidi".

Mtu anayefanya jambo aliloambiwa kutofanya anakuwa hatii.

Kutotii pia ina maana ya kukataa kufanya jambo ambalo liliamriwa.

Msemo "mkaidi" pia hutumika kuelezea silika ya mtu ambaye kimazoea hatii au huasi. Ina maana ya kwamba ni wenye dhambi au waovu.

Msemo "ukaidi" una maana "tendo la kutotii" au "tabia ambayo ni kinyume na kile Mungu anataka".

"Mtu kaidi" anaweza kutafsiriwa kwa "watu wanaondelea kutii" au "watu ambao hawafanyi kile Mungu anaamuru"

(**Rudi tena:** [02:11](#); [13:07](#); [13:09](#); [16:01](#); [16:02](#); [18:03](#); [35:12](#); [45:03](#); [50:16](#))

## ufalme

### Ufafanuzi

Ufalme ni kundi la watu linalotawalwana mfalme. Linamaanisha pia dola au sehemu za kisiasa ambalo mfalme au kiongozi mwingine ana madaraka na mamlaka.

Ufalme unaweza kuwa na ukubwa wowote kijiografia. Mfalme anaweza kutawala taifa au nchi au mji mmoja tu. Neno "ufalme" linaweza pia kumaanisha utawala wa kiroho au madaraka, kama usemi "ufalme wa Mungu." Mungu ni mtawala wa viumbe vyote, lakini usemi "ufalme wa Mungu" kwa mahsusi linamaanisha utawala juu ya watu waliomwamini Yesu na walionyenyeka kwa utawala wake. Biblia pia inazungumzia kuhusu Shetani kuwa na "ufalme" anao tawala kwa muda juu ya vitu vingi duniani. Ufalme wake ni uovu na unajulikana kama wa "giza."

(Rudi tena: [13:02](#); [18:04](#); [18:08](#); [18:10](#); [18:11](#); [21:08](#); [25:06](#); [39:10](#); [49:15](#); [50:15](#))

## ufalme wa Israeli

### Ufafanuzi

Usemi "ufalme wa Israeli" unamaanisha sehemu ya kaskazini mwa taifa la Israeli wakati makabila kumi na mbili ya Israeli yalipogawanyika katika falme mbili baada ya Sulemani kufa.

Ufalme wa Israeli wa kaskazini ulikuwa na makabila kumi na ufalme wa Yuda ulikuwa na makabila mawili. Mji mkuu wa ufalme wa Israeli ulikuwa Samaria. Ilikuwa kama kilomita 50 kutoka Yerusalemu, mji mkuu wa Yuda. Wafalme wote wa ufalme wa Israeli walikuwa waovu. Waliwashawishi watu kutumikia sanamu na miungu ya uongo. Mungu aliwatuma Waashuri kuvamia taifa la Israeli. Waisraeli wengi walikamatwa na kupelekwa kuishi Ashuru. Waashuri waliwaleta wageni kuishi miongoni mwa watu waliobaki wa Israeli. wageni hawa waliowana na Waisraeli, na uzao wao ukawa watu wa Samaria.

(Rudi tena: [18:08](#); [18:10](#); [18:12](#); [19:02](#); [19:05](#); [19:06](#); [20:01](#); [20:02](#); [20:03](#); [20:04](#); [20:05](#); [20:06](#))



## ufalme wa Mungu, ufalme wa mbinguni

### Ufafanuzi

Usemi wa "ufalme wa Mungu" na "ufalme wa mbinguni" zote zinamaanisha utawala wa Mungu na madaraka yake juu ya watu wake na viumbe vyote.

Wayahudi mara nyingi hutumia neno "mbingu" kumaanisha Mungu, ili kuepuka kutaja jina lake moja kwa moja. Katika kitabu cha Agano Jipya alichandika Mathayo, aliuita ufalme wa Mungu kama "ufalme wa mbinguni," inawezekana kwa sababu alikuwa akiwaandikia zaidi Wayahudi. Ufalme wa Mungu unamaanisha Mungu kuwatawala watu kiroho pamoja na kuwatawala katika dunia ya kimwili. Manabii wa Agano la Kale walisema kuwa Mungu atamtuma Masihi kutawala kwa haki. Yesu, mwana wa Mungu, ndiye Masihi atakaye tawala juu ya watu wa Mungu milele.

(Rudi tena: [24:02](#); [28:06](#); [29:02](#); [34:01](#); [34:03](#); [34:04](#); [34:05](#); [39:10](#); [40:04](#); [48:14](#); [49:05](#); [49:06](#); [49:15](#); [50:02](#); [50:08](#); [50:10](#); [50:17](#))

## Ufufuo

### Ufafanuzi

Ufufuo ni kitendo cha kuwa hai tena baada ya kufa.

- Kumfufua mtu inamaana kumrudisha mtu katika hali ya kuwa hai tena. Mungu pekee ndio mwenye nguvu ya kufanya hivi.
- Neno "ufufuo" mara nyingi humwelezea Yesu aliyekuwa hai tena baada ya kufa.
- Yesu aliposema "yeye ni ufufuo na uzima" alimaanisha kuwa yeye ni chanzo cha ufufuo na ndiye husababisha watu wawe hai tena.

(Rudi tena: [21:14](#); [37:05](#))

## upendo

### Ufafanuzi

Kumpenda mtu mwingine ni kumjali huyo mtu na kufanya vitu vitakavyo msaidia. Kuna maana tofauti za "upendo" ambazo lugha zingine zinawezakueleza kwa kutumia maneno tofauti:

Aina ya upendo utokao kwa Mungu unalenga kwa ajili ya mema ya wengine, hata kama hayamnufaishi mtu anayependa. Aina hii ya upendo inawajali watu bila kujali wanachokifanya. Mungu mwenyewe ni upendo na ndiye chanzo cha upendo wa kweli.

Yesu alionesha aina hii ya upendo kwa kujitolea maisha yake kama sadak ili kutuokoa kutoka kwenye dhambi na mauti. Aliwafundisha pia wafuasi wake kuwapenda wengine kwa kujitolea. Watu wanapowapenda wengine na aina hii ya upendo, inahusisha matendo yanayoonesha kuwa mtu anafikiria yale yatakomsaidia mtu mwingine kufanikiwa. Aina hii ya upendo inahusisha zaidi kusamehe wengine. Katika ULB, neno "upendo" linamaanisha aina hiiya upendo wa kujitoa, isipokuwa noti ya tafsiri iashirie maana tofauti.

Neno jingine katika Agano Jipya linamaanisha upendo wa kindugu au upendo kwa ajili ya rafiki au mwana familia.

Neno hili linamaanisha upendo wa asili wa binadamu kati ya marafiki na ndugu. Inawezekana kutumika katika mazingira kama, "Wanapenda kukaa kwenye viti muhimu katika sherehe." Hii inamaanisha "wanatamani sana" kufanya hivyo.

Neno "upendo" linaweza pia kumaanisha upendo wa kimapenzi kati ya mwanamme na mwanamke. Katika hali ya kimithali, "Yakobo nimempenda, lakini Esau nimemchukia", neno "mpenda" linamaanisha Mungu kumchagua Yakobo kuwa katika mahusiano ya maagano na yeye. Hii inaweza pia kutafsiriwa kama "kuchaguliwa." Ingawa Esau alibarikiwa pia na Mungu, hakupewa heshima ya kuwa katika maagano. Neno "kuchukia" linatumika kimithali hapa kumaanisha "kukataliwa" au "kutokuchaguliwa."

**(Rudi tena: [17:04](#); [17:05](#); [24:08](#); [27:02](#); [28:02](#); [28:03](#); [33:08](#); [36:05](#); [37:01](#); [39:10](#); [47:01](#); [48:01](#); [49:03](#); [49:04](#); [49:09](#); [49:13](#))**

## Uria

### Ufafanuzi

Uria alikuwa mwanaume mwenye haki na mmoja wanajeshi hodari wa Mfalme Daudi. Utajwa kama "Uria Mhiti"

- Uria alikuwa na mke mzuri sana aliye itwa Bathisheba.
- Daudi alifanya uasherati na mke wa Uria, na akashikwa mimba na mtoto wa Daudi.
- Kufunika hii dhambi, Daudi alisababisha Uria kufa kwenye pambano. Kisha Daudi akamuoa Bathisheba.
- Mwanaume mwingine aliye itwa Uria alikuwa kuhani wakati wa Mfalme Ahazi.

(Rudi tena: [17:12](#); [17:13](#))

## ushuhuda, shuhudia

### Ufafanuzi

Maneno, "ushuhuda" na "shuhudia" yanaeleza kutamka tamko kuhusu kitu ambacho mtu anajua kuwa ni kweli.

- Mara nyingi mtu anaye "shuhudia" kuhusu kitu alichu nacho amepitia moja kwa moja.
- Shahidi anaye toa "ushahidi wa uongo" hasemi ukweli kuhusu kilicho tokea.
- Wakati mwingine neno "ushuhuda" wa husu unabii ambao nabii amesema.
- Katika Agano la Kale, hili neno linatumika mara kadhaa kueleza jinsi wafuasi wa Yesu wana shuhudia kuhusu matukio ya maisha ya Yesu, kifo, na ufufuo.

(Rudi tena: [39:02](#); [39:04](#); [42:08](#); [43:07](#); [45:02](#))



## ushuru

### Ufafanuzi

Ushuru ni pesa au bidha watu wanazo lipa kwa serikali iliyo na mamlaka juu yao.

- Kiasi cha pesa kinacho lipwa kwa ushuru mara nyingi kina thamani ya bidha au kiasi ambacho mtu ana utajiri.
- Kama ushuru zisipo lipwa, serikali inaweza chukuwa hatua za kisheria dhidi ya mtu kupata pesa zinazo daiwa.
- Yusufu na Maria walisafiri Bethlehemu kuhesabiwa katika takwimu kwa lengo la kumtoza ushuru kila mtu anaye ishi katika Serikali ya Kirumi.
- Pia kulikuwa na "ushuru wa hekalu" ambao ulikuwa ni pesa watu waliyo weka katika sanduku la sadaka. Baadhi ya hizi pesa zilitumika kushughulikia jengo la hekalu.
- "Mtoza ushuru" ni mtu anaye fanya kazi serikalini kupokea pesa watu wanao takiwa kuwalipa.

(Rudi tena: [34:06](#); [34:07](#); [34:09](#); [34:10](#); [35:01](#))

## utukufu, fahari

### Ufafanuzi

Kwa ujumla, msemu "utukufu" una maana ya heshima, fahari, na ukuu wa hali ya juu sana. Kitu chochote ambacho kina utukufu kinasemekana kuwa na "fahari".

Mara nyingi, "utukufu" ina maana ya kitu chenye thamani kubwa na umuhimu. Katika muktadha zingine inawasilisha ufahari, mwanga, au hukumu.

Kwa mfano, msemu "utukufu wa wafugaji" una maana ya malisho yaliyostawi sana ambapo kondoo wao walikuwa na nyasi nyingi za kula.

Utukufu haswa hutumika kumfafanua Mungu, ambay ana ufahari zaidi ya yeyote au chochote katika ulimwengu. Kila kitu katika tabia yake huonyesha utukufu na ufahari wake.

Msemu "kutukuzwa na" una maana ya kujidai juu ya au kujivunia na kitu.

(Rudi tena: [23:07](#); [25:06](#); [37:01](#); [37:08](#))

## uzao, kutokana na

### Ufafanuzi

"Uzao" ni mtu ambaye ni ndugu wa damu moja kwa moja wa mtu mwingine nyuma kabisa katika historia.

Kwa mfano, Abrahamu alikuwa uzao wa Nuhu. Uzao wa mtu ni watoto wake, wajukuu, na watukuu, na kuendelea. Vizazi vya Yakobo vilikuwa makabila kumi na mawili ya Israeli.

msemo "kutokana na" ni njia nyingine ya kusema "uzao wa" kama vile "Abrahamu alitokana na Nuhu". Hii inaweza kutafsiriwa kama "kutokana na uzao wa"

(Rudi tena: [02:09](#); [04:06](#); [04:08](#); [04:09](#); [05:03](#); [05:10](#); [06:04](#); [08:15](#); [09:01](#); [13:09](#); [17:07](#); [18:13](#); [20:04](#); [21:01](#); [21:04](#); [48:04](#); [48:07](#); [49:08](#))

## Uzinzi, zinaa, mzinifu, mzinzi

### Ufafanuzi

Neno "uzinzi" hii ni dhambi ambayo inahusisha mwanandoa ambaye ana uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye sio mwenza wake.

- "Mzinifu" ni mtu yeyote anayefanya uzinzi.
- Mara nyingine mzinzi hutumika kuonesha kuwa ni mwanamke ndiye anayefanya uzinzi.
- Uzinzi huvunja ahadi ambayo mke na mume wamewekeana katika agano la ndoa.
- Mungu aliwaamuru Wana wa Israeli wasizini.
- Pia "zinaa" hutumika kama lugha ya picha kuwaelezea wana wa Israeli namna ambavyo hawakuwa waaminifu kwa Mungu, hasa walipokuwa wakiabudu miungu mingine.

(Rudi tena: [13:06](#); [28:02](#); [34:07](#))

## viongozi wa Kiyahudi, mamlaka ya Kiyahudi, viongozi wa dini

### Ufafanuzi

Usemi "viongozi wa Kiyahudi" au "mamlaka ya Kiyahudi" inamaanisha viongozi wa dini kama makuhani na walimu wa sheria za Mungu. Walikuwa na mamlaka yakufanya maamuzi ya mambo yasiyo yakidini pia.

- Viongozi wa Kiyahudi walikuwa ndio makuhani wakuu, waandishi (walimu wa sheria za Mungu).
- Makundi mawili makuu ya viongozi wa Kiyahudi walikuwa Mafarisayo na Masadukayo.
- Viongozi sabini wa Kiyahudi walikutana pamoja katika Baraza la Wayahudi Yerusalemu kufanya maamuzi kuhusiana na mambo ya sheria.
- Viongozi wengi wa Kiyahudi walikuwa na majivuno na walidhani ni watakatifu. Walimuonea wivu Yesu na walitaka kumdhuru. Walidai kumjua Mungu ila hawakumtii.
- Mara nyingi usemi "Wayahudi" inamaanisha viongozi wa Kiyahudi, hasa katika mazingira walipokuwa na hasira na Yesu na walipojaribu kumtega au kumdhuru.
- Maneno haya yanaweza pia kutafsiriwa kama "viongozi wa Kiyahudi" au "watu waliotawala juu watu wa Kiyahudi" au "Viongozi wa dini wa Kiyahudi."

(Rudi tena: 24:03; 24:04; 27:06; 34:06; 34:07; 34:09; 34:10; 35:02; 37:11; 38:02; 38:03; 38:14; 39:02; 39:04; 39:05; 39:08; 39:09; 39:11; 40:05; 40:09; 41:01; 44:09; 45:02; 45:04)



## Waasi, uasi.

### Ufafanuzi

Uasi ni kukataa kuitumikia mamlaka ya mtu fulani. Waasi ni watu wasiotii na kufanya mambo maovu. Mtu huyu anaitwa muasi.

- Mtu anaasi pale anapofanya jambo ambalo mamlaka iliyo juu yake imemkataza asifanye.
- Pia mtu anaweza kuasi akikataa kufanya analoamriwa afanye na mamlaka yake.
- Mara nyingine watu wanaasi juu ya serikali yao au kiongozi anayewaongoza.
- Uasi inamaana ya kukataa kutii au kuvunja sheria.

(Rudi tena: [14:14](#); [18:07](#); [18:09](#); [18:13](#); [20:07](#); [45:03](#))

## wema, uzuri

### Ufafanuzi

Neno "uzuri" una maana nyingi kutegemea na muktadha. Lugha nyingi hutumia maneno tofauti kutafsiri maana hizi tofauti.

Kwa ujumla, kitu ni kizuri kama kinalingana na tabia ya Mungu, kusudi na mapenzi.

Kitu ambacho ni "kizuri" kinaweza kufurahisha, bora, msaada, kinachofaa, chenye manufaa, au sahihi kimaadili.

Ardhi ambayo ni "nzuri" inaweza kuitwa "yenye rutuba" au "yenye kuzaa".

Zao "zuri" linaweza kuwa zao "la wingi".

Mtu anaweza kuwa "mzuri" katika kile afanyacho kama ana ujuzi katika kazi yao, yaani "mkulima mzuri".

Katika Biblia, maana ya jumla ya "nzuri" mara nyingi hutofautishwa na "uovu".

Msemo "wema" mara nyingi humaanisha kuwa mzuri kimaadili kwa kutoa mambo mazuri na yenye manufaa. Inaweza kumaanisha utimilifu wake wa kimaadili.

(Rudi tena: [01:02](#); [01:04](#); [01:05](#); [01:06](#); [01:07](#); [01:08](#); [01:11](#); [01:12](#); [01:15](#); [02:03](#); [02:04](#); [02:12](#); [08:12](#); [18:13](#); [28:01](#); [33:05](#); [33:09](#); [36:04](#); [50:05](#); [50:06](#); [50:08](#))

## Yakobo, Israeli

### Ufafanuzi

Yakobo alikuwa pacha mdogo aliyekuwa mwana wa Isaka na Rebeka.

Jina la Yakobo linamaanisha "anakamata kisigino" ambao ni usemi unaomaanisha, "hudanganya." Wakati yakobo alipozaliwa, alikuwa akishilia kisigino cha pacha wake Esau. Miaka mingi baadaye, Mungu alibalisha jina la Yakobo kuwa "Israeli," inayomaanisha, "anashindana na Mungu." Yakobo alikuwa mjanja na muongo. Alipata njia ya kupata baraka za mwana wa kwanza na kurithi haki kutoka kwa kaka yake, Esau. Esau alikasirika na kupanga kumuua, kwa hiyo Yakobo akaondoka nchini mwake. Lakini baada ya miaka Yakobo alirudi na wake zake na watoto katika nchi ya Kanaani ambamo Esau alikuwa akiishi, na familia zao ziliishi kwa amani zikiwa jirani. Yakobo alikuwa na wana kumi na mbili. Uzao wao ukawa makabila kumi na mbili ya Israeli. Mwanaume tofauti aitwaye Yakobo ameorodheshwa kama baba wa Yusufu katika ukoo wa Mathayo.

(Rudi tena: [06:07](#); [07:01](#); [07:02](#); [07:03](#); [07:04](#); [07:05](#); [07:06](#); [07:07](#); [07:08](#); [07:09](#); [07:10](#); [08:01](#); [08:03](#); [08:10](#); [08:11](#); [08:14](#); [08:15](#); [09:13](#); [09:14](#); [14:12](#); [19:10](#))

# Yaweh

## Ufafanuzi

Yaweh ni jina la Mungu alilolithirisha alipozungumza na Musa katika kichaka kinachowaka moto.

- Jina Yaweh linatokana na neno lenye maana ya "kuwepo."
- Maana nyingine ya Yaweh ni "Niko" au "anayesababisha kuwepo."
- Jina hili linadhahirisha kuwa Mungu alikuwepo na ataendelea kuishi daima. Pia inamaanisha kuwa yupo sasa.
- Tafsiri nyingi za Biblia zimetumia neno "BWANA" kuwakilisha Yaweh. Biblia za kisasa zimeandika BWANA kwa herufi kubwa kuonesha heshima kwa jina la Mungu na kutofautisha na Bwana ambayo ilitumika katika maneno ya Kiebrania.

(Rudi tena: [09:14](#); [13:04](#); [13:05](#); [16:01](#); [16:05](#); [16:13](#); [19:05](#); [19:06](#); [19:10](#); [19:11](#); [19:13](#); [23:02](#))

# Yeremia

## Ufafanuzi

Yeremia alikuwa nabii wa Mungu katika ufalme wa yuda. Kitabu cha Agano la Kale cha Yeremia kina unabii wake.

Kama manabii wengi, Yeremia mara nyingi ilimbidi kuwaonya watu wa Israeli kuwa Mungu atawaadabisha kwa dhambi zao. Yeremia alitabiri kuwa Wababeli wataiteka Yerusalemu, jambo lililowafanya baadhi ya watu wa Yuda kukasirika. Kwa hiyo walimuweka katika kisima kilichokauka na kumuacha humo kufa. Lakini mfalme wa Yuda aliwaamuru watumishi wake kumuokoa Yeremia kutoka katika kisima. Yeremia aliandika kuwa alitamani macho yake yawe "chemchemi ya machozi," kuonesha masikitiko yake makali kuhusu uasi na mateso ya watu wake.

(Rudi tena: [19:17](#); [21:05](#))



## Yeriko

### Ufafanuzi

Yeriko ulikuwa mji wenye nguvu katika nchi ya Kanaani. Ulikuwa magharabi mwa mto wa Yordani na kaskazini mwa Bahari ya Chumvi.

Kama Wakanaani wote, watu wa Yeriko waliabudu miungu ya uongo. Yeriko ulikuwa mji wa kwanza katika nchi ya Kanaani ambao Mungu aliwaambia Waisraeli kuuteka. Wakati Yoshua alipowaongoza Waisraeli dhidi ya Yeriko, Mungu alifanya muujiza mkubwa kuwasaidia kuushinda huo mji.

(Rudi tena: [15:01](#); [15:03](#); [15:05](#); [27:04](#))

## Yeroboamu

### Ufafanuzi

Yeroboamu mwana wa Nebati alikuwa mfalme wa kwanza wa ufalme wa kaskazini wa Israeli kati ya 900-910 K.K. Yeroboamu mwingine, mwana wa mfalme Yoashi, alitawala juu ya Israeli karibu miaka 120 baadaye.

Yahwe alimpa Yeroboamu mwana wa Nebati utabiri kwamba atakuwa mfalme baada ya Sulemani na kwamba atayatawala makabila kumi ya Israeli. Sulemani alipokufa, makabila kumi ya kaskazini mwa Israeli yalimkaidi mwana wa Sulemani, Rehoboamu na badala yake walimfanya Yeroboamu kuwa mfalme wao, wakimuacha Rehoboamu kama mfalme wa makabila mawili tu ya kusini, Yuda na Benyamini. Yeroboamu alikuwa mfalme muovu aliyewaongoza watu kutomuabudu Yahwe na badala yake aliweka sanamu kwa ajili yao kuabudu. Wafalme wengine wote wa Israeli walifuata mfano wa Yeroboamu na walikuwa wafalme waovu kama yeye alivyokuwa. Karibu miaka 120 baadaye, mfalme mwingine Yeroboamu alianza kutawala ufalme wa kaskazini mwa Israeli. Yeroboamu huyu alikuwa mwana wa Yoashi na alikuwa muovu kama wafalme wengine wote waliopita wa Israeli walivyokuwa. Licha ya haya yote, Mungu alikuwa na huruma juu ya Israeli na kumsaidia huyu mfalme Yeroboamu kuongeza ardhi na kuimarisha mipaka ya eneo lao.

(Rudi tena: [18:08](#); [18:09](#))

# Yerusalemu

## Ufafanuzi

Yerusalemu mwanzoni ulikuwa mji wa zamani wa Kikanaani ambao baadaye ulikuwa mji muhimu zaidi katika Israeli. Inapatikana karibu kilomita 34 magharibi mwa Bahari ya Chumvi na kaskazini mwa Bethlehemu. Bado ni mji mkuu wa Israeli ya leo.

Jina "Yerusalemu" imetajwa kwa mara ya kwanza katika kitabu cha YOSHUA. Majina mengine ya mji huu katika Agano la Kale ni pamoja na "Salemu", "mji wa Yebusi," na "Sayuni." "Yerusalemu" na "Salemu" zote zina msingi wa "amani" katika maana. Yerusalemu mwanzoni ilikuwa ngome ya Yebusi iitwayo "Sayuni" amabyo mfalme Daudi aliikamata na kuifanya kuwa mji wake mkuu. Mwana wa Daudi Sulemani alijenga hekalu la kwanza Yerusalemu, katika mlima Moria, ambao ulikuwa mlima ambao Abrahamu alimtoa Isaka kama sadaka kwa Mungu. Hekalu lilirudiwa kujengwa hapo baada ya kutetewa na Wababeli. Kwa sababu hekalu lilikuwa Yerusalemu, sherehe kuu za Kiyahudi ziliadhimishwa huko. Watu kawaida husema kwenda "juu" Yerusalemu kwa sababu palikuwa mlimani.

(Rudi tena: [17:05](#); [18:02](#); [20:07](#); [20:12](#); [20:13](#); [27:04](#); [36:03](#); [38:01](#); [38:02](#); [38:04](#); [42:02](#); [42:05](#); [42:08](#); [42:11](#); [43:01](#); [43:02](#); [43:04](#); [45:06](#); [45:07](#); [46:01](#); [46:08](#); [46:09](#))

## Yesu, Yesu Kristo, Kristo Yesu

### Ufafanuzi

Yesu ni mwana wa Mungu. Jina "Yesu" linamaanisha, "Yahwe anaokoa." Neno "Kristo" ni jina linalomaanisha "mtiwa mafuta" na ni jina jingine la Masihi.

Majina mawili mara nyingi yanaunganishwa kama "Yesu Kristo" au "Kristo Yesu." Majina haya yanasisitiza kuwa mwana wa Mungu ndiye Masihi aliyekuja kuwaokoa watu kutoadhibiwa milele kwa dhambi zao. Katika njia za kimiujiza, Roho Mtakatifu alisababisha mwana wa milele wa Mungu kuzaliwa kama binadamu. Wazazi wake wa duniani waliambiwa na malaika kumuita "Yesu" kwa sababu alikusudiwa kuwaokoa watu kutoka katika dhambi zao. Yesu alifanya miujiza mingi iliyoonesha kuwa yeye ni Mungu na ni Kristo, au Masihi.

(Rudi tena: 22:04; 23:02; 23:05; 23:08; 23:09; 23:10; 24:06; 24:07; 24:08; 24:09; 25:01; 25:02; 25:03; 25:04; 25:05; 25:06; 25:07; 25:08; 26:01; 26:02; 26:04; 26:05; 26:06; 26:07; 26:08; 26:09; 26:10; 27:01; 27:02; 27:04; 27:11; 28:01; 28:02; 28:03; 28:04; 28:05; 28:06; 28:08; 28:09; 28:10; 29:01; 29:09; 30:01; 30:02; 30:03; 30:04; 30:05; 30:08; 31:01; 31:04; 31:05; 31:06; 31:07; 31:08; 32:01; 32:02; 32:05; 32:06; 32:07; 32:09; 32:10; 32:11; 32:12; 32:13; 32:15; 32:16; 33:01; 33:02; 33:06; 34:01; 34:03; 34:06; 34:10; 35:01; 35:02; 36:01; 36:02; 36:03; 36:04; 36:06; 36:07; 37:01; 37:02; 37:03; 37:04; 37:05; 37:06; 37:07; 37:08; 37:09; 37:10; 37:11; 38:01; 38:02; 38:03; 38:04; 38:05; 38:06; 38:08; 38:09; 38:10; 38:11; 38:12; 38:13; 38:14; 38:15; 39:01; 39:02; 39:03; 39:04; 39:05; 39:06; 39:07; 39:08; 39:09; 39:10; 39:11; 39:12; 40:01; 40:02; 40:03; 40:04; 40:05; 40:07; 40:08; 40:09; 41:01; 41:03; 41:05; 41:08; 42:02; 42:03; 42:04; 42:05; 42:06; 42:07; 42:10; 42:11; 43:01; 43:02; 43:06; 43:07; 43:08; 43:09; 43:11; 44:02; 44:05; 44:08; 44:09; 45:01; 45:02; 45:03; 45:05; 45:06; 45:07; 45:12; 45:13; 46:01; 46:05; 46:06; 46:07; 46:09; 46:10; 47:01; 47:02; 47:05; 47:11; 47:13; 47:14; 48:04; 48:05; 48:06; 48:07; 48:08; 48:10; 48:12; 48:14; 49:02; 49:03; 49:05; 49:06; 49:08; 49:09; 49:10; 49:11; 49:12; 49:13; 49:14; 49:15; 49:16; 49:17; 50:01; 50:02; 50:03; 50:04; 50:05; 50:08; 50:11; 50:12; 50:13; 50:14; 50:15; 50:17)

## Yohana (Mbatizaji)

### Ufafanuzi

Yohana alikuwa mwana wa Zekaria na Elisabeti. Kwa kuwa "Yohana" lilikuwa jina lililozoeleka, mara nyingi huitwa "Yohana Mbatizaji" ili kumtofautisha na watu wengine waitwao Yohana, kama mtume Yohana.

Yohana alikuwa nabii ambaye Mungu alimtuma kuwaanda watu kumuamini na kumfuata Masihi. Yohana aliwaambia watu kutubu dhambi zao, kumgeukia Mungu, na kuacha kutenda dhambi, ili wawe tayari kumpokea Masihi. Yohana alibatiza watu wengi katika maji kama ishara ya kwamba wanatubu dhambi zao na kuziacha. Yohana alitwa "Yohana Mbatizaji" kwa sababu alibatiza watu wengi. Hakikisha kuwa watu wataelewa kuwa "Mbatizaji" haiimaanishi kanisa kwa hili jina. Inaweza kulazimu kusema, "Yohana aliyebatiza".

(Rudi tena: [22:02](#); [22:07](#); [24:01](#); [24:02](#); [24:03](#); [24:04](#); [24:05](#); [24:06](#); [24:07](#); [24:09](#))



## Yohana (mtume)

### Ufafanuzi

Yohana alikuwa mmoja wa mitume kumi na mbili na rafiki wa karibu wa Yesu.

Yohana na ndugu yake Yakobo walikuwa wana wa mvuvi wa samaki aitwaye Zebedayo. Katika injili aliyoandika kuhusu maisha ya Yesu, Yohana alijieleza kama "mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda." Hii inaonehsa kuwa Yohana alikuwa rafiki wa karibu wa Yesu. Mtume Yohana aliandika vitabu vitano katika Agano Jipya: injili ya Yohana, Ufuno wa Yesu Kristo, na barua tatu zilionadikwa kwa waumini wengine. Noti kuwa mtume Yohana alikuwa mtu tofauti na Yohana mbatizaji.

(Rudi tena: [36:01](#); [44:01](#); [44:06](#); [44:09](#))

# Yoshua

## Ufafanuzi

Kuna Waisraeli kadhaa kwenye Biblia waitwao Yoshua. Anayejulikana zaidi ni Yoshua mwana wa Nuni aliyekuwa msaidizi wa Musa na baadaye kuwa kiongozi muhimu wa watu wa Mungu.

Yoshua alikuwa mmoja wa wapelelezi kumi na mbili amabo Musa aliwatuma tafiti nchi ya ahadi. Pamoja na Kalebu, Yoshua aliwasihi watu wa Israeli watu kutii amri ya Mungu kuingia nchi ya ahadi na kuwashinda Wakanaani. Miaka mingi baadaye, baada ya Musa kufa, Mungu alimchagua Yoshua kuwaongoza watu Waisraeli kwenda nchi ya ahadi. Katika mapambano ya kwanza na maarufu zaidi dhidi ya Wakanaani, Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuuangamiza mji wa Yeriko. Kitabu cha Agano la Kale cha Yoshua kinaelezea jinsi Yoshua alivyowaongoza Waisraeli katika kuichukua mamlaka nchi ya ahadi na jinsi alivyopanga sehemu tofauti za nchi kwa kila kabila la Israeli kuishi. Yoshua mwana wa Yosadaki anatajwa katika vitabu vya Hagai na Zekaria; alikuwa kuhani mkuu aliyesaidia kujenga tena kuta za Yerusalemu. Kuna wanaume kadhaa wengine waitwao Yoshua waliotajwa katika koo na sehemu zingine katika Biblia.

(Rudi tena: [14:06](#); [14:07](#); [14:08](#); [14:14](#); [14:15](#); [15:01](#); [15:02](#); [15:03](#); [15:06](#); [15:07](#); [15:08](#); [15:11](#); [15:13](#); [16:01](#))

## Yuda Iskariote

### Ufafanuzi

Yuda Iskariote alikuwa mmoja wa mitume wa Yesu. Alikuwa ndiye aliyemsaliti Yesu kwa viongozi wa Kiyahudi.

Jina "Iskariote" inaweza kumaanisha "kutoka Keriothi", labada kuashiria kuwa Yuda alikulia katika huo mji. Yuda Iskariote alitunza fedha ya mitume na mara kwa mara aliiba kutumia kwa ajili yake. Yuda alimsaliti Yesu kwa kuwaambia viongozi wa dini mahali alipo Yesu ili wamkamate. Baada ya viongozi wa dini kumhukumu Yesu kifo, Yuda alijuta kuwa alimsaliti Yesu kwa hiyo akarudisha fedha ya usaliti kwa viongozi wa Kiyahudi na kisha kujiua. Mtume mwingine pia aliitwa Yuda na alikuwa mmoja wandugu wa Yesu. Kuna wanaume wengi waitwao Yuda katika Biblia, kama vile ndugu yake Yesu na mtume mwingine.

(Rudi tena: [38:02](#); [38:03](#); [38:06](#); [38:07](#); [38:14](#); [39:08](#))

## Yuda, ufalme wa Yuda

### Ufafanuzi

Kabila la Yuda lilikuwa kubwa zaidi kati ya makabila kumi na mbili ya Israeli. Ufalme wa Yuda uliundwa na makanila ya Yuda na Benyamini.

Baada ya mfalme Sulemani kufa, taifa la Israeli liligawanyika katika falme mbili: Israeli na Yuda. Ufalme wa Yuda ulikuwa ufalme wa kusini, uliokuwa magharabi mwa Bahari ya Chumvi. Mji mkuu wa ufalme wa Yuda ulikuwa Yerusalemu. Wafalme wanane wa Yuda walimtii Yahwe na kuwaongoza watu kumwabudu yeye. Wafalme wengine wa Yuda walikuwa waovu na kuwaongoza watu kuabudu sanamu. Zaidi ya miaka 120 baada ya Ashuru kuishinda Israeli (ufalme wa kaskazini), Yuda ilitekwa na taifa la Babeli. Wababeli waliangamiza mji na hekalu, na kuwachukua watu wengi wa Yuda kwenda Babeli kama watekwa.

(Rudi tena: [18:07](#); [18:09](#); [18:10](#); [18:13](#); [20:01](#); [20:05](#); [20:06](#); [20:07](#); [20:08](#); [20:09](#))

## Yusufu (Agano Jipya)

### Ufafanuzi

Yusufu alikuwa baba wa duniani wa Yesu na kumkuza kama mwanaye. Alikuwa mtu mwenye haki aliyefanya kazi kama seremala.

Yusufu alikuwa amemchumbia binti wa Kiyahudi aitwaye Mariamu, ambaye Mungu alimchagua kuwa mama wa Yesu Masihi. Malaika alimuambia Yusufu kwamba Roho Mtakatifu alimsababisha Mariamu kuwa na mimba, na kwamba mtoto wa Mariamu alikuwa ni mwana wa Mungu. Baada ya Yesu kuzaliwa, malaika alimuonya Yusufu kumpeleka mtoto na Mariamu Misri ili kumtoroka Herode. Yusufu na familia yake waliishi katika mji wa Nazareti ya Galilaya alipojipatia kipato kwa kufanya kazi ya useremala.

(Rudi tena: [22:04](#); [23:01](#); [23:02](#); [23:03](#); [23:04](#); [26:04](#))



## Yusufu (Agano la Kale)

### Ufafanuzi

Yusufu alikuwa mwana wa kumi na moja wa Yakobo na mwana wa kwanza wa mama yake Raheli.

Yusufu alikuwa mwana kipenzi wa baba yake. Ndugu zake walimuonea wivu na wakamuza katika utumwa. Wakati akiwa Misri, alisingiziwa na kuwekwa gerezeni. Licha ya mateso yake, Yusufu alibaki mwaminifu kwa Mungu. Mungu alimuweka katika nafasi ya pili ya madaraka katika Misri na kumtumia kuwaokoa watu katika kipindi ambapo kulikuwa na chakula kidogo. Watu wa Misri, pamoja na watu wake, waliepusha na njaa.

(Rudi tena: 08:01; 08:02; 08:03; 08:04; 08:05; 08:06; 08:07; 08:08; 08:09; 08:11; 08:12; 09:01; 09:02)

## Zakaria (Agano Jipya)

### Ufafanuzi

Katika Agano Jipya, Zakaria alikuwa kuhani wa kiyahudi aliyekuja kumzaa Yohana Mbatizaji.

- Zakari alimpenda Mungu na kumtii.
- Zakari na Elisabethi mkewe waliomba miaka mingi kwa uaminifu ili wapate mtoto lakini hawakupata. Lakini Mungu alijibu maombi yao wakiwa wazee, kwa kuwapa mtoto.
- Zakaria alitabiri kuwa Yohana mwanawe angekuwa nabii ambaye angetangaza na kuandaa njia ya Masiya.

(Rudi tena: [22:01](#); [22:02](#); [22:03](#); [22:07](#); [24:01](#))

# Washiriki

## Open Bible Stories Translation Notes Washiriki

Christina Abraham Kileo  
Cloud Roman  
Emmanuel Nyamalya  
Fred  
James Semnkai  
Joyce Gilbert Masasi  
Lameck Yakobo Tobotobo  
Majama, Musa Isaya  
Makene Mafwele  
Musa Luzali  
Raphael Musa  
Rev Melelo  
Zelote Loilang'akaki Lukumay

## Open Bible Stories Washiriki

Ev. Cloud Roman  
Ev. James A. Makula  
Ev. Lazaro Chalomhjala  
Ev. Mathew Kazimoto  
GS. Andrew Gewe  
Karen Riecks  
Miss Joyce Masasi  
Mr. Alex Nyuri  
Mr. Ezekiel Daudi  
Mr. James Semnkai  
Mr. Moses Marugu  
Pst. Isack A. Gomugo  
Pst. John Kerim  
Pst. Jordan  
Pst. Mathias William  
Rev. Catherin D. Matia  
Rev. Charles Mabisa  
Rev. Donald Dutuyi  
Rev. Dr. David Magoke  
Rev. Elias Ndema  
Rev. Elisande Mhanga  
Rev. Erasmus Malelo  
Rev. Gungutu Elias  
Rev. John Ndaluka  
Rev. Lameck Tobotobo  
Rev. Moses Eliakim Ndege  
Rev. Philipo Kanwele  
Rev. Yekonia M. Koko  
Rev. Yohana Batano  
Rev. Yohana S Dutuyi

## **unfoldingWord® Translation Academy Washiriki**

Jesse Griffin, BA in Biblical Studies, MA in Biblical Languages  
Perry Oakes, PhD in Old Testament, MA in Linguistics, MA in Theology, BA in Biblical Studies  
Susan Quigley, MA in Linguistics  
Henry Whitney, BA in Linguistics  
James N. Pohlig, M.Div., MA in Linguistics, D. Litt. in Biblical Languages  
Ben Jore, BA Biblical Studies, M.Div.  
Joel D. Ruark, PhD in Old Testament, MA in Theology  
Todd L. Price, PhD in New Testament/Linguistics  
Bev Staley  
Carol Brinneman  
Jody Garcia  
Kara Anderson  
Kim Puterbaugh  
Lizz Carlton  
Door43 World Missions Community

## **translationWords Washiriki**

Rev. Yohana Batano  
Ev. Lazaro Chalomhola  
Pst. Jordan  
Rev. Philipo Kanwele  
Kazwanomo  
Pst. John Kerim  
Rev. Charles Mabisa  
Yohana Magera  
Rev. Erasmus Malelo  
Joyce Gilbert Masasi  
Bariki Malisa  
Daudi Nungwana  
Enoch Nungwana  
Karen Riecks  
Ev. Cloud Roman  
Mr. James Semnkai